

# Kutembea Pamoja kwenye Njia ya Huduma



Taasisi ya Ruhi





Kitabu cha 7

# Kutembea Pamoja kwenye Njia ya Huduma

Taasisi ya Ruhi

Vitabu vilivyopo katika Mfuatano:

Hapa chini kuna majina ya vitabu vya sasa vilivyopo katika mfuatano uliosanifiwa na Taasisi ya Ruhi. Vitabu hivi vimekusudiwa kutumika kama mlolongo mkuu wa kozi katika jitihada ya hatua kwa hatua ya kuongeza uwezo wa vijana na watu wazima kuhudumia jumuiya zao. Taasisi ya Ruhi pia inaendelea kukuza seti ya kozi ambazo zinachepuka kutoka kitabu cha tatu kilichopo katika mfuatano kwa ajili ya kuwafunza walimu wa madarasa ya Kibahá'í ya watoto, hali kadhalika seti nyingine kutoka Kitabu cha 5 kwa ajili ya kuwainua wahuishaji wa vikundi vya vijana chipukizi. Hivi pia vimeainishwa katika orodha hapo chini. Sharti izingatiwe kwamba orodha inaweza kubadilika kadiri tajiriba ugani inavyoendelea, na vitabu vya ziada vitaongezwa kadiri idadi ya vipengele vya mtaala vinavyoendelea kukuzwa vitakapofikia hatua ambapo vitaweza kupatikana kwa wingi.

| | |
|---|---|
| Kitabu cha 1 | *Mawazo juu ya Maisha ya Roho* |
| Kitabu cha 2 | *Uinikaji kwa Kuhudumu* |
| Kitabu cha 3 | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 1* |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 2* (kozi ya mchepuo) |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 3* (kozi ya mchepuo) |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 4* (kozi ya mchepuo) |
| Kitabu cha 4 | *Wadhihirishaji Pacha* |
| Kitabu cha 5 | *Uachiliaji wa Uwezo wa Vijana Chipukizi* |
| | *Msukumo wa Awali: Mchepuo wa Kwanza wa Kozi ya Kitabu cha 5* |
| | *Upanuaji Wigo: Mchepuo wa Pili wa Kozi ya Kitabu cha 5* |
| Kitabu cha 6 | *Kufundisha Hoja* |
| Kitabu cha 7 | *Kutembea Pamoja kwenye Njia ya Huduma* |
| Kitabu cha 8 | *Agano la Bahá'u'lláh* |
| Kitabu cha 9 | *Kupata Mtazamo wa Kihistoria* |
| Kitabu cha 10 | *Kujenga Jumuiya Hai na Zenye Kupuma* |
| Kitabu cha 11 | *Nyenzo za Kimwili* |
| Kitabu cha 12 | *Familia na Jumuiya* |
| Kitabu cha 13 | *Kujihusisha katika Shughuli za Kijamii* |
| Kitabu cha 14 | *Kushiriki katika Mjadala wa Umma* |

Hatimiliki © 2003, 2025 na Ruhi Msingi, Colombia
Haki zote zimehifadhiwa. Toleo 2.1.1.PE Machi 2025
ISBN 978-628-96721-2-1

Taasisi ya Ruhi
Cali, Colombia
Barua pepe: instituto@ruhi.org
Tovuti: www.ruhi.org

# Yaliyomo


Mawazo Machache kwa ajili ya Mkufunzi .................................. v

Nguvu za Kiroho za Kusonga mbele kwenye Njia ya Huduma ... 1

Kuhudumu kama Mkufunzi wa Kozi za Taasisi ......................... 37

Ukuzaji Sanaa Mashinani ....................................................... 139

# Mawazo Machache kwa ajili ya Mkufunzi

Uinuaji wa ustaarabu mpya, unaostawi kimwili na kiroho, huhitaji uwezo uendelea kuongezeka daima wa watu binafsi, asasi na jumuiya, kuchota kwenye nguvu za ujengaji jamii zilizomo kiasili katika mafundisho ya Kibahá'í. Kuongeza uwezo huu ndiyo shabaha kuu ya mlolongo mkuu wa kozi za Taasisi ya Ruhi. Umaizi katika sura mbalimbali za uwezo huu, na jinsi unavyoweza kulelewa, hutafutwa kutoka vyanzo viwili vya msingi: kutoka bahari ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh na kutokana na tajiriba iliyozalishwa duniani kote katika kuiwezesha idadi ikuayo ya watu kutwaa hazina zake na kutoa maji yake yatiayo uzima kwa wote wanaowazunguka. Wale wanaohudumu kama wakufunzi wa kozi huleta katika jitihada zao siyo tu ujuzi walioupata kupitia masomo bali pia tajiriba yao wakati wa kutekeleza vitendo vya huduma vinavyotolewa na kozi hizi—vitendo vya huduma vinavyotaka kuanzisha mchakato wa mabadiliko ya mtu binafsi na ya pamoja kwenye ngazi ya mahali. Na, hakuna mahali popote ambapo ushiriki wao katika mchakato huu unakuwa wa muhimu zaidi kuliko hapa, katika Kitabu cha 7, ambapo mkufunzi, katika kuwasaidia wengine kutekeleza kitendo hiki cha huduma, atakuwa amawashirikisha washiriki katika uchunguzi wa njia ambayo yeye sasa anaifahamu fika kupitia tajiriba inayoendelea kwa kuitekeleza.

Uchunguzi huu huanza kwa kulenga juu ya asili ya ukuaji wa kiroho unasababishwa na huduma—mada ya kitengo cha kwanza, "Nguvu za Kiroho za Kusonga mbele kwenye Njia ya Huduma". Kitengo hiki kinawasilisha mlolongo wa mawazo ambayo yatawawezsha washiriki kutafakari juu ya mchakato wa mabadiliko ya kiroho ambao waliuanza kwa kumtambua Bahá'u'lláh na kwa kuinuka kuitumikia Hoja Yake na jamii ya wanadamu: hali ya moyo ambao umegeukia kwenye Jua la Ukweli, uwezo ambao kila mmoja wetu amejaliwa nao wa kumjua Mungu na kutafakari juu ya sifa Zake, nguvu ya upendo wa Mungu unaohuisha maisha yetu na mwangaza tuupatao kwa kutii amri Zake, uhakika tunaoupata kutokana na ujuzi Wake na imani na yakini vinavyotusukuma kutenda, hisia ya utumainifu ambayo sharti ipambanue mioyo yetu na matamanio makubwa ya kupata kusudi Lake ambalo sharti liwachochee, haja ya sisi kufanya jitihada na kutoa dhabihu, na hali ya shangwe ambayo sharti iharakishe hatua zetu.

Kwa washiriki, usomaji wa kitengo hiki utaongeza utambuzi wa dhana ambayo tayari wanaifahamu vizuri—kwamba ni katika uga wa huduma tu ndipo kila mmoja wetu ataweza kutambua uwezo tuliopewa na Mungu na kuchangia kwenye uboreshaji wa jamii. Kwenye ngazi ya ndani zaidi, wanapaswa waelewe kwamba, katika kuingia uga huu, tunasukumwa kuelekea hali ya utumishi, hali ambamo "kuwa" na "kutenda" vimeunganishwa kabisa, ile inayodai nguvu za utakaso na ujuzi, ya imani na utiifu, ya tumaini na shauku kubwa, ya dhabihu na furaha. Kutembea njia ya huduma katika hali kama hiyo hujenga mwingiliano hai kati ya uwezo uliomo ndani ya roho ya mwanadamu na nguvu madhubuti ambazo ujio wa Ufunuo wa Bahá'u'lláh umezichilia. Kama wakufunzi wachanga, washiriki wanahitaji waende mbele zaidi na kutambua kwamba ni nguvu hizi ambazo hubumba mahusiano yetu kadiri tutembeavyo njia hii pamoja, zinazokaza azma yetu na kukuza uwezo wa mtu binafsi na wa pamoja.

Baada ya kutafakari juu ya nguvu hizi za kiroho, washiriki wanapewa fursa ya kuchunguza jinsi mbinu ya kielimu ya Taasisi ya Ruhi na kozi zake zinavyowawezesha watu binafsi kuendelea katika njia hii—uchunguzi ambao ni kiini cha kitengo kinachofuata, "Kuhudumu kama Mkufunzi wa Kozi za Taasisi". Sehemu ya 15 huelezea mbinu hii kwa ufupi, kwa kuainisha baadhi ya fikra zilizosababisha maendeleo yake na kugusia juu ya baadhi ya dhana zake kuu—uendelezaji wa kusudi la kimaadili lenye pande mbili, ujihusishaji sanjari katika ujifunzaji na utendaji, uimarishaji wa uwezo—dhana ambazo ndizo msingi wa maudhui ya kozi na zinazoamua jinsi njia ya huduma inavyopaswa kukanyagwa. Sehemu zinazofuata hivyo huongelea, kila moja kwa zamu, vitabu sita vya mwanzo vya mlolongo mkuu katika jitihada ya kufafanua zaidi kanuni za kielimu zinazoongoza mtaala na kuwasaidia washiriki kupata uelewa wa kina zaidi wa kile ambacho nyenzo hizi hutaka kukitimiza. Hivyo, sehemu hizi za msingi hutegemea kwa kiasi kikubwa juu ya maneno ya utangulizi ya kila kitabu, "Mawazo Machache kwa ajili ya Mkufunzi".

Katika kuwaongoza washiriki kupitia sehemu hii kuu ya kitengo, mkufunzi hapaswi kupuuzia umuhimu wake. Dondoo kutoka maneno ya utangulizi na mazoezi ambatani, kwa kiasi fulani, vitatumika kama mbinu kwa ajili ya washiriki kuchambua maudhui ya vitabu ambavyo tayari wameshavisoma na kutafakari juu ya vitendo vya huduma vinavyohamasishwa. Lakini, muhimu zaidi, wanapaswa watambue baadhi ya sifa ambazo hupambanua mchakato wa kielimu ambao huichukulia huduma kwa Hoja na kwa wanadamu kama kanuni yake ya kiutaratibu. Kile kinachopaswa kuwa wazi kwao ni wajibu uliotolewa kukuza uelewa na kuendeleza sifa za kiroho katika mchakato huu. Ni umakinifu unaotolewa kuhakikisha kwamba vipengele hivi viwili huenda bega kwa bega ambapo huanzisha mchakato wa kielimu uliobuniwa na Taasisi mbali na kozi ambazo kwa ufinyu hulenga juu ya mafunzo katika stadi, zikiingiza tu ujuzi na habari ambavyo hutekeleza kazi mahsusi zihitajikazo.

Washiriki wataona kwa urahisi jinsi mada hii ilivyofumwa katika majadiliano ya vitabu sita vya mwanzo, iliyomo katika Sehemu ya 16 hadi 26, na mkufunzi sharti ajiandae kuwasaidia kutambua jinsi sifa zingine nyingi mno za mchakato wa kielimu zinavyopata maana kutoka humo. Miongoni mwa sifa hizi, zipo chache ambazo mkufunzi atahitaji hasa kuzikumbuka.

Kwanza, kile kinachopaswa kueleweka ni kwamba maisha yanayotolewa kwa ajili ya uendelezaji wa kusudi la kimaadili lenye pande mbili ni yale yaliyojikita juu ya Mungu na Ufunuo Wake. Huu, kwa kweli, ndio msukumo mkuu wa muundo na maudhui ya mlolongo wa kozi—ulio dhahiri tangu Kitabu cha 1. Kimekusudi kuamsha ndani mwa wale wanaokisoma hisia ya utambulisho wao wa kweli—utambulisho wa yule anayetembea njia ya huduma—kitabu hiki kinaanza kwa kuwamakinisha washiriki juu ya Maandiko Matakatifu na juu ya jitihada inayohitajika kuyaelewa na kuyatumia maishani mwao. Ni kwa muktadha huu tu ndipo kinaelekeza umakinifu wao kwenye maisha ya roho na chakula ambacho roho zao hupokea kupitia maombi na mazungumzo Naye. Inaweza kudhaniwa kwamba mchakato wa kielimu unaotafuta kuinua utambuzi kwa njia hii ungeweza kufaa zaidi kuwasaidia watu binafsi kutuliza "nafsi ng'ang'anivu" kuliko ile ambayo huhamasisha kujichunguza kwa muda mrefu kama njia ya msingi kwa ajili ya uachiliaji wa uwezo wa kiroho waliopewa.

Pili, sehemu hizi zinapaswa zitumike kutilia mkazo umuhimu unaotolewa kwenye kujenga uwezo wa mchakato wa kielimu. Kwamba mchakato huu unahusu yote mawili, ujuzi—hususan, ujuzi wa Ufunuo wa Bahá'u'lláh—na vitendo vinapaswa viwe shabaha kuu. Kwa hakika, ufaaji wake katika kuinua uwezo kimsingi hutegemea juu ya uwezo wake wa kutumia kikamilifu mwingiliano wa pamoja kati ya haya mawili: umaizi mpya unazalishwa pale uelewa unaopatikana kupitia ujifunzaji unapositawishwa kwa kuzingatia vitendo, na ujihusishaji

uendeleao katika vitendo vya huduma huongeza kiu kwa ajili ya ujuzi na kuchochea shauku ya kutafuta maana za ndani zilizofichika katika Maandiko ya Imani. Ni mkazo uliowekwa juu ya ujengaji uwezo ambao huufanya mchakato wa kielimu kuwa tofauti na aina mbalimbali za jitihada za kujiimarisha ambazo zimeibuka kwa miaka mingi ambazo, zikiwa zenye manufaa kama zilivyo, kwa ujumla hulenga juu ya ujifunzaji wa Maandiko uliotenganishwa na vitendo. Hapa, badala yake, upataji wa ujuzi hufuatiliwa katika muktadha wa kusudi lenye pande mbili la kushughulikia ukuaji wa kiroho na wa kiakili wa mtu binafsi na kuchangia kwenye mabadiliko ya jamii. Hivyo ndivyo ilivyo, basi, kwamba maendeleo ya mtu binafsi na upigaji hatua wa pamoja huletwa pamoja katika mjongeo mmoja uendeleao mbele.

Tatu, uchunguzi unapaswa utupe ufafanuzi juu ya asili ya stadi zinazokuzwa wakati wa kutembea njia ya huduma—siyo tu jinsi zinavyojengana bali pia zinavyohusiana. Dhana ya "stadi" bila shaka, ilitambulishwa kwa washiriki katika Kitabu cha 2, ambapo walihamasishwa kuinua uwezo wao wenyewe wa kuanzisha na kuendeleza mazungumzo yenye maana na yainuayo. Watakuwa wamepata hisia ya kung'amua juu ya kile ambacho istilahi hii hudokeza kupitia ujifunzaji wa kitabu hicho, na utambuzi wao wa umuhimu wake utakuwa umeongezeka wakati waliposaidiwa katika Kitabu cha 3, kama walimu watarajiwa wa watoto wadogo, katika kuelewa baadhi ya dhana za msingi za kielimu, katika kutafakari juu ya sifa na mielekeo ya kiroho ihusikayo, na katika kufanyia mazoezi ujuzi na uwezo uhitajikao. Pia, watakuwa wameona, jinsi ujifunzaji wa kila kozi iliyofuata ulivyochangia kuongeza zaidi uwezo, unaolingana na wigo uendeleao kupanuka wa huduma ambamo wao wanajihusisha.

Sasa, kama wakufunzi wachanga, watakuwa na fursa ya kutafakari juu ya dhana ya "ustadi" hasa kwa mara ya kwanza. Hapa wanapaswa waanze kutambua kwamba ukuzaji wa stadi, kama ulivyofikiriwa katika mchakato wa kielimu, unahusisha kuendelea katika seti ya sifa zinazohusiana—katika uelewa wa dhana, katika upataji wa sifa za kiroho, katika uundaji wa mienendo na mielekeo inayofaa na katika kunoa baadhi ya ujuzi na uwezo. Kuzifikiria stadi kwa namna hii, huwataka washiriki kutofautisha dhana kama ilivyotumika hapa na jinsi inavyotumika katika mazungumzo ya kila siku. Ili kuweza kufanya kitu fulani, katika mazungumzo ya kila siku, inaweza kumaanisha chochote kuanzia, tuseme, uokaji mkate hadi kutoa huduma kama mhuishaji wa kikundi cha vijana chipukizi. Dhana hii inapata maana yake iliyokusudiwa katika hali hiyo ya pili tu, kwani ili kuweza kuhudumu kama mhuishaji huhitaji mjumuiko wa sifa kadhaa kutoka kila kundi lililotajwa hapo juu. Katika kubaini mkusanyiko wa stadi, hali kadhalika zile sifa za muhimu zaidi kwao, Taasisi ya Ruhi imeepuka kuziweka bayana; iliamua mapema juu ya hilo kwamba isingekuwa na manufaa kufanya hivyo. Ilihisi ingetosha, kwa mchakato wa kielimu kutambua hitaji la kukuza sifa muhimu kwa namna ambayo ingewawezesha washiriki kutekeleza vitendo vya huduma vinavyoongezeka katika utata kwa ajili ya maendeleo ya jumuiya zao.

Hili, basi, huhusiana kwa karibu na kipengele kingine. Vitendo vya huduma vinavyoongelewa katika mlolongo mkuu wa kozi vinatekeleza kazi mbili kwa wakati mmoja: wakati vikiendeleza kwa kiwango kikubwa daima stadi za mtu binafsi, vitendo vya huduma huhakikisha kwamba jitihada zake husaidia kupanua na kuimarisha ruwaza zipumazo za maisha ya jumuiya. Kwahiyo, kitendo cha kwanza kwenye ya njia ya huduma—kushiriki sala na kutafakari juu yake na wengine, husasan na familia—siyo cha kuwekwa kando pindi tajiriba kidogo inapopatikana baada ya ujifunzaji wa Kitabu cha 1. Wala mtu haachi kufanya ziara za nyumbani katika kijiji au ujirani wake kufuatia vitendo vichache katika kuchunguza mada za kujiimarisha pamoja na familia, kama ilivyo pendekezwa katika Kitabu cha 2. Mtu binafsi, akiimarishwa na nguvu za kiini kikuacho cha marafiki waliojitoa, huendelea kupata tajiriba zaidi na zaidi, kupiga hatua katika stadi zinavyolingana kadiri afanyavyo hivyo, na husaidia

kwa namna hii kufuma mfumo wa jumuiya yenye dhamira kupitia ujihusishaji uendeleao na ukomavu wa tajiriba.

Kwa mkufunzi wa Kitabu cha 7, mawazo ya hapo juu yanapaswa yasaidie kuraghibisha majadiliano yenye mafanikio kuzungukia kiini cha kitengo cha pili. Wakati muda wa kutosha unapaswa kutolewa kwenye usomaji wa sehemu husika, pia inapaswa ikumbukwe kwamba washiriki watazirudia sehemu hizo tena na tena kadiri watakapoanza kufanya kitendo hiki cha huduma. Bila shaka, maneno ya utangulizi kwa kila kitabu, "Mawazo Machache kwa ajili ya Mkufunzi", yenyewe yatakuwa, nyenzo muhimu sana, kadiri wanavyotaka kupata umaizi zaidi kwenye asili ya mchakato wa kielimu, mchakato ambao utategemea sana juu ya uchangiaji wao kwa ajili ya ukunjukaji wake imara.

Kuhusiana na hili, itakuwa yenye msaada kwa mkufunzi kukumbuka muundo mzima wa kitengo hicho na kuwa na wazo kamili la nini kizitangulie na kizifuatie sehemu hizi kuu. Ili kuweka msingi kwa ajili ya uchunguzi unaofanyika hapo, mada mbili muhimu zinaongelewa katika sehemu ya kwanza ya kitengo. Sehemu ya 2 hadi ya 9 huchunguza wazo la hamasa, na Sehemu ya 10 hadi ya 14 hujadili mada ya ushiriki.

Kuhusu ile ya kwanza, kitengo kinapendekeza kwamba, vigezo vyovyote vile viwezavyo kuhusika, ni uelewa ambao ndiyo hamasa kuu kabisa. Mpaka hapo mchakato wa kielimu utakapoweza kulea ufahamu, ndipo utakapofanikiwa kugusa mizizi ya hamasa ambayo imo ndani kabisa ya roho ya mwanadamu. Sehemu ya 5 hutoa dondoo kutoka katika utangulizi wa Kitabu cha 1 ambaohuelezea kusudi la kitengo chake cha kwanza, "Ufahamu wa Maandiko ya Kibahá'í". Katika kufanya hivyo, humuongoza mkufunzi mwenye shauku kupitia tafakari juu ya dhana ya ufahamu, hususan kama inavyofungamana na Maandiko kama chanzo cha ujuzi halisi. Mazoezi ya sehemu hiyo yatawasaidia washiriki kutambua sura mbalimbali za uelewa ambazo kozi zinatumaini kuziendeleza, na itakuwa muhimu kwao kupata sura hizi akilini pale watakapoanza hatimaye kusoma kozi pamoja na kikundi cha marafiki. Hiyo humaanisha, kamwe lisifanyike jaribio lolote la kuyatua kwa ufinyu kabisa mawazo haya yaliyokwishajadiliwa. Taasisi ya Ruhi yenyewe, katika kutafakari juu ya jinsi mchakato wa kielimu unavyoweza kulea uelewa, imeepuka aina yoyote ya mbinu ya kifomyula. Badala yake imeweka imani katika uwezo wa washiriki kupata uelewa mkubwa zaidi na zaidi wa maana zisizo na kikomo zilizomo katika Neno Takatifu kadiri wanavyolisoma, kadiri wanavyojitahidi kulitumia kwenye uboreshaji wa maisha yao binafsi na maisha ya jumuiya yao, na katika uchambuzi wa mwisho, kadiri wanavyoliruhusu kubumba mawazo na vitendo vyao.

Kuhusu suala la "ushiriki", hii ni dhana ya kina iliyomo katika mlolongo mzima wa kozi. Hata hivyo, mchakato wowote wa kielimu unaohusiana na kukuza uwezo kwa ajili ya ujengaji wa ustaarabu wa ulimwengu ulioonwa na Bahá'u'lláh, Ambaye mafundisho Yake yamekusudiwa kwa ajili ya jamii nzima ya wanadamu, ungelazimika kutumia mbinu ambayo ni shirikishi kwa asili. Sehemu ya 10 huelezea kile ambacho hii humaanisha kwa mtindo wa ufundishaji-ujifunzaji uliotazamiwa katika kozi, na uangalifu wa kutosha unapaswa utolewe kwenye mawazo yaliyoongelewa. Kozi zimebuniwa ili kumwezesha kila mtu kuwajibika kwa ajili ya ujifunzaji wake mwenyewe. Mazungumzo ya kubuni katika Sehemu ya 12 na 14, ambayo hutilia mkazo baadhi ya athari za mbinu hii shirikishi kwa mkufunzi, yanapaswa yainue utambuzi kwa urahisi ambao kwao ujifunzaji wa kozi sharti uendewe. Wanapaswa wapate ufahamu, vile vile, wa hatari zilizomo kiasilia katika utumiaji wa mbinu ili kushawishi iushiriki uliotarajiwa na katika kuziruhusu kupata kupaumbele dhidi ya maudhui. Ugumu haumo tu katika kiwango cha nguvu na rasimali zinazoweza kutumika katika utafutaji wa mbinu bali, muhimu zaidi, jinsi kuzitegemea kunavyopunguza ufaaji wa ujifunzaji katika kufikia lengo lake

kuu—uongezekaji wa uelewa. Ingawa ni kweli kwamba baadhi ya mbinu rahisi wakati mwingine zinaweza kusaidia kwa ajili ya makusudi mahsusi, wakufunzi wenye shauku wanapaswa watambue kwamba hatimaye ni ufahamu wao wa maudhui ya kozi, vikiwemo vitendo vya huduma vinavyoviibua, ndivyo vitakavyowasaidia kubuni mtindo uhitajikao wa ufundishaji-ujifunzaji.

Baada ya kuelezea dhana ya ushiriki kama inavyohusiana na usomaji wa kozi, kitengo hujongea kwa namna ya kawaida katika uchunguzi wa mlolongo mkuu katika sehemu kuu zilizojadiliwa hapo juu. Kisha kinagusa kwa ufupi Sehemu ya 27, juu ya suala la kozi zinazochepuka kutoka mlolongo mkuu, kabla ya kugeukia mfumo wa uwasilishwaji wake. Kile kinachopaswa kieleweke ni kwamba mfumo huo siyo wa kiholela. Ukiwa umeundwa na vipengele vitatu vya msingi—mtaala, kikundi cha mafunzo na mkufunzi—unaakisi kanuni muhimu iliyopo kwenye kiini cha mchakato wa kielimu, kanuni ambayo hutumika sawia kwa ujifunzaji na kwa utendaji: watu binafsi, ambao hatimaye wanawajibika kwa ajili ya ujifunzaji wao wenyewe, sharti waruhusiwe kuendelea kwenye njia ya huduma kwa mwendo na hatua inayofaa kwa hali zao binafsi. Kwamba unyumbulifu wa kiasili uliomo katika mfumo unaokidhi kanuni hii ni jambo ambalo washiriki wanapaswa kulizingatia kama wakufunzi wa baadaye. Unyumbulifu huu huonekana hasa kwa jinsi mfumo unavyofanya kazi—kwa mfano, kwa namna vikundi vya mafunzo vinavyoundwa, kukutana kwao kwa mara kwa mara, na katika njia zinazokamilishana za uwasilishaji ambazo huruhusu mabadiliko machache katika ushadidi wa ujifunzaji. Katu isichukuliwe kwamba mantiki ya kimsingi ya mlolongo wa kozi yaweza kupuuzwa. Mara chache, zinaweza kutokea hali maalum ambapo katika kuitikia kwenye hitaji la wakati huo, kitabu kimoja au kingine husomwa kama kozi inayojitegemea au mpangilio wa masomo unarekebishwa kwa muda. Walakini, ni mjongeo wa watu binafsi kupitia kozi kwa mpangilio, ndio unaojenga uwezo. Siyo tu wao wanaweza kushughulika na maudhui yenye changamoto zaidi na zaidi kwa jinsi hii, wakipanua uelewa wao wa dhana juu ya msingi wa kile walichojifunza, bali pia wanaweza kutekeleza vitendo vihitajikavyo zaidi vya huduma, katika kila hatua kwenye njia hiyo, wanapata ujuzi wa kivitendo na umaizi uhitajikao kwa wao kupiga hatua zaidi.

Kuhusu mkufunzi—mtu muhimu sana kwa mfumo mzima wa kielimu—ujifunzaji wa kitengo hiki utakuwa umempa mwanga juu ya sifa zinazohusiana ambazo kitendo hiki cha huduma huhitaji: juu ya sifa za kiroho, mielekeo, stadi na vipawa vinavyotumika katika kukiongoza kikundi kupitia kozi, kwa kuongezea juu ya uelewa wa kina wa dhana na kanuni zinazoongoza mtaala. Katika hili, washiriki watakumbushwa kwamba, kama ilivyo katika stadi zozote, wale wanaohitajika kuhudumu kama wakufunzi kwa ufanisi mkubwa zaidi na zaidi, wataendelea kukua kadiri muda upitavyo kupitia tajiriba. Pia watahamasishwa kutumia fursa nyingi watakazozipata kutafakari kila mara juu ya maudhui ya kozi na kujifunza kutokana na tajiriba za wakufunzi wenzao katika mikutano ya kutafakari iliyoandaliwa kwa kusudi hili. Ili kuwasaidia kupata uelewa wa kile ambacho ushiriki wao katika mikusanyiko hii utahusisha, Sehemu ya 32 hadi 35 inawasilisha mazungumzo ya kubuni kati ya wakufunzi wachache na mratibu wa taasisi wa mlolongo mkuu wa kozi. Majadiliano yao kimsingi yanahusiana na ujifunzaji wa maudhui; walakini pia ingefaa kufikiria kwamba mkusanyiko kama huo ungetoa nafasi kwa ajili ya kugawa umaizi uliopatikana kutoka katika jitihada za kuwasaidia watu binafsi katika kutekeleza vitendo vya huduma ambavyo kwavyo kozi inajaribu kuwajengea uwezo.

Hapa wazo lingine linastahili kutajwa. Washiriki kwa namna moja au nyingine, tangu kurasa za mwanzoni mwa kitabu, watakuwa wamepata vianga vingi kwenye asili ya mchakato wa kielimu ambao hutafuta kuachilia uwezo wa kiroho na wa kiakili wa mtu binafsi katika

uendelezaji wa kusudi la maadili lenye pande mbili. Kwamba umakini unaotolewa kuendeleza stadi kwenye njia ya huduma, ambao kwa kiwango kikubwa, huchangia kwenye uwezeshaji watu binafsi kimaadili na kiroho utakuwa dhahiri kwa washiriki kadiri wanavyokaribia mwisho wa kitengo hiki. Kile ambacho wakufunzi wachanga hawapaswi kukipuuza—na, kwa hakika, kile kinachopaswa kuamsha jitihada zao za siku zijazo—ni uwezo uliomo kiasili katika mchakato wa kuzalisha mjongeo wa watu kuelekea Utaratibu wa Ulimwengu uliotazamiwa na Bahá'u'lláh. Kwa kuwa ni kadiri watu binafsi, safu juu ya safu, wanavyokanyaga njia moja kwa pamoja, wakiambatana na kusaidiana na kuhusisha ushiriki wa wengine wasiohesabika katika kuinua jumuiya zao, ndipo nguvu za kiroho zitakapoachiliwa kwa ukubwa uhitajikao na nguvu za mjongeo ulioanzishwa.

Kitengo cha tatu cha Kitabu cha 7 hufanyiza uhusiano wa kiasili na kile cha pili. Kikiwa kifupi kwa wastani, "Ukuzaji Sanaa Mashinani" hujenga juu ya umaizi ambao washiriki wameupata katika mchakato wa kielimu wa kuchunguza nafasi ya shughuli za kisanii katika kuendeleza mchakato huu na katika kuimarisha mtindo wa maisha ya jumuiya ambao huuibua. Hadi sasa washiriki watakuwa wamepata uelewa mzuri wa uhusiano wa karibu baina ya hivi viwili na watatambua kwamba, hususan katika muktadha wa mchakato wa kielimu, jitihada za pamoja kama vile kampeni za taasisi na kambi hutoa wigo mpana kwa ajili ya matumizi ya Sanaa katika aina mbalimbali—muziki, utambaji hadithi, maigizo na stadi za kazi. Kabla ya kutazama aina hizi za sanaa kwa utondoti kiasi, kila moja kwa zamu, washiriki, kwa zamu, hutafakari juu ya nukuu kadhaa kutoka Maandiko ambazo huongelea asili ya jitihada za kisanii na uwezo wake wa kuamsha katika roho ya mwanadamu nguvu ya mvuto kwa uzuri. Msukumo wa kuendeleza sanaa mashinani ni udhihirisho mmojawapo wa nguvu hii yenye uwezo, ambayo, katika uchambuzi wa mwisho, ni taswira tu ya nguvu ya mvuto kwa uzuri unaong'aa kutoka Ufunuo wa Bahá'u'lláh, ambao mbele yake "utukufu Wake asili yenyewe ya uzuri sharti ikwajuke na kusinyaa". Ni katika Neno la Mungu ambalo Yeye amelifunua kwa ajili ya uhuishaji wa jamii ya wanadamu, basi, kwamba sharti tutafute kiwango cha uwasilishaji wa kisanii, kwa vyote viwili katika kuinua roho ya mwanadamu na katika kujenga utamaduni unaobumbwa kupitia mafundisho ya Imani.



# Nguvu za Kiroho za Kusonga mbele kwenye Njia ya Huduma

## Kusudi

Kupata utambuzi uongezekao wa nguvu za kiroho
za uendeleaji kwenye njia ya huduma kwa Hoja na
binadamu na kujipatia ufahamu wa nguvu zitendazo kazi

## SEHEMU YA 1

Kama wengine ambao wameanza ujifunzaji wa Kitabu cha 7, hadi sasa mmepata fursa ya kupitia vitabu sita vilivyotangulia vya Taasisi ya Ruhi. Ushiriki wenu katika mchakato wa taasisi, tumetaja hapo awali, unaweza kuelezwa kwa namna ya kutembea kwenye njia ya huduma. Kadiri muendeleavyo kwenye njia hii, mnakua kiroho na kukuza stadi zihitajikazo kuchangia kwenye maendeleo ya jumuiya yenu, mkijihusisha katika maeneo ya shughuli zenye utata uongezekao. Mkitambua furaha iliyomo kiasilia katika kutembea njia ya huduma, sasa mngependa kuwasaidia wengine ambao wana shauku kuanza kutembea kwenye njia hii hii. Ikiwa mnataka kuwa wenye ufanisi zaidi na zaidi katika kufanya hivyo, itakuwa muhimu kwenu kutafakari mara kwa mara juu ya asili ya ukuaji wa kiroho—ukuaji ambao una uhusiano wa karibu sana na uachiliaji wa uwezo kuhudumia Hoja na wanadamu. Kitengo hiki kinatumaini kuwasaidia katika tafakari hii.

## SEHEMU YA 2

Juu ya uwanda huu wa kidunia wa uwepo, tunajitahidi kukuza sifa za kiroho ambazo kiasili tunazo. Jinsi tunavyomiliki sifa za kiroho ni tofauti sana na jinsi tunavyomiliki vitu vya kimwili. Pale kioo kinapoakisi jua, kwa namna fulani humiliki taswira ya jua. Lakini, kwa kweli, jua halimo ndani ya kioo hicho. Sifa zetu za kiroho ni zawadi kutoka kwa Mungu ambazo twazipokea tunapogeuza vioo vya mioyo yetu kumuelekea Yeye. Sifa takatifu, walakini, huakisiwa kwa uhafifu tu katika mioyo iliyotandwa na kutiwa giza na vumbi na uchafu wa ulimwengu huu. Huonekana inafaa, basi, kwamba kifungu cha kwanza tujifunzacho katika kitengo hiki, kinachotaka kuchunguza asili ya ukuaji wa kiroho, kinapaswa kuwa kile kinachosisitiza umuhimu wa ung'arishaji wa kioo cha moyo. 'Abdu'l-Bahá husema:

> **"Jambo muhimu kabisa ni kung'arisha vioo vya mioyo ili kwamba iweze kuwa iliyoangaziwa na pokevu kwa mwangaza mtakatifu. Moyo mmoja unaweza kuwa na uwezo wa kioo kilichong'arishwa; mwingine, ukatandwa na kutiwa giza na vumbi na uchafu wa ulimwengu huu. Ingawa Jua hilo hilo linawaka juu ya vyote viwili, katika kile kioo kilichong'arishwa, kisafi na kilichotakasika unaweza kuliona Jua katika ukamilifu, utukufu na nguvu zake zote, likifunua fahari na mng'ao wake; lakini katika kioo chenye kutu na kilichotiwa giza hakina uwezo wa kuakisi, ingawa kadiri Jua lenyewe linavyohusika, linaendelea kuwaka juu yake na halipunguki wala kunyimwa. Kwa hiyo, wajibu wetu umo katika kujitahidi kung'arisha vioo vya mioyo yetu ili kwamba tuweze kuwa waakisi wa mwanga huo na kuwa wapokeaji wa baraka takatifu ambazo zinaweza kufunuliwa kikamilifu kupitia kwayo."**[1]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. Tunapaswa __________________ vioo vya mioyo yetu ili kwamba iweze kuwa ___________________ na _________________ kwa mwangaza _______________ .

   b. Moyo mmoja unaweza ______________ uwezo wa kioo ___________________ moyo mwingine unaweza ____________________ na ____________________ na ___________________ na _________________ wa ulimwengu huu.

c. Jua hilo hilo ____________________ juu ya __________ kioo kilichong'arishwa na kioo kilichotiwa giza kwa vumbi na uchafu wa ulimwengu huu.

d. Katika kioo kilichong'arishwa, __________ na ___________________ tunaweza kuliona Jua katika ________________ , ___________ na __________ , zake zote, likifunua _________________ na _______________________ wake.

e. Katika kioo chenye ________________ na ________________ hakina ___________________ wa _______________________ .

f. Wajibu wetu umo katika kujitahidi kung'arisha vioo vya mioyo yetu ili kwamba tuweze kuwa ________________ wa mwanga mtakatifu na _________________ wa ________________________ ambazo zinaweza ______________ kikamilifu kupitia kwayo.

2. Amua kama kauli zifuatazo ni kweli:

_____ Kioo kilichong'arishwa huakisi mwanga wa jua la kimwili.

_____ Kioo chenye kutu na kilichofifia hakiwezi kuakisi mwanga wa jua la kimwili.

_____ Jua la Ukweli hung'aa juu ya mioyo safi.

_____ Jua la Ukweli hung'aa juu ya mioyo iliyotiwa giza na mavumbi na uchafu wa ulimwengu huu.

_____ Mioyo safi huakisi mwanga wa Jua la Ukweli.

_____ Mioyo iliyotiwa giza kwa vumbi na uchafu wa ulimwengu huu huakisi mwanga wa Jua la Ukweli.

3. Amua ni yapi kati ya yafuatayo ni "vumbi na uchafu" wa ulimwengu huu:

| | | | |
|---|---|---|---|
| _____ | mwambatano na mali za kiulimwengu | ____ | kujipendelea |
| _____ | upendo kwa wanadamu | ____ | ujuzi |
| _____ | uroho | ____ | kupenda starehe |
| _____ | husuda | ____ | kiburi |

4. Amua yapi kati ya yafuatayo hutusaidia "kung'arisha vioo vya mioyo yetu":

| | | | |
|---|---|---|---|
| _____ | shangwe | _____ | kuwapendelea wengine kuliko sisi wenyewe |
| _____ | imani | _____ | upendo kwa wanadamu |
| _____ | wema | _____ | upendo wa Mungu |
| _____ | ujuzi | _____ | sala |

______ kushindana na wengine

______ kufikiria kasoro

______ matendo mema

______ kujifunza Neno la Uumbaji na wengine

5. Ili kuzuia vumbi na uchafu wa ulimwengu huu kukusanyika juu ya vioo vya mioyo yetu, inatupasa kufanya jitihada kila wakati. Amua kama kauli zifuatazo ni kweli:

______ Sala pekee itang'arisha vioo vya mioyo yetu.

______ Matendo mema pekee yatang'arisha vioo vya mioyo yetu.

______ Sala pamoja na matendo mema yatang'arisha vioo vya mioyo yetu kwa sababu huvutia baraka za Mungu.

______ Ni kwa kupitia baraka za Mungu tu ndipo tunaweza kung'arisha vioo vya mioyo yetu.

______ Inawezekana kupoteza usafi wa moyo wa mtu.

______ Wakati fulani katika maisha yetu, kazi ya kung'arisha vioo vya mioyo yetu hufikia tamati.

6. Jibu maswali yafuatayo:

a. Ni lipi kusudi la moyo safi? ________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

b. Je, moyo ambao haujatakasika unaweza kupata nini? ______________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

c. Je, ni ipi hali ya moyo ambao haujageuziwa kuelekea Jua la Ukweli? __________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

7. Jadili swali lifuatalo pamoja na washiriki wengine wa kikundi chako: Jinsi gani mtu anayetembea katika njia ya huduma ataweza kujilinda dhidi ya vumbi na uchafu wa ulimwengu huu?

8. Pengine mngependa kukariri nukuu ifuatayo:

**"Sifa zote na utukufu ziwe kwa Mungu Ambaye, kupitia uwezo wa nguvu Zake, ameukomboa muumbo Wake kutoka utupu wa kutokuwepo, na kuuvika kwa vazi la uhai. Kutoka miongoni mwa vitu vyote vilivyoumbwa Yeye ameuteua kwa ajili ya fadhili Yake maalum uhalisia wa mtu uliotakasika, unaofanana na kito chenye thamani, na ameupa uwezo wa kipekee wa kumjua Yeye na wa kuakisi ukuu wa utukufu Wake."**[2]

## SEHEMU YA 3

Kila mmoja wetu amejaliwa uwezo wa kumjua Mungu na kutafakari juu ya majina na sifa Zake. Pia tumejaliwa uwezo mwingine usiyohesabika uliyojificha ndani mwetu. Walakini, kipimo cha uwezo hakilingani kwa kila mmoja, na Mungu hatatuuliza kile ambacho kipo nje ya uwezo wetu. Kile tunachoombwa kufanya ni kukuza kwa ukamilifu kabisa kile ambacho kwa asili tunacho. Bahá'u'lláh husema:

> **". . . Nimekamilisha ndani ya kila mmoja wenu muumbo Wangu, ili ubora wa kazi ya mikono Yangu uweze kufunuliwa kikamilifu kwa watu. Kinachofuata, kwa hiyo, ni kwamba kila mtu amekuwa, na ataendelea kuwa, mwenye uwezo yeye mwenyewe, kutambua Uzuri wa Mungu, Aliyetukuka. Laiti asingekuwa amejaliwa uwezo kama huo, angewezaje kuitwa kueleza sababu ya kushindwa kwake?"[3]**

Ili kupata sifa takatifu, sharti tutambue daraja la juu la kiroho ambalo Mungu amelikusudia kwa kila mmoja wetu na kuliendea kwa uthabiti. Mioyo yetu sharti ivutiwe kuelekea uzuri wa kweli, Uzuri wa Mtukufu Kabisa. Hicho ndicho kiwango kamili cha kuongoza fikra na vitendo vyetu; hatupaswi kuridhika na hali ya uduni. Kuishi kufuatana na viwango vya jamii ya leo hutuvuta kuingia katika hali ya uduni. Watu wengi hudhani kwamba ubora hupatikana kupitia ushindani na wengine. Lakini, kwa kweli, ushindani hutuzongomeza zaidi katika mitego ya ulimwengu huu. Nguvu inayotusukuma kuelekea ubora inapaswa iwe shauku yetu kuu ya kukifikia kile ambacho Mungu amekiamuru kwa ukarimu kwa ajili yetu. Kujitahidi kufikia ubora humaanisha kujitahidi kukuza kwa ukamilifu wake wote vipawa ambavyo tumejaliwa. Shoghi Effendi hutuambia kwamba wale ambao hutamani kusogea karibu zaidi na Mungu

> **"hawapaswi kutazama hali ya ukengeukaji wa jamii wanamoishi, wala kwenye shuhuda za mmomonyoko wa maadili na mwenendo wa kipuuzi ambao watu wawazungukao huuonesha. Hawapaswi kujiridhisha na utofauti linganifu na ubora pekee. Bali wanapaswa wakazie macho yao kwenye vilele bora zaidi kwa kuweka mashauri na maonyo ya Kalamu ya Utukufu kama lengo lao kuu kabisa. Hapo ndipo itakapotambulika mara moja ni nyingi kiasi gani hatua ambazo zingali bado kuvukwa na ni mbali kiasi gani kutoka hapo hadi lengo litamaniwalo lilipo—lengo ambalo si lingine bali ni kielelezo cha maadili na njema za kimbingu."[4]**

1. Kwa mujibu wa nukuu ya kwanza hapo juu, hebu tutafakari kwa ufupi juu ya dhana ya "uwezo". Amua kama kauli zifuatayo ni za kweli:

    _____ Watu wote wana uwezo wa kumjua Mungu na kuakisi majina na sifa Zake.

    _____ Sababu za baadhi ya watu kumkataa Mdhihirishaji wa Mungu ni kwamba hawana uwezo wa kumjua Mungu na kuutambua Uzuri Wake.

    _____ Mtu asiye mwema hana uwezo wa kuwa mwema.

    _____ Mtu aliyelelewa kutokuwa mwaminifu hana uwezo wa kuwa mwaminifu.

    _____ Inawezekana kuujua uwezo wa mwingine.

    _____ Kila mmoja wetu anaujua uwezo wake mwenyewe.

_____ Mungu pekee anajua kiasi cha uwezo wa kila mmoja wetu.

_____ Tunakuza vipawa vyetu kupitia juhudi zetu binafsi pekee.

_____ Tunakuza vipawa vyetu kupitia neema ya Mungu kadiri tunavyojitahidi kutakasa mioyo yetu na kuchangia kwenye mabadiliko ya jamii.

2. Sasa kwa kuwa tumetoa mawazo machache juu ya dhana ya "uwezo", tunaweza kuchunguza wazo linalohusiana la "ubora" ili kupata umaizi zaidi katika asili ya ukuaji wa kiroho. Ili kutusaidia kufanya hivyo, tutamakinikia juu ya nukuu ya pili hapo juu katika zoezi hili na mengine kadhaa yanayofuata Jaza nafasi zilizoachwa wazi katika sentensi zifuatazo:

a. Shoghi Effendi hutuambia tusitazame

– ______________________________________________

– ______________________________________________

______________________________________________

b. Tusijiridhishe na

– ____________________ linganifu.

– ____________________ linganifu.

c. Badala ya kuridhika na ubora linganifu, tunapaswa ____________________

______________________________________________

d. Tunapaswa tukazie macho yetu kwenye vilele bora zaidi, kwa ku __________

______________________________________________

______________________________________________

e. Mara tunapoweka mashauri ya Mungu kama lengo letu kuu kabisa, tutatambua

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

3. Ili kuinuka dhidi ya hali ya ukengeukaji na mmomonyoko wa maadili ya jamii, tunahitaji kukuza maadili na njema za kimbingu. Hapa chini kuna orodha ya baadhi ya hali zilizomo katika jamii. Kwa kila mojawapo, chagua sifa moja au zaidi ya zifuatazo ambazo zinaelekea kupingana nayo moja kwa moja:

ubikira, utii kwa sheria za Mungu, upendo ukumbatiao vyote,
ukweli, kujitenga, unyoofu wa tabia, uelewa, haki, unyenyekevu

Ukandamizaji: ____________________________________

Uyakinifu: ____________________________________

Utovu wa sheria: ____________________________________

Ulegevu wa maadili: ______________________________

Ufisadi: ______________________________

Ubaguzi: ______________________________

Kiburi: ______________________________

Chuki: ______________________________

Ufuatiliaji wa starehe potofu: ______________________________

4. Ni ipi baadhi ya mielekeo na tabia zinazotulinda dhidi ya mwenendo wa kipuuzi? ___

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

5. Safu ya kwanza hapa chini inatoa mifano michache ya ubora linganifu na ya pili mifano michache ya ubora wa kweli. Oanisha mifano ya ubora linganifu na ile ya ubora wa kweli.

_____ Kusoma sana ili tuweze kuwapita wengine darasani mwetu

_____ Kuchangia kwenye mfuko kiasi cha fedha kilichobakia baada ya kulipia gharama za matumizi yetu ya kila mwezi na kutenga kiasi kwa ajili ya burudani

_____ Kuwatendea watu wa mbari na matabaka mengine kwa uvumilivu

_____ Kuepuka kufanya makosa kwa sababu tunafikiri tunaweza kukamatwa

_____ Kutomdhuru yeyote

a. Daima kutenda kwa unyoofu wa mwenendo, katika hali zote

b. Kujitahidi kuelewa kikamilifu mada tunazosoma darasani

c. Kuwa na upendo unaofurikka na heshima kwa wanadamu wote

d. Kuendeleza kwa bidii usitawi wa wanadamu wenzetu

e. Kutoa kwenye Mfuko kwa ukarimu na dhabihu

6. Jadili maswali yafuatayo na washiriki wa kikundi chako:

a. Kwa nini hatupaswi kuridhika na "ulinganifu wa utofauti na ubora"?

b. Kiwango chetu cha ubora kinapaswa kiwaje?

c. Baadhi ya watu hudhani kwamba ushindani ndio njia pekee ya kufikita ubora. Katika Maneno Yaliyofichwa, Bahá'u'lláh hutuambia: "Mzembe kabisa kati ya watu wote ni yule ambaye hubishana bure na kutafuta kujikweza mbele ya ndugu yake." Unadhani ubora unaweza kupatikanaje, kama si kwa kupitia ushimdani?

d. Kufuatilia ubora huhitaji kwamba tujitahidi kutukuza uwezo wetu kwa ukamilifu kabisa. Je, tunaweza kudiriki kusema kwamba tumefikia lengo la "kuwa mfano wa maadili na njema za kimbingu"?

## SEHEMU YA 4

Moyo wa mwanadamu uliumbwa kupenda. Ni hulka yake kujifungamanisha na kitu fulani. Usipojiambatanisha na vitu vya kidunia, na kuweza kuakisi mwanga wa Mungu, unapaswa ujifungananishe Naye. Kuna njia nyingi za kuonesha upendo. Tunapenda familia zetu, marafiki zetu, jumuiya yetu na nchi yetu. Walakini, aina zote hizi za upendo zina mipaka. Upendo pekee usio na mipaka ni upendo wa Mungu. Upendo Wake ni ule ukumbatiao vyote. Pale mioyo yetu inapokuwa safi na kuakisi upendo Wake, tunaonesha upendo usio na mipaka na usio na ubinafsi kwa mbari nzima ya wanadamu. Vinginevyo upendo wetu kwa wengine umeangaziwa na upendo wa Mungu usio na mipaka, unaweza kuwa na tabia zisizofaa, kama vile wivu, ubabe na ubaguzi.

Kuna sifa moja muhimu sana ya upendo ambayo sote sharti tuielewe. Upendo daima huambatana na hofu. Hii haimaanishi kwamba tunawaogopa wale tunaowapenda. Kile tunachohofia ni ama kuwapoteza wapendwa wetu au kupoteza upendo wao. Hivyo, pamoja na upendo wa Mungu, sharti pia tuwe na kicho cha Mungu ndani ya mioyo yetu—hofu kwamba vitendo vyetu, makosa yetu, vitauzuia upendo wa Mungu kutufikia. Hii haimaanishi kusema kwamba vitendo vyetu vitamzuia Mungu kutupenda, kwa kuwa upendo Wake hauna kikomo na hauachi kamwe kuwanyeshea wanadamu. Lakini mambo tuyaifanyayo yanaweza kuwa kama vikwazo ambavyo haviwezi kuruhusu upendo Wake kutufikia. Bahá'u'lláh husema katika Maneno Yaliyofichwa:

> **"Ewe Mwana wa Kuwa! Unipende ili Nami nipate kukupenda. Kama hunipendi, upendo Wangu kwa vyovyote hauwezi kukufikia pia. Elewa hili, Ewe mtumishi."**[5]

Ukuzaji wa sifa za kiroho utategemea kabisa juu ya yote mawili upendo wa Mungu na kicho cha Mungu. Vifungu vingi kutoka katika Maandiko huweka wazi uelewa wetu wa nguvu hizi mbili muhimu za maisha yetu ya kiroho. 'Abdu'l-Bahá husema:

> **"Kwa kuwa upendo wa Mungu na mvuto wa kiroho husafisha na kutakasa moyo wa mwanadamu na kuuvika na kuupamba kwa vazi la utakatifu lisilo na doa; na pindi moyo utakapoambatana kabisa na Bwana, na kujifungamanisha kabisa kwa Mkamilifu Aliyebarikiwa, ndipo neema ya Mungu itakapofunuliwa.**

> **"Upendo huu siyo wa mwili bali hasa ni wa roho. Na zile roho ambazo uwepo wao wa ndani umewashwa kwa upendo wa Mungu ni kama vile miale itawanyikayo ya mwanga, na zitang'aa mithili ya nyota za utakatifu katika mbingu safi na angavu kabisa. Kwa kuwa upendo wa kweli, upendo halisi, ni upendo kwa Mungu, na huu ni umetakasika kupita dhana na mawazo ya wanadamu."**[6]

Bahá'u'lláh husema:

> **"Yule atafutaye kuwa msaidizi wa Mungu katika Siku hii, mwache afumbe macho yake kwa chochote anachomiliki, na ayafumbue kwa mambo ya Mungu. Hebu**

**aache kujishughulisha na kile kinachomnufaisha, na ajishughulishe mwenyewe na kile ambacho kitalitukuza jina lishurutishalo vyote la Mwenyezi. Sharti autakase moyo wake kutokana na hisia zote ovu na tamaa potofu, kwa kuwa kicho cha Mungu ndio silaha inayoweza kumfanya mshindi, chombo cha msingi ambacho kwacho yeye anaweza kutimiza kusudi lake. Kicho cha Mungu ni ngao inayoilinda Hoja Yake, kikingio kinachowawezesha watu wake kufikia ushindi. Ni beramu ambayo hakuna mtu awezaye kuishusha, nguvu ambayo hakuna mamlaka inayoweza kuishinda. Kwa msaada wake, na kwa idhini ya Yule Ambaye ni Bwana wa Majeshi, wale ambao wamemkaribia Mungu wameweza kuzitiisha na kuzishinda ngome za mioyo ya watu.”**[7]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

a. Tusipo _________ Mungu, upendo wake kwa vyovyote hauwezi ____________ .

b. Upendo wa Mungu na mvuto wa kiroho _____________ na _____________ roho ya mwanadamu.

c. Pindi moyo wa mwanadamu utakapo _______________ kabisa na Bwana, na ___________ kwa Mkamilifu Aliyebarikiwa, ndipo ___________ Mungu itakapofunuliwa.

d. Upendo huu siyo __________ bali hasa ___________ .

e. Zile roho ambazo uwepo wake wa ndani _________ kwa upendo wa Mungu ni kama vile miale itawanyikayo ya _____________ .

f. Zile roho ambazo uwepo wake wa ndani umewashwa kwa upendo wa Mungu ___________________ kama vile __________ za ___________________ katika mbingu safi na angavu kabisa.

g. Kwa kuwa upendo wa ____________ , upendo ____________ , ni upendo kwa ____________ , na huu umetakasika kupita _____________ na _______________ ya wanadamu.

2. Jibu maswali yafuatayo:

a. Kitu gani husafisha na kutakasa moyo wa mwanadamu? ____________________
_____________________________________________________________________

b. Je, ni sharti gani ambalo moyo unapaswa kulitimiza ili uweze kuvutia neema ya Mungu? ____________________________________________________________
_____________________________________________________________________

c. Je, upendo wa Mungu ni hali ya kimwili au ya kiroho? _____________________

d. Tunakuwaje pale ambapo roho zetu zinapoangaziwa kwa upendo wa Mungu? ___

______________________________________________

e. Upendo wa kweli ni nini? ______________________________

3. Jadili swali lifuatalo pamoja na washiriki wa kikundi chako: Jinsi gani wale ambao uwepo wao wa ndani umeangaziwa kwa upendo wa Mungu, ambao hung'aa mithili ya nyota za utakatifu katika mbingu safi na angavu kabisa., wanavyowaathiri watu wanaowazunguka?

4. Udhihirisho wote wa upendo una mipaka isipokuwa kama umeangazIwa kwa upendo wa Mungu usio na mipaka, ukumbatiao vyote. Kwa kutumia maneno yaliyoorodheshwa hapa chini, andika sentensi zinazoelezea wazo hili. Mifano michache imetolewa kukusaidia.

| | |
|---|---|
| Shangwe | Upendo wa Mungu huleta shangwe katika mioyo yetu. |
| Uhuru | Chanzo cha uhuru wetu wa kweli ni upendo wa Mungu na kujifungamanisha Naye. |
| Uroho | Upendo wa vitu vya kiulimwengu unaweza kusababisha uroho. |
| Wivu | Kama upendo kwa marafiki zetu haukuangaziwa kwa upendo wa Mungu, unaweza kusababisha wivu. |
| Mwanga | ______________________ |
| Huzuni | ______________________ |
| Kukata tamaa | ______________________ |
| Uhai | ______________________ |
| Matamanio | ______________________ |
| Shauku | ______________________ |
| Neema | ______________________ |
| Udhanifu | ______________________ |
| Ubabe | ______________________ |
| Kicho | ______________________ |
| Huruma | ______________________ |
| Rehema | ______________________ |
| Utakatifu | ______________________ |
| Ubaguzi | ______________________ |
| Haki | ______________________ |
| Ujuzi | ______________________ |
| Ujasiri | ______________________ |

5. Kamilisha sentensi zifuatazo:

a. Kicho cha Mungu ________________ inayoweza kutufanya washindi pale tunapochagua kuwa wasaidizi wa Mungu katika Siku hii.

b. Kicho cha Mungu ni ________________________________ ambacho kwacho tunaweza kufikia kusudi letu.

c. Kicho cha Mungu ni ________________ inayoilinda Hoja Yake.

d. Kicho cha Mungu ni ________________ kinachowawezesha watu Wake kufikia ushindi.

e. Kicho cha Mungu ni ______________________ ambayo hakuna awezaye kuishusha.

f. Kicho cha Mungu ni _______________ hakuna mamlaka inayoweza kuishinda.

g. Kicho cha Mungu huwasaidia wale waliomkaribia Yeye ____________ na __________________________________ za mioyo ya watu wa ulimwengu.

6. Jadili maswali yafuatayo pamoja na kikundi chako:

a. Kwa nini upendo wa Mungu ni muhimu katika ukuzaji wa sifa za kiroho?

b. Kwa nini kicho cha Mungu ni muhimu katika ukuzaji wa sifa za kiroho?

7. Pengine ungependa kukariri nukuu ifuatayo:

> **"Mtafutaji, anapokuwa amezama katika bahari ya upendo wa Mungu, ataguswa na matamanio makubwa na atainuka kutekeleza sheria za Mungu."[8]**

## SEHEMU YA 5

Upendo kwa Mungu ndiyo nguvu ihamasishayo ambayo hutusukuma kutembea njia ya huduma kwa Hoja Yake. Kila hatua tunayoichukua katika njia hii huongeza upendo wetu Kwake. Na kwa kila hatua, vioo vya mioyo yetu hung'arishwa zaidi na tunakuza zaidi sifa zetu za kiroho. Kile kinachoangazia fikra zetu, kuongoza vitendo vyetu kwenye njia hii, ni Sheria ya Mungu. Vinginevyo tusipotii sheria Zake, tutajikuta wenyewe gizani na kupotea njia. Katika Kitáb-i-Aqdas, Bahá'u'lláh husema hivi kuhusu wajibu wetu pacha, kumtambua Mdhirishaji wa Mungu na kufuata amri Zake:

> **"Wajibu wa kwanza ulioamriwa na Mungu kwa watumishi wake ni utambuzi wa Yule Ambaye ndiye Chimbuko la Ufunuo Wake na Chemchemi ya Sheria Zake, Ambaye huwakilisha Uungu katika vyote viwili; Ufalme wa Hoja Yake na ulimwengu wa muumbo. Yeyote atimizaye wajibu huu amefikia mema yote; na yeyote aliyenyimwa hilo amekengeuka, japokuwa awe mwanzilishi wa kila tendo**

**jema. Inampasa kila mmoja afikiaye daraja hili adhimu kabisa, kilele hiki cha utukufu wa juu kabisa, kuzingatia kila agizo la Yule ambaye ndiye Haja ya ulimwengu. Wajibu huu pacha hautenganishiki. Mmoja haukubaliki bila ule mwingine. Hivyo ndivyo ambavyo imeagizwa na Yule Ambaye ndiye Chanzo cha uvuvio Mtakatifu."**[9]

Kuhusiana na sheria za Mungu, Bahá'u'lláh hutuambia:

**"Ee enyi watu wa ulimwengu! Mjue kwa hakika kwamba amri Zangu ni taa za majaliwa Yangu ya upendo miongoni mwa watumishi Wangu, na funguo za rehema Yangu kwa viumbe Vyangu."**[10]

Katika mojawapo ya Nyaraka Zake, Yeye husema:

**"Kwa hakika, sheria za Mungu zinafananishwa na bahari na watoto wa watu ni kama samaki, laiti wangelijua hilo."**[11]

Bahá'u'lláh zaidi hutangaza:

**"Kwa hakika, sheria Zake hufanyiza ngome imara kabisa kwa ajili ya ulinzi wa ulimwengu na usalama wa watu wake—mwanga juu ya wale ambao hukiri na kutambua ukweli, na moto kwa wale ambao hugeukia mbali na kukana."**[12]

**"Sema: Kwa Mungu! Sheria Yake ni ngome kwenu, laiti mngelielewa."**[13]

Kurejelea kwenye Kitáb-i-Aqdas, ambacho kina sheria na amri za Kipindi Chake Kitakatifu, Yeye hutuonya:

**"Sema: Kishikilieni hicho, enyi watu, na kitiini kile ambacho kimetelemshwa ndani mwake juu ya mafundisho ya ajabu ya Bwana wenu, Msamehevu, Mwenye Baraka tele. Kwa kweli kitawasitawisha katika ulimwengu huu na katika ule ujao na kitawaondolea chochote kile chenye madhara kwenu."**[14]

Na katika mojawapo ya Maandiko Yake, tunasoma:

**"Sheria za Mungu zimetelemshwa kwenu kutoka katika mbingu ya Ufunuo Wake bora kabisa. Wote sharti wazitii kwa dhati kabisa. Heshima kuu kabisa ya mtu, maendeleo yake ya kweli, ushindi wake wa mwisho, daima umetegemea, na utaendelea kutegemea, juu yake. Yeyote afuataye amri ya Mungu atafikia furaha ya milele."**[15]

1. Nukuu za hapo juu humaanisha kwamba:

   ______ Wajibu wetu wa kwanza ni kumtambua Mdhihirishaji wa Mungu.

   ______ Baada ya kumtambua Yeye, wajibu wetu unaofuata ni kumtii.

   ______ Umtambuzi wa Mdhihirishaji wa Mungu ni muhimu zaidi kuliko utii kwa sheria Zake.

   ______ Utii kwa sheria ni muhimu zaidi kuliko utambuzi wa Mdhihirishaji wa Mungu.

______ Utambuzi wa Mdhihirishaji wa Mungu na utii kwa sheria Zake una umuhimu sawa; mmoja haukubaliki bila mwingine.

______ Mungu ametupa sheria kwa sababu anatupenda.

______ Mungu ametupa sheria ili tumuogope.

______ Tunapaswa tutii sheria za Mungu kutokana na kuogopa adhabu.

______ Tunapaswa kutii sheria za Mungu kwa sababu tunampenda.

______ Tunapaswa tutii sheria za Mungu ili kuvutia rehema Zake.

______ Mungu huwapenda tu wale wanaomtii Yeye.

______ Wale wanaomtii Mungu hufungua mioyo yao kupokea upendo Wake.

______ Hatuwezi kuishi nje ya bahari ya sheria za Mungu.

2. Katika nukuu za hapo juu, sheria za Mungu zinaelezwa kama

– _______________ za majaliwa ya upendo wa Mungu.

– funguo za _______________ za Mungu.

– _______________ ambamo wanadamu wote wamezamishwa.

– ngome imara kabisa kwa ajili ya _______________ na _______________ wa watu wa ulimwengu.

– _______________ juu ya wale wanaokiri na kutambua ukweli na _______________ kwa wale wanaogeukia mbali na kuukana.

– _______________ kwetu.

3. Sasa orodhesha hapa chini, baada ya mifano miwili iliyotolewa, baadhi ya sheria na amri za Mungu. Jinsi gani kutazama kila moja kwa mujibu wa vifungu vya maneno vya hapo juu huongeza uelewa wetu juu ya maana zake katika maisha yetu na ufaaji wa jitihada zetu katika njia ya hudumai?

Kusoma na kutafakari juu ya Neno la Mungu kila asubuhi na jioni

Kutongoa sala ya faradhi kila siku

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

4. Humaanisha nini kuwa mtumishi mtiifu wa Mungu?

_____ Daima kushuku busara ya kile ambacho Mungu amekiamuru

_____ Daima kupinga dhidi ya au kupuuzia maamuzi ya asasi za Kibahá'í

_____ Kuwafuata kwa upofu watumishi wengine wa Mungu

_____ Kuchunguza ukweli kwa madhumuni ya kuukubali na kuuishi

_____ Kutembea katika njia ya Mungu kwa hatua thabiti

_____ Kujitahidi kupatanisha fikra na matendo yetu na mafundisho ya Mungu

_____ Kushikilia kwa furaha Sheria za Mungu na kulitukuza Neno Lake

_____ Kuwa thabiti katika uaminifu wetu kwa sheria za Mungu, bila kujali hali yoyote iwayo

_____ Kutofikiria sana madhaifu na mapungufu yetu, tukiweka imani na matumaini yetu yote katika neema na fadhili za Mungu

5. Kariri aya ifuatayo kutoka Kitáb-i-Aqdas, kama bado hujafanya hivyo katika nafasi za hapo awali:

**"Ulimi wa uwezo Wangu, kutoka mbingu ya utukufu Wangu wenye nguvu kabisa, umeuambia muumbo Wangu maneno haya: 'Tiini amri Zangu kwa ajili ya upendo wa uzuri Wangu.'"**[16]

## SEHEMU YA 6

Utambuzi wa Mdhihirishaji wa Mungu hufumbua macho yetu. Tunaanza kujua kile kinachochangia uinuliwaji wetu na kile ambacho husababisha utwezo wetu. Kadiri tujifunzavyo Ufunuo ulioletwa kwetu na Mdhihirishaji, tunakuja kutambua kusudi la Mungu kwa wanadamu. Katika kila kitu tunaona ishara ya ukuu Wake na hekima Yake isiyofahamika. Ujuzi tunaoupata kupitia Mdhihirishaji wa Mungu na upendo tunaouhisi kumuelekea Yeye hutupa uhakika. Mioyo yetu haiyumbi wala kutetemeka tena.

Kadiri tutembeavyo kwa unyenyekevu njia ya huduma, tunakua kiimani na kiyakini. Na kadiri kipimo cha imani yetu kinavyoongezeka, ndivyo uwezo wetu wa kupokea baraka za Mungu na kukuza sifa zetu za kiroho unavyokua kwa ulingano. Tunageuzia macho yetu kuelekea Jua la Ukweli na daima kupokea mwangaza. Hivyo, ni kwamba kila kitendo katika njia hii hufanywa kwa utambuzi—utambuzi wa Mungu, wa Ufunuo Wake, na wa kusudi Lake kwa wanadamu. Hiki ndicho imani humaanisha. 'Abdu'l-Bahá husema:

**"Hata vipendeze na vikubalikeje vitendo vya mtu mwadilifu mbele ya Kizingiti Kitakatifu cha Mungu, bado matendo hayo sharti yatokane na utambuzi. Hata kama kazi ya mikono ya mtu asiyeona iwe nzuri na ya kupendeza namna gani, bado yeye mwenyewe amenyimwa kuiona. Ni kwa sulubu jinsi gani baadhi ya wanyama hufanya kazi kwa niaba ya mwanadamu, ni mizigo mizito jinsi gani hubeba kwa ajili yake, kwa kiasi kikubwa jinsi gani wao huchangia kwa ajili ya raha na starehe yake; na bado, kwa sababu hawatambui, hawapati fidia ya**

**maumivu yao yote. Mawingu hunyesha baraka zake, yakikuza mimea na maua, na yakileta ubichi na uzuri nyikani na mbugani, misituni na bustanini; hata hivyo, kwa kuwa hayana utambuzi wa matokeo na matunda ya mmiminiko wake, hayapati sifa wala heshima yoyote, wala kupata shukrani na ridhaa ya mtu yeyote. Taa hutoa mwanga, lakini kwa kuwa haina utambuzi wa kufanya hivyo, hakuna yeyote anayedaiwa nayo. Mbali na hili, mtu mwadilifu na mwenye mwenendo mzuri kwa hakika atageukia kuuelekea Mwanga, popote pale auonapo. Maana ni hii, kwamba imani hujumuisha vyote viwili utambuzi na utendaji wa amali njema."**[17]

Bahá'u'lláh hutusihi:

**"Sema: Enyi watu! Msijinyime wenyewe neema ya Mungu na rehema Yake....Yeye ndiye aliyefunua hazina za ujuzi Wake mbele ya macho yenu, na kuwawezesha kupaa hadi kwenye mbingu ya yakini—yakini ya Imani Yake isiyozuilika, isiyokanushika na iliyotukuka kabisa."**[18]

**"Jivikeni wenyewe enyi watu, kwa vazi la yakini, ili liweze kuwalinda kutoka mishale ya mawazo ya bure na fikra potofu na ili muweze kuhesabika miongoni mwa wale waaminifu katika siku hizi—siku ambamo hakuna yeyote anayeweza kufikia yakini wala kupata uthabiti katika Hoja ya Mungu isipokuwa kwa kukikana kile ambacho ni cha kawaida miongoni mwa watu na kwa kugeukia kumuelekea Uzuri huu mtakatifu na ung'aao."**[19]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo kwa mujibu wa nukuu ya kwanza hapo juu:

    a. Kazi ya mikono ya mtu asiyeona inaweza kuwa nzuri na ya kupendeza, lakini ___

    ______________________________________________________________

    b. Baadhi ya wanyama hufanya kazi ya sulubu kwa niaba ya mwanadamu, hubeba mizigo mizito na kuchangia kwa ajili ya raha na starehe yake, na bado ________

    ______________________________________________________________

    c. Mawingu hunyesha baraka zake, yakikuza mimea na maua, na yakileta ubichi na uzuri nyikani na mbugani, misituni na bustanini; lakini ______________________

    ______________________________________________________________

    ______________________________________________________________

    ______________________________________________________________

    d. Taa hutoa mwanga, lakini ______________________________________________

    ______________________________________________________________

    e. Mtu hufanya matendo maadilifu, lakini matendo yake sharti yatokane na _______

2. Sasa, rejelea kwenye nukuu mbili zinazofuatia, kamilisha sentensi zifuatazo:

    a. Hatupaswi kujinyima wenyewe ______________________________ .

b. Mungu amefunua mbele ya macho yetu ________________________________ na kutuwezesha ________________________________________________ yakini—yakini Yake ____________________ , ___________________ , na ______________________________ .

c. Tunapaswa ____________ wenyewe kwa vazi la _______________ , ili liweze ________________ kutoka kwa mishale ya ________________________ na _________________________ .

d. Hizi ni siku ambamo hakuna yeyote anayeweza kufikia ______________ wala kupata __________ katika Hoja ya Mungu isipokuwa kwa ________________ kile ambacho ni cha kawaida miongoni mwa watu na kwa ___________________ Uzuri huu mtakatifu na ung'aao.

3. Kwa kila neno hapa chini, andika sentensi ambayo hujumuisha neno "imani". Mfano umetolewa ili kuwasaidia.

| | |
|---|---|
| Isiyoyumba | Imani yake katika Agano iilikuwa kama mlima; ilikuwa haiyumbi. |
| Isiyopingwa | ____________________ |
| Uhai | ____________________ |
| Imara | ____________________ |
| Ongezeka | ____________________ |
| Iliyoamshwa hivi karibuni | ____________________ |
| Kweli | ____________________ |
| Thabiti | ____________________ |
| Pasi na shaka | ____________________ |
| Halisi | ____________________ |
| Isiyotikisika | ____________________ |

4. Amua kama kauli zifuatazo ni kweli:

_____ Chanzo cha imani ni kumjua Mungu na utambuzi wa Mdhihirishaji Wake.

_____ Kumwamini Bahá'u'lláh humaanisha kutii amri Zake.

_____ Kama mtu anamwamini Mdhihirishaji wa Mungu, mtu huyo daima atatii amri Zake.

_____ Kuwa na imani humaanisha kamwe kutouliza maswali.

_____ Imani huongezeka kadri utambuzi wa mtu juu ya Mungu unavyoongezeka.

_____ Imani huongezeka kadiri mtu anavyotenda kufuatana na mafundisho ya Mdhihirishaji wa Mungu.

______ Kuwa mwenye imani isiyoyumba ni sawa na kuwa mwenye kushupaa.

______ Imani siyo kitu ambacho mtu anaweza kupoteza.

______ Ikiwa tuna imani, kamwe hatutakuwa na shaka juu ya uelewa wetu wa mafundisho.

______ Ikiwa tuna imani, kamwe hatutakuwa na shaka juu ya ukweli wa mafundisho ya Mdhihirishaji wa Mungu.

______ Kuufahamu ukweli wa Ufunuo na kusita kuufanyia kazi, huonesha udhaifu wa imani.

______ Kwa kawaida tunapitia hatua za shaka hadi kufikia hali ya yakini.

______ Kadiri tukuavyo katika imani, ndivyo tunavyoweza kuachana na mawazo ya bure na fikra potofu.

______ Ili kufikia hali ya yakini katika ukweli wa Ufunuo wa Mungu huhitaji imani.

5. Andika baadhi ya mambo ambayo unauhakika nayo. Mifano miwili imetolewa ili kukusaidia.

a. Nina uhakika kwamba Utaratibu wa Ulimwengu wa Bahá'u'lláh utasimamishwa.

b. Nina uhakika kwamba Imani itashinda vikwazo vyovyote katika njia yake na kutimiza kusudi lake la juu.

c. ______________________________
______________________________

d. ______________________________
______________________________

e. ______________________________
______________________________

f. ______________________________
______________________________

6. Jadili yafuatayo pamoja na kikundi chako:

a. Kama una yaamini mafundisho ya Bahá'u'lláh, lakini katika hali ngumu na chini ya shinikizo la hali ya juu, unamua kwamba haikusaidii kutenda kufuatana na kanuni ya ukweli, je, unashuku nini?

b. Je, kupata utambuzi pekee kunatosha kuimarisha imani yetu? Namna gani utambuzi na vitendo kwa pamoja hutusaidia kuondokana na shaka na kupata uhakika?

c. Je, tunaweza kufikia imani na yakini bila maombi ya bidii ya hali ya juu kabisa kwa Mwenyezi na mmiminiko wa neema Yake?

## SEHEMU YA 7

Imani ni msingi ambao juu yake tunajenga uwepo wetu wa kiroho. Tunaamini katika ukweli wa Ufunuo wa Mungu na hatusiti kutenda kufuatana na sheria na maonyo Yake. Tu thabiti katika upendo wetu kwa Mungu na Mdhihirishaji Wake. Tuna hakika kwamba Mapenzi ya Mungu yatatimizwa na kuyasalimisha mapenzi yetu wenyewe Kwake. Walakini, utambuzi wetu wa muumbo wa kiroho na kimwili wa Mungu ni wenye mipaka, na kamwe hatujui kitakachotokea kutoka siku moja hadi nyingine. Hivyo, kwa mioyo iliyojaa matumaini, daima tunatarajia mmiminiko wa fadhili za Mungu juu yetu. Tunaamini katika rehema ya Mungu na daima tu wenye matumaini ya kupokea baraka Zake. 'Abdu'l-Bahá husema:

> **"Kamwe usipoteze imani yako katika Mungu. Daima uwe mtumainifu, kwa kuwa fadhili za Mungu kamwe hazikomi kumiminika juu ya mtu. . . . Mtu katika hali zote amezamishwa katika bahari ya baraka za Mungu. Kwa hiyo, usikate tamaa katika hali yoyote ile, bali zaidi uwe thabiti katika tumaini lako."[20]**

> **"Ikiwa moyo wako utageukia mbali na baraka ambazo Mungu hutoa unaweza kutumaini kupata furaha? Kama hauweki matumaini na imani yake katika rehema za Mungu, wapi utapata pumziko? Aah, mwamini Mungu! Kwani fadhili Zake ni za milele, na Baraka Zake, kwa sababu ni nzuri sana. Aah! Weka imani yako kwa Mwenyezi, kwa kuwa Yeye hashindwi na wema Wake hudumu daima! Jua lake hutoa Mwangaza wakati wote, na mawingu ya Rehema Yake yamejaa Maji ya Huruma ambayo kwayo Yeye humwagilia mioyo ya wote wanaomwamini. Upepo Wake mwanana uburudishao daima hubeba uponyaji katika mabawa yake kwa roho zenye kiu za watu!"[21]**

Na kuhusu chanzo cha tumaini letu, Yeye husema:

> **"Habari njema za furaha za Ufunuo zilitangazwa, na moto uwakao wa Kichaka Kiwakacho uliwaka kwa wangavu. Mawimbi ya bahari ya umoja, kama vile majeshi ya uongozi, yalipiga juu ya fuko za utengano na kutawanya lulu za thamani za umoja na upatano kila mahali. Majira matakatifu ya machipuo yaliizingira dunia, maua ya mbinguni yalichanua, mvua za vuli zilinyesha, na pepo zijaliazo uhai zilivuma kila upande, hadi mwishowe wote walijazwa na tumaini kwamba uzuri wa Umoja ungefunuliwa katika mkusanyiko wa ulimwengu, na kwamba wangavu wa wajihi wake ungeng'aa kwa wangavu katika maeneo yote."[22]**

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. Tunapaswa tuwe watumainifu, kwa kuwa ______________ za Mungu kamwe hazita ___________ kumiminika juu ya wanadamu.

   b. Hatupaswi kukata tamaa katika hali yoyote ile, bali tuwe __________ katika ____________ letu.

   c. Hatupaswi _________________ kaiika hali yoyote ile, bali tuwe thabiti katika tumaini letu.

d. Mawingu ya __________ ya Mungu yamejaa Maji ya ___________________ .

e. Kwa Maji ya ____________________ , Mungu humwagilia ______________ ya wote ambao _____________ Yeye.

2. Amua kama kauli zifuatazo ni za kweli:

_____ Kumtumaini Mungu ni chanzo kisichoshindwa cha tumaini.

_____ Chanzo halisi cha tumaini ni mtu kuamini katika uwezo wake.

_____ Tumaini huchipuka kutokana na imani katika rehema ya Mungu ikumbatiayo vyote.

_____ Imani katika ukweli wa mafundisho ya Mdhirishaji wa Mungu ni chanzo kisicho na kikomo cha tumaini.

_____ Vyanzo vikubwa kabisa vya tumaini ni umiliki wa mali za kimwili na kuwa na uhusiano na watu wenye mamlaka.

_____ Ni wasiojua tu ndio watumainifu. Mwerevu ana sababu ya kushuku kila kitu.

_____ Tumaini huchipuka tu kutoka kwenye mioyo ya wapumbavu.

_____ Daima tunabakia watumainifu pale tunaporidhika na Mapenzi ya Mungu katika hali zote.

_____ Daima tunabakia watumainifu pale tunapokuwa na imani kamili kwamba fadhili za Mungu zitanyesha bila kukoma juu ya yetu.

_____ Kamwe hatutapoteza tumaini ikiwa tutakuwa na imani kwamba Utaratibu wa Ulimwengu wa Bahá'u'lláh hatimaye utasimamishwa.

3. Utumainifu humaanisha kwamba pale tunapotamani kukuza sifa za kiroho,

_____ tuna hakika kwamba tutafanikiwa kufanya hivyo, bila kujali ni juhudi kiasi gani tunafanya.

_____ tunahitaji kujikumbusha mara kwa mara kwamba pengine hatutafanikiwa kufanya hivyo.

_____ hatuhitaji kufanya jiuhudi yoyote.

_____ tunahitaji tu kuamini katika uwezo wetu wenyewe wa kufanya hivyo, kwa kuwa hicho ndicho kigezo kikubwa kitakachoamua mafanikio yetu.

_____ tuna hakika kwamba, ikiwa tutafanya jitihada ya dhati, tutafanikiwa kupitia baraka na neema za Mungu.

4. Ni zipi miongoni mwa sentensi zifuatazo husemwa na mtu mwenye matumaini?

_____ Mimi sifai, na hakuna maana ya kujaribu kubadilika.

_____ Licha ya kujua kwamba nina mapungufu, daima najaribu kufanya kadiri niwezavyo.

_____ Katika wakati mgumu kabisa wa maisha yangu, ninasali nipate msaada mtakatifu na nina imani kwamba nitasaidiwa kufuatana na Mapenzi ya Mungu.

_____ Asili ya chini ya mwanadamu daima huishinda asili ya juu, na kamwe sitaiona siku ambapo watu watatenda kwa ubora.

_____ Ninaamini katika ubora wa kila mwanadamu ambao hutuwezesha kuendelea kuwa tuliojifunga kwa huduma.

_____ Baadhi ya watoto katika darasa langu hukosa adabu, lakini najua kwamba nikiwasaidia kwa uvumilivu wataendelea.

_____ Nguvu hasi za kijamii zinazofanya kazi kwa vijana chipukizi zina nguvu mno kiasi kwamba haisaidii kuwasaidia kuzuia athari zake.

_____ Licha ya nguvu zinazohamasisha utepetevu kwa vijana chipukizi, wengi wao, kwa malezi sahihi na endelevu, wataweza kujifunza kuushinda ushawishi wake na kujitoa wenyewe kuitumikia jumuiya.

_____ Vikwazo tunavyokabiliana navyo katika njia ya huduma aghalabu vinaweza kugeuzwa kuwa ngazi kwa ajili ya maendeleo.

_____ Jumuiya yetu inapitia wakati mgumu, lakini nina hakika kwamba tutaweza kuyashinda matatizo yoyote na kuendelea kusonga mbele kwa kutumia nguvu zilizomo ndani ya Hoja.

_____ Kuna utengano mkubwa mno katika jamii kiasi kwamba jumuiya hazitaweza kupata umoja.

_____ Ingawa mara nyingi huonekana kuwa ni kazi ngumu sana, tunaweza kuchota kutoka kwenye kanuni za kiroho kwa ajili ya kujenga umoja mkubwa zaidi.

5. Kariri sala ifuatayo:

**“Yeye ni Mwenye Huruma, Mkarimu—Kabisa! Ee Mungu, Mungu wangu! Wewe waniona, Wewe wanifahamu; Wewe ni Mahali pangu pa usalama na Kimbilio langu. Sijamtafuta yeyote wala sitamtafuta yeyote ila Wewe, hakuna njia ambayo nimeikanyaga wala yoyote nitakayoikanyaga ila njia ya upendo Wako. Katika usiku wa giza usio na matumaini, jicho langu hugeukia kwa matazamio na likijawa na matumaini kwa asubuhi ya fadhili Zako nyingi na kwenye saa za alfajiri roho yangu ififiayo huchangamshwa na kuimarishwa kwa kumbukumbu ya Uzuri na ukamilifu Wako. Yule ambaye neema ya rehema Yako humsaidia, japokuwa awe tone tu, atakuwa bahari isiyo na mwisho, na chembe ndogo kabisa ambayo mmiminiko wa wema wa upendo Wako huisaidia, itang’aa kama vile nyota angavu.**

**“Mlinde chini ya himaya Yako, Ewe Roho ya utakaso, Wewe Ambaye u Mpaji Mkarimu—Kabisa, mtumishi Wako huyu, aliyefanywa mtumwa Wako aliyewashwa. Msaidie katika ulimwengu huu wa uhai kubakia thabiti na imara katika upendo Wako na ujalie kwamba ndege huyu aliyevunjika mabawa afikie kimbilio na hifadhi katika kiota Chako kitakatifu kikaacho juu ya mti wa mbinguni.”**[23]

## SEHEMU YA 8

Mwenzi wa karibu wa tumaini ni shauku kuu. Moyo usio na shauku ya kupokea fadhili za Mungu hauna uhai. Roho isiyowaka kwa shauku ya kufika kwenye uwepo wa Mungu itaweza tu kutangatanga katika jangwa la uasi. Shauku ni mali ya moyo wa mwanadamu. Lakini lengo la shauku lazima liwe sifa za kimbingu, shangwe ya kiroho, kukubalika mbele ya Kizingiti Kitakatifu na huduma nyenyekevu kwa Hoja Yake. Kwa kuwa kama msukumo wa nafsi na tamaa huielekeza shauku kwenye ulimwengu na starehe zake, nguvu yenyewe ambayo husukuma maendeleo ya roho itakwisha. ‘Abdu’l-Bahá husema:

> **“Chemchemi ya ukarimu mtakatifu inafoka, lakini sharti tuwe na kiu ya maji ya uzima. Vinginevyo kuna kiu, maji yafaayo hayawezi kuzima kiu. Vinginevyo roho ina njaa, vyakula vitamu vya meza ya mbinguni havitatupa riziki. Vinginevyo macho yaonayo hufumbuliwa, mwanga wa jua hautashuhudiwa. Hadi hapo tundu za pua zitakaposafishwa, manukato ya bustani takatifu ya mawaridi hayatavutwa. Vinginevyo moyo umejazwa na shauku, fadhili za Bwana hazitadhihirika....Kama bahari ya maji yenye afya hufura na hatuna kiu, je, kuna faida gani tunayopata? Kama mshumaa umewashwa na hatuna macho, ni furaha gani tunapata kutoka kwake? Kama nyimbo zenye lahani tamu zingeinuliwa hadi mbinguni na tumenyimwa usikivu, je, tunaweza kupata furaha gani?”**[24]

Katika barua iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi, tunasoma:

> **“Acha kutazama madhaifu yako, kwa hiyo; uwe na matumaini kamili kwa Mungu; acha moyo wako uwake kwa shauku ya kutumikia ujumbe Wake na kutangaza mwito Wake; na utaona jinsi ufasaha na nguvu ya kubadilisha mioyo ya wanadamu vitakavyokuja kwa namna ya kawaida.”**[25]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. Chemchemi ya ukarimu mtakatifu _________________ , lakini lazima tuwe na _______________ ya maji ya uzima.

   b. Chemchemi ya ___________________________________ inafoka, lakini sharti tuwe na kiu ya __________________________________ .

   c. Vyakula vitamu vya meza ya mbinguni havitatupa riziki vinginevyo roho zetu _________________ .

   d. _________________________________ vya meza ya mbinguni havitatupa riziki vinginevyo roho zetu zina njaa.

   e. Fadhili za Bwana zitadhihirika pale mioyo yetu itakapokuwa imejazwa na ____________ .

   f. ____________ za Bwana zita ______________ pale mioyo yetu itakapokuwa imejazwa na shauku.

g. Sharti tuache kutazama ___________________ yetu.

h. Mioyo yetu inapaswa _________ kwa _____________ ya kutumikia ujumbe Wake na kutangaza mwito Wake.

i. Mioyo yetu inapaswa iwake kwa shauku ya _______________________________ na ____________________________________ .

j. Ufasaha na nguvu ya kubadilisha mioyo ya wanadamu vitakuja kwa namna ya kawaida tutakapo ___________________________________________________ na kuacha ________________________________________________________ .

2. Kwa mujibu wa nukuu ya kwanza hapo juu, andika sentensi tano zinazoanza na neno "vinginevyo ".

a. Vinginevyo ________________________________________________________
_____________________________________________________________________

b. Vinginevyo ________________________________________________________
_____________________________________________________________________

c. Vinginevyo ________________________________________________________
_____________________________________________________________________

d. Vinginevyo ________________________________________________________
_____________________________________________________________________

e. Vinginevyo ________________________________________________________
_____________________________________________________________________

3. Amua kama kauli zifuatazo ni kweli:

_____ Shauku zote zinastahili sifa.

_____ Shauku kwa ajili ya ukamilifu wa mbinguni hustahili sifa.

_____ Ikiwa hatutamani ukamilifu wa mbinguni, hatutoufikia.

_____ Tungekuwa wenye furaha zaidi kama tusingekuwa na matamanio yoyote.

_____ Shauku ya kuleta shangwe ya kweli kwa kila moyo ni ya kustahili sifa.

_____ Mioyo yetu hujawa shangwe pale tunapokuwa tunatamani kile tu ambacho Mungu anatamani kwa ajili yetu.

_____ Matamanio ya kibinafsi daima hupinga kile ambacho Mungu hutamani kwa ajili yetu.

_____ Tunapotenda kwa mioyo iliyojawa shauku kuu ya kufundisha Hoja, tunapokea mathibitisho matakatifu.

______ Shauku kuu ni kigezo kwa ajili ya kupokea fadhili za Mungu.

______ Shauku ya kuboresha hali za kimwili za mtu inakubalika, ilimradi haiizuii shauku ya kumpendeza Mungu.

______ Daima tunapaswa tuwe waangalifu ili shauku za kiulimwengu zisitawale maisha yetu.

______ Tunapoitakasa mioyo yetu kutokana na shauku za kibinafsi, tunamkaribia zaidi Mungu.

______ Shauku ya mwisho kabisa ni kuingia kwenye uwepo wa Mungu.

4. Zipi kati ya shauku zifuatazo hazikubaliki? Kwa nini?

______ Mtu kufikia ubora katika kazi yake

______ Kuona amani inasimamishwa duniani

______ Kufundisha Hoja

______ Kuwa na familia yenye furaha

______ Kukua katika imani na yakini

______ Kubakia thabiti katika Agano

______ Kuitumikia Hoja na jamii ya wanadamu bila ubinafsi

______ Kujulikana kwa ajili ya huduma kwa Hoja na jamii ya wanadamu

______ Kukuza sifa za kiroho

______ Kufanya kazi kwa ajili ya furaha ya wengine

______ Kuchaguliwa katika Baraza la Mahali

______ Kushuhudia maendeleo ya Hoja

______ Kupata hadhi ya juu katika jamii

______ Kutumia madaraka yako juu ya wengine

______ Kushuhudia maendeleo ya wengine

______ Kuendeleza raghba binafsi

______ Kuendeleza bila ubinafsi maslahi bora kabisa ya Imani

5. Jadili pamoja na washiriki wengine katika kikundi chako kauli mbili zifuatazo:

a. Kutaamuli juu ya maisha baada ya kifo hutusaidia kupata kiu ya mambo ya kiroho.

b. Shauku ya mwisho kabisa ni shauku ya kuteketeza kabisa utando wa nafsi na kuingia katika uwepo Mungu.

## SEHEMU YA 9

Ujuzi, imani na yakini, tumaini na shauku kuu ni vya lazima kwa wale watembeao njia ya huduma. Lakini havitoshi; Lazima tuimarishe dhamira ya kutenda na wakati wote tufanye juhudi, ikiwa tunataka kupiga hatua za maana katika njia hii na kutimiza kusudi letu lenye pande mbili, la kukua kiroho na kiakili, na kuchangia kwa maendeleo ya jamii. Bahá'u'lláh husema:

> **"Kwa kila mmoja kimeagizwa kipimo kilichoamriwa tangu awali, kama ilivyoamriwa katika Nyaraka za Mungu zenye nguvu na zilindwazo. Vyote vile ambavyo kwa asili unavyo vinaweza, Walakini, kudhihirishwa tu kutokana na hiari yako mwenyewe. Matendo yako mwenyewe huthibitisha ukweli huu."**[26]

'Abdu'l-Bahá husema:

> **"Msiiendekeze miili yenu kwa mapumziko, bali fanyeni kazi kwa roho zenu zote na kwa mioyo yenu yote pazeni sauti na mwombeni Mungu awajaalie msaada na neema Yake. Hivyo ndivyo mnaweza kuufanya ulimwengu huu kuwa Paradiso ya Abhá, na tufe hili la dunia uwanja wa gwaride wa milki ya juu. Kama tu mkifanya juhudi, ni hakika kwamba miangaza hii itang'aa, mawingu haya ya rehema yatanyesha mvua yake, pepo hizi ziletazo uhai zitainuka na kuvuma, miski hii inukiayo itatawanyika kila mahali."**[27]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. Vyote vile ambavyo ______________________ tunavyo vinaweza kudhihirishwa __________ kutokana na hiari yetu wenyewe.

   b. Kila kitu ambacho kwa asili tunacho kinaweza ______________________ tu kutokana na ____________________________________ .

   c. Hatupaswi _____________ miili yetu kwa ____________ , bali tu __________ kwa ____________ zetu zote na tu __________________ kwa Mungu kwa _______________ yetu yote na _________ Yeye atujalie _________________ na _____________ Yake. Kwa jinsi hii ndipo tunaweza kulifanya tufe hili la dunia ____________________________ wa ____________ ya __________ wa ya juu.

   d. Kama tu tukifanya juhudi, ni hakika ____________________________________
   __________________________________________________________________

   e. Kama tu tukifanya juhudi, ni hakika ____________________________________
   __________________________________________________________________

   f. Kama tu tukifanya juhudi, ni hakika ____________________________________
   __________________________________________________________________

g. Kama tu tukifanya juhudi, ni hakika ____________________________________

______________________________________________________________________

2. Yapi kati ya yafuatayo humaanishwa na nukuu ya kwanza?

_____ Kwa kuwa uwezo wetu umeamriwa tangu awali na Mungu, utakuzwa bila kujali chaguzi tunazozifanya maishani mwetu.

_____ Kwa kuwa uwezo wetu umeamriwa tangu awali na Mungu, utakuzwa iwe tunafanya juhudi au la.

_____ Mungu amempa kila mmoja wetu uwezo fulani fulani, lakini utaweza kukuzwa tu kupitia utendaji wa hiari yetu wenyewe.

_____ Kupitia nguvu ya hiari yetu wenyewe, kila mmoja wetu ataweza kuyashinda mapungufu yote ya kibinadamu na kufikia hali ya ukamilifu kabisa.

_____ Haidhuru tunaweza kuendelea kwa kiasi gani kiroho, hakuna yeyote kati yetu anayeweza daima kuudhihirisha kikamilifu uwezo ambao Mungu ameuamuru tangu awali kwa ajili yetu; kwa hiyo lazima tuendelee kufanya juhudi kuukuza zaidi.

3. Jibu kila moja ya maswali yafuatayo na elezea sababu ya jibu lako:

a. Je, ukweli kwamba Mungu tayari anajua uwezo wetu wa kupata ukamilifu wa mbinguni humaanisha kwamba upatikanaji wake haumo katika uwezo wetu bali katika Wake?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

b. Je, tuna hiari ya ama kukuza uwezo wetu wa kiroho au kutokuukuza?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

c. Je, kweli kwamba tuna hiari humaanisha kwamba tunawajibika kwa Mungu kwa ajili ya chaguzi tunazozifanya maishani mwetu?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

d. Mathalani mwanafunzi hajajiandaa kwa ajili ya mitihani yake, na akafeli. Je, anaweza kusema kwamba ni bahati mbaya ndio imemfanya afeli?

e. Mathalani mwanafunzi amekuwa mwenye bidii na dhamira sana katika masomo yake na kupata alama nzuri kabisa. Je, mafanikio yake yanaweza kuhusishwa na "bahati nzuri"?

f. Ikiwa utapata vipingamizi katika kujaribu kutimiza moja kati ya malengo yako kadhaa yenye ustahiki sawa sawa, je, inamaanisha kwamba halikukusudiwa kuwepo na unapaswa kuachana nalo? Ukiendelea kufanya jitihada bila mafanikio, je, inamaanisha kwamba basi uachane nalo? Unajuaje ni wakati gani unapaswa kuacha kujaribu kutimiza lengo hili maalum na badala yake kufuatilia lingine?

g. Je, ukweli kwamba lazima tujitahidi kukuza sifa zetu za kiroho humaanisha kwamba tunaweza kufanya hivyo bila kumuomba Mungu kupata msaada Wake?

h. Je, jitihada ambayo mtu hufanya katika njia ya huduma—kwa vyote viwili kukuza uwezo wa mtu mwenyewe na kuchangia kwenye mabadiliko ya jamii—ni muhimu sawa na mafanikio yanayopatikana katika njia hiyo?

4. Kwa mujibu wa aya hapa chini, jadilini uhusiano kati ya utashi na jitihada ya mwanadamu na uwezo wa msaada mtakatifu:

**". . . kusimama au kusogea kwa mtu kwenyewe hutegemea juu ya msaada wa Mungu. Ikiwa msaada huu hushindwa kumfikia, yeye hawezi kufanya mema wala**

**maovu. Lakini pale ambapo msaada wa Bwana mwenye baraka kabisa unapojalia uhai juu ya mtu, anaweza kufanya yote mawili mema na maovu. Na laiti msaada huo ukiondolewa, mtu huyo angekuwa dhaifu kabisa. Ndio maana auni na msaada wa Mungu vimetajwa katika Maandiko Matakatifu. Hali hii inaweza kulinganishwa na ile ya merikebu ambayo husogea kwa uwezo wa upepo au mvuke. Laiti uwezo huu ungeondolewa, merikebu hiyo isingeweza kabisa kusogea. Hata hivyo, mwelekeo wowote usukani uzungukiapo, uwezo wa mvuke huisukuma merikebu hiyo kuelekea huko. Ikiwa usukani umegeuziwa mashariki, merikebu itaelekea mashariki, na kama ukielekezwa magharibi, merikebu itaelekea magharibi. Mjongeo huu hautokani na merikebu yenyewe, bali hutokana na upepo au mvuke.**

**"Vivyo hivyo, vitendo vyote vya mwanadamu vinaendelezwa kwa nguvu ya msaada mtakatifu, lakini chaguo la wema au uovu ni lake pekee."[28]**

## SEHEMU YA 10

Kadiri tutembeavyo njia ya huduma, lazima tuendelee kutambua kwa umakini kwamba ukamilifu wa mbinguni haupatikani bila dhabihu. Fumbo la dhabihu limo katika ukanaji wa vyote vinavyofungamana na milki ya nafsi ili kufikia kwenye kile kilichopo katika milki za juu zaidi za Utakatifu. 'Abdu'l-Bahá hutuelezea fumbo la dhabihu kupitia mfano wa chuma kinachotupwa katika moto. Chuma kina rangi ya kijivu, cha baridi na kigumu. Lazima kiachane na sifa zake hizi ili kipate sifa za moto—ili kiwe chekundu, cha moto na kimiminika. Dhabihu huhusisha kuachana na vitu ambavyo tunavipenda, na kwa hiyo huleta maumivu. Walakini, kwa moyo unaofahamu, maumivu ni matamu, kwa kuwa ni mbebaji wa furaha ya kweli. 'Abdu'l-Bahá hutuambia:

**". . . nitazame mimi, nifuateni mimi, muwe kama Mimi; msijifikirie wenyewe au maisha yenu, iwe mnakula au mnalala, iwe mna starehe, iwe mu wazima au wagonjwa, iwe mpo na marafiki au maadui, iwe mnapata sifa au lawama; kwa mambo yote haya sharti msiyajali kabisa. Nitazame mimi na muwe kama Mimi; lazima mfe kwa nafsi zenu wenyewe na kwa ulimwengu, ili muweze kuzaliwa upya na kuingia ufalme wa mbinguni. Tazameni mshumaa, jinsi utoavyo mwanga. Hupoteza uhai wake, tone kwa tone ili kutoa mwale wake wa mwanga."[29]**

Mahali pengine Yeye huelezea:

**". . . ukaribu na Mungu hulazimu dhabihu ya nafsi, kujitenga na kuvikabidhi vyote Kwake. Ukaribu ni ufanani."[30]**

Na kama tunataka kuona matunda ya matumaini yetu ya juu kabisa, lazima tuwe tayari kufanya jitihada na kutoa dhabihu zinazohitahijaka. 'Abdu'l-Bahá husema:

**"Huu ni wakati wa furaha, ni siku ya shangwe na bashasha, kwani, Mungu asifiwe, milango yote imefunguliwa wazi kupitia fadhili za Uzuri wa Abhá. Lakini jitihada ya hali ya juu na dhabihu ya mtu binafsi huhitajika na umakinifu wa fikra za mtu huhitajika ili mti wa tumaini uweze kuzaa matunda yake na matokeo yapatikane."[31]**

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

Ikiwa tunataka kumfuata 'Abdu'l-Bahá, hatupaswi ____________________ au __________________ yetu, iwe ___________ au ________ , iwe ____________ , iwe _____________________ au ___________ , iwe tupo na _______ au ____________ , iwe tunapata ________ au ____________ ; kwa mambo yote haya sharti tusiyajali kabisa. Lazima _______ na kwa _______________ , ili tuweze _______________ na ___________ ufalme wa mbinguni.

2. Jibu maswali yafuatayo:

a. Nini hutokea wakati mshumaa ukiwashwa? ______________________________

b. Je, inawezekana kwa mshumaa kutoa mwanga bila kuteketea? _______________

c. Mshumaa ambao haujawashwa una thamani gani? ________________________

d. Je, mbegu inaweza kufikia uwezo wake wa asili kwa kuendelea kubaki katika umbo la mbegu? ____________________________________________________

e. Mbegu hutoa dhabihu gani ili iwe mti? ___________________________________

f. Ni yapi baadhi ya mambo tunayohitaji kuachiana nayo ili kutambua uwezo tuliopewa na Mungu uliomo ndani mwetu? ______________________________
_________________________________________________________________
_________________________________________________________________
_________________________________________________________________
_________________________________________________________________
_________________________________________________________________

g. Je, tunaweza kumkaribia Mungu bila dhabihu? ___________________________

h. Je, tunaweza kukuza sifa za kiroho bila dhabihu? ________________________

i. Je, maisha yetu yatakuwa na thamani gani ikiwa hatujitahidi kukuza sifa za kiroho?
_________________________________________________________________
_________________________________________________________________

j. Kwa nini dhabihu binafsi na umakinifu wa fikra zetu ni muhimu, ikiwa tunataka jitihada zetu zizae matunda tunayoyatarajiia? ___________________________
_________________________________________________________________
_________________________________________________________________

3. Kusudi la dhabihu nini

_____ kufikia uhai wa milele

_____ kumkaribia Mungu

_____ kuachana na mali zetu za kidunia

_____ kuachana na tamaa zetu za kibinafsi

_____ kujitahini

_____ kukuza sifa za kiroho

_____ kuteseka

_____ kufuata mfano wa ‘Abdu’l-Bahá

_____ kuleta mwanga wa uongozi katika mioyo ya wanadamu

4. Daraja la dhabihu ni kubwa kwa hakika. Tunapaswa tuhakikishe kwamba hatulipuuzii kwa kujidai wakati wote kwamba kila jambo dogo tufanyalo ni kitendo kikubwa cha dhabihu. Hebu tufikirie kuhusu sentensi ambamo neno “dhabihu” pengine siyo chaguo sahihi, kwa mfano: “Nilijitoa dhabihu kutoangalia kipindi nikipendacho cha runinga ili kwenda kwenye Karamu ya Siku Kumi na Tisa.” Je, neno “dhabihu” linafaa hapa? Ni kweli kwamba jambo fulani limeachwa, lakini je, hatulipnguzii thamani daraja la dhabihu kwa kuliita jambo hilo kama “dhabihu”? Hebu tuchukue mfano mwingine: “Nimejitoa dhabihu siku zangu za mwisho wa juma ili nishiriki katika kampeni shadidi ya ufundishaji Hoja katika ujirani wangu.” Je, sentensi hii humaanisha nini? Je, inamaanisha kwamba tunatambua furaha ya kweli inayotokana na ufundishaji Hoja? Ni kitu gani ambacho tumeachana nacho? Je, inaweza kulinganishwa na baraka za kupata neema na fadhili za Mungu? Andika sentensi chache ambamo matumizi ya neno “dhabihu” hayana sababu.

a. ______________________________________________________________

______________________________________________________________

b. ______________________________________________________________

______________________________________________________________

c. ______________________________________________________________

______________________________________________________________

d. ______________________________________________________________

______________________________________________________________

e. ______________________________________________________________

______________________________________________________________

f. ______________________________________________________________

______________________________________________________________

g. ______________________________________________

______________________________________________

5. Jadili kauli zifuatazo pamoja na kikundi chako:

Tangu mwanzo wa Imani yetu, hadi nyakati za hivi karibuni zaidi, maelfu ya roho wamejitoa dhabihu za hali ya juu kabisa, wakitoa maisha yao yenyewe kwa ajili ya Hoja ya Mungu. Wengi wetu hatuitwi kujitoa kuwa wafia dini kishahidi, lakini lazima tuhuishwe kwa roho hiyo hiyo ya kujitoa katika kutembea njia ya huduma. Dhabihu ndiyo sifa bainifu ya maisha ya huduma.

6. Jadilini uhusiano uliopo kati ya dhabihu, maumivu na furaha.

7. Kariri nukuu zifuatazo:

**"Huyo kwa kweli ni mtu ambaye, leo, hujitoa mwenyewe kwa ajili ya huduma ya mbari nzima ya binadamu. Yule Aliye Mkuu husema: Amebarikiwa na ni mwenye furaha yule ambaye huinuka kuendeleza raghba bora kabisa za watu na koo za dunia."**[32]

**"Hivyo namsihi kila mmoja wenu . . . kutoa dhabihu ya fikra zenu zote, maneno matendo ili kuleta utambuzi wa upendo wa Mungu katika kila moy."**[33]

## SEHEMU YA 11

Katika kozi hii nzima, tumechunguza nguvu za kiroho za kutembea kwenye njia ya huduma. Tumechunguza hali ya moyo unaoakisi sifa za Mungu. Tumetaamuli juu ya upendo wa Mungu na kicho cha Mungu na juu ya ulazima wa kutii amri Zake. Tumefikiria ulazima hasa wa imani, tumaini na shauku kuu katika kupiga hatua kwenye njia hii. Tumeona jinsi ufuatiliaji wa maendeleo ya mtu mwenyewe ya kiakili na ya kiroho na kuchangia kwenye uboreshaji wa jamii unavyohitaji nia, dhamira na juhudi na haja ya dhabihu. Kile tunachopaswa kukumbuka ni kwamba licha ya shida na nyakati za hatari, tunatembea njia hii katika hali ya furaha. Furaha ni sifa ya roho ya mwanadamu na siyo hisia inayotokana na ushawishi wa nje. Kwa kawaida, kuna nyakati ambapo tunahisi huzuni na kuna nyakati ambapo tunahisi furaha. Lakini hali ya kimsingi ya mioyo yetu ni ile yenye furaha—furaha ya kumjua Mungu, furaha ya kumtambua Mdhihirishaji Wake, furaha ya kuzamishwa katika bahari ya rehema Zake, furaha ya kuhudumu kwenye Kizingiti Chake Kitakatifu.

'Abdu'l-Bahá alikuwa kiini cha furaha. Katika maisha yako yote mara kwa mara unapaswa usome maneno ya 'Abdu'l-Bahá, kuyakariri na kutafakari juu ya maana zake wakati ukikumbuka mfano wa maisha Yake. Kusoma kwako maneno na kauli Zake kunapaswa kuwe kwa kina mno kiasi kwamba kuwe sehemu muhimu ya fikra zako. Kila wakati, uwe mwenye furaha au huzuni, wakati wa shida au raha, kazini au mapumzikoni unapaswa uweze kuyakumbuka maneno Yake na kumfikiria Yeye, na Kujawa na furaha. Kwa mujibu huu, pengine ungependa kutafakari juu ya nukuu zifuatazo kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá na kukariri nyingi kadiri uwezavyo:

**“. . . ninyi lazima katika jambo hili—yaani, kuwatumikia wanadamu—myatoe dhabihu maisha yenu wenyewe, na wakati mjitoavyo wenyewe, shangilieni.”[34]**

**“Kama tu mngejua ni daraja kuu jinsi gani lililokusudiwa kwa zile roho ambazo zimejitenga na ulimwengu, ambazo kwa uwezo mkubwa zimevutiwa kwenye Imani, na zinaendelea kufundisha, chini ya kivuli kisetiricho cha Bahá’u’lláh! Jinsi gani ungefurahia, jinsi gani, kwa shangwe na furaha kubwa, ungekunjua mabawa yako na kupaa kuelekea mbinguni—kwa kuwa mfuasi wa njia kama hiyo, na msafiri anayeelekea kwenye Ufalme kama huo.”[35]**

**“Shikilieni kwa uthabiti kwenye pindo la vazi la Mungu, na elekezeni juhudi zenu zote kwa ajili ya uendelezaji wa Agano Lake, na daima kuwaka kwa uwangavu zaidi kwa moto wa upendo Wake, ili mioyo yenu iweze kuruka kwa furaha katika pumzi za utumishi ambazo hububujika kutoka katika kifua cha ‘Abdu’l-Bahá.”[36]**

**“Hebu tuweka kando fikra zote za nafsi; hebu tufumbe macho yetu kwa vyote vilivyomo duniani, hebu tusiyaoneshe mateso yetu wala kulalamika juu ya makosa yetu. Bali hebu tuzisahau nafsi zetu wenyewe, na tukigugumiza divai ya neema za mbinguni, hebu tupaze sauti za furaha yetu, na tujipoteze katika uzuri wa Mtukufu—Kabisa.”[37]**

**“Wakati wote nawataja na kuwakumbuka. Namuomba Bwana, na kwa machozi namsihi Yeye kunyesha baraka zote hizi juu yenu, na kufurahisha mioyo yenu, na kuzipa roho zenu furaha kamili, na kuwajalia furaha isiyo kifani na furaha za mbinguni.”[38]**

**“Furaha yangu pekee katika ulimwengu huu upitao kwa kasi ilikuwa kukanyaga njia ya Mungu yenye mawe na kustahimili majaribu magumu na huzuni zote za kimwili. Kwani vinginevyo maisha haya ya kidunia yangethibitika kuwa matupu na bure, na kifo kingekuwa bora. Mti wa uzima usingezaa matunda yoyote; shamba lililopandwa la uwepo huu lisingetoa mavuno yoyote. Hivyo ni tumaini langu kwamba kwa mara nyingine tena hali fulani itafanya kikombe changu cha maumivu kufurika, na ule Upendo mzuri, yule Muuaji wa roho, atawabumbuaza tena watazamaji. Ndipo moyo huu utakapofurahi sana, roho hii itakapobarikiwa.”[39]**

**“Ndipo jua la Ukweli likachomoza na utukufu wa Ufalme ukatawanywa kote mashariki na magharibi. Wale ambao walikuwa na macho yaonayo walifurahia habari njema za furaha na kupaza sauti: ‘Aah tumebarikiwa, tumebarikiwa sisi!’, na walishuhudia uhalisia wa ndani wa vitu vyote, na kufumbua mafumbo ya Ufalme. Wakikombolewa kutokana na mawazo yao ya kipuuzi na mashaka yao, waliona mwangaza wa ukweli, na walikuwa wamefurahishwa mno kutokana na kunywa kalisi ya upendo wa Mungu, kiasi kwamba waliusahau kabisa ulimwengu na nafsi zao wenyewe. Wakichachawa kwa furaha waliharakia mahali pa kuuawa kwao kishahidi, na hapo ambapo watu hufa kwa ajili ya upendo, walitupilia mbali vichwa na mioyo yao.”[40]**

# MAREJELEO


1. Kutoka mazungumzo yaliyotolewa mnamo 14 Aprili 1912, kuchapishwa katika *Utangazaji wa Amani ya Ulimwengu: Mazungumzo yaliyotolewa na ‘Abdu’l-Bahá wakati wa ziara Yake huko Marekani na Canada mnamo mwaka 1912* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2012), aya. 4, uk. 19 (toleo la Kiingereza).

2. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1983, chapisho la 2017), XXXIV, aya. 1, uk. 86 (toleo la Kiingereza).

3. Kama hapo juu., LXXV, aya. 1, uk. 162 (toleo la Kiingereza).

4. Kutoka barua ya 30 Oktoba 1924 iliyoandikwa na Shoghi Effendi kwa Baraza la Kiroho la Mahali la Ṭehrán, imechapishwa katika Maisha ya *Ubikira na Matakatifu: Dondoo kutoka Maandiko Kibahá’í*, zilizokusanywa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu (Ingleside: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í Australia, 2021), na. 7, ku. 11–12 (Kiingereza).

5. Bahá’u’lláh, *Maneno Yaliyofichwa* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2003, chapisho la 2022), Kiarabu na. 5, uk 4.

6. *Mateuzi kutoka Maandiko ya ‘Abdu’l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2010, chapisho la 2015), na. 174.2–3, ku. 280–81 (toleo la Kiingereza).

7. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh*, CXXVI, aya. 4, ku. 307–8 (toleo la Kiingereza).

8. *Mwangaza wa Ulimwengu: Nyaraka Zilizoteuliwa za ‘Abdu’l-Bahá* (Haifa: Makao Makuu ya Kibahá’í ya Ulimwengu, 2021), na. 6.7, uk. 20 (toleo la Kiingereza); pia katika *Umuhimu wa Sala za Faradhi na Mfungo: Dondoo kutoka Maandiko Kibahá’í*, zimekusanywa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu (Ingleside: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í Australia, 2021), na. 23, uk. 15.

9. Bahá’u’lláh, katika *Kitáb-i-Aqdas: Kitabu Kitakatifu Kabisa* (Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, New Delhi, India chapisho la Kiswahili la 2024), aya. 1, uk. 19; pia katika *Buga kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh*, CLV, aya. 1, uk. 375 (toleo la Kiingereza).

10. Bahá’u’lláh, katika *Kitáb-i-Aqdas*, aya. 3, uk. 20; pia katika *Buga kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh*, CLV, aya. 3, uk. 376 (toleo la Kiingereza).

11. Bahá’u’lláh, imenukuliwa katika utangulizi ulioandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu wa *Kitáb-i-Aqdas*, uk. 5.

12. *Nyaraka za Bahá’u’lláh zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’I, 1988, chapisho la 2021), na. 5.10, uk. 54 (toleo la Kiingereza).

13. Bahá’u’lláh, katika *Umuhimu wa Sala za Faradhi na Mfungo*, na. 14, uk. 11 (toleo la Kiingereza).

14. *Nyaraka za Bahá’u’lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas*, na. 17.109, uk. 321 (toleo la Kiingereza).

15. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CXXXIII, aya. 1, uk. 327 (toleo la Kiingereza).

16. Bahá'u'lláh, katika *Kitáb-i-Aqdas*, aya. 4, uk. 20; pia katika *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CLV, aya. 4, ku. 376–77 (toleo la Kiingereza).

17. Kutoka Waraka wa 'Abdu'l-Bahá. (tafsiri Iliyoidhinishwa)

18. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, LII, aya. 1, uk. 118 (toleo la Kiingereza).

19. *Siku za Ukumbusho: Mateuzi kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh kwa ajili ya Sikukuu Takatifu za Kibahá'í* (Haifa: Makao Makuu ya Kibahá'í ya Ulimwengu, 2016), na. 29.9, uk. 146 (toleo la Kiingereza).

20. Mateuzi kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá, na. 178.1, uk. 284 (toleo la Kiingereza).

21. Kutoka mazungumzo yaliyotolewa mnamo 21 Novemba 1911, kuchapishwa katika *Mazungumzo ya Paris: Hotuba Zilizotolewa na 'Abdu'l-Bahá mnamo 1911* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2006, chapisho la 2016), na. 34.8, uk. 133 (toleo la Kiingereza).

22. *Mwangaza wa Ulimwengu*, na. 4.3, uk. 9 (toleo la Kiingereza).

23. 'Abdu'l-Bahá, katika *Sala za Kibahá'í: Mateuzi ya Sala Zilizofunuliwa na Bahá'u'lláh, Báb na 'Abdu'l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2002, chapisho la 2020), ku. 131–32 (toleo la Kiingereza).

24. Kutoka kwa mazungumzo yaliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá mnamo 16 Juni 1912, kuchapishwa katika *Utangazaji wa Amani ya Ulimwengu*, aya. 1, uk. 273 (toleo la Kiingereza).

25. Kutoka barua ya 31 Machi 1932 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa muumini binafsi, katika *Nguvu ya Msaada Mtakatifu: Dondoo kutoka katika Maandiko Kibahá'í*, zilizokusanywa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu (Ingleside: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, Australia, 2020), na. 66, uk. 36 (Kiingereza).

26. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, LXXVII, aya. 1, uk. 169 (toleo la Kiingereza).

27. *Mateuzi kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá*, na. 200.9, ku. 338–39 (toleo la Kiingereza).

28. 'Abdu'l-Bahá, katika *Baadhi ya Maswali Yaliyojibiwa* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2014, chapisho la 2022), na. 70.6–7, ku. 288–89 (toleo la Kiingereza).

29. 'Abdu'l-Bahá, katika *Maandiko Matakatifu ya Kibahá'í*: *Mateuzi kutoka maneno ya Bahá'u'lláh na 'Abdu'l-Bahá* (New York: Kamati ya Uchapishaji ya Kibahá'í, 1928), na. 969, uk. 503 (toleo la Kiingereza).

30. Kutoka mazungumzo yaliyotolewa na ‘Abdu’l-Bahá mnamo 26 Mei 1912, kuchapishwa katika *Utangazaji wa Amani ya Ulimwengu*, aya. 2, uk. 205.

31. Kutoka Waraka wa ‘Abdu’l-Bahá. (tafsiri Iliyoidhinishwa)

32. *Nyaraka za Bahá’u’lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas*, na. 11.12, uk. 205; pia katika *Buga kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh*, CXVII, aya. 1, uk. 282 (toleo la Kiingereza).

33. Kutoka mazungumzo yaliyotolewa na ‘Abdu’l-Bahá mnamo 9 Novemba 1911, kuchapishwa katika *Mazungumzo ya Paris*, na. 27.11, uk. 99 (toleo la Kiingereza).

34. *Mateuzi kutoka kwa Maandiko ya ‘Abdu’l-Bahá*, na. 35.9, uk. 105 (toleo la Kiingereza).

35. Kama hapo juu, na. 64.2, uk. 1.

36. Kama hapo juu, na. 42.3, uk. 123.

37. Kama hapo juu, na. 195.5, uk. 327.

38. Kama hapo juu, na. 17.8, uk. 56.

39. Kama hapo juu, na. 190.10, uk. 313.

40. Kama hapo juu, na. 16.1, uk. 50.



# Kuhudumu kama Mkufunzi wa Kozi za Taasisi

## Kusudi

Kuelewa baadhi ya dhana na kujipatia baadhi
ya sifa za kiroho, mielekeo na stadi zinazochangia
kwenye uwezo uhitajikao kusaidia
kikundi cha marafiki kupitia kozi za taasisi

## SEHEMU YA 1

Washiriki katika mchakato wa kielimu ulioazishwa na Taasisi ya Ruhi kwa ajili ya wale wenye umri wa miaka kumi na tano na zaidi kujifunza mlolongo wa kozi zilizokusudiwa kuwaandaa kutekeleza vitendo vya huduma—vitendo ambavyo huchangia katika mtindo hai wa maisha ya jumuiya. Kutoka miongoni mwa hivi, kitendo kimoja cha huduma hakiepukiki, kwani, bila hicho, hatimaye itathibitika kuwa haiwezekani kwa mtindo huu kudumishwa na kuimarishwa. Kwa hakika, ukunjukaji wa mchakato wa kielimu wenyewe hutegemea juu yake—yaani, kwa idadi inayoongezeka ya watu binafsi kukuza uwezo kutoa huduma kama wakufunzi wa kozi za taasisi, wakiwasaidia washiriki kuendelea katika njia ya huduma. Mlolongo wa kozi ambao aghalabu husomwa miongoni mwa kikundi cha marafiki ambacho hukutana mara kwa mara katika ujirani au kijiji katika mazingira ya kikundi cha mafunzo. Wakati mwingine, walakini, vikundi huundwa kama sehemu ya kampeni iliyoandaliwa kwa ajili ya mafunzo shadidi au wakati wa kambi ambayo hufanyika katika kipindi cha likizo za shule. Katika fursa yoyote ile, mshiriki mmoja wa kikundi hutenda kama mkufunzi.

Kukuza ustadi wa mkufunzi anayefaa huhitaji mafunzo machache ya mwanzoni yakifuatiwa na ushiriki katika mikusanyiko ya mara kwa mara kwa ajili ya tafakari, ambamo maudhui ya kozi huchunguzwa na tajiriba huchambuliwa. Tunajua kwamba sifa za kiroho hujenga msingi wa uwezo wetu wote na huamua, katika uchambuzi wa mwisho, kiwango cha ufaaji wetu. Ndio maana kitengo cha kwanza cha kitabu hiki kilihusu asili ya nguvu za kiroho zinazotokana na kutembea njia ya huduma iliyodokezwa na kozi. Katika kitengo hiki cha pili, tutamakinikia zaidi juu ya baadhi ya dhana za kielimu ambazo sharti tuzielewe, njia na mbinu ambazo tunahitaji kuzifuata, na sifa za kiroho, mielekeo, stadi na vipawa tunavyotakiwa kukuza kupitia tajiriba iendeleayo, ikiwa tunataka kuthibitisha kuwa tuna uwezo wa kukisaidia kikundi hadi kikundi kupitia mlolongo wa kozi.

## SEHEMU YA 2

Hebu tuanze majadiliano yetu kwa kuchunguza dhana ya hamasa. Bila hamasa, washiriki wa kozi watajifunza kidogo na idadi yao itapungua. Jinsi ya kugusa mizizi ya hamasa na kudumisha kiwango cha juu cha shauku ni suala ambalo aghalabu utajiuliza mwenyewe. Utakabiliana na changamoto hii wakati wowote utakapowaalika marafiki zako na wengine katika jumuiya kujiunga nawe katika usomaji wa kozi na, baadaye, kila wakati mnapokutana kama kikundi.

Kama hatua ya awali katika uchunguzi wetu wa suala hili, tunaweza kuyagawa mambo ambayo huwahamasisha watu katika makundi mawili: ya mpito na ya kudumu. Katika hiyo ya kwanza huangukia yale mambo yote ambayo huwasisimua watu kwa muda mfupi na kuwasukuma kutenda, aghalabu kwa kipindi cha muda mfupi. Kundi la pili hujumuisha yale mambo ambayo huleta hamasa, yenye mizizi inayozama kwa kina katika moyo na roho ya mtu. Utakumbuka kutoka kitengo cha tatu cha Kitabu cha 2 mazungumzo ya kina kati ya Alejandra na Beatrice ambayo yalisababishia Beatrice kuingia katika mchakato wa taasisi. Fikiria kama Alejandra badala yake angempa tu mwaliko ufuatao rafiki yake:

> "Ningependa kukukaribisha kujiunga na kikundi cha mafunzo tulichokianzisha hivi karibuni katika jumuiya yetu. Tayari kuna watu kumi na wawili katika kikundi chetu, na nina hakika utampenda kila mmoja wao. Tunapata furaha kubwa pamoja. Tunasoma

mara mbili kwa juma kwa saa kadhaa lakini pia tunajihusisha katika shughuli zingine. Jumamosi hii, kwa mfano, tutakuwa na mandari, ambapo unakaribishwa sana, na baadhi yetu tunafikiria kucheza mpira wa wavu baada ya hapo."

Ni katika kundi gani ungeweka aina hii ya hamasa inayotafutwa na ombi hili? Bila shaka, hakuna kosa lolote kwa mwaliko kama ulivyoandaliwa hapo juu. Shughuli za ziada zilizotajwa zinafaa kwa kikundi cha mafunzo, hususan kile chenye vijana. Kwamba shughuli kama hizo zingeweza kumshawishi mtu kujiunga na kikundi cha mafunzo halina mjadala pia. Kile kinachoongelewa hapa, walakini, ni kwamba aina hii ya hamasa kwa kawaida ni ya mpito. Hufanya kazi kwa muda lakini hatimaye hukoma kuwa yenye kufaa. Unapotegemea tu juu ya shauku iliyofanyizwa kwa njia hii, unajiweka katika hali ngumu sana. Wakati wote utalazimika kubuni "mambo ya kufurahisha kufanya", hadi hatimaye, unakuwa umechoka. Kwamba ujifunzaji unapaswa kuwa wenye furaha haimaanishi kwamba elimu ni sawa na burudani.

Ili kutimiza kusudi la kozi, ambalo ni uwezeshaji wa kiroho na kimaadili wa washiriki, utapaswa kutafuta vyanzo vya hamasa ambavyo ni vya kudumu zaidi. Tayari unafahamu fika vingi vya vyanzo hivi na utavikumbuka kwa urahisi kama ukitafakari juu ya sababu zako mwenyewe za kushiriki katika mchakato wa taasisi. Kitu gani kilicho kushawishi kusoma kozi mbalimbali, na sasa kitu gani kinasababisha ndani mwako shauku ya kukuza uwezo utakaouhitaji ili uweze kutenda kama mkufunzi wa kozi hizi hizi?

## SEHEMU YA 3

Umesikia ikisemwa kwamba shauku inaambukiza. Ari na nguvu ambavyo kwavyo unakiendea kitendo hiki cha huduma, kwa hiyo, vitasaidia kuwahamasisha marafiki zako katika usomaji wao wa kozi. Shauku hii isieleweke kama msisimko tu, kama hisia ya mpito na ya kijuujuu tu. Ni udhihirisho wa asili wa furaha ya ndani, furaha ambayo ni sifa ya roho ya mtu na siyo matokeo ya hali za mpito. Katika vitengo ambavyo tayari umeshavimaliza na ambavyo hivi punde utavisoma pamoja na watu wenye kuvutiwa, aghalabu furaha hii hurejelewa—kwa mfano, katika kitengo cha kwanza cha Kitabu cha 2, ambayo mada yake ni furaha ya ufundishaji. Sehemu ya 11 ya kitengo kilichotangulia pia kinahusu furaha. Soma tena sehemu hiyo. Namna gani maoni yaliyotolewa pale yanaweza kutumika katika shauku yako ya kuhudumu kama mkufunzi? Pamoja na kikundi ambacho unasoma nacho kitengo hiki, jadilini jinsi kutafakari juu ya maisha ya 'Abdu'l-Bahá, kusoma na kukariri maneno Yake, na kukumbuka upendo Wake usiokwisha vitakuwa chanzo cha furaha ya kudumu kwenu.

Ni dhahiri, furaha ambayo kwayo huleta ari yako ya kuhudumu kama mkufunzi, na ambayo kwa hiyo italeta shauku ndani mwa washiriki wa kikundi cha mafunzo, ni sifa ya moyo msafi. Tena usafi wa moyo imekuwa mada ya majadiliano yetu katika nafasi mbalimbali, kikiwemo kitengo cha kwanza cha kitabu hiki. Katika kitengo cha pili cha Kitabu cha 6 tulijadili juu ya uchafu wa aina tatu ambao huathiri jitihada zetu za ufundishaji: tamaa ya kutambulika, hisia ya kujikweza na tamaa ya makuu. Hebu tufikirie jinsi vitu hivi vitatu vinavyoweza kupunguza ufanisi wa mkufunzi:

1. Je, unadhani washiriki wanaweza kuhisi usafi wa nia ya mkufunzi?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

2. Jinsi gani hamasa ya washiriki itaathiriwa kama wakihisi kwamba mkufunzi wa kikundi anajiona bora kuliko wao?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

3. Jinsi gani hamasa yao ingeathiriwa kama wangehisi kuwa mkufunzi alikuwa anafanya kitendo cha huduma kwa sababu alitumaini kupata wadhifa katika jamii?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

Ili kufikiri zaidi juu ya suala la usafi, tazama orodha hapa chini. Inatoa baadhi ya sababu ambazo mtu anaweza kuwa nazo kwa kutoa huduma kama mkufunzi. Chache miongoni mwao hazikubaliki kabisa na zimewekwa hapa kwa ajili ya kutofautisha tu. Kwanza weka alama ya herufi “H” kwa zile ambazo, bila mjadala, hazikubaliki. Kisha fikiria zile zinazobaki na jadilini, pamoja na washiriki wengine wa kikundi chenu, kile wanachohitaji kujitenga nacho, wakizingatia mambo kama vile tamaa za binafsi, tamaa ya mafanikio na kutambulika, anasa za ulimwengu na misukumo ya nafsi.

Mtu anaweza kuhudumu mkufunzi kwa sababu yeye

_____ hufurahia kuwaona watu wakiendelea.

_____ hutaka kukua kiroho na kuchangia katika shughuli za kujenga jumuiya katika kijiji au ujirani wake.

_____ hutumaini hatimaye kuwa mratibu wa kanda na kupokea ujira mdogo.

_____ hutaka kumpendeza Mshauri Msaidizi.

_____ hutaka wengine wamuige.

_____ hutaka kupendwa na watu wengine.

_____ hutaka kuheshimiwa na watu wengine.

_____ hupenda kufanya mambo na kupata matokeo.

_____ hutaka kuchukuliwa kama kiongozi katika jumuiya.

_____ amevutiwa na Mpendwa-Kabisa.

_____ anafurahishwa sana na mwito wa Mungu.

_____ hutaka kuchangia kwenye Mipango ya kiulimwengu iliyotolewa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa ulimwengu wa Kibahá'í.

_____ amevuta manukato ya huduma isiyo na raghba kwa Hoja.

_____ hutaka kuvutia baraka za Mungu kwa jumuiya yake.

_____ hana tamanio lingine bali kumpendeza Mungu.

## SEHEMU YA 4

Kadiri mnavyojitahidi kuwasaidia wengine katika usomaji wa kozi za Taasisi ya Ruhi, ndivyo mtakavyoendelea kuhakikishiwa kwamba uelewa wenyewe ndiyo hamasa kubwa kabisa. Kuna shauku katika kila moyo wa mwanadamu ya kujua maana; kuna hitaji la kiasili la kupata ujuzi wa uhalisia wa nje na wa ndani wa muumbo. Elimu inapaswa ishughulikie shauku hii. Ikifanya hivyo, inafanikiwa kugusa mizizi ya hamasa. Tunapendekeza kwamba utafakari juu ya maneno yafuatayo ya 'Abdu'l-Bahá kutoka Waraka ambamo Yeye anasifu juhudi za Mbahá'í mmoja maarufu, za kuwafunza, kupitia kile anachokiita "mkutano wa ufundishaji", wale wanaoinuka kufundisha Hoja:

**"Enyi Kundi la Mungu! Kwa kila kitu kilichoumbwa, Mamlaka ya Kale yamegawa ukamilifu Wake yenyewe, sifa mahsusi na ubora wake maalum, ili kila mmoja katika kiwango chake aweze kuwa alama inayoonesha uadhama wa Mwelimishaji wa kweli wa wanadamu, na kwamba kila mmoja, kama vile fuwele, aweze kushuhudia juu ya neema na utukufu wa Jua la Ukweli.**

**"Na kutoka miongoni mwa viumbe vyote Yeye amemteua mtu, akamjalia zawadi Yake ya kustaajabisha kabisa, na amemfanya afikie baraka za Kundi la Juu. Zawadi ya thamani kabisa kati ya zote ni ufikiaji kwenye mwongozo Wake usioshindwa, ili uhalisia wa ndani wa mwanadamu uweze kuwa kama kishubaka cha kushikilia taa hii; na wakati miangaza itawanyayo ya mwanga huu inapogonga kwenye kioo king'aacho cha moyo, usafi wa moyo hufanya miale kuwaka kwa nguvu zaidi kuliko hapo mwanzoni, na kung'aa kwa utukufu kwenye akili na roho za watu.**

**"Ufikiaji wa mwongozo huu mkuu kabisa hutegemea juu ya ujuzi na hekima, na baada ya kujulishwa mafumbo ya Maneno Matakatifu. Kwa hiyo wapendwa wa Mungu, wawe vijana au wazee, wawe wanaume au wanawake, kila mmoja kufuatana na uwezo wake, lazima wajitahidi kupata matawi mbalimbali ya maarifa, na kuongeza uelewa wake wa mafumbo ya Vitabu Vitakatifu, na ustadi wake katika kukusanya mathibitisho na shuhuda takatifu.**

**"Mwadhama Ṣadru'ṣ-Ṣudúr, ambaye kwa kweli amefikia daraja tukufu kabisa katika Makimbilio ya Furaha kuu, alizindua mkutano wa ufundishaji. Yeye alikuwa roho ya kwanza iliyobarikiwa kuweka msingi wa asasi hii muhimu. Mungu asifiwe, katika kipindi cha uhai wake yeye aliwaelimisha watu ambao leo ni watetezi imara na wenye ushawishi wa Bwana Mungu, wafuasi ambao kwa hakika ni wazawa safi na wa kiroho wa yule aliyekuwa karibu sana na Kizingiti Kitakatifu. Baada ya kufariki kwake, baadhi ya watu waliobarikiwa walichukua**

**hatua ya kuendeleza kazi yake ya ufundishaji, na Aliposikia hili moyo wa Mfungwa huyu ulifurahishwa.”[1]**

Maneno haya ya ‘Abdu’l-Bahá yanatupa umaizi wenye thamani katika mienendo inayohitajika ya kikundi cha mafunzo. Kufuatana na aya ya hapo juu, zawadi kubwa kabisa tuliyojaliwa na Mungu ni zawadi ya kuufikia mwongozo Wake. Ili kuufikia “mwongozo huu mkuu kabisa”, tunahitaji ujuzi na hekima na sharti tuwe tuliohabarishwa mafumbo yaliyomo katika Maneno Matakatifu. Ni kawaida tu, hivyo, kwamba upokeaji wa baraka za mwongozo Wake usioshindwa na kuchunguza mafumbo ya Maneno Matakatifu yenyewe hufanya chanzo kikuu cha hamasa. Changamoto yako ni kuhakikisha kwamba washiriki wa kikundi cha mafunzo kwa kweli wanajishughulisha na uchunguzi unaosisimua kama huu na kupokea zawadi hii ya ajabu.

Ili kuelewa zaidi jambo hili, sasa geukia kwenye kitabu cha kwanza katika mlolongo wa kozi na bainisha angalau sehemu tatu ambazo ziliongeza kwa kiwango kikubwa uelewa wako wa somo la kiroho. Taja baadhi ya umaizi uliopata kutoka usomaji wa kila sehemu.

1. ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

2. ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

3. ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

Katika Waraka huo huo uliowasilishwa kwenu hapo juu, ‘Abdu’l-Bahá anafunua sala yenye uzuri wa kipekee. Pengine ungependa kuikariri na kuikumbuka kila mara unapoinuka kuhudumu kama mkufunzi.

> **“Ee Mungu, Ewe Ambaye umetawanya utukufu Wako juu ya uhalisia ung’aao wa watu, ukitawanya juu yao miangaza ing’aayo ya ujuzi na mwongozo, na umewachagua kati ya vitu vyote vilivyoumbwa kwa neema hii itokayo juu, na umewafanya wavizingire vitu vyote, kuelewe asili yao ya ndani kabisa, na kufichua siri zao, ukiwatoa gizani na kuwaleta katika ulimwengu uonekanao! ‘Yeye kwa kweli humwonesha huruma Yake maalum yeyote amtakaye.’**

**"Ee Bwana, uwasaidie wapendwa Wako kupata ujuzi na sayansi na sanaa, na kufumbua siri ambazo zimehifadhiwa katika uhalisia wa ndani kabisa wa vitu vyote vilivyoumbwa. Uwafanye wasikie kweli zilizofichwa ambazo zimeandikwa na kuzamishwa katika moyo wa kila kitu kilichopo. Uwafanye wawe bendera za mwongozo miongoni mwa viumbe vyote, na miale ipenyezayo ya akili ikitawanya mwangaza wake katika huu, 'uhai wa kwanza'. Uwafanye wawe viongozi Kwako, miongozo kwenye njia Yako, wakimbiaji wakiwasihi watu kwenye Ufalme Wako.**

**"Wewe kwa kweli u Mwenye Uwezo, Mlinzi, Mwenye Nguvu, Mtetezi, Mwenyezi, Mkarimu—Kabisa."[2]**

## SEHEMU YA 5

Wakati wa kusoma kozi pamoja na kikundi kidogo, utahitaji kutathmini kama washiriki wamepata kiwango kinachohitaji cha uelewa wa nyenzo. Katika muktadha huu, unapaswa utambue kwamba, kwa ujumla, uelewa siyo kitu ambacho mtu anaweza kukipata na amemaliza. Ni kweli kwamba kuna mawazo mengi ambayo yanaeleweka mara moja. Lakini ufahamu wa kina wa masuala mengi hukua kwa muda mrefu. Swali unaloweza kujiuliza mara kwa mara kwa hiyo, siyo kama washiriki "wameelewa" bali kama wao "wanaendelea katika uelewa wao" wa mada husika. Soma na kutafakari juu aya zifuatazo kutoka sehemu za mwanzoni za Kitabu cha 1, "Mawazo Machache kwa ajili ya Mkufunzi", zinazolenga juu ya dhana ya uelewa. Wakati unafanya hivyo, rejelea kwenye sehemu husika za kitengo cha kwanza za kitabu zilizotajwa.

Kutembea njia ya huduma iliyofunguliwa na kozi za taasisi huhitaji uelewa unaoendelea kuimarishwa wa mafundisho ya Bahá'u'lláh, ambayo nyenzo hizi zinajitahidi kuyawasilisha kwa uwazi. . .

Haishangazi basi, kwa kuwa suala la uelewa ni muhimu sana kwa vitabu vyote kwenye mlolongo, kwamba hiki cha kwanza ndicho huanza nalo. Kusoma Maandiko Matakatifu siyo sawa na kusoma maelfu ya kurasa ambazo mtu huziona maishani mwake, na kitengo, "Ufahamu wa Maandiko ya Kibahá'í", hutafuta kukuza tabia ya kusoma vifungu kutoka Maandiko Matakatifu kila siku na kutaamuli juu ya maana zake, tabia ambayo itawasaidia sana washiriki kadiri wanavyoianza njia ya huduma. Ili kuwaongoza katika usomaji wake, mkufunzi sharti amakinikie sana juu ya suala la uelewa.

Maandiko Kibahá'í yana kweli za kina za kiroho, na hata kama tukijitahidi kuendelea katika uelewa wetu wa maana zake zisizo na mwisho, tunajua kwamba kamwe hatuwezi kufikia mwisho kamili. Kwa kawaida tunapata uelewa wa msingi wa maana ya papo hapo ya kifungu pale tunapokisoma kwa mara ya kwanza, na Sehemu ya 1 ya kitengo hiki hulichukulia hili kama mahali pa kuanzia. Hivyo, baada ya kusoma nukuu, "Uboreshaji wa ulimwengu unaweza kutimizwa kwa matendo safi na mema, kwa mwenendo usifikao na unaostahili", washiriki huulizwa tu, "Uboreshaji wa ulimwengu unaweza

kutimizwaje?” Kwa mtazamo wa mara moja, maswali na mazoezi mengi ya aina hii huonekana rahisi sana. Lakini tajiriba ya miaka mingi huonekana kuhalalisha uamuzi wa Taasisi wa kuanza kwa namna hii. Sote tunahitaji tujikumbushe kwamba, katika haraka yake ya kutafuta matabaka ya ukweli katika aya, akili haipaswi kupuuzia maana yake ya wazi. Uzingatiaji kwenye ngazi hii ya kwanza ya ufahamu pia huthibitisha kuwa muhimu kwa ajili ya ushauriano wa kikundi; unaimarisha umoja wa fikra, unaopatikana kwa urahisi pale maoni binafsi yanarupohusiwa kuangaziwa na hekima Takatifu.

Ni muhimu kutanabahi hapa kwamba kuelewa maana ya papo hapo ya vifungu vingi hakutokani na majadiliano marefu ya neno moja moja nje ya muktadha. Baada ya kusema hayo, inaweza kuwa muhimu mara moja moja kikundi kutafuta neno katika kamusi. Kile ambacho kingeweza kuzaa matunda, walakini, ni kwa washiriki kujifunza kubaini maana za maneno kutokana na sentensi na aya nzima.

Ili uelewa uweze kupanuka zaidi ya milki ya maana ya papo hapo, mifano inayoonesha jinsi mawazo yanavyoweza kuelezwa inaweza kuwa ya msaada. Kile kinachotakiwa kuhusiana na hili ni mazoezi yaliyo wazi. Katika Sehemu ya 2, mathalani, washiriki wanaambiwa kuamua, kufuatana na aya waliyoisoma hivi punde, kama baadhi ya sifa zinazostahili. Katika zoezi kama hilo hilo katika Sehemu ya 4, wanahamisishwa kutaja njema tano na kisha waamue kama inawezekana kupata japo mojawapo pasipo na ukweli—kama ilivyoelezwa katika Maandiko kuwa “msingi wa njema zote za binadamu”.”

Sasa, kwa mujibu wa tafakari zako juu ya dhana ya uelewa, jibu maswali hapa chini.

1. Jinsi gani umakinikiaji juu ya maana ya papohapo ya vifungu kutoka Maandiko huchangia kwenye ujengaji wa umoja wa fikra katika kikundi?

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

2. Kwa nini ni muhimu kwenda mbali zaidi ya maana ya papohapo ya kifungu na kufikiri jinsi inavyoweza kidhihirika katika maisha yetu?

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

3. Jinsi gani kupata umaizi katika maana pana zaidi za vifungu kutoka Maandiko hutusaidia kupatanisha fikra na matendo yetu na mafundisho ya Imani?

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

## SEHEMU YA 6

Uwezo wako wa kulea uelewa utakuhitaji kuendelea kukuza sifa kama vile utambuzi, kujitenga na ukarimu, na kuchota kwenye nguvu ya mtazamo wa kiroho. Utahitaji kumsikiliza kila mmoja kwa makini. Wakati mwingine, mtu, wakati akielewa vyema kabisa mada inayojadiliwa, hana maneno ya kutosha kuelezea mawazo yake. Hupaswi kumakinikia juu ya maneno pekee, bali unapaswa kutazama maana iliyokusudiwa. Ili kufanya hivyo, lazima uwaamini marafiki zako na uwe na imani kwamba kila mmoja ana mambo ya maana ya kusemaessi minis et quip feummod dio essi ero odigniamet quip enis ing amconsequis lumsan an con.

Ili kutafakari juu ya uwezo wa kulea uelewa, soma kila sentensi hapa chini na weka alama zile ambazo unakubaliana nazo.

_____ Ninaposoma kifungu kutoka katika Maandiko pamoja na wengine, ni wajibu wangu kama mkufunzi kuhakikisha kwamba wanakielewa kifungu hicho sawa na ninavyokielewa.

_____ Ninaposoma kifungu kutoka katika Maandiko pamoja na wengine, ni lazima niheshimu uelewa wao lakini bado nikashikilia mawazo yangu mwenyewe, kwa kuwa yapo sahihi. Hata hivyo, mimi ndiyo mkufunzi na nina uelewa mzuri zaidi kuliko wengine.

_____ Ninaposoma kifungu kutoka katika Maandiko pamoja na wengine, ninajifunza mambo mengi kutoka katika majadiliano yetu, haidhuru tayari najua kiasi gani.

_____ Ninaposoma kifungu kutoka katika Maandiko pamoja na wengine, napaswa kushiriki uelewa wangu kwa unyenyekevu na uwazi.

_____ Ninapokuwa nahudumu kama mkufunzi, ingawa kamwe sipaswi kuchukulia kuwa uelewa wangu wa nyenzo umekamilika, nahitaji kuhakikisha kwamba washiriki hawafikiii mahitimisho kinyume na maana dhahiri ya kifungu kutoka katika Maandiko.

_____ Kamwe sipaswi kuelezea maoni na msimamo wangu mwenyewe ninapohudumu kama mkufunzi.

_____ Kusudi la majadiliano katika kikundi chetu cha mafunzo ni mimi kufundisha maana sahihi ya nyenzo.

_____ Kusudi la majadiliano katika kikundi chetu cha mafunzo ni kwa kila mtu kuelezea chochote kinachokuja akilini mwake kwa sababu kujieleza ni suala lenye thamani ya hali ya juu kabisa tulilolishikilia.

_____ Kusudi la majadiliano katika kikundi cha mafunzo ni kwa washiriki kusaidiana kufikia uelewa wa kina zaidi wa kile kinachosomwa.

_____ Kujitenga na maoni yangu mwenyewe humaanisha kwamba napaswa kuruhusu majadiliano miongoni mwa washiriki kuendelea, hata kama naona hayafiki popote.

_____ Kama kweli wamejitenga na maoni yao wenyewe, washiriki wa kikundi cha mafunzo watakubali kama ukweli kila kitu kinachosemwa na kila mtu.

_____ Kujitenga na maoni binafsi hurahisisha majadiliano ya wazi, yenye adabu, na ya kweli wakati wa usomaji wa nyenzo.

_____ Ninapohudumu kama mkufunzi, napaswa nimuombe Mungu kwa bidii dhati afungue malango ya uelewa wa kweli.

## SEHEMU YA 7

Jambo linalohusiana kwa karibu na kiu ya ujuzi na uelewa ni nguvu ya kiroho yenye uwezo: mvuto kwa uzuri. Fikiria kifungu kifuatacho kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh:

> **"Nisikilizeni enyi ndege wa umauti! Katika Bustani ya Mawaridi ya utukufu usiobadilika Ua limeanza kuchanua, likilinganishwa nalo kila ua lingine ni mwiba tu, na mbele ya wangavu wa utukufu Wake asili yenyewe ya uzuri lazima ikwajuke na kusinyaa. Inukeni, kwa hiyo, na, kwa shauku yote ya mioyo yenu, kwa ari yote ya roho zenu, nguvu zote za nia yenu, na juhudi zilizolimbikizwa za uwepo wenu wote, jitahidini kuifikia paradiso ya uwepo Wake, na jitahidini kuvuta manukato ya Ua lisiloharibika, kuvuta harufu nzuri za utakatifu, na kujipatia sehemu ya marashi haya ya utukufu wa mbinguni. Yeyote afuataye ushauri huu ataikattilia mbali minyororo yake, ataonja uachaji wa upendo wenye furaha kubwa, atafikia haja ya moyo wake, na ataisalimisha roho yake katika mikono ya Mpendwa wake. Akipasua kizimba chake kwa nguvu, kama vile ndege wa roho, atapaa kuelekea kwenye kiota chake kitakatifu na cha milele. . . .**
>
> **"Mshumaa wa milele unawaka katika utukufu wake mtupu. Tazama jinsi ulivyoteketeza kila utando wa umauti. Enyi wapenzi mfananao na nondo wa mwangaza Wake! Kabilianeni na kila hatari, na zitoeni wakfu roho zenu kwenye mwale Wake uteketezao. Enyi wenye kiu Naye! Jivueni kila huba ya kidunia, na harakieni kumkumbatia Mpendwa wenu. Kwa shauku kubwa ambayo hakuna awezaye kuifikia harakieni kufika Kwake. Ua, ambalo lilikuwa limefichwa hadi sasa kutoka macho ya watu, limefunuliwa mbele ya macho yenu. Katika wangavu dhahiri wa utukufu Wake, Yeye husimama mbele yenu. Sauti Yake huziita nafsi zote takatifu na zilizotakasika kuja na kuungana Naye. Ni mwenye furaha yule**

**ambaye hugeukia hapo; heri ni yake yule ambaye ameufikia, na kuutazama mwanga wa wajihi wa ajabu kama huo.”[3]**

Lazima uhisi kwa hakika moyoni mwako kwamba wale unaosoma nao kozi wana mvuto wa kiasili kwa uzuri. Ikiwa wakati wa mafunzo yao ya kozi za taasisi, wanasaidiwa kuuona utukufu wa Ufunuo wa Mungu na kuutambua uzuri wa Neno lililofunuliwa, furaha watakayoihisi katika kila kipindi itakuwa chanzo kikubwa kabisa cha hamasa kwao. Kadiri unavyotafakari juu ya jambo hili, utaona inafaa kupitia Kitabu cha 1 na kuchagua sehemu tatu au nne ambazo zilikupa vianga vya Uzuri wa Mpendwa.

1. ______________________________

2. ______________________________

3. ______________________________

4. ______________________________

## SEHEMU YA 8

Maana ya kina na uzuri wa Neno lililofunuliwa, zilizomo katika vifungu vingi vilivyonukuliwa katika nyenzo, zitakuwa chanzo chenye nguvu kabisa cha mvuto kwa washiriki. Lakini mazingira ambayo washiriki huyatengeneza katika kikundi cha mafunzo, kwa msaada wa mkufunzi, pia yatakuwa muhimu. Mvuto kwa uzuri ni nguvu inayotoka ndani ya kikundi cha watu wanaofanya kazi pamoja katika mazingira yenye upendo. Hivyo, wakati wote utahitaji kutambua mazingira ya kikundi cha mafunzo na kuhakikisha kwamba yanachangia kwa ajili ya uinuaji wa kiroho wa washiriki.

Jambo moja muhimu litakuwa mazingira ambamo kikundi hukutana. Kwa bahati mbaya, katika ulimwengu wa leo, uzuri wa kimwili aghalabu unahusishwa na utajiri. Lakini mandhari yenye anasa siyo kitu kinachohitajika. Uzuri umo katika mazingira ya asili, katika mpangilio, katika unadhifu. Utataka kuhakikisha kwamba mazingira ambamo kila kikundi hujifunzia ni yale ambayo hukidhi shauku ya mtu kwa uzuri na ukamilifu, iwe kikundi kinakaa chini ya kivuli cha mti au hukutana katika sebule iliyopambwa kwa gharama, kibanda cha kawaida au katika jengo la taasisi.

Mwenendo wako mwenyewe ni jambo lingine litakalochangia kwenye mazingira. Mwenendo unaweza kuwa mzuri na, kwa hiyo, unaweza kuwa na uwezo wa kuvutia. Kuna uzuri katika wema, katika upole, katika heshima kwa wengine. Ili kulitazama zaidi jambo hili, fikiria matukio mbalimbali ambapo hisia yako ya uzuri ilifedheheshwa. Inasikitisha kwamba, hili mara nyingi hutokea mahali pa kazi, sehemu za starehe, katika mikusanyiko ya marafiki, katika mikusanyiko ya kifamilia, na hata katika taasisi za kielimu. Mifano ya aina hii ya mwenendo hujumuisha:

- Watu kupigizana makelele
- Watu kutumia lugha yenye kuudhi
- Mtu kumwaibisha mtu mwingine mbele ya wengine
- Watu kuwatazama na kuwatendea wengine kana kwamba ni vyombo vya ngono
- Watu kutenda kazi kwa uraibu wa vilevi

Ni vigumu kudhani kwamba mwenendo mbaya uliotajwa hapo juu ungeweza kuoneshwa na washiriki wa kikundi cha mafunzo. Lakini mkufunzi atapaswa kuwa makini juu ya aina ya mwenendo wa kichinichini zaidi ambao ungeweza kudhoofisha mazingira ya wema wa upendo. Hapa kwa mfano, kuna baadhi ya hali ngumu. Kwa kila moja, umepewa jibu lisilofaa, ambalo unaombwa kulisahihish.

a. Mmoja wa washiriki amejibwaga na kuchorachora juu ya nyezo zake. Jibu lisilofaa lingekuwa: “Unakuwa mzembe na unaliangusha kundi lote”. Wewe ungesema:

________________________________________

________________________________________

________________________________________

b. Mmoja wa washiriki huzungumza kwa sauti ya chini sana kiasi kwamba ni vigumu kwa wengine kumsikia. Jibu lisilofaa lingekuwa: "Huwezi kuongea kwa sauti kubwa zaidi?" Wewe ungesema:

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

c. Mmoja wa washiriki hutoa jibu ambalo ni dhahiri si sahihi kwa swali. Jibu lisilofaa lingekuwa: "Kuna yeyote mwenye jibu sahihi?" Wewe ungesema:

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

d. Wawili kati ya washiriki hunong'onezana na kuchekecheka. Jibu lisilofaa lingekuwa: "Mngependa kushiriki nasi utani wenu?" Wewe ungesema:

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

e. Mmoja wa washiriki huuliza swali ambalo halihusiani na kile ambacho kikundi hujifunza. Jibu lisilofaa lingekuwa: "Hilo halina uhusiano na kile tunachokizungumzia." Wewe ungesema:

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

f. Wawili kati ya washiriki huanza kubishana juu ya zoezi mojawapo, kila mmoja akisisitiza kwamba maoni yake ndiyo sahihi. Jibu lisilofaa lingekuwa: "Nyamazeni. Ninyi nyote mmekosa." Wewe ungesema:

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

g. Mmoja wa washiriki hutoa jibu ambalo halikubaliani na nukuu inayosomwa. Jibu lisilofaa lingekuwa: "Huielewi nukuu unayoisoma?" Wewe ungesema:

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

h. Mmoja wa washiriki anatoka nje ya mada. Jibu lisilofaa lingekuwa: "Tafadhali zingatia mada." Wewe ungesema:

___

___

___

Inapendekezwa kwamba ukariri nukuu ifuatayo, iliyonukuliwa kutoka katika kifungu kikubwa zaidi kutoka kitabu cha *Mungu Yu* Nasi ambamo Shoghi Effendi huelezea vipengele vikuu vya Kitáb-i-Aqdas. Wakati unapofanya hivyo, tafakari juu ya jinsi utiifu kwa mafundisho yaliyoelezwa katika nukuu hii hauepukiki kwa ajili ya kujenga mazingira yafaayo ya kikundi cha mafunzo.

> **". . . Bahá'u'lláh huwasihi wafuasi Wake kuandamana, kwa moyo wa urafiki na upatano na bila ubaguzi, na wafuasi wa dini zote; huwaonya kujilinda dhidi ya kushupaa, uchochezi, kiburi, ugomvi na kushindana; huingiza juu yao usafi usio na mawaa, ukweli thabiti, ubikira usio na doa, uaminifu, ukarimu, usahihi, adabu, ustahimilivu, haki na kutopendelea: huwashauri kuwa kama vile 'vidole vya mkono mmoja na viungo vya mwili mmoja; huwataka kuinuka na kuitumikia Hoja Yake; na huwahakikishia msaada Wake usio na shaka."**[4]

## SEHEMU YA 9

Uchunguzi wetu katika sehemu nane za kwanza za kitengo hiki ulizungukia mada ya hamasa. Kwa udhahiri, katika majadiliano mafupi kama hayo, tusingeweza kutenda haki kwa mada hii muhimu. Kile ambacho tungeweza kufanya ni kuvifikiria vyanzo vichache vya hamasa kwa matumaini kwamba, kadiri tajiriba yenu iongekavyo, pole pole mtagundua siri za kudumisha kiwango cha juu cha shauku miongoni mwa wale ambao mnasoma nao kozi. Ili kuimarisha umaizi ulioupata hadi sasa, chukua muda kidogo kupitia sehemu zilizotanguia na kisha andika aya moja kuhusu hamasa kwa kutumia maneno na virai vifuatavyo: ya mpito: ya kudumu, furaha, usafi wa moyo, uelewa, kuendelea, Neno la Mungu, mazingira, chimbuko, kiu ya ujuzi, kufikia kwenye mwongozo usioshindwa wa Mungu, mvuto kwa uzuri.

___

___

___

___

___

___

___

___

___

___

___

## SEHEMU YA 10

Mada inayofuata ambayo tunapaswa kujadili ni ushiriki, ambayo kwa kawaida hufuatia wazo illilotangulia, kwa kuwa, ni pale tu wale wanaosoma kozi wakijishughulisha kikamilifu katika ujifunzaji ndipo watadumisha kiwango cha juu cha hamasa.

Aghalabu inasemekana kwamba kozi za Taasisi ya Ruhi ni shirikishi. Kuhusiana na hili, huenda mmekuwa mkisikia kirai "mbinu shirikishi". "Njia", "uendeaji", "mbinu", na "taratibu" ni maneno ambayo kwa kawaida hutumika katika nyanja mbalimbali, lakini, kwetu sisi ni muhimu kupata utambuzi wa maana ya maneno kama hayo katika muktadha wa elimu. Kile kinachopaswa kusisitizwa hapa ni kwamba lengo la kinsingi la Taasisi ya Ruhi kuhusu ushiriki, halipo kwenye kiwango cha mbinu na taratibu. Kile tunachokitafuta ni kwa mshiriki kuwajibika kwa ajili ya ujifunzaji wake mwenyewe. Hili linaweza kutokea hata pale ambapo mbinu za ujifunzaji, kusema kweli, siyo shirikishi. Mfano mmoja utasaidia kufafanua kipengele hiki. Hebu tuseme kuwa wewe unahudhuria mhadhara unaotolewa na profesa katika kongamano la mada inayokuvutia. Profesa huwasilisha mazungumzo marefu kiasi lakini anaeleza mawazo kikamilifu na kwa namna ya wazi na inayeleweka. Kutokana na wingi wa hadhira, msemaji anaweza kuchukua maswali machache tu, na haiwezekani kuwa na majadiliano yanayomhusisha kila mmoja. Kwa udhahiri njia iliyotumika katika tukio hili si shirikishi hasa. Walakini, wewe unajishughulisha kikamilifu katika ujifunzaji wakati wa mhadhara nzima kwa sababu una shauku ya kupanua uelewa wako mwenyewe juu ya mada zaidi ya kile ambacho tayari unakijua. Unasikiliza, unalifikiria kila wazo linalowasilishwa na msemaji, unapanga orodha ya maswali akilini mwako, na baadaye unatazama kupitia vyanzo kadhaa vya kuaminika ili kupata majibu.

Sasa fikiria maelfu kwa maelfu ya wanafunzi kote ulimwenguni ambao wamekaa darasani, wakiwa wamechoka, wakipiga miayo, wakiwasikiliza walimu wanaowahadhiri. Hii siyo taswira inayopaswa kuonekana katika kila shule, lakini kuna madarasa ya kutosha kama hayo, ambayo pengine umewahi kuona moja au mawili. Kuna tofauti gani kati ya hali hizo mbili, ambamo mbinu hiyo hiyo ya ufundishaji imetumika?

Tofauti, bila shaka, imo katika kiwango cha ushiriki. Katika kisa cha kwanza, unajihusisha kikamilifu. Profesa hutoa mhadhara, lakini wewe unawajibika na ujifunzaji wako mwenyewe. Unabeba jukumu la kuchunguza mawazo yaliyowasilishwa na, kwa maana hii, unashiriki kikamilifu katika shughuli hii ya kielimu. Kinyume chake kinatokea katika kisa cha pili. Wanafunzi ni watepetevu. Mwalimu, ingawa ni amilifu hushindwa kuhamasisha ushiriki wa wanafunzi.

Ulinganishaji huu mfupi wa hali hizi mbili za kielimu huweka wazi kile kinachomaanishwa kwa kauli kwamba mbinu ya Taasisi ya Ruhi ni shirikishi. Hii humaanisha kwamba, pale utakapokuwa unahudumu kama mkufunzi wa kozi, utawasaidia washiriki kuchukua umiliki wa elimu yao wenyewe. Katika saa mtakapokuwa mnasoma pamoja, akili zao zinapaswa kuwa zinashughulishwa kikamilifu katika uchunguzi wa maudhui yaliyowasilishwa, na kila mshiriki anapaswa ahisi hisia kali ya wajibu wa ujifunzaji wake mwenyewe.

Tofauti na mfano wa mahudhurio yako mwenyewe kwenye kongamano, haiyumkiniki kabisa kwamba kiwango kihitajikacho cha ushiriki kinaweza kupatikana katika kikundi cha mafunzo ikiwa wewe unawahotubia tu washiriki wake. Vitabu vya Taasisi ya Ruhi vitakupatia zana ambazo zitakuwezesha kuzingatia mbinu yake shirikishi.

Kabla ya kuendelea na majadiliano yetu juu ya mada hii, tunakuomba uvute taswira kadhaa akilini mwako na kuzifikiria katika muktadha wa kikundi cha mafunzo. Wakati hakuna taswira yoyote hapa chini zinazochora picha kamili za mtindo wa ufundishaji-ujifunzaji inayohitajika hapa, itakayokupatia umaizi unaofaa. Baadhi ya taswira hizi hazifai kabisa. Zifutilie mbali na toa sababu zako za kufanya hivyo. Kwa zile zinazobakia elezea ni kwa namna gani kila taswira hufaa.

a. Moto unaouchochea: ____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

b. Bilauri tupu ambazo unazijaza: ____________________________________

____________________________________________

____________________________________________

c. Akaunti za akiba katika benki ambamo unaweka fedha: __________________

____________________________________________

____________________________________________

d. Mishumaa unayoiwasha: ________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

e. Urafiki unaoulea: ___________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

f. Timu ambayo pamoja nayo unajenga kitu fulani: _______________________

____________________________________________

____________________________________________

g. Msingi wa jengo kubwa mnaouweka kwa pamoja: ____________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

h. Machimbo yenye vito vya thamani ambavyo unaving'arisha: ___________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

i. Mchezo wa mpira wa miguu ambapo wewe ni mwamuzi: ______________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

j. Shindano ambalo wewe ni mwamuzi: ___________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

k. Mimea unayoimwagilia: _____________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 11

Kile tulichosema kuhusu ushiriki humaanisha kwamba kila mtu anayehusika katika mchakato wa kielimu unaoelewa na kozi za Taasisi ya Ruhi lazima awajibike kikamilifu katika ujifunzaji wake mwenyewe. Pia tumeonesha kwamba vitabu vyake vitakupa zana ambazo zitakuwezesha wewe kama mkufunzi kufuata mbinu yake shirikishi. Tunapaswa kugeuzia umakinifu wetu, kwa hiyo, kwenye usomaji wa vitabu na kujaribu kupata umaizi kuhusu jinsi mkufunzi anavyoweza kulea aina ya mitindo iliyotazamiwa ya ufundishaji-ujifunzaji.

Kwanza, ni lazima iwe wazi kwako kwamba uhusiano kati ya mkufunzi na washiriki wengine siyo ule wa mwalimu na mwanafunzi. Lakini hii haimaanishi kwamba yeye anaweza kuwa mwezeshaji aliyejitenga na mtepetevu wa majadiliano. Wakati wote, mkufunzi anapaswa awe macho, makini na mchunguzi. Fikra zake wakati wote zinapaswa zielekezwe juu ya jinsi ya kumsaidia kila mshiriki kupata uelewa kamili zaidi wa kile kinachosomwa.

Wakati wa kuanza masomo ya kitengo chochote pamoja na kikundi, mkufunzi ataanza kwa kuelezea kusudi lake, aghalabu akitilia mkazo dhana muhimu ambazo kinagusa. Kisha washiriki watasoma na kujadili kila sehemu, wakifanya mazoezi yanayo ambatana nayo, kama mtu mmoja mmoja au kama kikundi. Kwa hakika, mazoezi haya hufanyiza zana muhimu katika kukuza uelewa na katika kuwasaidia washiriki kujihusisha na mchakato wa ujifunzaji.

Wakati baadhi ya mazoezi yanaweza kufanywa kwa msaada mdogo wa mkufunzi, kutakuwa na nyakati ambapo yeye atahitaji kutoa maoni ya kuwasaidia washiriki kuimarisha

uelewa wao wa dhana. Dondoo ifuatayo kutoka sehemu ya "Mawazo Machache kwa ajili ya Mkufunzi" wa Kitabu cha 1 hutoa mwanga juu ya jinsi mazoezi yanavyopaswa kuendewa:

> Kwa vyovyote mazoezi katika kitengo hiki yanajaribu kujumuisha upana wa maana zilizomo katika aya inayojadiliwa. Swali moja ambalo kila mkufunzi lazima alitafakari ni kwa kiasi gani majadiliano yanapaswa yafanyike katika zoezi lolote husika. Hapa ni muhimu kukumbuka kwamba kurefusha majadiliano kwa kutambulisha dhana nyingi zinazohusiana lakini zipo nje, kunaweza kupunguza ufaaji wa zana. Kila kikundi kinahitaji kuanzisha mdundo ufaao wa maendeleo; washiriki wanapaswa wahisi kuwa wanaendelea kwa uthabiti kufuatana na uwezekano wao wenyewe. Mkufunzi, hata hivyo, lazima awe makini, ili baadhi ya sehemu zisije zikapitiwa kwa haraka na kijuujuu bila uchambuzi makini wa mazoezi; vikundi vilivyoendeshwa kwa namna hii, kwa kujaza tu majibu, kamwe havikupata matokeo ya kudumu.

Ni mielekeo gani miwili ambayo mkufunzi anapaswa aiepuke wakati akikisaidia kikundi kupitia kila sehemu ili kuhakikisha kwamba kusudi la nyenzo linafikikiwa?

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

Kile kinachoweza kukusaidia sasa ni kuchagua sehemu chache za vitengo vitatu vya Kitabu cha 1 na kupitia mazoezi. Amua ni sehemu zipi zinaweza kuvutia majadiliano ambayo yangeweza kuhitaji mwongozo kutoka kwako kama mkufunzi. Ziandike hapa chini.

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

## SEHEMU YA 12

Ili kuweka wazi baadhi ya mambo yanayojadiliwa, hebu tutazame maongezi ya kubuni kati ya mkufunzi ambaye anakusaidia kusoma Kitabu cha 7 na mmoja wa washiriki wakati wa mapumziko.

– *Mshiriki: Naanza kuelewa dhana ya ushiriki katika namna mpya. Hapo mwanzoni nilidhani njia ya kusoma kozi za taasisi ilikuwa rahisi tu kwamba washiriki wa kikundi cha mafunzo wangesoma vifungu kutoka katika Maandiko, kujibu baadhi ya maswali, na kisha kwa zamu kuelezea maoni yao binafsi.*

– *Mkufunzi: Pia nimewahi kusikia hapo zamani maelezo yaliyorahisishwa mno kama hayo. Kwa bahati mbaya hii hutoa picha ya kwamba ushiriki ni aina fulani ya fomyula.*

– *Mshiriki: Lakini mara baada ya kuingia katika mchakato wa taasisi, mtu hutambua kwamba kuna mambo mengi zaidi katika njia hii kuliko mtu anavyofikiria mwanzoni.*

– *Mkufunzi: Bila shaka, ukweli ni kwamba, nyenzo tunazojifunza hutegemea sana juu ya Maandiko ya Kibahá'í na huweka msisitizo mkubwa juu ya usomaji na uelewa wa vifungu kutoka katika Maandiko. Pia ni kweli kwamba maswali na mazoezi huwahitaji washiriki wajadili juu ya mawazo husika miongoni mwao wenyewe.*

– *Mshiriki: Lakini baadhi husema kwamba majadiliano hayapaswi kuhamasishwa — kwamba, katika jitihada ya kuendelea kuwa waaminifu kwa nyenzo, tunapaswa kumwambia kila mtu ajibu maswali na kisha aendelee na yanayofuata. Sasa naona, kwamba kusudi la mazoezi haliwezi kufikiwa kama yakichukuliwa tu kama karatasi za kufanyia kazi. Pale ambapo majibu ya maswali mengi, kijuu-juu huonekana kuwa rahisi, yanapaswa kuvutia kiwango fulani cha fikra na tafakari kutoka kwa kila mshiriki.*

– *Mkufunzi: Upo sahihi kabisa. Ndiyo maana mkufunzi anahitaji kuwa makini hasa. Yeye anapaswa kuwa na utambuzi fulani wa kile kinachomaanishwa kufikiwa kwa kupitia kila sehemu za kitengo husika na, katika muda muafaka, anzisha majadiliano miongoni mwa washiriki, ukiwasaidia kutafakari zaidi juu ya matumizi na maana za dhana na mawazo yaliyowasilishwa. Baadhi ya mawazo pengine.*

– *Mshiriki: Mara chache, wakati wa kusoma kozi, nimegundua kwamba baadhi ya mazoezi yanafanyika kwa kiwango fulani cha ung'ang'anivu. Kwa mfano, kulikuwa na msisitizo juu ya kutoa jibu sahihi la "ndiyo" au "hapana" katika mazoezi yanayotutaka tuchague kutoka katika orodha ya zile kauli ambazo ni za kweli.*

– *Mkufunzi: Pale ambapo jibu la zoezi kama hilo halipo wazi, limewekwa hivyo kwa makusudi ili washiriki, kupitia majadiliano na tafakari, wapata umaizi katika masuala tata kwa mujibu wa Maandiko. Tena, mkufunzi lazima ahamasishe uchunguzi.*

– *Mshiriki: Nadhani kama mkufunzi mpya, mwanzoni naweza kuwa mwoga wa kufanya kazi hii, nikichelea kuwa majadiliano yaneweza kuwa shaghalabaghala, na huenda nisiweze kuyaongoza ipasavyo au kujibu maswali wanayoweza kuuliza.*

- *Mkufunzi: Ni kawaida kabisa kujihisi hivyo, lakini nakuhakikishia kwamba kadiri unavyoendelea kupata tajiriba ndivyo utakavyojifunza kuwasaidia washiriki kujihusisha katika ushauriano wenye nidhamu. Wataona kwamba uwasilishaji tu wa mawazo yasiyo na mpangilio hauongezi uelewa. Utajifunza kuongoza majadiliano bila kuwa mng'ang'anivu mno. Ni sawa kwa watu waseme wanachotaka, japokuwa wakati mwingine michango yao itakuwa haina uhusiano na ushauriano. Walakini, ikiwa utaona kikundi kinatoka nje kabisa ya mada na kwa muda mrefu sana basi hapo utahitaji kuwasaidia marafiki zako kurejea kwenye ujifunzaji wa nyenzo. Hili kwa kweli halitakuwa gumu sana, kwa sababu, uhusiano wako na kikundi utakuwa umeegemezwa kwenye adabu na wema.*

- *Mshiriki: Lakini haitakuwa rahisi wakati wote. Katika kikundi cha mafunzo nilichoshiriki, wakati mwingine kulikuwa na watu ambao hawakuweza kuacha kuongea. Halafu kulikuwa na wengine wachache ambao kamwe hawakusema neno lolote.*

- *Mkufunzi: Bila shaka, suala hasa siyo urefu au ufupi wa mchango wa mtu juu ya majadiliano, bali, kama mawazo yaliyoelezwa yanaongeza uelewa wa pamoja wa kikundi. Unahitaji kuzingatia jambo hili. Licha ya hilo, ni muhimu kabisa kukumbuka kamwe usimwaibishe yeyote, yule msemaji sana au mkimya. Inadai uhakikishe kwamba usiwe mwenye kuhamaki kwa wale wanaochukua muda mrefu wa kikundi. Aghalabu wao huamini kwamba wanakisaidia kikundi kuendeleza majadiliano, na pengine hawatambui kama wanakwenda mbali mno. Bila shaka, wakati mwingine wanaweza tu kujiambatanisha mawazo yao wenyewe. Vyovyote iwavyo, kama umeanzisha fundo la upendo na urafiki na washiriki wa kikundi, utatafuta namna ya kurejesha mazungumzo na kuwaleta wengine katika majadiliano bila kuwafanya wale waongeaji kujisikia vibaya.*

- *Mshiriki: Na wale wakimya?*

- *Mkufunzi: Hiyo kwa kweli ni mada inayovutia sana. Unaona, wakati mwingine tunakuwa na mwelekeo wa kuweka umuhimu mkubwa sana kwenye kuzungumza. Kama mtu haongei, tunakuwa na wasiwasi. Hadi tunafikiria kwamba wale ambao ni wakimya au wenye aibu, hawana akili sana au kwamba hawasikilizi. Uongeaji siyo lazima uwe kiashiria cha ushiriki. Kama utakitazama kikundi, ambacho hata hivyo siyo kikubwa, utaweza kubaini nani anajishughulisha na ujifunzaji, nani anayesikiliza, anayefikiria, na anayefanya mazoezi kwa bidii. Washiriki wenye aibu wa kikundi, pole pole wataanza kujiamini na watashiriki katika majadiliano, lakini acha hili lijitokeze kiasilia.*

Ukiwa na majadiliano ya hapo juu akilini, andika katika nafasi hapa chini baadhi ya mawazo yako kuhusu nini humaanishwa kwa mkufunzi kuwa anayejihusisha kikamilifu katika kipindi chote cha mchakato wa ufundishaji-ujifunzaji.

________________________________________________________

________________________________________________________

________________________________________________________

________________________________________________________

## SEHEMU YA 13

Changamoto ya kuyadumisha majadiliano kwenye mwelekeo wakati huo huo mkisonga mbele kwa mwendo thabiti siyo rahisi, na utaimarisha uwezo wako wa kufanya hivyo kadiri unavyoendelea kupata tajiriba ya kivitendo. Hapa chini kuna baadhi ya hali. Majibu mawili yaliyopendekezwa katika kila hali, zote mbili ni sahihi, lakini katika hali tofauti. Eleza hali ambamo kila jibu lingefaa zaidi. Je, unaweza kufikiria jibu lingine ambalo lingeweza kufaa zaidi kufuatana na hali hizo?

1. Unamuomba mmoja wa washiriki kutoa mawazo machache juu ya swali, lakini yeye anachukua muda mrefu kujibu.

   a. Unasubiri kwa utulivu hadi mwishowe anajibu:

   b. Unalielekeza swali hilo kwa upole kwa mshiriki mwingine, ukimuomba mawazo yake:

   c.

2. Mmoja wa washiriki daima ni wa kwanza kujibu maswali, na kufanya iwe vigumu kwa wengine kuongea.

   a. Unayaelekeza baadhi ya maswali kwa mshiriki mmoja mmoja wa kikundi, ukimuita kwa jina:

b. Wakati fulani, unapokuwa nje ya kikundi na una mazungumzo ya kirafiki na mshiriki, unamuuliza amepata umaizi gani kwa kusikiliza michango waliyoitoa wengine katika majadiliano:

______________________________

______________________________

______________________________

c. ______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

3. Mmoja wa washiriki hajachangia katika majadiliano kwa muda kirefu.

a. Unapobaini kuwa mshiriki ana kitu cha kusema, unamuuliza swali la moja kwa moja:

______________________________

______________________________

______________________________

b. Unamuacha mshiriki huyo peke yake, ukimruhusu kukaa kimya kwa muda wote anaotaka:

______________________________

______________________________

______________________________

c. ______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

4. Katika kujibu mojawapo ya mazoezi, washiriki wachache huanzisha mawazo kadhaa yasiyo muhimu sana, na majadiliano yanaenda nje ya mada.

a. Unawasaidia washiriki kurejea kwenye mada inayojadiliano kwa kuwakumbusha kusudi la zoezi hilo:

______________________________

______________________________

______________________________

b. Unamuita mmoja wa washiriki ambaye anaonekana kuwa ameelewa vizuri kusudi la zoezi, na unamuuliza swali la moja kwa moja ili kukirudisha kikundi kwenye mada inayojadiliwa:

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

c. _______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

## SEHEMU YA 14

Majadiliano katika sehemu iliyotangulia yatakuwa yamekusaidia kuona kwamba hakuna fomyula yoyote kwa mkufunzi kufuata wakati wa kusoma vitabu vya Taasisi ya Ruhi pamoja na kikundi. Kwa kweli, kila mkufunzi lazima avipinge vishawishi vya kuupunguza usomaji wa kozi hadi kuwa mlolongo wa hatua rahisi za kufuatwa. Hii siyo rahisi sana pale tunapopewa mbinu za kiufundi zinazotuahidi utatuzi wa takriban kila aina ya changamoto tunazokabiliana nazo, zikiwemo pia zile zinazohusiana na elimu. Lazima tuwe waangalifu sana, kwamba, katika shauku yetu ya kukuza tajiriba ya ufundishaji-ujifunzaji, tusijeingiza bila kujua, mbinu na taratibu za ujifunzaji ambazo zitazuia jitihada za washiriki kujihusisha ipasavyo na nyenzo.

Urahisi wa kimsingi huainisha mchakato wa kielimu unaolelewa na kozi za Taasisi ya Ruhi. Mazingira yoyote ambamo nyenzo zake husomwa yanapaswa yatawaliwe na moyo wa urafiki na furaha. Katika uchambuzi wa mwisho, siyo kaida, taratibu na mbinu ambazo zitalea ujifunzaji bali ni hamasa za kutafuta ujuzi na kuhudumu.

Hayo hapo juu hayamaanishi kwamba hakuna mbinu fulani ambazo zinaweza kurahisisha mchakato wa ujifunzaji. Lakini "mbinu" haiwezi kuutawala mchakato. Wala kuweza kuruhusiwa kupuuzia utafutaji wa dhati wa uelewa au kulipunguzia hadhi Neno Takatifu, la muhimu sana kwa mchakato wa kielimu. Mazungumzo yafuatayo ya kubuni kati ya mtu anayehudumu kama mkufunzi wa Kitabu cha 7 na kikundi cha washiriki ambao wamesoma sehemu hizi hivi karibuni pengine yanaweza kukusaidia kubaini mitego inayoweza kuwepo na kujifunza kuepukana nayo:

– *Mshiriki wa 1: Inasaidia sana kujua kwamba hakuna kaida zozote au seti zilizowekwa za hatua za kufuatwa wakati wa kusoma kozi za Taasisi ya Ruhi. Kuna mambo niliyoyabaini kwa namna wakati mwingine usomaji wao unavyofanyika ambayo nilidhani ni sehemu ya "mbinu" za Taasisi, lakini sasa natambua kuwa siyo hiyo.*

– *Mshiriki wa 2: Kwa mfano jinsi kukariri kunavyofanywa wakati mwingine. Walimu wa madarasa ya watoto huwasadia watoto kukariri sala au nukuu kwa kutumia mbinu rahisi, ambayo watoto hurudia sentensi ya kwanza au kirai cha nukuu hadi wanaijua kimoyomoyo na kisha kuendelea kuongeza nyingine inayofuatia, na kwa namna hii*

*wanakariri nukuu nzima. Hiyo ni mbinu rahisi lakini inayofaa, na, kama vile mtu mzima, mimi aghalabu naitumia kukariri vifungu virefu kutoka katika Maandiko. Lakini, baadaye, niliona kuwa nguvu nyingi zinaweza kutumika kutafuta mbinu inayoweza kuwasaidia washiriki kukariri nukuu na wakati huo huo "wakifurahia".*

– *Mshiriki wa 3: Kwa mfano, mimi nimeona kuwa wakati mwingine mkufunzi huandika nukuu nzima ubaoni na kumuomba mshiriki mmoja asome kwa sauti. Kisha mkufunzi hufuta neno moja au zaidi, na mshiriki mwingine huisoma kwa kukumbuka maneno yanayokosekana. Mchakato huo huendelea hadi kubakia maneno machache sana. Njia hii ya kukariri inaweza kurefushwa pasipo na ulazima.*

– *Mshiriki wa 4: Nakumbuka kwamba nilipokuwa nasoma Kitabu cha 1, wote tuliambiwa kuchora mchoro kwa kila nukuu. Niwe mkweli, sikuelewa kusudi lake, na baadhi yetu hatukuifurahia shughuli hii, kwa kuwa ilileta ugumu zaidi kuimakinika na kuufuata mlolongo wa dhana. Badala yake, tungeendelea kwa kasi zaidi kupitia nyenzo hizo. Ilikuwa baada ya miezi mingi ndipo niligundua kuwa hiyo haikuwa sehemu ya mbinu za kusoma kozi.*

– *Mshiriki wa 2: Naweza kuona kwamba suala la "mbinu" siyo mara zote lipo wazi, na kama wakufunzi, tunahitaji kuwa na imani kwamba washiriki watapata furaha kutokana na jitihada ya dhati ya kutafuta uelewa. Kutokana na yote ambayo tumeyajadili katika sehemu hizi, inaonekana ni muhimu kwamba, katika shauku yetu kuwasaidia washiriki kujihusisha na mchakato wa ujifunzaji, hatuangukii kwenye shughuli ambazo hufuata kaida na ambazo mwishowe, zingedhoofisha ufanisi wa kozi.*

– *Mkufunzi: Ninyi nyote mmefikia hitimisho muhimu. Wakati ni kawaida kwamba baadhi ya wakufunzi wanaweza kujumuisha baadhi ya shughuli katika usomaji wa kozi, tunapozirejelea kama vipengele vya "mbinu ya Ruhi", huingiza ung'ang'anivu katika mchakato ambao vinginevyo ni rahisi sana, wenye furaha, na unajali anuai ya mahitaji. Bila shaka unatambua kwamba Taasisi ya Ruhi haiwezi kutoa mfuatano wa mambo ya kufanya na ya kutofanya kwa sababu hii, yenyewe, ingesababisha ung'ang'anivu. Kwa hiyo, mengi yameachwa kwenye uamuzi wa mkufunzi wakati wa kuamua kile kinachochangia kuongeza uelewa, wakati huo huo kutoruhusu mbinu kufunika mambo ya msingi kabisa yaliyomo katika nyenzo inayoendelea kusomwa au kuzuia urahisi wa mchakato.*

## SEHEMU YA 15

Lazima iwe wazi kwako hadi sasa kwamba, mbali na uwezo wa kuongoza majadiliano, wakufunzi wanahitaji kuzifahamu vyema nyenzo zinazosomwa ikiwa wanataka kuwasaidia washiriki kuendeleza uelewa wao wa maudhui na katika kuchukua umiliki wa ujifunzaji wao wenyewe. Bila shaka, wewe mwenyewe umemaliza vitabu sita vya kwanza vya Taasisi ya Ruhi kwa msaada wa mkufunzi na kupata tajiriba kubwa wakati wa kutekeleza vitendo vya huduma vilivyoshauriwa—hii, kama sehemu ya kiini kikuacho cha watu binafsi katika kijiji au ujirani wako wanaofanya kazi kwa ajili ya usitawi wake. Sasa, walakini, kama mkufunzi mwenye shauku, unahitaji kwenda mbele zaidi na kutafakari juu ya baadhi ya dhana kuu na kanuni zilizowekwa ambazo zimesaidia kuunda maudhui ya kozi. Kwa kuanza, soma dondoo ifuatayo kutoka katika maneno ya utangulizi yaliyotolewa kwa wakufunzi wa Kitabu cha 1:

> Tangu mwanzoni, sharti iwe dhahiri kwa kila mshiriki kwamba kozi za Taasisi ya Ruhi huchora njia ya huduma kwa wanadamu, ambayo juu yake kila mmoja wetu anaweza kutembea kwa hatua yake mwenyewe, akiwasaidia na akisaidiwa na wengine. Kukanyaga njia hii humaanisha uendelezaji wa kusudi la kimaadili lenye pande mbili: kufikia ukuaji wa kiroho na kiakili wa mtu mwenyewe na kuchangia kwenye mabadiliko ya jamii. Maendeleo katika njia hii huhuisha ukuzaji wa idadi fulani ya stadi zinazohitaji uelewa na ujuzi, sifa za kiroho na mielekeo istahiliyo sifa, hali kadhalika vipawa vingi na stadi. Vyanzo vya ujuzi ambavyo kwavyo vitabu vya Taasisi huchota, kwa upande mmoja, ni mafundisho ya Imani ya Kibahá'í na, kwa upande mwingine, tajiriba iliyokusanywa ya jumuiya ya Kibahá'í ulimwenguni kote katika kuendeleza ustaarabu wa kimwili na kiroho. Ni muono wa Bahaullah wa aina ya watu tunaoweza kuwa na wa ustaarabu tuwezao kuujenga ndiyo unaoivuvia Taasisi.

Mwanzoni mwa kitabu hiki ulipata fursa ya kuchunguza asili ya kiroho ya njia ambayo umekuwa ukiikanyaga kwa muda sasa. Wakati wote huo, uendelezaji wa kusudi la maadili lenye pande mbili umeimarisha hatua zako na kuchapuza juhudi zako kwenye huduma. Umejionea mwenyewe jinsi uwezo wa kuhudumu unavyoongezeka kadiri mtu anavyopiga hatua katika njia hii na amepata umaizi mwingi wenye thamani sana katika nguvu ya mabadiliko ya mtu binafsi na ya pamoja.

Ni muhimu kutanabahi hapa kwamba, katika jitihada ya kuandaa kozi ambayo ingeweza kukuza ndani ya watu binafsi uwezo unaohitajika, Taasisi ya Ruhi hapo awali ilikuwa na idadi kadhaa za machaguo. Kwa mfano, ingeweza kuchukua njia iliyozoeleka zaidi ya programu za kujiimarisha za Kibahá'í—yaani, zile za kumpatia mwanafunzi ufahamu wa kutosha wa Imani: kanuni zake, mafundisho yake ya kiroho na ya kijamii, historia yake, sheria zake na utawala wake. Kisha ingetarajiwa kuwa ufahamu huu wenyewe, ungewapa hamasa watu binafsi kuinuka na kuitumikia Hoja. Kile ambacho kingeweza kuongezwa ni mafunzo machache ya stadi maalum, ambayo yangeimarishwa na uhamasishaji wa mara kwa mara.

Baada ya kuchunguza njia kadhaa mbadala kama hizo, Taasisi iliamua kwamba ingechukua njia ya kielimu ambamo mafunzo na vitendo vinaunganishwa. Taasisi iliamini kwamba ni kupitia muungano wa ujuzi na utendaji kwamba uwezo kwa ajili ya huduma kwa Hoja na wanadamu ungeweza kujengwa. Hususan, hakuna njia inayotafuta kukuza uwezo wa kuathiri aina ya mabadiliko ya mtu binafsi na ya pamoja yaliyotazamiwa katika Maandiko ya Kibahá'í ambayo ingeweza kupuuzia umuhimu wa vitendo katika kukuza uelewa. Usomaji pekee—utafutaji wa ujuzi nje ya uga wa huduma—usingetosheleza.

Ni kawaida kwamba, msisitizo mkubwa ungehitaji kuwekwa juu ya usomaji wa vifungu kutoka katika Maandiko. Lakini msisitizo huo huo ungepaswa utolewe kwenye utumiaji wa mafundisho ya Kibahá'í katika maisha ya mtu mwenyewe na kwa maisha ya kijiji au ujirani wake. Mchakato wa kielimu siyo tu ungehitaji kuwaunganisha washiriki na Ufunuo wa Bahá'u'lláh bali pia na tajiriba ya Kibahá'í katika kuyatumia mafundisho na kanuni za Imani. Zaidi ya hapo, ungehitaji kuhakikisha kwamba washiriki wanachangia kwenye ukunjukaji zaidi wa tajiriba hii na kwenye uenezaji wake.

Hatimaye Taasisi ya Ruhi ilichukua kanuni za ufundishaji ambazo wakati huo huo zingesimamia maarifa na tabia, stadi na vipawa, mielekeo na sifa za kiroho ambavyo vingepatikana hatua kwa hatua na wale wanaopenda kutoa nguvu zao kwa ajili ya maendeleo ya jumuiya zao. Dhana ya "uwezo", ambayo ilileta pamoja mahitaji haya, hivyo ilianza kuibuka. Ili kuongeza uwezo wa idadi iongezekayo ya watu kuitumikia Hoja na wanadamu, Taasisi ya Ruhi iliamua kupangilia kozi zake katika mlolongo ulioelezewa kama "njia ya huduma". Taasisi ilihisi kwamba, kwa jinsi hii, ingewasaidia washiriki kujifunza kuhusu njia za mabadiliko ya mtu binafsi na ya pamoja kadiri waitembeavyo kutekeleza vitendo mahsusi vya huduma.

Njia hiyo ingepaswa kuwekwa wazi kwa namna ambayo washiriki wangeweza kuendelea hatua kwa hatua kwenye njia hiyo kadiri wakuzavyo uwezo wao kwa ajili ya huduma. Vivyo hivyo, vitendo vya huduma vingepaswa kuimarishana, vikiongeza utata kutoka kozi moja hadi nyingine. Na, popote watu binafsi wajikutapo kwenye njia ya huduma, pia wangeambatana na wengine mapema zaidi kwenye njia hiyo hiyo katika juhudi zao, wakiwasaidia kuendelea. Hii, ilikuwa dhahiri kwamba, ni asili ya mchakato wa kujenga uwezo. Wale wenye tajiriba zaidi huwasaidia wale wenye tajiriba kidogo kadiri wanavyojitahidi kutembea katika njia na kujifunza, kadiri wakati upitavyo, kuwasaidia wengine.

Inaweza kuwa msaada kwako kusita kidogo hadi hapa na kujadili pamoja na kikundi chako mawazo yaliyoorodheshwa hapa chini. Kisha andika mawazo machache kwa kila moja. Kadiri muda upitavyo utaweza kuona jinsi uelewa wako wa mawazo haya utakavyoendelea kukua.

a. Umuhimu ambao kozi hutoa kwa uelewa wa Ufunuo wa Bahá'u'lláh na utumiaji wake katika maisha ya mtu binafsi na ya pamoja: ___________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

b. Nafasi ya vitendo, ikijumuishwa na ujifunzaji, katika kukuza uelewa: __________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

c. Ukuzaji wa uwezo kwenye njia ya huduma: ________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

d. Mchakato wa mabadiliko ya mtu binafsi na ya pamoja unaokuzwa na njia ya huduma iliyowekwa wazi na kozi: ________________________________________

## SEHEMU YA 16

Ili kuchunguza zaidi jinsi mbinu ya kielimu iliyojadiliwa hapo juu na dhana zilizomo ndani mwake ilivyozipatia umbo nyenzo za Taasisi ya Ruhi, tutatazama njia ya huduma iliyowekwa wazi na kozi sita za mwanzo, ambazo unazifahamu vyema. Ili kufanya hivyo, tutaangalia kirai, "Natembea njia ya huduma." Ni upi utambulisho wa kweli wa "Mimi" katika sentensi hii? Ni nini asili ya njia, na kuitembea kunamaanisha nini?

Kitabu cha 1 huongelea swali la kwanza kati ya haya. Vipengele vitatu vya utambulisho wa kweli wa mtu zinachunguzwa: "Uhalisia wa uwepo wangu ni roho yangu ambayo hupita katika ulimwengu huu kupata sifa inazozihitaji kwa ajili ya safari ya milele na tukufu kuelekea kwa Mungu. Nyakati zangu ninazozipenda sana ni zile ninazozitumia kuongea na Mungu, kwa kuwa ibada ni chakula cha kila siku ambacho roho yangu lazima ipokee kama inataka kutimiza kusudi lake lililotukuka. Kazi yangu kubwa ni kujifunza Ufunuo wa Bahá'u'lláh, nikiimarisha uelewa wangu wa mafundisho ya Mungu kwa ajili ya zama hizi, na kujifunza kuyatumia maishani mwangu na katika maisha ya jumuiya." Ili kujenga utambuzi kwamba hivi ndivyo, kwa kweli, vipengele vya utambulisho wa kweli wa mtu ndiyo lengo la *Mawazo juu ya Maisha ya Roho.*

Tayari unatambua, bila shaka, kwamba mawazo matatu yaliyotajwa hapo juu kwa kweli yanatendewa kinyume na mpangilio uliomo katika kitabu hicho. Taasisi imegundua kwamba, huu, hujenga muono wa maisha ambayo yamejikita juu ya Mungu na Ufunuo Wake, badala ya mtu mwenyewe. Maoni na mazoezi katika sehemu hii na sehemu zingine mbili zinazofuatia vitakusaidia wewe na washiriki wengine wa kikundi chako katika uchunguzi wenu wa mada hii.

Kitengo cha kwanza cha Kitabu cha 1, "Ufahamu wa Maandiko ya Kibahá'í", hulenga juu ya kauli ya sentensi moja kutoka Maandiko. Kama ilivyooneshwa hapo mwanzo, katika Sehemu ya 5, mkazo upo kwenye maana ya papo hapo ya kila kauli na matumizi yake ya moja kwa moja juu ya maisha ya mtu, hali kadhalika maana pana zaidi. Zaidi, kuna msisitizo wa kuyaweka majadiliano kwenye kiwango fulani cha "urahisi". Urahisi, walakini, haumaanishi ukosefu wa kina. Wala haimaanishi kuwa mada tata zinapunguzwa kuwa mawazo machache rahisi. Ili kulitambua hili, jaribu kuelezea aina nne zifuatazo za nyenzo za kielimu na baadhi ya athari zake kwa wanafunzi:

a. Rahisi na ya kijuujuu

b. Rahisi na ya kina

c. Tatanishi na ya kijuujuu

d. Tata na ya kina

Kwa nini, tunaweza kuuliza, mbinu ya moja kwa moja ya kujifunza Maandiko yaliyowasilishwa katika Kitabu cha 1 inasaidia sana kwa wale wanaoanza njia ya huduma? Jibu moja lingekuwa kwamba wao wanatambua zaidi thamani ya tafakari ya kina ya kile wanachosoma kutoka katika Maandiko. Wanaanza kuona jinsi, kadiri wajengavyo tabia ya kusoma na kutafakari juu ya vifungu kutoka katika Maandiko kila siku, mafundisho huendelea kubumba fikra na vitendo vyao.

Hapo chini kuna seti mbili za kauli. Kauli zilizopo katika safu ya kwanza huelezea mielekeo ambayo, ingawa haipendezi, ni ya kawaida. Zile zilizopo katika safu ya pili zina malengo yanayotamaniwa kufikiwa. Katika kutembea njia ya huduma, kila mmoja wetu anajongea kuelekea malengo haya. Chora mshale kutoka kwenye kila kauli katika safu ya kushoto na ile ya safu ya kulia kuonesha mjongeo huu.

| | |
|---|---|
| Mitazamo yetu juu ya ulimwengu hubumbwa na maoni ya mpito tu. | Maamuzi hufanywa kufuatana na mafundisho ya Imani. |
| Ni vigumu kwetu kutofautisha kati ya mema na mabaya, sahihi na kosa; yote huonekana yanalingana. | Mahitaji na matarajio ya mtu binafsi hupatanishwa na yale yanayochangia kwenye usitawi wa wote. |
| Dhana yetu ya uhuru hutufanya tuwe wenye hadhari na kwa chochote ambacho huweka mipaka juu ya kile tunachosema na kufanya. | Kiwango cha Imani mara kwa mara hutumika kupima thamani ya maneno na vitendo. |
| Maamuzi yetu hutegemea kabisa juu ya hisia za wakati huo. | Muundo unaovuviwa na Ufunuo wa Bahá’u’lláh huundwa |

Ni vigumu kuzizuia zile jumbe zinazotuambia kwamba tunapaswa tufuate kila tamaa zetu, bila kujali athari zake.

Maslahi yetu wenyewe hupewa kipaumbele zaidi kuliko usitawi wa wote.

ambamo kwamo ulimwengu hutazamwa.

Inatambulika kwamba uhuru wa kweli unapaswa upatikane kwa kuyakabidhi mapenzi ya mtu kwenye Mapenzi ya Mungu.

Utambuzi wa athari za kuendekeza tamaa za mtu huchochewa, kama ilivyo nidhamu ya kutenda kwa namna ambazo huwiana na hadhi ya daraja la mwanadamu.

## SEHEMU YA 17

Kitengo cha pili cha Kitabu cha 1 kinalenga kukuza uelewa wa umuhimu wa sala na kuwasaidia watu binafsi kukuza mazoea ya kusali mara kwa mara. Tangu ulipoanza njia ya huduma, bila shaka umeimarisha mazoea haya katika maisha yako mwenyewe na umechukua fursa za kushiriki sala pamoja na wana-kaya ndani ya kijiji au ujirani wako na umefanya kila jitihada kuimarisha hali ya kiibada ya jumuiya yako. Hadi kufikia hapa, ingekuwa yenye manufaa kwako kusoma dondoo ifuatayo kutoka "Mawazo Machache kwa ajili ya Mkufunzi" katika Kitabu cha 1 na kupitia kitengo hicho pamoja na mawazo yaibukayo akilini:

> Kitengo cha pili cha kitabu hiki kinahusiana, kama kile cha kwanza, na mazoea ya lazima kwa maisha ya kiroho: kusali mara kwa mara. Huweka wazi katika sehemu ya ufunguzi dhana ya "njia ya huduma", kikipendekeza kwamba, kutembea njia hii, lazima tujazwe na kusudi lenye pande mbili. Washiriki huchunguza seti ya nukuu zinazotoa umaizi katika asili ya kusudi hili, mada ambayo itaelezwa katika kozi za siku zijazo.
>
> Katika muktadha wa mada hii kitengo huanza uchunguzi wake wa umuhimu wa sala. Kinachukua njia inayofanana na ile iliyoelezwa katika aya zilizotangulia. Maswali na mazoezi yameandaliwa ili kukuza uelewa wa maana ya vifungu kutoka katika Maandiko yanayosomwa. Kadiri kikundi kinavyoendelea kupitia kitengo hicho, mkufunzi atatakiwa kuondoa shaka kwa kuchambua mawazo yaliyokita mizizi kwenye fasiri na mazoea ya wakati ulipita. Katika baadhi ya mila, kaida na desturi pole pole vimefunika umuhimu wa hali ya ndani, na nyingi sana zilipuuzia ulazima wa sala, ambayo, kwa roho ya mwanadamu, ni ya muhimu kama kilivyo chakula katika kurutubisha mwili.
>
> Juu ya yote, hivyo, kitengo kinalenga kuamsha ndani mwa washiriki shauku ya "kuzungumza na Mungu" na kumkaribia Yeye. Miongoni mwa mawazo

yanayoongelewa ni kile kinachomaanishwa kuingia katika hali ya sala, hali ya mioyo na fikra zetu tufanyapo hivyo, na hali zinazopaswa kutengenezwa katika mazingira yetu, iwe tupo peke yetu au katika mkusanyiko. Kwa hakika, baada ya kufikiria kidogo juu ya nguvu zinazofanyizwa kupitia ibada ya kiusharika, washiriki wanaombwa kufikiria kukaribisha mkusanyiko kwa ajili ya sala na ibada.

1. Kuna uhusiano gani kati ya sala, ukuaji binafsi na juhudi za kuchangia kwenye uboreshaji wa jamii ambao sehemu mbili za kwanza za kitengo huuanzisha?

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

2. Ni dhana zipi ambazo kitengo huwasaidia washiriki kuelewa kuhusu asili ya sala?

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

3. Ni zipi baadhi ya dhana potofu kuhusu sala zilizoenea katika jamii yenu ambazo usomaji wa kitengo hiki husaidia kuziondoa?

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

4. Tafakari juu ya maana ya kauli ya ‘Abdu’l-Bahá kwamba “Mtu lazima aishi katika hali ya sala.” Baini vile vifungu vilivyomo katika kitengo hiki ambavyo unahisi huchangia zaidi kwenye jitihada za washiriki kuifikia hali hii ya kuwa.

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

5. Inatumainiwa kuwa, baada ya kumaliza kitengo hiki, washiriki watafanya jitihada kuelekea usitawishwaji wa hali ya kiibada wa jumuiya yao—kwa mfano, kwa kuzitembelea nyumba kwa ajili ya kushiriki sala pamoja na wana-kaya, kwa kuusaidia kwa shauku mkusanyiko wa ibada katika kijiji au ujirani wao, na hatimaye kwa kukirimu mmoja wao wenyewe. Kwa jinsi hii, kitengo mara moja huwataka washiriki kutumia ujuzi walioupata siyo tu katika maisha yao wenyewe, bali pia katika maisha ya jumuiya yao—kupitia mfuatano wa vitendo vidogo ambavyo vitatoa msingi kwa ajili ya vitendo vya huduma watakavyoitwa kufanya hapo baadaye. Ili kufikiria kuhusu umuhimu wa kuwasaidia washiriki kutenda, mapema sana katika mchakato wa kielimu, tafakari juu ya kile kinachokunjuka katika kijiji au ujirani wako mwenyewedip amconsequis feuguer, heniamc eu ecte la etuerosto re elis ero hendrem in velesequipit.

a. Kushiriki sala na mtu fulani, ingawa huonekana rahisi, kwa kawaida siyo rahisi kwa washiriki. Ni ujifunzaji gani unapatikana katika kijiji au ujirani wako kuhusu kushiriki sala na marafiki na familia, na vijana na wazee na kutafakari juu ya maana zake?

b. Jinsi gani hatua hii ionekanayo rahisi, kadiri inavyotekelezwa na watu wengi zaidi na zaidi katika jumuiya, husababisha uanzishwaji wa nafasi ambapo idadi ikuayo huletwa pamoja kwa ajili ya ibada mazungumzo yainuayo?

c. Jinsi gani jitihada za kuwasaidia washiriki wa Kitabu cha 1 katika kushiriki sala na watu binafsi na familia zinavyoendelea katika Kijiji au ujirani wako?

d. Jinsi gani ungeieleza kuelezea hali ya kiibada ya jumuiya yako?

## SEHEMU YA 18

Sasa tutageuzia umakinifu wetu kwenye kitengo cha tatu cha Kitabu cha 1. Soma kila dondoo iliyopo hapa chini kutoka "Mawazo Machache kwa ajili ya Mkufunzi" na fanya mazoezi yanayofuata.

> Usomaji wa kitengo cha tatu cha kitabu, "Uhai na Kifo", inatumainiwa kwamba, utaimarisha kujidhatiti kutembea katika njia ya huduma na kuijalia maana ya kina zaidi. Huduma katika ulimwengu huu inaeleweka vyema zaidi katika muktadha kamili wa maisha, ambao huenda mbali zaidi ya uwepo wa kimwili na huendelea daima kadiri roho zetu zinavyoendelea katika malimwengu yote ya Mungu. Katika mchakato wa kielimu, tofauti na mafunzo ya kiufundi, washiriki wanapaswa kuendelea kuongeza ufahamu wa maana na umuhimu wa kile wanachokifanya. Ni pale tu ufahamu huu utakapokua, tajiriba huonesha, ndipo watakapojiona wenyewe kama "wamiliki" amilifu, wanaowajibika na ujifunzaji wao wenyewe.

1. Utambuzi kwamba uhai wa kiroho huendelea mbele zaidi ya huu wa kimwili huimarisha kujitoa kwetu kutembea katika njia ya huduma na hukijalia kile tunachofanya maana ya kina zaidi. Soma kauli zifuatazo, ambazo hupanua wazo hili, kisha andika mawazo mengine machache:

   – Utambuzi kwamba maisha hayajumuishi mabadiliko na nasibu za ulimwengu huu, hutusaidia kustahamili katika jitihada zetu, licha ya vikwazo ambavyo hatuna budi kukutana navyo katika njia ya huduma.

   – Kukumbuka kwamba maisha ya duniani ni awamu mojawapo tu ya safari yetu ya milele kumuelekea Mungu hutusaidia kuendelea kuwa makini juu ya ukuzaji wa sifa za kiroho ambazo hutuleta karibu zaidi Kwake na kujitoa wenyewe kuiendeleza jamii ya binadamu kuelekea hatma yake iliyokusudiwa.

   – ____________________

   – ____________________

   – ____________________

–

–

–

> Kila sehemu ya kitengo hiki hufunguliwa na nukuu moja hadi tatu kutoka Maandiko ya Kibahá'í, ikifuatiwa na mazoezi machache. Lugha ya vifungu vilivyonukuliwa katika kitengo hiki ni ngumu zaidi kuliko katika vile viwili vilivyotangulia. Hakuna haja, bila shaka kwa kikundi kupoteza muda kwenye maneno magumu; mkufunzi atahitaji kuhakikisha kwamba kila mmoja anapata wazo kuu linaloongelewa katika kila sehemu, jambo ambalo ndilo hasa mazoezi hujaribu kutoa.
>
> Kwa kuzingatia asili ya mada, mazoezi yanayohusu mifano halisi ni machache na nadra. Mengi sana yanafanya kazi kwenye kiwango cha kufikirika. Kile kinachopaswa kuzingatiwa ni kwamba baadhi ya maswali yaliyoulizwa katika mazoezi hayawezi kujibiwa haraka au katika njia iliyo wazi. Yanatambulishwa kwa ajili ya kuongeza utambuzi juu ya mada; Ikiwa washiriki watafikiria tu kuhusiana na maswali kama haya, lengo la ujifunzaji litakuwa limetimia.

2. Rejea kwenye kitengo hicho na pitia sehemu zake. Andika katika nafasi iliyotolewa, baadhi ya mawazo makuu yaliyotambulishwa.

3. Baini mazoezi machache katika kitengo hicho yanayoibua maswali ambayo hayasaidii kujibu maswali kwa uwazi. Mifano miwili imetolewa.

- Zoezi la kwanza la Sehemu ya 2: “Ni wakati gani roho ya mwanadamu hupata uhai wake?”
- Zoezi la tatu la Sehemu ya 5: “Je, unaweza kutoa mifano ya ushawishi na utendaji wa roho bila viungo vya mwili?”
- __________
- __________
- __________

Kwa nini ni muhimu kuepukana na majadiliano marefu juu ya aina ya maswali kama ya hapo juu, ambayo yamewekwa tu kuongeza ufahamu?

Sehemu kadhaa za mwanzo zinalenga juu ya uhusiano kati ya roho na mwili, ambavyo kwa pamoja, humfanya mwandamu katika ulimwengu huu wa uwepo. Wazo kuu lililowasilishwa katika sehemu hizi ni kwamba roho siyo kitu cha kimwili; uhusiano wake na mwili unaweza kulinganishwa na mwanga unaonekana ndani ya kioo. Si vumbi linalotanda uso wake wala uvunjikaji

wake huweza kuathiri mng’ao wa mwanga wenyewe. Kifo ni mabadiliko tu ya hali, pale muungano kati ya mwili na roho unapovunjika; baadaye, roho huendelea milele kuelekea kwa Muumba wake.

Baada ya hapo kitengo kinageukia suala la kusudi la uhai—kumjua Mungu na kufikia uwepo Wake. Majadiliano hapa huzungukia mada pana mbili. Ya kwanza ni kusudi la maisha yetu katika ulimwengu huu, na ya pili ni safari ya roho baada ya kifo. Roho ni ishara ya Mungu na inaweza kuakisi majina na sifa Zake zote. Walakini uwezo uliomo ndani ya mwanadamu umejificha; unaweza kukuzwa tu kwa msaada wa Wadhihirishaji wa Mungu, wale Viumbe waliotakasika Ambao huja kipindi hadi kipindi kuwaongoza wanadamu. Kupitia elimu ya kiroho Wanayoitoa, hazina zilizofichwa ndani mwetu, zinaweza kufunuliwa.

Kuhusiana na safari ya roho baada ya kifo, mfuatano wa mawazo umewekwa kwa ajili ya washiriki kutafakari: kwamba wale ambao ni waaminifu kwa Mungu watafikia kwenye furaha ya kweli; kwamba hakuna hata mmoja wetu awezaye kujua mwisho wake mwenyewe na, kwa hiyo, tunapaswa tusameheane na tusijikweza dhidi ya wengine; kwamba katika ulimwengu ujao, kama katika huu, roho itaendelea kwenda mbele na vipawa vya kiroho tulivyovikuza hapa vitatuauni na kutusaidia huko; kwamba tutawatambua wapendwa wetu katika milki za juu, tutayakumbuka maisha yetu katika ulimwengu huu, na tutafurahia urafiki na roho takatifu na zilizotakasika.

4. Aya tatu za hapo juu hutaja mawazo makuu ambayo tayari umeshayatambua kutokana na upitiaji wako wa kitengo hiki. Mawazo haya yanawakilisha kweli za kiroho, na mkufunzi anapaswa kuhakikisha kwamba washiriki hawakanganywi katika kufikiri kwao kwa kutoa tafsiri zisizo za lazima. Ukiwana hili akilini, tazama jozi hapa chini. Kwa kila moja, amua ni ipi mkufunzi anapaswa kuifanya, ikiwa anataka washiriki wapate uelewa wa dhana inayojadiliwa. Usiridhike tu na kuwekea alama chaguo, ambalo linaweza kuonekana la dhahiri, lakini andika mawazo machache kuhusu uamuzi wako.

_______ Ingiza katika majadiliano baadhi ya mawazo mengine kuhusu maisha baada ya kifo, yaliyomo katika utamaduni, ambayo aghalabu ni mada za uzushi

_______ Kaa mbali na baadhi ya mawazo mengine kuhusu maisha baada ya kifo yaliyomo katika utamaduni, ambayo aghalabu ni mada za uzushi

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

_______ Puuzia swali analouliza mshiriki kwa sababu linahusu wazo potofu, kama vile kutwaa tena mwili mpya

_______ Fafanua swali la mshiriki linalohusiana na wazo potofu, kama vile kutwaa tena mwili mpya huku ukiepukana na majadiliano marefu

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______ Jibu swali linalohusiana na wakati ambao huashiria mwanzo wa uhai wa roho kwa kuchunguza mada nyingi husika, kisheria na kitabibu

_______ Waambie tu washiriki warejelee tena kwenye nukuu husika kutoka katika Maandiko katika kujibu swali linalohusiana na wakati ambao huashiria mwanzo wa uhai wa roho

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

Hatimaye, kama ujuavyo, sehemu ya mwisho ya kitengo hiki huwakumbusha washiriki juu ya dhana ya kusudi la maadili lenye pande mbili lililotambulishwa katika kitengo cha pili. Inawaomba watafakari juu ya umuhimu wa kushughulikia vipengele viwili vya kusudi hili, kutokana na umaizi walioupata katika maendeleo ya roho. Wanahamisishwa kujumuisha katika majadiliano yao mada zifuatazo:

1. Kukuza sifa za kiroho
2. Kutii sheria za Mungu
3. Kuchangiaji kwenye usitawi wa mbari ya wanadamu
4. Kuendelea katika njia ya huduma

Kwa nini ni muhimu kwa mkufunzi kuhakikisha kwamba washiriki wanafanya majadiliano yenye ufanisi kuzungukia mada zilizotajwa hapo juu?

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

## SEHEMU YA 19

Tayari tumekwishaona jinsi Kitabu cha 1 kinavyotukaribisha kutafakari juu ya maana ya neno “Mimi” katika sentensi “Mimi natembea njia ya huduma.” Ingawa kwa kiasi kikubwa kinashughulikia suala la utambulisho, kama tulivyojadiliana, kinapaswa kichochee baadhi ya shughuli kwa wale wanaokisoma—hususan, kushiriki sala na wana-kaya katika jumuiya yao. Kitabu cha 2, *Kuinuka Kuhudumu*, kimekusudiwa kuwasaidia kuchukua hatua chache zinazofuata katika njia hii na kukuza zaidi uwezo wao wa kutoa huduma.

Maneno ya utangulizi ya Kitabu cha 2, “Mawazo Machache kwa ajili ya Mkufunzi”, yanajadili uwezo ambao kinahitaji kushughulikia, na malengo ya kila moja ya vitengo vyake vitatu. Ingawa utapenda kusoma utangulizi huu kikamilifu kwa ajili ya maandalizi ya kukiongoza kikundi kupitia kozi, kwa kuwa makusudi yetu hapa, unashauriwa kusoma dondoo ifuatayo, ambayo huelezea lengo la jumla la kitabu na muundo wake:

> Kitabu hiki, cha pili katika mlolongo mkuu wa kozi zinazotolewa na Taasisi ya Ruhi, kinahusiana na uwezo ambao hutuwezesha kuchangia kwenye mazungumzo ya maana na yainuayo. Kitendo mahsusi cha huduma ambacho kitabu humakinikia kimeelezwa katika kitengo cha tatu. Katika ulimwengu ambamo nguvu zenye uwezo zinayararuria mbali mafundo ya kijamii, tabia ya kuwatembelea marafiki na majirani katika kaya zao kwa ajili ya kuchunguza mada kuu za maisha ya kijamii, itaweza, kama kikiwa kipengele kinachojulikana cha utamaduni, kuponya baadhi ya maradhi yanayosababishwa na utengano uongezekao. Kitengo hiki kinapendekeza kwamba mafundo ya urafiki yaliyoundwa kwa namna hii, husaidia kuimarisha mchakato wa ujengaji jumuiya hai na yenye upatano.
>
> Programu endelevu ya ziara za nyumbani katika ujirani au kijiji huhitaji kiwango fulani cha mpangilio, ikihusisha kiini cha marafiki waliojiitoa wakisaidiwa na asasi za kiutawala na mawakala husika. Katika kukiongoza kikundi kupitia kitabu hiki, mkufunzi anapaswa akumbuke kwamba washiriki wanaandaliwa kujiunga na jitihada kama hiyo inayoendelea. Ziara zilizoandaliwa kwa ajili yao kama sehemu ya ujifunzaji wao zinapaswa kuongoza kwenye kujidhatiti kushiriki katika juhudi hizi mwaka hadi mwaka, sura muhimu ya maisha ya huduma.
>
> Tabia ya kutembelea kaya zao kwa ajili ya kusudi maalum la kuchunguza mada zenye umuhimu wa kiroho na kijamii kwa uwazi husitawisha utamaduni wa jumuiya. Yenye umuhimu sawa na huo kuhusiana na hili, ni majadaliano mengi yasiyo rasmi ambayo hufanyika nyumbani na katika mahali pa kazi, shuleni na sokoni. Ili kutambulisha kanuni za kiroho katika mazungumzo ya

kila siku wakati hadi wakati, hivyo, ni uwezo unaostahili umakini. Maendeleo yake ndiyo lengo la kitengo cha pili, yakiweka, kwa jinsi hii, msingi kwa ajili ya masomo yaliyosomwa kwenye kile cha tatu.

Ili mazungumzo yetu pamoja na marafiki na majirani yawe yainuayo, lazima tuweze kuleta furaha kwenye miingiliano yetu na wao. Hii ni mada inayoongelewa katika kitengo cha kwanza, "Furaha ya Ufundishaji". Vitendo vyote vya huduma vilivyoshauriwa na Taasisi ya Ruhi kwa asili huhusisha, kushirikiana na wengine, lulu za hekima takatifu tunazozigundua katika bahari ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh. Usomaji wa kitengo cha kwanza umekusudia kuongeza utambuzi wa furaha iliyomo kiasili katika shughuli hii. Washiriki wanaombwa katika sehemu kadhaa kufikiri kuhusu Neno la Mungu na ni baraka iliyoje kushiriki na wengine. Kutoka kitendo hiki, kitengo hueleza, huinuka furaha ambayo huharakisha hatua zetu kadiri tutembeavyo njia ya huduma.

Kama ilivyooneshwa hapo juu, kitengo cha pili, "Mazungumzo Yainuayo", kinahusiana na baadhi ya ujuzi, stadi na mienendo muhimu kwa ajili ya kujihusishaa katika mazungumzo ya maana katika nafasi mbalimbali za kijamii. Washiriki wanaombwa kujifunza idadi kadhaa za kauli fupi juu ya kanuni mbalimbali za Imani ambazo zimeegemezwa kwenye maneno ya 'Abdu'l-Bahá. Kwa kufanya hivyo, wanajifunza kuchota kutokana na ufafanuzi Wake na kwa jinsi hii wanahamasika kuchukua mwelekeo ambamo wanamgeukia Yeye katika jitihada zao za kuelewa vizuri zaidi maana na athari za mafundisho ya Bahá'u'lláh na kushiriki na wengine. Ni jinsi gani utekelezaji wa kila moja ya shughuli zifuatazo huimarisha kwa washiri uwezo uhitajikao kuanzisha na kudumisha mazungumzo ya maana na yainuayo?

a. Kubaini mlolongo wa mawazo katika kila mojawapo ya kauli na kisha kupeana zamu katika kikundi, kuyasema hadi watakapoweza kuyaeleza kwa urahisi

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

b. Kufikiria kuhusu miingiliano yao na marafiki, wana-familia na jamaa na kubaini baadhi ya mada zinazoshughulisha akilini, na mada ambazo hutoa uwezekano wa kushiriki mawazo yaliyomo katika kauli hizo

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

c. Kuchagua kauli moja au zaidi wakati usomaji wa kitabu unaendelea na kujaribu kuongelea juu ya mawazo yaliyomo pamoja na marafiki wawili au wana-familia

Pengine sasa ungependa kukiwasilishia kikundi unachosoma nacho leo, nyakati chache ambapo uliweza kuingiza katika mazungumzo yako kwa njia ya kawaida baadhi ya kanuni za kiroho zilizotambulishwa katika kitengo cha pili cha Kitabu cha 2.

Kuhusu kitengo cha tatu, kinalenga juu ya kitendo cha huduma kilichoongelewa katika Kitabu cha 2—kuwatembelea marafiki na majirani kwa ajili ya kujadili mada muhimu kwa maisha ya jumuiya. Maudhui kwa aina tatu za mazungumzo yameainishwa. Unajua kutokana na usomaji wako wa kitabu kwamba sehemu kubwa ya kitengo hiki inaongelea mazungumzo ya kwanza kati ya hayo matatu. Kinaelezea mfuatano wa mada ambazo zinaweza kujadiliwa pamoja na wana-kaya hizo kama sehemu ya programu ya kimpangilio ya ziara za nyumbani, zikiwa na shabaha ya kimsingi ya kuwasaidia kuimarisha uelewa wao wa Imani. Maudhui kwa ile aina ya pili ya mazungumzo huitikia tajiriba ikuayo kote ulimwenguni kwa kufanya ziara za mara kwa mara kwa wazazi wa vijana waliomo katika madarasa ya elimu yao ya kiroho na katika vikundi kwa ajili ya uwezeshwaji wao wa kiroho—kitendo ambacho sasa ni kipengele muhimu cha jitihada ya ujengaji jumuiya. Mwishowe, kitengo kinaainisha kwa ufupi mfuatano wa mawazo yanayohitaji kuingizwa katika mazungumzo na vijana ambayo huelezea shauku yao ya kutafuta njia za huduma. Mazungumzo kama hayo aghalabu huwaongoza vijana kujiunga na kozi za taasisi kama njia ya kukuza uwezo uhitajikao. Jadili pamoja na washiriki wengine wa kikundi chako maswali yanayofuata:

a. Wengi wa wale wanaosoma Kitabu cha 2 wataweza kuimarisha zaidi uelewa wao wa mbinu na dhana za msingi za programu za kielimu kwa ajili ya watoto na vijana chipukizi pale watakapoendelea kujifunza Kitabu cha 3 na cha 5, na baadhi yao watachagua kutekeleza vitendo hivi mahsusi vya huduma. Ni kwa jinsi gani kuwa na utambuzi wa umuhimu wa programu hizi kuanzia Kitabu cha 2 na kujihusisha katika mazungumzo na wazazi kwa msaada wa walimu na wahuishaji, kama ilivyopendekezwa hapo, kutakavyoharakisha hatua za washiriki kwenye njia ya huduma?

b. Jinsi gani ujifunzaji wa maudhui ya mazungumzo yanayokunjuka kati ya Alejandra na Beatrice, vijana wawili ambao wana shauku ya kuhudumia jumuiya yao, huthibitisha yenye kufaa kwa wale wote watembeao kwenye njia ya huduma?

c. Kadiri kitendo cha kuzitembelea kaya na kuwahusisha wanakaya wake katika mazungumzo yenye maana na yainuayo kinavyoendelea kuwa utamaduni wa ujirani au kijiji, ndivyo mfumo wa kiroho na kijamii wa maisha ya jumuiya unavyoongezeka nguvu. Jinsi gani ujifunzaji wa kushiriki mada muhimu za kiroho pamoja na wanakaya—kuanza na zile zilizotambulishwa katika kitengo cha tatu—unavyoongeza uwezo wa wale wanaotembea njia ya huduma kuchangia kwa mchakato wa ujengaji jumuiya?

________________________________________________________

________________________________________________________

________________________________________________________

________________________________________________________

Pale Taasisi ya Ruhi ilipoanza kutoa maudhui ya kile ambacho sasa ni kitengo cha tatu, ilionekana kwamba baadhi ya wale waliotembelea kaya waliendelea kuimarika katika juhudi zao, wakati wengine punde waliacha. Tofauti ilionekana kuwa wale walioendelea walihisi furaha katika kitendo chenyewe cha ufundishaji, pasi na kutegemea matokeo ya papo hapo. Kitengo cha kwanza cha Kitabu cha 2 kiliandaliwa kuelezea suala hili. Kinafuata mlolongo wa mawazo yaliyopo hapa chini. Soma kupitia mawazo na yafikirie kama jitihada zako kuhudumu kama mkufunzi. Kisha andika aya fupi inayoelezea ni kwa jinsi gani kitendo hiki cha huduma kitakuwa chanzo endelevu cha furaha kwako.

- Ufunuo wa Bahá'u'lláh unaweza kulinganishwa na bahari ambamo katika vina vyake zimo lulu za mwongozo mtakatifu. Tunapogundua lulu za busara zilizomo katika Ufunuo wa Bahá'u'lláh na kushiriki pamoja na watu wengine, mioyo yetu inajawa na furaha.

- Tunapata fadhili za bahari ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh kwa uwiano na juhudi tunazofanya.

- Bahari ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh ipo karibu vya kushangaza nasi. Kama tu tukitaka tunaweza kufika kwenye fuko zake kufumba na kufumbua.

- Baada ya kupata baraka ya kumtambua Bahá'u'lláh, tunachota kutoka kwa hazina za bahari ya Ufunuo Wake na kushiriki kwa uhuru na bila masharti na wengine lulu zake za mwongozo mtakatifu.

- Neno la Mungu ni chanzo endelevu cha uvuvio kadiri tunavyoendelea katika njia ya huduma. Tunashiriki Neno la Mungu na wengine, kwa kuwa lina nguvu na athari maalumi juu ya moyo wa wanadamu.

- Kati ya shughuli zote tunazojishughulisha nazo katika maisha yetu ya kila siku, zile ambazo huhusu kuwasaidia wengine kugundua lulu zilizofichwa katika bahari Ufunuo wa Bahá'u'lláh zimejaliwa baraka maalum.

- Furaha tunayoipata kutoka kwenye huduma imo katika kitendo chenyewe. Kama tumejiambatanisha mno na matokeo au kuathiriwa na sifa au ukosoaji, tunaipoteza furaha hii. Kujitenga ni hitaji kwa ajili ya huduma yenye furaha.

- Pia lazima tuwe tayari kufanya bidii na kutoa dhabihu. Sharti tukumbuke, kwamba dhabihu ni kuvikana vile vya chini kwa ajili ya vile vya juu. Tunapofanya hivyo, tunapata furaha ya kiroho na kuendeleza maendeleo yetu ya kiroho.

- Lazima tuoneshe umakini kwa yote mawili, nguvu na ubora wa juhudi ihitajikayo kwa kila jitihada tunayoifanya katika njia ya huduma.

- Kuwa wenye matumaini na shukrani ni mielekeo miwili ya msingi kwenye njia ya huduma.

Sasa, kufuatana na uchunguzi wako wa hapo juu, soma dondoo ifuatayo kutoka katika maneno ya utangulizi kwa ajili ya mkufunzi wa Kitabu cha 2:

> Inapaswa itambulike kwamba vitendo vya huduma vilivyoelezwa katika mfuatano huu wa vitabu, ingawa ni muhimu kwa ajili ya ukuaji na maendeleo ya jumuiya, ni zaidi ya vipengele vyote vya mchakato unaotafuta kuinua uwezo

wa mtu binafsi kupitia kujifunza na kutenda. Kile ambacho kila mkufunzi anapaswa atambue ni kwamba vitendo hivi huimarishana, vikiongezeka katika utata kutoka kitabu kimoja hadi kingine. Kujifunza kutekeleza kila kitendo cha huduma ipasavyo huthibitisha kuwa muhimu kwa uwezo uhitajikao kutekeleza vile vinavyofuata. Ili kudumisha mazungumzo yaendeleayo katika kipindi cha ziara kadhaa kwa kaya moja, kama ilivyaopendekezwa katika kitabu hiki, ni dhahiri kuwa ni kazi kubwa zaidi kuliko shughuli inayohamasishwa katika Kitabu cha 1, ile ya kukirimu mkusanyiko wa ibada wa mara kwa mara, iwe ni yeye peke yake au kwa ushirikiano na wengine wachache. Na siyo vigumu kuona jinsi, ili kufanya vitendo tata zaidi vya huduma huko mbele, itakuwa muhimu kwa washiriki kuendeleza uwezo ulioongelewa hapa.

Jadili pamoja na kikundi chako jinsi uwezo ulioongelewa katika Kitabu cha 2—uwezo unaotuwezesha kuchangia kwenye mazungumzo ya maana na yainuayo —kujenga juu ya ujuzi na uwezo washiriki wanaoupata kutoka ujifunzaji wao wa Kitabu cha 1 na ujihusishaji wao katika shughuli zinazoibuka humo, hususan kitendo cha kushairiki sala na wengine.

## SEHEMU YA 20

Kitendo kinachofuata cha huduma kinachoongelewa na mlolongo wa kozi kimo katika eneo la elimu ya kiroho ya watoto. Kitabu cha 3, *Ufundishaji wa Madarasa ya Watoto, Daraja la 1*, humakinikia juu ya baadhi ya ujuzi, stadi na uwezo, na sifa na mielekeo ihitajikayo kwa wale wanaotaka kuingia eneo hili la jitihada.

Bila shaka, wengi wanaosoma kitabu hiki, wakati wanatembea kwa uthabiti katika njia ya huduma, pengine wasingependelea kufundisha madarasa hayo. Walakini, suala la elimu ya kiroho ya vijana ni la wote. Kama wana-familia, kama wana-jumuiya, na kama wajumbe wa asasi na mawakala wa Imani, wote tunapaswa tuzingatie juu ya umuhimu wa jukumu hili lenye umuhimu mkubwa kabisa. Kwa kuongezea kwenye lengo lake la msingi, hivyo, Kitabu cha 3 kinatumaini kuimarisha uelewa wa pamoja kama huo. Ukiwa na hili akilini, soma dondoo ifuatayo kutoka sehemu ya "Mawazo Machache kwa ajili ya Mkufunzi" na ijadili pamoja na washiriki wengine wa kikundi chako:

Kutoka usomaji wao wa kitengo cha pili cha Kitabu cha 2, washiriki tayari wanafahamu kauli ya 'Abdu'l-Bahá kwamba elimu ni ya aina tatu: ya kimwili, ya kibinadamu na ya kiroho. Hapa watapewa fursa kuendeleza uelewa wao wa aina hii ya mwisho ya elimu, ambapo kwa msaada wake asili ya kiroho, asili ya juu zaidi, ya mtu binafsi inakuzwa. Kile kinachopaswa kieleweke tangu mwanzoni ni kwamba elimu ya kiroho kwa ajili ya watoto kama inavyoonwa katika Imani ya Kibahá'í kimsingi hutofautiana na uingizwaji wa elimu ya imani za kidini ambazo wakati mwingine zinahusishwa na mafunzo ya kidini.

Badala yake, inaIenga kulea upendo kwa maarifa, mwelekeo wa wazi kuelekea ujifunzaji na shauku endelevu ya kuchunguza uhalisia.

Vile vile ni muhimu kukiri kwamba, katika elimu ya vijana, mafundisho ya kidini hayawezi kuwekwa kando, kwa kuwa, kufanya hivyo ingekuwa sawa na kuwanyima kupata kweli takatifu na kanuni za kiroho, kanuni ambazo hazinabudi kutawala mawazo na vitendo vyao. Wale wanaounga mkono dai kwamba ni bora kuwaacha vijana wapate viwango vyao wenyewe na maoni ya ulimwengu kutokana na mwingiliano wa vitendo vyao na jamii, mathalani kwa chaguo huru, hawaoneshi kukubaliana jinsi nguvu za kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni zinavyoendeleza kwa ushari ruwaza za itikadi na mienendo inayowasaidia kupata maslahi yao wenyewe. Lakini hata kama hili lisingekuwa hivyo, hakuna sababu ya kudhani kwamba vizazi vijavyo vitaweza kuumba ulimwengu mzuri zaidi bila elimu ambayo hulea asili ya kiroho ya mtu binafsi. Jamii ya wanadamu ikinyimwa mwongozo wa Mwelimishaji Mtakatifu haiwezi kuzalisha chochote zaidi ya vurugu, utovu wa haki na mateso.

Dondoo ya hapo juu inaelezea kwamba elimu ya kiroho ya watoto, kama inavyoonwa katika Imani, haina uhusiano wowote na mafundisho ya kidini. Lakini pia inaweka wazi kwamba elimu kama hiyo huchota kutoka kwenye kweli takatifu na kanuni za kiroho zinazopatikana katika Ufunuo wa Bahá'u'lláh, Mwelimishaji wa ulimwengu wa jamii ya wanadamu kwa Siku hii.

a. Ni zipi baadhi ya sifa za elimu ya kiitikadi ya kidini—sifa ambazo maalum tu kwa muktadha wa kidini?

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

b. Utamjibuje mtu anayesema kwamba kukariri Neno la Mungu ni itikadi ya kidini?

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

c. Wakati watoto wanaponyimwa kupata kweli na kanuni za kiroho zilizomo katika Ufunuo mtakatifu, wanaweza kwa urahisi kutekwa na tabia za uyakinifu uliokithiri unaovamia tamaduni za watu mbalimbali ulimwenguni. Ni zipi baadhi ya tabia hizi?

______________________________

______________________________

d. Jinsi gani tabia ulizozitaja hapo juu hudhoofisha maendeleo ya asili ya kiroho ya mwanadamu?

Unajua kutokana na usomaji wako wa vitengo viwili vya Kitabu cha 3 kwamba programu ya Taasisi ya Ruhi kwa ajili ya elimu ya kiroho ya watoto inahusiana na kuwasaidia watoto kukuza tabia istahiliyo sifa na mwenendo mwadilifu. Mielekeo na tabia ambazo hutofautisha mwenendo usifikao, bila shaka, itakita mizizi tu kama ni udhihirisho wa sifa za kiroho, na masomo ya Daraja la 1, yanalenga ipasavyo juu ya uleaji wa sifa kama hizo kwa watoto wenye umri wa miaka mitano hadi sita. Aya ya hapa chini kutoka katika "Mawazo Machache kwa ajili ya mkufunzi" inajadili wazo hili, ambalo linashughulikiwa tena katika kitengo cha kwanza cha kitabu hicho.

> Miongoni mwa vito ambavyo kila mtu amejaliwa, kitengo hueleza, ni vile vinavyoitwa "sifa za kiroho", ambavyo huonwa kama miundo ya kudumu ambayo juu yake tabia bora na nyoofu yaweza kujengwa. Kwamba zinaunda aina ya kipekee ya "njema"—istilahi ya jumla inayotumika kwa kila aina ya tabia isifikayo, zikijumuisha desturi na mielekeo hali kadhalika stadi na vipawa—ni wazo muhimu ambalo washiriki wote wanapaswa kulifahamu kwa kiasi cha kutosha. Sehemu 6 na 7 huzingatia baadhi ya maana za kauli hii. Mkufunzi atapenda kuhakikisha kwamba washiriki wa kikundi wanaweza kuhusisha kile wanachojadili katika masomo yao ya kitengo cha tatu cha Kitabu cha 1, ambapo walifikiria kuhusu jinsi sifa za kiroho, kama vipawa vya roho ya mwanadamu, sharti vikuzwe katika maisha haya kwa ajili ya kutusaidia na kutuauni katika safari yetu kuelekea kwa Mungu. Upendo wa Mungu na ujuzi wa Mungu haviepukiki katika ukuzaji wa sifa za kiroho. Ni muhimu kwa washiriki kuona jinsi mawazo katika sehemu hizi mbili yanavyotofautisha masomo ya Daraja la 1 na, tuseme, kozi juu ya njema ambayo huchukulia kujali muda na ukweli kama sifa ya aina moja. Na, wakati walimu wanapotambua tofauti hii wataepuka mwelekeo wa kuona maendeleo ya tabia njema kimsingi kama urekebishaji wa mwenendo.

Imependekezwa hapo juu kwamba, katika kuwasaidia watoto kurekebisha tabia yao, walimu wanapaswa watambue tofauti kati ya sifa za kiroho—sifa muhimu za roho ya mwanadamu—na "njema" kwa ujumla, ambayo ndiyo istilahi itumikayo kurejelea sifa zote zinazofikiriwa kama zisifikazo, zikiwemo desturi, stadi na mielekeo. Kauli zifuatazo haangazia zaidi kwa nini ni muhimu kuzingatia hili akilini wakati wa kufundisha masomo ya Daraja la 1. Je, unaweza kuongezea kauli zingine chache kwenye orodha hii? Katika kufanya zoezi hili,

utaona inafaa kusoma na kutafakari juu ya mawazo yaliyowasilishwa katika Sehemu ya 6 na ya 7 ya kitengo cha kwanza.

- Katika kukuza sifa za kiroho, watoto wanaongozwa kuielekeza mioyo na akili zao kwa Mungu kama Chanzo kisichokwisha ambamo sifa hizo hutoka.

- Mielekeo na tabia zisifikazo, haidhuru ingeimarishwa kwa kiwango gani na desturi za kijamii, kiasili ni za mpito na zenye mipaka vinginevyo kama zimejengwa juu ya misingi ya sifa za kiroho.

- Kukuza ndani ya watoto sifa za kiroho kama vile huruma, upendo na ukarimu kutaingiza ndani mwao mielekeo na desturi zinazofaa kama vile kuguswa kihisia, kujali na kugawana.

- Kujifunza kuishi kufuatana na desturi za kiutamaduni na kijamii pekee yake, hakuwezi kuongoza maendeleo ya sifa za kiroho.

- Hamasa ya kudhihirisha sifa za kiroho inapaswa itokane na shauku ya kufikia ridhaa njema ya Mungu, siyo kutokana na shauku ya kupata ridhaa ya watu wengine.

- Ufaaji—kufanikiwa kupata maslahi ya mtu binafsi kwa namna yoyote—inaweza kuwa kigezo Madhubuti cha hamasa katika kuonesha mwenendo ambao kwa nje hustahili sifa; lakini hauna nafasi yoyote katika shauku ya kudhihirisha sifa za kiroho.

- ______________________________
______________________________

- ______________________________
______________________________

- ______________________________
______________________________

- ______________________________
______________________________

- ______________________________
______________________________

Sasa chukua dakika chache kupitia Sehemu ya 1 hadi ya 17 ya kitengo cha kwanza cha Kitabu cha 3, ambazo huchunguza baadhi ya kanuni za kielimu zinazopatikana katika Maandiko ya Kibahá'í. Kisha orodhesha katika nafasi hapa chini dhana kuu zilizoongelewa katika sehemu hizi—dhana ambazo wale wanaohusika na maendeleo ya kiroho ya watoto, hususan walimu wa Daraja la 1, ambao wanatarajiwa kuzifahamu.

______________________________

______________________________

______________________________

Kama ulivyoona, mojawapo ya dhana muhimu iliyochunguzwa katika kitengo hiki ni nidhamu. Dondoo hapa chini kutoka katika "Mawazo Machache kwa ajili ya Mkufunzi" inaeleza jinsi dhana hii inavyopaswa kuonwa kama mchakato wa kielimu unaohusika na kukuza sifa za kiroho, kinyume na ile inayotafuta kurekebisha mienendo kwa namna zingine.

> Majadiliano juu ya dhana na mawazo ya hapo juu yanapaswa kuwaongoza kiroho, watoto wanapaswa wachukulie upataji wa sifa za kiroho kama zawadi jinsi zilivyo na umiliki wa tabia zisizo stahiki kama adhabu kubwa kabisa.
>
> Haya yote, hivyo, yanapaswa kuwawezesha washiriki kuona marekebisho ya mienendo kwa watoto kutoka mtazamo sahihi—siyo kama lengo kuu, bali kama msaada kwa ajili ya urekebishaji wa tabia. Vivyo hivyo, watapata njia zifaazo, katika miingiliano yao na watoto ili kuhamasisha mwenendo uhitajikao na kuzuia ruwaza ya mienendo isiyofaa, na baadhi ya hizi zimetajwa katika Sehemu ya 13. Dhana zingine zinazoongelewa kwa ufupi katika sehemu hii ni zile zinazohusiana na uhuru na nidhamu. Ambapo ni adhabu kali ni dhahiri haina nafasi katika elimu ya watoto, kuwapa uhuru uliopitiliza kufanya wanavyotaka vile vile kuna madhara kwa maendeleo yao ya kiroho.

Hapo chini kuna kauli chache. Amua ni zipi zinazowiana na dhana ya nidhamu kama ilivyowasilishwa katika kitengo hicho.

_____ Nidhamu inapaswa kuwa kali.

______ Nidhamu, kama inatakiwa iwe ya kudumu, sharti itoke ndani mwa mtu.

______ Uhuru wa kweli hutegemea juu ya nidhamu binafsi.

______ Nidhamu inapolazimishwa, huzuia ubunifu.

______ Nidhamu hulinda ari ya ubunifu dhidi ya kujiendekeza.

______ Ikiwa mwalimu atawajaza upendo wa Mungu wanafunzi, hakuna haja ya kuweka viwango vya mwenendo.

______ Bila nidhamu binafsi, haiwezekani kukuza sifa za kiroho.

______ Watoto wanahitaji uhuru ili kugundua vitu wao wenyewe; nidhamu itaingilia tu mchakato wa ugunduzi na ujifunzaji wa kweli.

______ Watoto hufanikiwa kutokana na nidhamu; wanajifunza vizuri zaidi katika mazingira yaliyoandaliwa na kupangiliwa vyema.

______ Watu hupata hekima kwa kuchukua mwelekeo wa unyenyekevu wa mwanafunzi. Nidhamu inayojengwa na mwelekeo huu wa ujifunzaji humweka mtu huru dhidi ya hofu ya kushindwa na hufungua njia kwa ajili ya mazoezi yenye ari yajengayo.

______ Kujenga nidhamu hakupaswi kuchukuliwe kumaanisha aina yoyote ya vurugu au uonevu, uwe wa kisaikolojia au wa kimwili, kwa kuwa kimsingi vurugu haipatani na ubora wa roho ya mwanadamu na huyadhuru maendeleo ya mwanadamu.

Sasa, chukua muda kidogo kujadili swali lifuatalo na kikundi chako: ni kwa namna gani dhana ya nidhamu inavyotumika kwenye kikundi cha mafunzo, ikiwa washiriki siyo watoto bali ni vijana na watu wazima wenye umri mkubwa?

Kuhusu kitengo cha pili, kinajumuisha sehemu mbili: masomo ishirini na nne yaliyopendekezwa kwa ajili ya daraja hili na sehemu za awali zilizoandaliwa kuwawezesha walimu kujifahamisha vyema maudhui ya masomo, ambalo kila moja limeandaliwa kuendeleza sifa mahususi ya kiroho. Unajua kwamba ili kukuza sifa za kiroho kwa watoto, masomo yamewaunganisha moja kwa moja na Neno la Mungu na kuwahamasisha kwa hadithi za ‘Abdu’l-Bahá, ambaye ni mfano halisi wa maadili bora kabisa ya mwanadamu. Sala, kukariri nukuu na hadithi vinaunda vipengele vya msingi vya masomo haya, na sehemu za mwanzoni za kitengo cha pili huchukua masomo manne kwa wakati na kuwaongoza washiriki kurudia vipengele hivi vya msingi kwa kila moja. Pengine ungependa kuchunguza sehemu hizi na kisha andika sentensi moja au mbili kuhusu kazi ya vipengele hivi katika elimu ya kiroho ya watoto.

Sala: ______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

Kukariri nukuu: ______________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

Hadithi: ______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

Sasa, unaweza kusema maneno machache kuhusu kazi ya kila moja ya vipengele vingine vya masomo?

Nyimbo: ______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

Michezo shirikishi: ______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

Kupaka rangi: ______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

Kitengo hicho cha pili huwahamasisha washiriki kufanya zoezi la uwasilishaji wa vipengele mbalimbali vya masomo kama sehemu ya usomaji wao wa nyenzo, ikijumuisha, pengine, kuvipitia pamoja na watoto watatu au wanne. Baadhi ya vikundi vinaweza kuendelea kupitia kitengo kizima kwa namna hii, vikisoma masomo manne kwa wakati mmoja, kabla ya kupata tajiriba na darasa la watoto. Pia inawezekana kwa washiriki kujifunza seti ya masomo manne na kisha papo hapo kupata tajiriba kidogo—ama kwa kumsaidia mwalimu mwingine au kwa kuanzisha darasa lao wenyewe. Jadilini ni aina gani ya ujuzi mkufunzi angeweza kuhitaji kuwa nao kuhusu kile kinachokunjuka katika kijiji au ujirani wake ili aweze kuchukua njia nyumbulifu na inayokidhi kama hiyo.

## SEHEMU YA 21

Baada ya kupata utambuzi wa kina zaidi wa vitendo vya huduma ambavyo kwavyo usomaji wa vitabu vitatu vya mwanzo huviibua, hebu sasa tutazame kitabu kinachofuata katika mlolongo mkuu wa Taasisi, ambacho kinageukia tena kwenye suala la utambulisho wa Kibahá'í, neno "Mimi" katika kauli "Mimi natembea njia ya huduma." Historia hubumba kwa kiasi kikubwa utambulisho wa mtu binafsi, vile vile ule wa watu wote. Pale uhusiano na historia unapovunjika, ghasia hutokea na watu wanakuwa kama miti isiyo na mizizi. Lakini wapi, tunaweza kuuliza, katika kipindi hiki cha mpito katika maisha ya jamii ya wanadamu, ambapo utaratibu wa zamani unaendelea kumomonyoka na muumbo mpya unajitokeza badala yake, wapi kila mtu atapata chimbuko la kihistoria la uwepo wake? Hili ni swali gumu kwa wengi, lakini kwa Wabahá'í, jibu ni rahisi sana: tunapaswa tutafute vipengele vya utambulisho wetu katika matukio lukuki ambayo yameileta Hoja ya Mungu mbele kutoka ule usiku wa kukumbukwa ambapo Báb alimtangazia Mullá Ḥusayn Ujumbe Wake.

Kitabu cha 4, *Wadhihirishaji Pacha,* kimeandaliwa mahsusi kwa ajili ya ujifunzaji wa Historia ya maisha ya Báb na Bahá'u'lláh. Katika kitengo cha kwanza, umuhimu wa Siku hii, Siku ya Mungu, huchunguzwa kwa ufupi. Kitengo cha pili na cha tatu, kwa hiyo, vinawafahamisha washiriki Vipindi vya Utumishi wa Nafsi hizi mbili Takatifu. Umuhimu wa kiroho wa matukio unatiliwa mkazo kupitia ujifunzaji wa vifungu husika kutoka katika Maandiko, ambavyo huangazia mada za kina zinazohusishwa na utokeaji wa Wadhihirishaji wa Mungu. Haidhuru ni muhimu jinsi gani kwa washiriki kujifunza mambo ya msingi kuhusu maisha ya Báb na Bahá'u'lláh, ni uelewa wanaoupata kupitia tafakari juu ya mada hizi ambao utawadumisha kwenye njia ya huduma. Kuhusiana na hili, maneno ya utangulizi kwa ajili ya mkufunzi hueleza:

> Katika kujiandaa kukisaidia kikundi kupitia kitengo cha pili na cha tatu, hivyo, mkufunzi anapaswa kufikiria kwa uangalifu mada za kiroho zinazoongelewa. Miongoni mwa hizi, kwa mfano, ni kwamba kila Nyota Takatifu hudhihirishwa katika ulimwengu wa wanadamu siyo kwa uamuzi Wake Mwenyewe, bali kwa Mapenzi ya Mungu, na amejaliwa Naye ujuzi wa kuzaliwa; kwamba wale wa kwanza kulitambua Daraja Lake wanaitwa kufanya vitendo vya ushujaa mkubwa, vitendo ambavyo huthibitisha nguvu ibadilishayo ya Imani Yake; kwamba Yeye hukubali kustahamili maisha ya mateso ili kuiongoza jamii ya wanadamu kwenye ukweli na kuyafanya Mapenzi ya Mungu na kusudi Lake vijulikane kwa muumbo Wake; na kwamba hakuna nguvu duniani, hata iwe na uwezo jinsi gani, inayoweza kupunguza ushawishi Wake au kumzuia kutimiza Dhima Yake aliyokabidhiwa. Kuhusiana na hili, dhana moja muhimu inayoongelewa katika kitengo cha tatu ni ile ya hali ya hatari na ushindi. Uelewa wa dhana hii—kwamba kila hali ya hatari katika Hoja ya Mungu hutumika kuachilia kiwango kipya cha uwezo wake wa asili—ni muhimu kwa wale wote waikanyagayo njia ya huduma, siyo tu ili waweze kuitambua Historia ya Imani bali pia ili waweze kuchangia kwenye ukunjukaji wake thabiti katika ujirani na vijiji vyao, mchakato ambao daima hupitia mfuatano wa hali ya hatari na ushindi.

Katika jitihada yako ya kuhudumu kama mkufunzi, uelewa wako mwenyewe wa maana ya kiroho ya matukio yaliyozungukia maisha ya Wadhihirishaji Pacha utaatharije jinsi washiriki watakavyojihusisha na nyenzo hizi?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

Washiriki katika kozi wanapaswa kuhamasishwa kusimulia Historia wanayojifunza kwa utondoti kiasi. Mkufunzi atawasaidiaje kukuza kipaji cha kufanya hivyo?

Kama ilivyotanabaishwa hapo juu, mada iliyomo katika kitengo chote cha tatu ni ile ya hali ya hatari na ushindi. Mojawapo ya changamoto yako itakuwa ile ya kuhakikisha kwamba washiriki wanapata uelewa wa kina wa kanuni hii. Ili kupata uelewa kamili zaidi wa nguvu za hali ya hatari na ushindi, pengine ungependa kuandaa orodha ya matukio muhimu yaliyoelezwa katika kitengo cha tatu cha kitabu katika utaratibu wa wendo. Baada ya kufanya hivyo, amua ni matukio yapi huashiria mwanzo wa hatua mpya ama hali ya hatari au ushindi.

Sasa, fikiria kuhusu jumuiya yako. Ni jinsi gani maendeleo yalivyopatikana kupitia uainishaji wa hali ya hatari na ushindi?

Inapaswa kukumbukwa kwamba, katika kitabu hiki, washiriki wanatakiwa kukariri vifungu kutoka Maandiko, ambavyo ni virefu zaidi kuliko vile walivyokariri katika vitabu vilivyotangulia. Katika kitengo cha pili wanahamasishwa kujifunza kukariri hotuba ya Báb kwa Herufi za Walio Hai na, katika kile cha tatu, aya tano za mwanzo za Kitáb-i-Aqdas. Kwamba mchakato huu wa kielimu unaokuzwa na kozi za Taasisi ya Ruhi hutia mkazo juu ya kukariri ni dhahiri tangu mwanzoni. Ingawa hakuna shinikizo kamwe lililowekwa juu ya wale wanaopata ugumu, hadi watakapofikia Kitabu cha 4, washiriki wote watakuwa wenye utambuzi zaidi juu ya umuhimu wa kukariri vifungu kutoka Maandiko na watakuwa wamepata umaizi mwingi kuhusu athari za Neno la Mungu juu ya moyo wa wanadamu. Kumbuka usomaji mwenyewe. Ni jinsi gani uwezo wako wa kukariri vifungu virefu katika Kitabu cha 4 ulivyokuwa taratibu kadiri ulivyoendelea kupitia kila moja ya kozi zilizotangulia?

## SEHEMU YA 22

Kitabu cha tano katika mlolongo mkuu, sawa na Kitabu cha 3, kinaongelea suala la elimu ya vijana. *Uachiliaji wa Uwezo wa Vijana Chipukizi* hujitahidi kuwasaidia wale wanaotamani kuhudumu kama “wahuishaji” kukuza uwezo uhitajikao kuhusisha makundi ya vijana kati ya umri wa miaka kumi na miwili na kumi na mitano katika programu ya miaka mitatu kwa ajili ya uwezeshwaji wao wa kiroho. Kama ilivyo kwa Kitabu cha 3, inatumainiwa kwamba kila mmoja anayeendelea kupitia mlolongo mkuu wa kozi atanufaika kwa namna fulani kutoka katika usomaji wao wa kitabu hiki. Lakini wakufunzi wanapaswa watambue kwamba kitendo hiki cha huduma kimsingi kinakusudiwa, ingawa siyo kwa ukamilifu, kufungua mbele ya vijana kutoka kila usuli, njia ambayo kwayo wataweza kuchangia kwenye uboreshaji wa jamii. Sehemu ya utangulizi kwa ajili ya mkufunzi inaongelea kipengele hiki na kuelezea jinsi mchakato wa kujenga uwezo utakavyokuwa umewaandaa washiriki hao kufanya kitendo hiki cha huduma:

> Kile ambacho wale wanaotenda kama wakufunzi wa Kitabu cha 5 wanapaswa kukitambua ni kwamba, miongoni mwa washiriki, kutakuwa na vijana wengi walio mwishoni mwa ujana wao au mwanzoni mwa miaka ya ishirini ambao huingia katika mlolongo mkuu wa kozi kwa shauku ya wazi ya kuhudumu

kama mhuishaji na kwa uwezo wote uliofichika uhitajikao kufanya hivyo. Baadhi pengine watakuwa wameshakutana na Imani kupitia majadiliano na wana-rika wenzao ambayo husisitiza nafasi wanayoweza kuwa nayo katika kuelimisha vizazi vichanga. Wengine watakuwa wamekwishapitia programu ya uwezeshaji wa kiroho wao wenyewe walipokuwa vijana chipukizi na kuanza kusoma Kitabu cha 1 mara baada ya hapo. Njia yoyote iwayo iliyowaleta kwenye mchakato wa taasisi, sasa watakuwa sehemu ya kiini kikuacho cha watu binafsi katika kijiji au ujirani wao waliojidhatiti kwenye uboreshaji wake na, katika muktadha huu, watapata tajiriba watakapokuwa wanazitembelea kaya ili kuchunguza pamoja na familia mada kuu za Imani—kitendo cha huduma kinachoongelewa katika Kitabu cha 2. Kama sehemu ya kiini hiki, idadi yao kubwa pia itajihusisha kwa karibu sana na angalau kikundi kimoja cha vijana chipukizi katika eneo na watakuwa wanamsaidia mhuishaji kutekeleza shughuli mbalimbali na kuungana naye katika ziara za mara kwa mara kwa wazazi ili kujadili dhana na mbinu zinazohusiana na programu hii. Hadi hapa, wote watakuwa wamepata ujuzi wa kutosha wa mafundisho ya Kibahá'í, ambao utakuwa umeimarika kupitia ujifunzaji wao wa Kitabu cha 3 na cha 4, na wataonesha stadi, uwezo, mielekeo na sifa za kiroho zihitajikazo kuanzisha na kudumisha mazungumzo ya maana na marafiki na majirani. Hususan hapa, watakapofika kwenye Kitabu cha 5, kwamba umuhimu wa mchakato wa kujenga uwezo uliomo kiasili katika mlolongo mkuu wa kozi za Taasisi ya Ruhi—mchakato ulioonwa kwa maana ya kutembea njia ya huduma—utakuwa dhahiri. Kukihusisha kikundi cha vijana chipukizi katika programu ya miaka mitatu kwa ajili ya uwezeshaji wao wa kiroho ni kitendo kihitajikacho sana cha huduma, na jitihada za wahuishaji wachanga kufanya hivyo zitategemea, kwa kiwango kikubwa, juu ya uwezo ambao wameujenga kwa uthabiti kwenye njia hii hadi sasa.

Kama mkufunzi mwenye shauku, ingefaa kwako kufikiria kuhusu kijana ambaye ameendelea hatua kwa hatua kupitia katika mlolongo mkuu wa kozi kwa namna iliyoelezwa hapo juu na sasa amefikia Kitabu cha 5. Ni zipi baadhi ya sifa zitakazompambanua? Chache zimetajwa hapo chini. Je, unaweza kuongeza baadhi kwenye orodha hii?

- Uelewa kwamba ni kupitia uimarishaji wa asili ya juu zaidi ya mtu ndipo mtu huweza kufikia daraja lake la kweli
- Hisia ya uwajibikaji kwa ajili ya ukuaji binafsi na kwa ajili ya maendeleo ya jumuiya yake
- Uelewa kwamba ni katika uga wa huduma kwamba mtu anaweza kuendeleza kusudi la kimaadili lenye pande mbili, kuwajibika kwenye ukuaji wake mwenyewe wa kiakili na wa kiroho na kuchangia kwenye uboreshaji wa jamii
- Utambuzi wa uwezo ubadilishao wa Neno la Mungu
- Uwezo fulani wa kutambulisha kanuni za kiroho katika mazungumzo ya kila siku
- Utambuzi madhubuti wa historia na uelewa wa asili wa kipindi hiki cha kihistoria na nafasi ya mtu ndani yake

– Uthabiti mbele ya majaribu na mitihani ambayo mtu hana budi kukutana nayo katika njia ya huduma

– ________________________________________________
– ________________________________________________
– ________________________________________________
– ________________________________________________
– ________________________________________________
– ________________________________________________
– ________________________________________________
– ________________________________________________
– ________________________________________________
– ________________________________________________
– ________________________________________________
– ________________________________________________
– ________________________________________________
– ________________________________________________
– ________________________________________________
– ________________________________________________

Sasa, unajua kwamba kitengo cha kwanza cha Kitabu cha 5, “Kipindi cha Mchipuo wa Maisha”, kinajumuisha uteuzi wa vifungu kutoka katika Maandiko ambavyo, kwa ujumla wake, hutoa taswira ya kijana ambaye anaweza kutenda ipasavyo katika wakati huu wa historia ya mwanadamu. Sasa kipitie kitengo hicho. Baada ya kufanya hivyo, amua kama ungenda kuongeza sifa zingine zozote kwenye orodha ya hapo juu.

Shabaha ya kitengo cha pili, “Rika la Matumaini”, kimsingi lina pande mbili. Kinataka kuimarisha katika fikra za wale wanaokisoma, uelewa kwamba vijana chipukizi ni washiriki wa kikundi cha rika maalum, lile lenye sifa zake za kipekee. Wakati huo huo, kinatumaini kuweka wazi kwamba mbinu iliyochukuliwa na jumuiya ya Kibahá’í kuelekea kipindi hiki cha maisha, ikibumbwa na Maandiko ya Imani, kimsingi ni tofauti kabisa na mbinu zilizoegemezwa kwenye dhana na nadharia zilizoenea. Tena, hebu tusome kutoka kwenye sehemu ya mkufunzi:

> . . . kitengo hiki kinaangazia kwa ufupi kwenye asili ya ujana wa awali na kisha huwaomba washiriki kutafakari juu ya changamoto ya kuongoza ipasayo utambuzi uongezekao wa vijana katika rika hili. Katika hili, kitengo kinatoa angalizo kwamba jitihada hizo lazima ziepukane na mitego ya baadhi ya programu, ambazo badala ya kuelekeza utambuzi binafsi ukuao wa wale ambao wamo katika kipindi hiki cha ujenzi cha maisha kuelekea huduma isiyo na ubinafsi kwa wengine, na kukigeuzia kwenye “nafsi” na, kwa huzuni kuwafanya waishie kuwa mateka wa “nafsi ng’ang’anivu”. Sehemu ya 5 hadi

ya 9 hujaribu kuwatahadharisha washiriki kuhusu baadhi ya hatari za kichini-chini za mtego huu kwa kuwapitisha katika mfuatano wa nukuu husika kutoka katika Maandiko ya Kibahá'í. Kitengo kinaendelea kuchunguza athari za mazingira ya kijamii juu ya maisha ya vijulanga, kinatambulisha dhana ya "kikundi cha vijana chipukizi" kama mazingira ya kusaidiana, na hueleza msimamo unaopaswa kuchukuliwa na wote wanaoinuka kuhudumu kama wahuishaji wa vikundi kama hivyo.

Chukua muda kidogo kukipitia kitengo hiki na kisha sema maneno machache kuhusu kile unachofikiri washiriki wanapaswa kukielewa kuhusu kila moja ya zifuatazo kupitia usomaji wao. Ni aina gani ya dhana wanapaswa kuachana nazo ili kupata uelewa huu?

a. Asili ya ujana wa awali: ______________________________

______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________

b. Changamoto ya kuelekeza utambuzi ukuao wa vijana chipukizi: ______________

______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________

c. Athari za mazingira juu ya maisha ya vijana chipukizi: ______________________

______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________

d. Dhana ya kikundi cha vijana chipukizi kama mazingira ya kusaidiana: ________

______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________

e. Msimamo unaopaswa kuchukuliwa na wale wote wanaoinuka kuhudumu kama wahuishaji: ________________________________________

Utambuzi wa uwezo uliofichika wa vijana chipukizi kwa idadi iongezekayo ya watu katika kijiji au ujirani huchangia kwenye utamaduni ambao huendeleza mielekeo kwa vijana ambayo ni tofauti na ile inayodumishwa leo katika jamii. Ni aina gani ya mabadiliko ya mielekeo uliyoyabaini kwenye ngazi ya jumuiya katika kijiji au ujirani wako kadiri usomaji wa Kitabu cha 5 unavyozidi kupanuka?

Kitengo cha tatu, "Kuhudumu kama Mhuishaji", kinajenga juu ya umaizi wa washiriki uliopatikana katika kitengo cha pili ili kufungua majadiliano kuzungukia lengo kuu la programu ya vijana chipukizi —kuachilia uwezo wao wa kiroho, kimaadili na kiakili. Katika kujiandaa kukisaidia kikundi cha wahuishaji wachanga kupitia kitengo hiki, itakubidi kufikiria kwa kina suala la uwezeshaji wa kimaadili na kiroho. Walakini suala hili, bila shaka, litakuwa la kipaumbele zaidi akilini mwako katika jitihada zako zote za kuhudumu kama mkufunzi. Soma na tafakari juu ya dondoo hapa chini, ambayo huashiria upatikanaji wa uwezo ambao kimsingi ni tofauti na ule ulioenea katika jamii leo.

> Suala la uwezeshaji wa kiroho huhitaji, kwa ujumla, fikra na tafakari ya kiwango kikubwa ya wakufunzi. Kwa hakika, mchakato wa kielimu ulioanzishwa na kozi za taasisi, katika uchambuzi wa mwisho, unaweza kuonwa kama mbinu ya uwezeshaji wa kimaadili na kiroho, ile ambayo kwayo watu wa matabaka yote ya maisha na kila usuli wanawezeshwa kuinuka na kushiriki katika kujenga ulimwengu bora zaidi. Dhana ya uwezo iliyotumika hapa hutofautiana sana na maana zilizozoeleka zinazoihusisha dhamira ya kutawala au kuwashawishi wengine wakubaliane na matakwa na mahitaji ya mtu. Badala yake, shabaha ni kuwa mfereji wa kutiririsha uwezo wa roho ya mwanadamu: uwezo wa umoja, wa upendo, wa huduma nyenyekevu, wa matendo safi. Jinsi ya kuchangia kwenye nguvu ihitajikayo kwa mchakato kama huo kuendelea—la, kuuchapuzwa—ni muhimu kwa kitendo cha kuhudumu kama mkufunzi, na kwa tajiriba ya kukihusisha kikundi hadi kikundi

katika usomaji wa kozi, kila mkufunzi anaweza kupata vianga vya mambo mengi husika yanayoingiliana, ambayo hakuna hata moja lenye nguvu zaidi kuliko ukuzaji wa uelewa wa kweli.

Mwanzoni mwa kitengo hiki tulijadili mada ya hamasa. Huko pengine utakuwa umepata umaizi wa awali wa asili ya mchakato wa kielimu unaoachilia uwezo wa kiroho na kiakili uliofichika ndani ya mtu. Kipengele kimoja cha mchakato huu ambacho kitakuwa ndiyo lengo la tafakari yako ya mara kwa mara ni mwingiliano kati ya unyenyekevu na uwezo. Soma Sehemu ya 19 ya kitengo cha tatu cha Kitabu cha 5, ambayo hujadili mada hii, na kisha andika maneno machache kuhusu jinsi, bila sifa ya kiroho ya unyenyekevu, ule uwezo tunaoutafuta utabakia bila kuguswa.

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

Kitengo cha tatu cha Kitabu cha 5 kinaeleza kwamba, mchakato wa kielimu unaotafuta kuwawezesha wale wenye umri wa miaka kati ya 12 na 15, hauna budi kuhusisha uendelezaji wa mtazamo wa kiroho, kukuza uwezo wa kujieleza na kujenga muundo thabiti wa kimaadili. Juu ya mada hii, maneno ya utangulizi kwa mkufunzi yanaendelea:

Katika kitabu hiki, bila shaka, shughuli iliyopo mbele ya mkufunzi huenda mbele zaidi, hadi kwenye kizazi kinachofuata na kwa asili ya mchakato wa kielimu ambao utawawezesha vijulanga wadogo kutumia uwezo wao unaoendelea kuibuka kwa mafanikio. Kwenye moyo wa mchakato huu zipo nguvu zinazoimarishana za fikra na kujieleza. Uwezo wa akili kujishughulisha na fikra za kinadharia, ambao unaongezeka sana mnamo kipindi cha ujana wa awali, unaimarishwa kwa vijana chipukizi kadiri wanavyojifunza kutumia dhana husika za kisayansi, za kimaadili, na za kiroho katika uchambuzi wao wa ulimwengu unaowazunguka na kwa majaribio yao ya mwanzo ya kutenda katika jamii. Walakini, haidhuru ni muhimu jinsi gani uwezo wa uchambuzi wa kimantiki unahitaji mtazamo wa kiroho. Kupitia huo, njia za uelewa, ambazo hazipatikani kupitia matumizi ya uwezo wa kiakili pekee, hufunguka. Vijana chipukizi, basi, lazima wasaidiwe kutambua nguvu za kiroho na kubaini kanuni za kiroho katika hali wanazokutana nazo ikiwa wao wanahitaji machaguo sahihi ya kimaadili. Kwamba muundo wa kimaadili unaoongoza fikra na mwenendo wa mtu una uhusiano wa karibu sana na muundo wa lugha ambamo yeye huelezea fikra ni kigezo cha msingi cha mchakato wa kielimu uliotazamiwa. Umaizi wowote ule unaoweza kuwa umetolewa na vitengo viwili vya kwanza vya Kitabu cha 5 katika mchakato huu, Sehemu ya 5 hadi

ya 19 ya kitengo cha tatu zinajitahidi kuweka wazi sura zake mbalimbali, zikitumia mifano kutoka matini yanayotumika katika programu, kadiri ihitajikavyo. Kila mkufunzi angefanya vyema kupitia tena sehemu hizi kwa uangalifu katika kujiandaa kukiongoza kikundi kujifunza. Inatumainiwa kwamba washiriki kupitia usomaji wao watapata uelewa wa uwezo wa matini kuwawezesha vijana chipukizi wa tamaduni anuai.

Hapa siyo mahali pa kuchambua matini yanayosomwa na vijana chipukizi ili kuona, katika mada na dhana zinazoongelewa na lugha iliyotumika, jinsi yanavyochangia kwenye shabaha za programu kama zilivyoelezwa hapo juu. Bila shaka, utahitaji kujiandaa kufanya hili katika muktadha wa kikundi cha mafunzo kinachomakinikia Kitabu cha 5 na kuwasaidia washiriki wake kupata kiasi fulani cha uelewa wa uwezo wa matini kuendeleza mtazamo wa kiroho, kukuza uwezo wa kujieleza na kujenga muundo thabiti wa kimaadili kwa vijana chipukizi. Mazoezi katika sehemu zilizotajwa, hali kadhalika katika Sehemu ya 20 hadi 23, yatakusaidia katika suala hili.

Kinachoweza kukusaidia kufanya hapa ni kutafakari juu ya dhana ya mtazamo wa kiroho kwa kuwa huhusiana na jitihada zako kama mkufunzi. Mtazamo wa kiroho ni ule wa zile nguvu za roho ya mwanadamu ambazo wakufunzi wanahitaji kukuza ikiwa wanataka kuwasaidia washiriki katika kila kozi ya taasisi kufika kwenye fuko za uelewa wa kweli. Kwa mujibu huu, inapendekezwa kwamba upitie tena Sehemu ya 5 hadi ya 7 ya kitengo cha tatu cha Kitabu cha 5, zinazo chunguza dhana hii, na kisha useme maneno machache kuhusu jinsi mkufunzi anavyoweza kunoa kipaji hiki cha ndani.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

## SEHEMU YA 23

Kutembea njia ya huduma katika maisha yote ya mtu ni dhahiri kwamba humaanisha kufundisha. Ingawa usambazaji wa Ujumbe wa Bahá'u'lláh ni mojawapo ya huduma muhimu kabisa tunayoweza kuitoa, ufundishaji pia ni hali ya kuwa, ambamo tunaendelea kushiriki na wengine kile ambacho kwa baraka kubwa kimejaliwa kwetu. Kwa kuwa asili ya mada hii ni ya kina sana, tutakijadili Kitabu cha 6, Kufundisha Hoja, kupitia sehemu tatu, hapa tukiangalia kitengo cha kwanza na viwili vinavyofuata katika Sehemu ya 24 na 25.

Mwanzoni, sharti iwe dhahiri kwako kwamba uwezo wa kufundisha Hoja ya Mungu, iwe kulingana na mipango binafsi au kupitia utendaji wa pamoja, hauwezi kukuzwa katika kozi moja. Hali ya jamii ya wanadamu hutofautiana kwa kiasi kikubwa kutoka sehemu moja hadi

nyingine, na kila utamaduni, kila kundi rika na kila watu huwasilisha seti yake yenyewe ya hali ambayo wale ambao hutamani kushiriki mafundisho ya Imani na wanadamu wenzao huhitaji kuzingatia. Hata hivyo, kuna baadhi ya kweli za kimsingi za jumla ambazo juu yake uwezo unaohitajika unaweza kujengwa, na ni haya ambayo ndiyo mambo makuu ya Kitabu cha 6.

Miongoni mwa kweli hizi, hakuna ambayo ni muhimu zaidi hapa kuliko ukamilishanaji wa "kuwa" na "kutenda". Katika kuhudumu kama mkufunzi wa kitabu hiki, utahitaji kuhakikisha kwamba utegemeanaji wa hayo mawili hutambuliwa kikamilifu na washiriki. Kwa hakika, mada hii ipo kwenye msingi wa mchakato wa kielimu unaoendelezwa na mlolongo mkuu wenyewe —mchakato ambamo mafunzo na vitendo vimeunganishwa. Kwa jumla mlolongo wa kozi unajaribu kufuma pamoja vipengele kadhaa ambavyo wakati mwingine huchukuliwa kama vinapingana, lakini kwa kweli ni sura zinazokamilishana za uhalisia mmoja. Inatumainiwa kwamba kwa namna hii, kadiri watu binafsi watakavyondelea kupitia kozi, ile desturi ya kuupunguza uhalisia hadi kuwa seti ya uwili kinzani pole pole itaachiliwa. Dondoo hapa chini kutoka katika nyenzo ya utangulizi kwa wakufunzi huangazia mada hii:

> Katika kuchunguza asili ya wajibu ulioamriwa na Bahá'u'lláh juu yetu kufundisha Hoja Yake, kitengo cha kwanza hubeba dhana kadhaa za kimsingi. Miongoni mwa zile zilizotambulishwa awali katika kitengo ni dhana ya "uwakaji". Washiriki wanahamasishwa kutambua kwamba wajibu wetu wa kufundisha unahusiana hasa na hali yetu ya ndani sawa na vitendo tunavyovitekeleza. Kwamba "kuwa" na "kutenda" ni vipengele viwili vinavyokamilishana vya maisha yanayofuata mafundisho ya Kibahá'í ni mada iliyopo kwenye msingi wa mlolongo mzima wa kozi. Hapa inawekwa wazi na kwa hakika, inabumba muundo mzima wa kitabu. Sehemu za mwanzo za kitengo hiki zitawasaidia washiriki kupata umaizi wa kiroho kuhusu wazo hili kwa kuwa linahusiana na ufundishaji wa Imani. Sitiari kadhaa zilizomo katika Maandiko zinatumika kuwasaidia kuona uhusiano uliopo kati ya "kuwa" na "kutenda"—hasa, taswira ya mwale, ambao haidhuru ni mdogo kiasi gani, hutoa joto na mwanga. Kitendo cha ufundishaji, inasemekana ni udhihirisho wa kiasili wa hali ya kuwa, ile ambayo inaweza kuelezwa vyema kabisa kama hali ya uwakaji, ambamo upendo wa Mungu huwaka kwa wangavu mno katika myoyo yetu ambapo tunajitahidi bila kuchoka kueneza Neno Lake.

Pengine sasa itakusaidia kupitia Sehemu ya 1 hadi ya 13 ya kitengo cha kwanza cha Kitabu cha 6. Jinsi gani uelewa ambao washiriki huufikia kupitia usomaji wao wa vifungu vya sehemu hizi huwawezesha kutambua jinsi ukamilishanaji wa "kuwa" na "kutenda" unavyodhihirishwa kivitendo katika uga wa huduma? Katika hili, athari za baadhi ya dhana zinazoshikiliwa na wengi ambazo huyatenganisha haya mawili itabidi ziwekwe wazi kwa washiriki, ikiwa wanataka kuondokana na fikra zenye uwili kinzani kama huo kushawishi jinsi wanavyoyatazama maisha yaliyotolewa wakfu kwa ajili ya uendelezaji wa Hoja. Hapa chini kuna baadhi ya mawazo kuhusu ufundishaji ambayo wanaweza kuwa nayo wakati wanapoanza kozi. Jinsi gani kufikiri kwao kutakuwa kumebadilika kutokana na usomaji wao wa sehemu hizi?

a. “Ni wale tu ambao wana ujuzi wa kina wa Hoja ndio wanapaswa kufundisha.”

b. “Tunapaswa tusubiri mpaka tumeimarika kikamilifu kabla ya kufundisha.”

c. “Jambo muhimu ni kumwambia mtafutaji yaliyo muhimu; hali yetu ya kiroho ni ya umuhimu wa pili.”

d. “Hali yetu ya ndani ndio muhimu zaidi; kwa hiyo hatupaswi kufundisha mpaka tumepata sifa za Mbahá’í wa kweli. Ndipo mfano wetu utakapokuwa mwalimu mzuri kabisa, na maneno hayatahitajika.”

Inatumainiwa kwamba, katika kujadili sehemu hizi, washiriki watakuja kuona kwamba kusudi la kimaadili lenye pande mbili wanaloliendeleza tangu kuingia katika njia ya huduma hufungamanisha pamoja kila sura ya maisha yao—utafiti wao wa ujuzi, utiifu wao kwa sheria Takatifu, jitihada zao kumtumikia Mungu na kumkaribiza zaidi Yeye na kupata sifa za kiroho na kurekebisha tabia yao. Jinsi gani utahakikisha kwamba wataweza kuuweka uhusiano huu katika muktadha wa ufundishaji wa Imani?

Kama utakavyokumbuka kutokana na usomaji wako wa Kitabu cha 6, ukweli mwingine uliochunguzwa katika kitengo hiki ni asili takatifu ya ufundishaji, ambayo inaweza kuonwa kama ufunguaji wa mji wa moyo wa mwanadamu kwa Ufunuo wa Bahá’u’lláh kwa ufunguo wa matamshi. Sehemu ya 14 hadi ya 17 hutambulisha dhana hii kwa washiriki, na

maneno ya utangulizi kwa mkufunzi husisitiza umuhimu wa sehemu hizi, tin dio ulputpatetue feuisis ros ril ullum tisiscipis unt ullamcommy te lutem velenibh:

> Katika sehemu hii, wanaombwa kufikiria juu ya jinsi ya kuinua ufahamu wa utakatifu wa kitendo hiki hakuongezi tu ufanisi wa jitihada ugani. Bali, na muhimu zaidi, huachilia nguvu za kiroho zinazohitajika kuinua jitihada kama hizo juu ya masuala ya kiulimwengu, hivyo, zikianzisha michakato inayoweza kuleta mabadiliko ya kimsingi ya mtu binafsi na ya pamoja. Katika Sehemu ya 17 washiriki watatumia kiasi fulani cha muda kuchunguza matokeo ya ufahamu huu uliokuzwa. Miongoni mwa mambo ambayo Mkufunzi atataka kuhakikisha yamewafikia, mawili yanajitokeza: Kwanza, watalazimika kuwa waangalifu, wasije wakachukua mielekeo fulani ambayo, ingawa imeenea katika jamii, ingeingiza katika jitihada zao za ufundishaji, mitazamo na desturi ambazo zingehatarisha asili yao takatifu. Kitendo cha ufundishaji hakipaswi kuendewa kana kwamba mtu anaandikisha wajumbe wa hoja endelevu ya kijamii, hata kidogo isifikiriwe katika muktadha wa uuzaji wa bidhaa, haidhuru kina manufaa kiasi gani kwa mtumiaji. Pili, wanapaswa kutambua kwamba, kwa kuwa shughuli zote kwenye njia ya huduma inahusisha kuikutanisha mioyo na Neno la Mungu, hizi, pia, ni takatifu kiasili na zinapaswa kuendewa kwa utambuzi huu.

Sasa pitia tena Sehemu ya 14 hadi ya 17. Ni umaizi gani unatumaini washiriki wataupata hususan kutokana na usomaji wa Sehemu ya 17, kuhusu athari za utakatifu katika kitendo cha ufundishaji? Ni fikra za aina gani zingewasaidia kuzuia tabia ya kutumia katika kitendo cha ufundishaji mawazo na mbinu zilizomo katika utamaduni uliotawala? Fikiria mawazo yaliyopo hapo chini ambayo mtu anaweza kuwa nayo kuhusu ufundishaji Hoja. Kila moja linaelezaje kuhusu ujumbe unaotolewa? Ni mtazamo gani yaliyonayo kwa wanadamu ambao tunatumaini kushiriki nao ujumbe huo?

a. “Jinsi ujumbe wetu ulivyofungashwa ndiyo hasa muhimu.”

________________________________________

________________________________________

________________________________________

b. “Ufundishaji Hoja ni kama kuwaandikisha watu kujiunga na harakati ya maendeleo ya kijamii. Inatosha kushiriki kanuni za Imani na watu kwa sababu hilo ndilo linalowavutia zaidi.”

________________________________________

________________________________________

________________________________________

c. “Tunapofundisha Hoja ya Mungu, tunaongea na moyo wa mwanadamu, ambao ni mali Yake, na tunatumia ufunguo wa matamshi yetu kufungua malango ya mji wa moyo huo kwa Ufunuo wa Bahá’u’lláh.”

________________________________________________________

________________________________________________________

________________________________________________________

Baada ya majadiliano juu ya utakatifu, kitengo kinashughulikia ukweli mwingine wa kiroho wa kina katika Sehemu ya 18—kwamba pale malango ya mji wa moyo wa mwanadamu yanapofunguliwa na moyo kuunganishwa na Ufunuo wa Bahá’u’lláh, mchakato wa kudumu wa mabadiliko huanza. Bila shaka, katika Kitabu cha 5, ulifikiria mabadiliko ya aina mbili—kwenye ngazi ya mtu binafsi na katika muundo wa jamii—ambao umetazamiwa katika Maandiko ya Imani. Kwamba kuna uhusiano wa kutendeana kati ya ukuaji wa kiakili na kiroho wa mtu binafsi na mabadiliko ya ukuaji endelevu katika miundo ya kijamii ambayo hadi sasa, ni muhimu kwa fikra zako mwenyewe. Katika hili, utakumbuka kauli ya Mlinzi kwamba moyo wa mwanadamu hauwezi kutenganishwa na mazingira, kwa kuwa viwango na mienendo ya watu binafsi hubumba mazingira yao na wakati huo huo wao hubumbwa na miundo na michakato ya kijamii. Jinsi gani uelewa wa dhana hii ya kina unavyosonga mbele kupitia majadiliano katika kitengo cha kwanza cha Kitabu cha 6, yakianza katika Sehemu ya 18, kuhusu nguvu ya Neno la Mungu kuubadilisha moyo wa mwanadamu?

## SEHEMU YA 24

Baada ya kuwasaidia washiriki kufikiria kuhusu jinsi ufundishaji unaofaa unavyohusisha yote mawili “kuwa” na “kutenda”—umakini wa hali ya ndani ya mtu hali kadhalika shughuli mara kwa mara—Kitabu cha 6 hugeukia moja kwa moja zaidi kwenye hali yetu ya ndani. Kitengo cha pili, hivyo, humakinikia juu ya baadhi ya sifa na mielekeo ya lazima kwa ajili ya ufundishaji, kikisisitiza tangu mwanzoni wazo kwamba ukamilifu wa tabia ya mtu binafsi, kwa kawaida hujionesha katika jitihada ya kuwatumikia wengine, ambapo shauku ya mtu kuwatumikia wengine huongeza uboreshaji wa tabia ya mtu. Kwa mkufunzi, katika kujiandaa kukisaidia kikundi kupitia kitengo hiki, hii ni fursa ya kufikiri kwa mara nyingine tena kuhusu asili ya kiroho ya njia ya huduma ambayo kila mmoja wetu, kulingana na hali zetu wenyewe, huikanyaga. Kwa mujibu huu, sehemu ya utangulizi kwa mkufunzi, kwa namna fulani, huchukua majadiliano katika Kitabu cha 3 juu ya sifa za kiroho na huyapanua zaidi:

> Ukuzaji wa sifa za kiroho, pamoja na mielekeo inayolingana, ni mada inayozungumziwa mara kwa mara katika kozi za Taasisi ya Ruhi, lakini daima katika muktadha wa ujenzi wa uwezo maalum—uwezo unaohitajika, kwa mfano kuchangia kwenye tabia ya kiibada ya jumuiya, kushiriki pamoja na wengine lulu za hekima kutoka Ufunuo wa Bahá’u’lláh, kuendesha madarasa kwa ajili ya elimu ya kiroho ya watoto. Kwa namna hii, uelewa wa washiriki wa sifa hizi muhimu za roho ya mwanadamu huongezeka na hujitwalia kina kikubwa zaidi kadiri muda upitavyo, kadiri wachunguzavyo mienendo ya kila

moja kwa mtazamo mpya na kushuhudia utendakazi wake katika eneo fulani jipya la utendaji.

Katika kuongoza kikundi kupitia kitengo hiki, mkufunzi atahitaji kukumbuka dhana kuu kwa ajili ya uchunguzi wa sifa za kiroho, ambazo zimo katika kozi zote za mlolongo mkuu, anasonga mbele katika hili—yaani, sifa kama hizo hutegemea moja juu ya nyingine kwa ajili ya udhihirisho wake unaostahili. Jambo lenye umuhimu maalum katika kitendo cha ufundishaji ni uelewa wa jinsi ujasiri unavyohitaji hekima; jinsi hekima inavyobaki bila kudhihirishwa kwa kutokuwepo kwa ujasiri; jinsi gani usafi unavyohitaji kujitenga na tamaa za kiulimwengu, vile vile kutokuwa na ubinafsi; jinsi gani wema, usiporekebishwa na imani katika uwezo wa watu, unaweza kufunikwa na ubaba au jinsi, bila uaminifu, kiuhalisia, si kingine bali unafiki.

Wakufunzi hadi sasa wanalijua wazo hili, lililoelezewa katika Kitabu cha 3, kwamba sifa za kiroho ni ile miundo ya kudumu inayotuainisha jinsi tulivyo kama wanadamu. Upataji wa sifa hizi hutuwezesha kuonesha mielekeo ifaayo katika miingiliano yetu na wengine na kuepukana na ile isiyofaa ambayo pengine tumeipata kupitia malezi na utamaduni wetu. . . .

Wale wanaohudumu kama wakufunzi, bila shaka wanatambua pia kwamba ukuzaji wa sifa yoyote ya kiroho huhusisha uelewa wa idadi kadhaa ya dhana zinazohusiana. Tukichukua mfano mmoja, ufikiaji wa viwango vya juu zaidi na zaidi vya usafi, unahitaji uelewa fulani wa kile ambacho moyo wa mwanadamu umeumbwa kukiakisi, wa kile kinachofanyiza vumbi na uchafu ambavyo vinaweza kuficha wangavu wake, na wa kile kinachohitajika kuufanya uendelee kusafishwa kutoka takataka kama hizo. Lakini, mbali na uelewa unaoendelea kuongezeka wa dhana kama hizo, mtu lazima awe na nia na shauku ya kweli kuendelea kiroho. Nia na shauku haijengeki kwa majadiliano ya kitaaluma tu, kuna haja ya tafakari ya kina na ya undani zaidi kwa kila mtu kuhusu hali yake ya ndani. Ni kazi ya kila mkufunzi, kwa hiyo, kujenga mazingira rafiki ya tafakari kama hiyo—mazingira ambayo hayaibui hisia ya hatia, ambayo hayahitaji maungamo, ambayo hayahamasishi tuhuma, yale ambamo kikundi cha marafiki wanaweza kujadiliana bila jazba juu ya masuala yote mawili ya kinadharia na ya kivitendo, yakimwacha kila mmoja kutafakari kwa faragha juu ya kile kinachohitajika kutoka kwake.

Imetanabahishwa hapo juu kwamba uelewa wetu wa sifa za kiroho hupanuka pale tunapotumia uwezo tunaoukuza wakati wa kutekeleza vitendo vya huduma. Fikiria sifa mbili hapa chini, ambazo zimekuwa mada ya tafakari tangu Kitabu cha 2. Je, unaweza kusema maneno machache kuhusu jinsi uelewa wako juu yake ulivyoongezeka kadiri ulivyosonga mbele kwenye njia ya huduma na kutembelea kaya kwa ajili ya kuzihusisha katika mazungumzo yenye umuhimu wa kiroho, jinsi ulivyoendesha madarasa ya watoto na ulivyosaidia kikundi cha vijana chipukizi kama mhuishaji?

Kujitenga: ____________________________________________

____________________________________________

Unyenyekevu:

Hebu twende mbele zaidi sasa. Unafahamu vyema juu ya maudhui ya kozi sita za mwanzo za taasisi: umepitia nyenzo hizi mara moja kama mshiriki, umefanya vitendo vya huduma ambavyo vimeongeza uelewa wako wa utumiaji na athari za mafundisho katika maisha yako mwenyewe na katika maisha ya jumuiya, na umetafakari hapa juu ya dhana na kanuni zinazobumba mchakato wa kielimu. Kufuatana na tajiriba hii ya kutosheleza, tafakari juu ya dhana ya "stadi", ambazo ukuzaji wake, tumesema, huhitaji maarifa, sifa za kiroho na mielekeo inayostahili, hali kadhalika uwezo mwingi na ujuzi. Kwani hakuna uwezekano halisi kwamba, bila ukuzaji wa sifa za kiroho na kulea uelewa, mchakato wa ujengaji uwezo ungeishia kuwa si chochote zaidi ya mafunzo ya kiufundi, katika baadhi ya maana finyu ya istilahi, inayohusiana tu na usimilishaji wa taarifa na upataji wa stadi?

Sasa, mkufunzi huhakikishaje kwamba umakini wa kutosha na unaofaa unatolewa kwa ajili ya kujenga mazingira yanayowawezesha washiriki katika kikundi cha mafunzo kujihusisha na aina ya tafakari ya kina iliyotajwa katika nukuu ya hapo juu, ambayo ni sehemu muhimu ya kila kozi ya taasisi?

## SEHEMU YA 25

Kitengo cha tatu cha Kitabu cha 6 humakinikia juu ya kitendo chenyewe cha ufundishaji. Miongoni mwa uwezo uhusikao, uwezo wa aina mbili huongewelwa katika kitengo hicho: uwezo wa kutambua na kuulea upokevu kwa Ujumbe wa Bahá'u'lláh na uwezo wa kuwasilisha mafundisho ya Kibahá'í kwa namna ya kusadikisha, inayofaa kulingana na mazingira. Kiini cha kitengo hiki ni maalum kwa sehemu hii ya pili, na unakumbuka vyema kwamba, ili kuwasaidia washiriki kufikiri kuhusu asili yake, kisa cha kubuni kinawasilishwa ili waweze kukichambua—ni mazungumzo kati ya vijana wawili, Anna na rafiki yake Emilia. Kama mkufunzi, utapaswa kuhakikisha kwamba washiriki wanachukua vipengele viwili muhimu vinavyohusiana na uwezo unaoongelewa, wa kwanza umeelezwa hapa chini.

> . . . ni lazima kwamba washiriki siyo tu watambue tofauti kati ya dhana na taarifa, zilizoibuliwa katika Sehemu ya 4 hadi ya 6, lakini pia kwa nini tofauti hiyo ni muhimu sana. Hata hivyo, ni uelewa wa dhana na kweli za ndani ambazo huziwezesha roho kumkaribia Bahá'u'lláh, siyo uchukuaji tu wa taarifa. Kwa kiwango ambacho kitendo cha ufundishaji kinavyohusiana na uinuaji wa dhamiri na kulea uelewa, kinaweza kuonekana kama njia ya kusaidia kuwawezesha watu binafsi, kiakili na kiroho. Hapa, uwezo ambao washiriki wamekuwa wakiukuza tangu walipoingia katika mchakato wa taasisi wa kukutana na Neno la Mungu na kupata uelewa utaanza kufanya kazi, kadiri sasa wanavyowaza juu ya jinsi ya kuwaongoza wengine kuelekea kwenye fuko za ujuzi wa kweli.

Sasa unahamasishwa kusoma tena Sehemu ya 4 hadi ya 6. Jinsi gani uwezo wa kuona tofauti kati ya dhana na taarifa

– unavyotumika katika jitihada zetu za kufundisha Imani kwa wanadamu wenzetu na kuwasaidia kufika kwenye fuko za ujuzi wa kweli?

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

– unavyoongeza uwezo wa mkufunzi kuchangia kwenye maendeleo ya uelewa, ambayo ni muhimu sana kwa mlolongo mzima wa kozi?

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

Kuhusu suala la pili linalohusiana na uwezo wa kuwasilisha mafundisho kwa namna ya kusadikisha, washiriki wanapaswa waone kwamba, ingawa hakuna fomyula ya kufuata, siyo kila njia ya kuweka mawazo pamoja inafaa. Uchambuzi wa mazungumzo ya Anna na Emilia utawasaidia kutambua uwasilishaji wa kusadikisha huhusisha. Kwamba washiriki

wanahitaji kuelewa kuwa mazungumzo hayawakilishi seti isiyobadilika ya mawazo ambayo wangepaswa kuyafuata bila kuchagua. Kwa hakika, mazoezi yamejumuishwa kwa uwazi ili kuwahamasisha kufikiri kuhusu jinsi ambavyo wangeweza kutumia uwasilishaji huo kuitikia kwenye mahitaji usuli na shauku mbalimbali. Katika hili, kile wanachopaswa kukitambua ni kwamba uwasilishaji ufaao wa Imani una baadhi ya sifa zinazofanana. Kwa kuzingatia uwasilishaji wa Anna, amua zipi miongoni mwa zifuatazo ni sifa za uwasilishaji unaofaa (I) na zipi hazifai kabisa (H):

Uwasilishaji unaofaa

_____ ni rahisi na wa kina.

_____ ni wazi.

_____ siyo wazi.

_____ huonesha mwelekeo wa uwazi.

_____ huakisi kina cha Imani ya mwasilishaji.

_____ humakinikia juu ya Bahá'u'lláh kama Mdhihirishaji wa Mungu—Mwelimishaji wa ulimwengu—na huyaainisha kwa uwazi mafundisho Yake kama chanzo cha kile kinachoongelewa.

_____ hutambulisha dhana kwamba kuna sheria katika Imani ambazo ni udhihirisho wa upendo wa Mungu na rehema na kwamba zinapofuatwa huwa ni chanzo cha ukuaji na maendeleo.

_____ hutoa kianga cha wajibu wa wahusika watatu wanaofanya kazi pamoja kwa ajili ya kujenga ustaarabu mpya—mtu binafsi, jumuiya na asasi za Imani—na uhusiano wa upendo na uaminifu ambao huwaunganisha.

_____ hutoa mwonekano kwamba jumuiya ya Kibahá'í ni kamili kama ilivyo leo.

_____ huwatambulisha Wakuu wa Imani.

_____ huelezea kiasi cha kutosha cha Historia ya Imani kwa ajili ya kuunda uhusiano kati ya msikilizaji na Wadhihirishaji Pacha.

_____ huepuka kuingia kwenye uchambuzi wa kiutondoti wa uhusiano wa Bahá'u'lláh na Wadhihirishaji waliotangulia.

_____ huleta shauku.

_____ inavutia.

_____ inashinikiza.

_____ huchota ifaavyo kwenye vifungu vya Maandiko.

_____ hutumia mifano ya kulinganisha.

_____ ina mantiki.

_____ hutegemea hasa matabiri.

_____ ni yenye mabishano.

_____ huvutia vyote viwili moyo na akili ya msikilizaji.

_____ hulaghai hisia za mtafutaji.

_____ huweka wazi kwamba kuwa Mbahá'í hubeba na majukumu.

_____ hucheza na hofu za mtafutaji.

_____ huepuka kumuelemeza mtafutaji kwa maelezo mengi mno.

_____ hutoa taarifa nyingi.

_____ humakinikia kwenye maelezo tata.

_____ huakisi imani kwenye uwezo wa msikilizaji kumtambua Mdhihirishaji wa Mungu kwa wakati huu.

Kilichomo kiasili katika uchunguzi wa uwezo unaohitajika kuwasilisha Imani kwa namna ya kusadikisha, kulingana na mazingira, ni uelewa kwamba mazungumzo kama hayo yanaweza kufanyika katika muktadha wa jitihada za ufundishaji wa mtu binafsi au kampeni za pamoja. Washiriki, wanapofikiria kuhusu ile ya mwanzo, wanahamasishwa kuona jinsi jitihada kama hizo zinavyokamilishana—na, kwa hakika, zinafumwa katika —shughuli za pamoja. Wanapaswa wapewe fursa ya kutafakari juu ya hali zao binafsi na jitihada zao za kukuza mtindo wa maisha ambamo ufundishaji Imani hufanyiza sehemu ya lazima. Sehemu ya 26 na 27 zimekusudiwa kuwasaidia kuhusiana na hili. Ni muhimu kiasi gani kwa mkufunzi ambaye alishafanya mazoezi katika Sehemu ya 26 na kuandaa mpango wake mwenyewe wa ufundishaji katika Sehemu ya 27—mpango ambao utakuwa umeboreshwa wakati hadi wakati kupitia utendaji—kwa kuwahamasisha washiriki wa kikundi cha mafunzo kufanya vivyo hivyo?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

Katika muktadha huu wa ujirani au kijiji unamoishi, eleza jinsi jitihada zako binafsi za kufundisha Imani zinavyokamilishana na utendaji wa pamoja uliomakinikia juu ya upanuzi na uimarishaji wake.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

Mada ya utendaji wa pamoja inaongelewa katika Sehemu ya 28 na ni shabaha ya sehemu ya kitengo iliyobakia. Hapa mazoezi siyo marefu, na wajibu utakuwa juu ya mkufunzi kuwasaidia washiriki kuhusianisha kile wanachosoma kwa tajiriba yao wenyewe. Watapaswa kuona, katika utendaji wa pamoja, jinsi kila mtu anavyopaswa kuchangia kwenye mazingira yaliyopambanuliwa kwa viwango viongezekavyo vya umoja, katika sura zake mbalimbali. Wanapaswa kupata muono wa jinsi utendaji uliounganika mashinani, pamoja na juhudi za mtu

binafsi, husaidia kuendeleza shughuli ya kiulimwengu ambamo jumuiya ya Kibahá'í inajihusisha. Aya hii huelezea asili ya kazi anayotakiwa kuifanya mkufunzi:

> Kufikia hapa, sehemu hizi zinaibua maswali kadhaa ambayo washiriki watayazingatia: Nini asili ya utendaji wa pamoja? Imaanisha kusema utendaji wa pamoja lazima uwe umeunganika? Ni zipi sifa za njia za ukuaji wa Imani ulimwenguni kote, na ni upi wajibu wa kampeni shadidi? Ni zipi baadhi ya sifa bainifu za watu ambao miongoni mwao wao wanafanya kazi, wawe wakazi wa kijiji au umati mpokevu unaoishi katika ujirani au waliosambaa kila mahali katika klasta? Ni imara kiasi gani nguvu zinazozalishwa kupitia utendaji wao wa pamoja kusukuma mjongeo wa umma kuelekea muono wa Utaratibu wa Ulimwengu wa Bahá'u'lláh? Je, uwezo unaojengwa kupitia mchakato wa kielimu unaoendelezwa na taasisi kwa watoto, vijana chipukizi, vijana na watu wazima una uhusiano wa karibu kiasi gani na ukuaji wa Imani? Je, mazingira yanayohitajika kwa ajili ya utendaji wa pamoja wenye ufanisi yanaendelea kujengwa? Je, mafundo ya undugu yanaendelea kuimarishwa? Je, umoja wa kusudi unaendelea kupatikana miongoni mwa washiriki katika utendaji wa pamoja? Je, unadhihirishwa katika shughuli zenye furaha na shadidi? Ni kwa kiwango gani mwelekeo wao wa ujifunzaji kuhusu ukuaji unavyoweza kutafsiriwa kwa vitendo, tafakari juu ya utendaji na ushauriano? Umuhimu wa swali hili la mwisho hauwezi kutiwa chumvi kwa kuwa hicho ndicho kiwango kinachotakiwa kuwa mtindo wa utendaji miongoni mwa kiini kinachoendelea kupanuka cha marafiki ambacho kitaweza kujenga viwango vya juu zaidi na zaidi vya umoja wa fikra, ambao ni wa lazima sana ikiwa wanataka kugundua kile kinachohitajika kuendelea kutoka hatua moja ya ukuaji hadi nyingine.

Itakuwa muhimu kwa mkufunzi, wakati wa kupitia sehemu za mwisho za kitengo hicho pamoja na kikundi, kutambua fursa za kufungua majadiliano kuzungukia maswali yaliyopo hapo juu. Hadi kufikia hapa, ingekusaidia kufikiria kila moja ya swali pamoja na washiriki wengine wa kikundi chako leo. Katika kufanya hivyo, jaribu kutowahusisha katika majadiliano ya kinadharia na chota kutoka mifano ambayo kwayo una tajiriba nayo moja kwa moja. Ingekuwa stahiki hasa kufikiria maswali yaliyopo hapa chini, katika muktadha wa ujirani au kijiji chako.

Ni kwa jinsi gani ukuaji wa Imani, katika kipindi hiki cha historia, hautenganishiki na uwezo uliojengwa kupitia mchakato wa kielimu unaoendelezwa na kozi za taaisisi, hususan uwezo wa vijana kadiri waendeleavyo kupitia mlolongo mkuu?

________________________________________________________

________________________________________________________

________________________________________________________

________________________________________________________

________________________________________________________

________________________________________________________

Ruwaza ya utendajii, tafakari juu ya utendaji na ushauriano miongoni mwa kiini cha marafiki wanaofanya kazi katika kijiji au ujirani, huwawezesha kuchukua umiliki wa pamoja wa ujifunzaji. Je, mchakato wa ujifunzaji ambao unasukumwa na ruwaza kama hiyo unavyoweza kupunguzwa hadi kuwa upangaji na utekelezaji tu wa kampeni ili kuzidisha shughuli? Jinsi gani mchakato huu hutofautiana na ule ambao huhusisha tu ufuataji wa hatua kadhaa bila kufikiri? Ni kwa namna gani ruwaza kama hiyo inavyoruhusu uzalishaji wa umaizi katika mabadiliko ya mtu binafsi na ya pamoja ndani ya uhalisia maalum ambamo marafiki hujikuta?

## SEHEMU YA 26

Inatumainiwa kwamba muhutasari huu wa vitabu sita vya mwanzo vya Taasisi ya Ruhi vimekupatia umaizi katika baadhi ya kanuni za kielimu zinazotawala mtaala wake, hasa jinsi ulivyopangiliwa juu ya mchakato wa ujengaji uwezo unaofananishwa na ule wa kutembea njia ya huduma. Kitabu cha 7, unachokisoma hivi sasa, kimeandaliwa maalumu kwa ajili ya kitendo cha huduma ambacho tumesema kuwa ni muhimu kwa ajili ya upanuzi wa mchakato wa kielimu wenyewe—yaani, kukisaidia kikundi baada ya kikundi kupitia kozi za mlolongo mkuu. Kama ujuavyo, mlolongo mkuu hauishii hapa bali huendelea na kozi zingine kadhaa zinazoongelea vitendo viongezekavyo utata vya huduma. Hata hivyo hatuhitaji, kuvifikiria kwa wakati huu. Kwa sasa, unahamasishwa kuchukua muda kidogo kutafakari juu ya umuhimu wa kukuza uwezo kwa utaratibu kupitia mlolongo wa kozi. Soma dondoo ifuatayo kutoka ujumbe wa 27 Desemba 2005 ulioandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ambao, unasisitizia maendeleo yaliyofanyika katika miaka iliyotangulia, husema:

> **"Maendeleo tangu wakati huo yametumika tu kuonesha zaidi ufaaji wa mlolongo wa kozi unaotafuta kujenga uwezo kwa ajili ya huduma kwa kumakinikia juu ya matumizi ya umaizi wa kiroho unaopatikana kupitia usomaji wa kina wa Maandiko. Washiriki wanaoneshwa chombo cha ujuzi unaokuza seti ya tabia, mielekeo na sifa zinazohusiana na wanasaidiwa katika kunoa stadi na uwezo fulani uhitajikao kutekeleza vitendo vya huduma. Majadiliano yanayozungukia Neno la Uumbaji, katika mazingira makini na yainuayo ya kikundi cha mafunzo, huinua kiwango cha ufahamu kuhusu wajibu wa mtu kwa Hoja na hujenga utambuzi wa furaha mtu anayoipata kutokana na ufundishaji wa Imani na kutumikia raghba zake. Muktadha wa kiroho ambamo matendo mahsusi huongelewa huyapa maana. Kujiamini hujengwa kwa subira kadiri marafiki wanavyojishughulisha katika vitendo vya huduma vinavyoendelea kuwa tata na vihitajikavyo zaidi. Walakini, zaidi ya yote, ni kumtegemea Mungu ambako huwadumisha katika jitihada zao. Ni mengi jinsi gani masimulizi ya waumini ambao huingia katika uga wa ufundishaji kwa wasiwasi, lakini wanajikuta**

**wameimarishwa kwa mathibitisho kutoka kila upande. Wakiona uwezekano na fursa zilizo mbele yao kwa macho mapya, wao wenyewe hushuhudia nguvu ya msaada Mtakatifu, kadiri wanavyojitahidi kutekeleza kile wanachojifunza na kupata matokeo yanayopita kabisa matarajio yao. Kwamba roho ya Imani iliyozaliwa kutokana na mguso wa karibu sana na Neno la Mungu una athari kama hiyo juu ya roho kwa vyovyote si jambo jipya hata kidogo. Kinachotia moyo ni kwamba mchakato wa taasisi unasaidia idadi kubwa kama hiyo kupata tajiriba ya nguvu ibadilishayo ya Imani.”**[5]

Kutokana na tajiriba yako mwenyewe ya kukanyaga njia ya huduma inayofunguliwa na kozi za Taasisi ya Ruhi, sema maneno machache kuhusu jinsi kila kitabu kinavyojenga juu ya kile cha kabla yake, kikiwawezesha washiriki kutekeleza vitendo vya huduma vinavyoongezeka katika utata.

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

Sasa, kuimarisha umaizi ambao umeupata katika dhana kuu na kanuni zilizopo kwenye msingi wake ambazo zimebumba maudhui na mpangilio wa mlolongo wa kozi, tafakari juu ya dondoo hapa chini kutoka ujumbe wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu.

**“Bila kikwazo, baada ya kushuhudia wao wenyewe athari zibadilishazo za mchakato wa taasisi, marafiki katika klasta kama hizo wanajitahidi kupata utambuzi kamili zaidi wa nguvu zilizomo– moyo wa undugu unaoujenga, mbinu shirikishi unaochukua, kina cha uelewa unaokuza, vitendo vya huduma unaopendekeza na, zaidi ya yote, utegemeaji wake juu ya Neno la Mungu. Kila jitihada inafanyika kuhakikisha kwamba mchakato huu unaakisi ukamilishano wa ‘kuwa’ na ‘kutenda’, ambao kozi za taasisi huweka wazi; umuhimu ziutoao kwa ujuzi na utumiaji wake; msisitizo ziuwekao juu ya kuepukana na uwili bandia; mkazo ziutiliao juu ya kukariri Neno la Uumbaji; na uangalifu ziutumiao katika kuinua ufahamu, bila kuamsha nafsi ng’ang’anivu.”**[6]

Bila shaka utapata umaizi uongezekao katika nguvu ya mchakato wa taasisi kadiri unavyoendelea kutembea njia ya huduma inayoifungua. Kwa uelewa ambao umeupata hadi sasa, andika baadhi ya mawazo kuhusu malengo yafuatayo ya kozi:

a. Kuweka bayana ukamilishano wa ‘kuwa’ na “kutenda”: ____________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

b. Kuupa umuhimu ujuzi na utumiaji wake: ______________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

c. Kuweka mkazo juu ya uepukanaji wa uwili bandia: _____________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

d. Msisitizo juu ya kukariri Neno la Uumbaji: ___________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

e. Kuwa mwangalifu katika kuinua utambuzi, bila kuamsha nafsi ng’anganivu: ____

______________________________________________________________

______________________________________________________________

Sasa sema maneno machache kuhusu asili ya mchakato wa kielimu ambao kozi huhitaji kuukuza, kadiri inavyohusiana na kila moja ya yafuatayo:

a. Moyo wa urafiki unaojengwa na mchakato wa kielimu: ____________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

b. Mbinu shirikishi unaoihamasisha: _________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

c. Kina cha uelewa unaotaka kuukuza: _________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

d. Kitendo cha huduma unachokipendekeza: ____________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

e. Utegemeaji juu ya Neno la Mungu ambao mchakato wa kielimu huendeleza: ___

______________________________________________________________

______________________________________________________________

## SEHEMU YA 27

Kabla ya kumaliza majadiliano ya mtaala wa Taasisi ya Ruhi, pengine inaweza kusaidia kujadili kwa ufupi kozi zinazochepuka kutokana na mlolongo wake mkuu. Asili ya njia ya huduma, kama ilivyoelezwa katika mlolongo mkuu, hutoa fursa kwa ajili ya njia maalum zinazohusu ujuzi, sifa za kiroho na stadi zinazohitajika katika maeneo maalum ya utendaji. Kwa wakati huu, kuna mfuatano wa aina mbili za kozi za mchepuo zinazoelezwa na Taasisi ya Ruhi. Kuhusiana na hili Nyumba ya Haki ya Ulimwengu inaeleza katika barua 12 Desemba 2011:

> **"Adiam num nissectet ing acidui modip nim vullutat od velis et verciduisi ros wissim an Kwa sasa kuna vipengele viwili katika mlolongo mkuu ambavyo kwavyo mtu binafsi anaweza kuchagua kufuata njia maalum ya huduma. Cha kwanza inatokea katika Kitabu cha 3. Kutoka miongoni mwa marafiki ambao wamehitimu kitabu hicho na wanaoanza kuendesha madarasa ya kawaida ya watoto katika daraja la kwanza la program ya elimu yao ya kiroho, asilimia fulani watataka kujitoa wenyewe katika uga huu wa huduma wakifuata kadiri muda upitavyo mfuatano wa kozi za mchepuo zinazoendelea kuwa tata zaidi kwa ajili ya kufundisha Daraja la 2 hadi la 6. Hii haimaanishi kwamba wataacha kusoma mlolongo mkuu. Kwa hakika, kozi ambazo huunda njia maalum ya huduma huleta matumaini kwamba washiriki wanaendelea kusonga mbele, kila mmoja kwa hatua inayolingana na hali yake, katika njia iliyochorwa na mlolongo mkuu. Kitabu cha 5, ambacho hutaka kuwainua wahuishaji wa vikundi vya vijana chipukizi, huunda kipengele cha pili ambapo mfuatano wa kozi huchipuka.**
>
> **"Njia za nyongeza za uchunguzi bila shaka zitajitokeza katika mlolongo mkuu wakati ukifika. Baadhi pengine ziinaweza kuwa zenye maslahi ya wote, kama hizo mbili zilizotajwa hapo juu, ambapo zingine zinaweza kuwa kwa ajili ya mahitaji maalum ya mahali fulani. Kama ilivyo kwa mlolongo mkuu wenyewe, maudhui na muundo lazima viibuke kutokana na tajiriba endelevu ya pamoja ugani, tajiriba ambayo siyo ya kiholela au inayotegemea nguvu za matakwa binafsi bali inayoongozwa na asasi za Imani. Uzalishaji wa tajiriba kama hiyo utahitaji uingizaji mkubwa zaidi wa nguvu kwa sehemu kubwa zaidi ya idadi ya watu . . ."[7]**

Muhimu kwetu kutambua ni kwamba kozi za mchepuo, kama zilivyooneshwa katika kifungu hapo juu, zinatakiwa ziibuke kutokana na tajiriba ya pamoja chini ya mwongozo wa asasi na mawakala wa Imani. Nyumba ya Haki inaeleza zaidi juu ya kipengele hiki katika ujumbe wa 1 Januari 2022:

> **"Hapo nyuma tuliufananisha mlolongo mkuu na shina la mti ambalo hushikilia kozi zingine zinazochipuka kutokana nalo, kila tawi likishughulikia baadhi ya maeneo maalum ya kiutendaji. Maandalizi ya kozi za mchepuo kama hizo lazima yatokee baada ya muda kupitia ruwaza inayooneshwa na utendaji na tafakari na ambayo kwayo ufafanuzi wa dhana na shughuli za ugani huenda bega kwa bega. Kuna mahitaji kadhaa kwa taasisi za mafunzo ambazo huchukua jukumu hili. Watahitaji waweze kuelewa kwa kina maudhui ya mlolongo mkuu wa taasisi na kanuni za ufundishaji zihusikazo, kuchambua kwa uwazi tajiriba zinazoibuka mashinani kadiri shughuli zinavyosonga mbele, kushirikiana na timu za marafiki waliojitoa kwa ajili ya maendeleo ya vipengele mahsusi vya mchakato wa ujengaji jumuiya, kutenda kazi katika mtindo wa ujifunzaji na kuwatumia katika kazi zao watu binafsi wenye uwezo uhitajikao kwa ajili ya kuandaa nyenzo. Mara**

**itakapokuwa tayari, kozi za mchepuo ingeweza kuwasaidia marafiki kuendeleza shughuli inayohusiana ili kuimarisha zaidi uwezo wao, na ingeweza kuchangia kupanua mchakato unaohusika wa ujifunzaji katika maisha ya watu. Kozi hii pia ingetumika kama ghala ya kuhifadhia maarifa na kama njia kwa ajili ya uenezaji wake."[8]**

Mbinu ya uandaaji wa mtaala inayotumiwa na Taasisi ya Ruhi siyo lengo la kozi hii. Walakini, kama mkufunzi mwenye shauku wa vitabu vyake, unapaswa kutambua kwamba vitabu hivyo siyo matokeo ya akili za mtu mmoja, wala havikuibuka kupitia ushauriano wa kikundi uliofanyika kinadharia, bila vitendo. Bali vimeandikwa kwa miongo mingi kadiri taasisi ilivyojifunza, kupitia mchakato shadidi wa utendaji na tafakari, jinsi ya kuinua kwa mpangilio rasilmali watu kwa ajili ya maendeleo ya Hoja na maendeleo ya jamii. Ikiwa mtu atafuata mbinu hii, ufafanuzi wa nyenzo lazima uchukue muda mrefu. Mchakato huu ni wa pole pole na wa hatua kwa hatua, lakini subira inahitajika kuzaa matunda ya kudumu.

## SEHEMU YA 28

Hadi sasa katika kitengo hiki umechunguza kwa kina kidogo mbinu ya kielimu ya Taasisi ya Ruhi na nyenzo ilizotengeneza. Tangu mwanzoni umuhimu uliowekwa na taasisi kwa ushirikiano umeiongoza kukuza nyenzo hizi kwa ajili ya mafunzo ya vikundi. Pia ilitambua mapema kwamba mbinu yake lazima iheshimu hatua za kujifunza za watu mbalimbali. Kila mtu angeendelea kulingana na uwezekano wake mwenyewe, ambao ungeendelea kukua kadiri ambavyo kila mmoja angesonga mbele katika mchakato wa kielimu. Mashindano yasingekuwa na nafasi yoyote katika mchakato huu.

Hivyo, kuna kipengele kimoja zaidi kinachostahili kujadiliwa hapa kuhusiana na mbinu ya kielimu—yaani, kilichomo kiasili katika sifa za nyenzo hizo ni mfumo wa utoaji wa kozi, ule ambao huuwezesha mchakato wa kielimu kuendeleza na kujipanua wenyewe mashinani. Ukiandaliwa kuzungukia dhana ya kikundi cha mafunzo na mkufunzi, pamoja na nyenzo, mfumo huu unaruhusu vikundi vikuavyo daima vya watu binafsi, ambao husaidiana na kuambatana, kujenga uwezo wao kwa ajili ya huduma. Tayari unao ujuzi kiasi wa mfumo huu, kama sehemu ya vikundi hivi, na umepata umaizi zaidi kuhusu jinsi unavyofanya kazi kadiri ulivyoendelea kupitia kitengo hiki. Ikirejelea kwenye athari za mfumo huu wa elimu masafa na uwezo wake kuifikia idadi kubwa, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu husema:

**"Hebu asiwepo yeyote atakayeshindwa kutambua fursa zilizoanzishwa kwa jinsi hii. Utepetevu unalelewa na nguvu za jamii leo. Shauku ya kuburudishwa inalelewa tangu utotoni, kwa ufanisi uongezekao, ikikuza vizazi vilivyo tayari kuongozwa na yeyote anayeonesha ustadi wa kuwavutia kwenye hisia za kijuu-juu. Hata katika mifumo mingi ya kielimu wanafunzi wanatendewa kana kwamba wao ni vyombo vilivyotengenezwa kupokea taarifa. Kwamba ulimwengu wa Kibahá'í umefanikiwa kukuza utamaduni unaoendeleza njia ya kufikiri, kusoma na kutenda, ambamo wote hujichukulia wenyewe kama wanaokanyaga njia moja ya huduma—wakisaidiana na kusonga mbele pamoja, wakiheshimu ujuzi ambao kila mmoja anao katika wakati wowote ule na kuepukana na muelekeo wa kuwagawa waumini katika makundi kama vile walioelimika na wasiojua—ni mafanikio makubwa mno. Na humo ndimo zilimo nguvu za mjongeo usiozuilika."[9]**

Sasa mnahamasishwa kuchunguza aya zifuatazo, ambazo huelezea sifa za jumla za mfumo na zijadilini katika kikundi chenu:

*Kikundi cha mafunzo ni kipengele kimojawapo cha mfumo wa elimu masafa, unaosimamiwa na taasisi ya mafunzo ya kitaifa au kanda, iliyokusudiwa kuupeleka mlolongo wa kozi kwenye ngazi ya mahali. Kwa kawaida hujumuisha watu binafsi kadhaa kutoka eneo fulani, ambao, kwa msaada wa mkufunzi, husoma kozi kwa pamoja kwa mwendo wao wenyewe. Kama mshiriki wa kikundi, mkufunzi anajihusisha zaidi katika mchakato wa kujifunza sanjari na wengine lakini, kwa kuwa amemaliza kozi zilizohitajika na kupata tajiriba kidogo, anaweza kusaidia kuhakikisha kwamba kusudi la kozi inayosomwa linafikiwa. Kwa lengo hili, kama idadi ya washiriki ni kubwa, mkufunzi huenda anaweza kukigawa kikundi katika vikundi viwili au vitatu vidogo zaidi ya kile anachofanya nacho kazi kwa wakati mmoja.*

*Kuna kiwango kikubwa cha unyumbulifu katika utendaji na katika ushiriki wa kikundi. Baadhi ya vikundi pengine vingependa kukutana mara moja kwa juma kwa kipindi kirefu, ambapo wengine wanaweza kuchagua kukutana kila siku, au mwisho wa juma mara kwa mara. Baada ya kumaliza kozi moja, washiriki wote wanaweza kuendelea kusoma inayofuata kwa pamoja. Lakini baadhi wanaweza kuacha kikundi na kujiunga na kikundi kingine hapo baadaye. Mkufunzi huyo huyo anaweza kuendelea na kikundi hicho hicho kutoka kozi moja hadi nyingine. Lakini pia inawezekana kwa mkufunzi kubadilika mwisho wa kozi.*

*Washiriki wanaweza kuja kujiunga na kikundi cha mafunzo katika njia mbalimbali. Katika vijiji na ujirani ambako kuna kiini kikuacho cha wasaidizi amilifu wa Imani, vikundi vya mafunzo aghalabu huundwa katika muktadha wa jitihada za kupanua na kuimarisha jumuiya kupitia duru za miezi mitatu ya shughuli. Kadiri jitihada za kuzifikia shule, vilabu na mashirika ya mahali zinavyozidi kuzaa matunda, ndivyo washiriki wanavyovutika kutoka kwenye safu za vijana ambao, wakiwa na shauku ya kuingia katika uwanja wa huduma, wanapenda kukuza uwezo wao kupitia usomaji wa kozi. Bado wengine wenye umri wa miaka kumi na mitano – au kumi na sita ambao wamemaliza programu ya uwezeshaji wa kiroho wa vijana chipukizi na ambao tayari wamejaliwa utambuzi thabiti wa kusudi la kimaadili lenye pande mbili.*

*Matokeo yake ni kwamba, kambi zinazofanyika wakati wa likizo ya shule zimekuwa fursa nyingine kwa ajili ya usomaji wa kozi. Hizi pia na kampeni za taasisi huwakusanya pamoja katika eneo moja idadi kubwa ambao, hugawanywa katika vikundi vidogo vidogo, hujishughulisha katika usomaji shadidi wa kozi mbalimbali, kila kikundi kwa msaada wa mkufunzi mmoja au wawili. Kwa hakika, ni mchanganyiko wa kampeni kama hizo, kambi na vikundi vya mafunzo vinavyofanywa mara kwa mara ambavyo vinakuja kudhihirika kuwa vinafaa kabisa. Unyumbulifu utolewao na mbinu hizi tofauti tofauti za uwasilishaji hufanya iwezekane kwa kila mshiriki kuendelea katika mchakato wa kielimu kwa mdundo wa ufaao kulingana na hali yake mwenyewe. Kwa kawaida, vikundi vidogo vidogo vya watu ambao wamefikia takriban hatua hiyo hiyo katika mlolongo wa kozi huishia kusoma pamoja. Na, mwishowe, baadhi wanaweza kufikia hatua ambapo wanaweza kutenda kama wakufunzi na kuchangia kwenye uzidishaji wa vikundi vya mafunzo.*

*Kama kipengele cha mfumo wa elimu masafa, kikundi cha mafunzo kina kazi mbili ya muhimu: Moja ni usomaji wa nyenzo, na nyingine inahusiana na tajiriba.*

*Ikiwa washiriki wanataka kukuza uwezo kwa ajili ya huduma iliyotazamiwa katika kozi, haitoshi kwao kusoma tu nyenzo, kufanya mazoezi na kutekeleza shughuli zozote zilizopendekezwa katika kikundi chao. Fursa huhitaji kutengenezwa kwa wao kupata tajiriba halisi. Kwa mfano, kama washiriki wa kikundi cha mafunzo wanataka kukuza uwezo wa kuchunguza mada kuu za maisha ya jumuiya pamoja na marafiki na majirani, ambalo ni lengo la kitengo cha tatu cha Kitabu cha 2, hawawezi kuridhika tu na mazoezi wanayoyafanya miongoni mwao. Watahitaji kupata fursa kuzitembelea kaya za familia, hususan za watoto na vijana chipukizi, wakiwa na marafiki wakongwe zaidi na kupata tajiriba ya kutekeleza kitendo hiki cha huduma—kitendo ambacho kinapaswa kuwa muhimu kwa maisha yao wenyewe kama watu binafsi, ambacho hujidhirisha katika jitihada za pamoja za kiini kikuacho kwa ajili ya usitawi wa kijiji au ujirani, duru hadi duru. Kupitia utendaji kazi wa kiini kipanukacho kama hicho, mkufunzi anaweza kuwapatia washiriki msaada na usaidizi, kadiri wanavyohudumu bega kwa bega.*

*Hivyo, kazi ya mkufunzi haiishii tu kwenye matukio ambapo washiriki huja pamoja kujifunza nyenzo. Yeye huhakikisha kwamba wanasindikizwa kutekeleza kitendo husika cha huduma, hususan katika hatua za mwanzoni. Asasi na mawakala, hususan Kamati ya Ufundishaji ya Eneo na waratibu wa taasisi, wapo kwa ajili ya kutoa msaada kwa watu binafsi na vikundi katika maeneo mahsusi ya huduma: katika kukaribisha mikutano ya ibada, katika kufanya ziara za kimpangilio kwenye kaya na katika kuhudumu kama walimu wa madarasa ya watoto, kama wahuishaji wa vikundi vya vijana chipukizi au kama wakufunzi wa vikundi vya mafunzo. Kitendo chochote kihusikacho cha huduma, mafunzo na vitendo vinavyofanywa na washiriki vinapaswa kusaidia kuwaunganisha pamoja kwa urafiki, kuwavutia wengine kwenye njia yao ya ujifunzaji.*

Baada ya kujadili aya hapo juu katika kikundi chako, elezea njia mbalimbali za utoaji wa kozi zinazotumika katika eneo lako. Jinsi gani njia hizo huwezesha idadi iongezekayo ya ya watu kuendelea kwenye njia ya huduma, njia inayopambanuliwa kwa ujifunzaji na utendaji?

____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________

## SEHEMU YA 29

Baada ya kutafakari juu ya njia mbalimbali za utoaji wa kozi, hebu tutazame hasa kikundi cha mafunzo, kama mojawapo ya vipengele vikuu ambavyo kwavyo mfumo wa

kielimu umejengwa, na kuchunguza kwa ufupi jinsi kinavyoendeshwa, kutokana na mtazamo wa mkufunzi. Tayari unajua kwamba hakuna utaratibu maalum ambao kikundi hulazimika kuufuata. Hivyo kile tutakachofanya ni kufikiria baadhi ya matukio ya shughuli katika kikundi cha mafunzo. Hali zinazoelezwa zitakuwa tofauti na siyo lazima ziwe zile utakazokutana nazo wakati wa kuhudumu kama mkufunzi. Lakini kwa kuyafikiria maswali yaliyowasilishwa mwishoni mwa kila mojawapo kutakusaidia kufikiri jinsi utakavyoweza kuitikia hali kama hizo unazoweza kukabiliana nazo.

1. Ndio tu umeanzisha kikundi cha mafunzo chenye vijana wanane. Umri wao ni kati ya miaka 16 hadi 19. Baada ya ibada, unasema maneno machache juu ya asili ya kozi za taasisi kwa ujumla na kisha unawauliza kama wana mawazo yoyote wangependa kushiriki. Ni watatu tu kati yao hutoa maoni na unapoona wengine wakisitasita, huwalazimishi kufanya hivyo. Unaendelea kukitambulisha kitengo cha kwanza cha Kitabu cha 1, ukielezea kusudi lake na maudhui yake. Wewe unasemaje?

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

2. Katika kipindi hicho hicho, mara baada ya utambuisho wako, washiriki wanaanza kujifunza Sehemu ya 1 ya kitengo cha kwanza. Unaamua kwamba njia nzuri kabisa ya kupitia sehemu hii ni kumuomba mmoja miongoni mwa washiriki kusoma nukuu ya kwanza kwa sauti na kisha kuuliza swali linalofuata kwa waliobaki. Unaelezea kwamba kusudi la zoezi hili ni kuwasaidia kumakinikia juu ya maana ya papo hapo na iliyo wazi ya nukuu kabla ya kufikiri kuhusu matumizi na matokeo yake. Wote wanaiangalia tena nukuu hiyo na baadhi yao hujibu swali hilo kwa kuitongoa. Kisha unamuomba mshiriki mwingine kufanya vivyo hivyo nukuu kwa pili na kuendelea hivyo hadi mwisho wa sehemu. Baadaye, unapofika kwenye seti ya nukuu inayofuata katika Sehemu ya 3, unawagawa washiriki katika makundi manne ya wawili wawili, ukiwakaribisha kutekeleza shughuli hii katika jozi. Je, wewe utakuwa unafanya nini wakati zoezi hili linaendelea? Je, utatazama jinsi kila jozi inavyofanya shughuli hii? Je, utafanya nini ikiwa utaona kuwa jozi moja huliona zoezi hili kuwa rahisi na kulifanya kikamilifu lakini kwa haraka?

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

3. Majuma kadhaa baadaye, kikundi hicho hicho kinasoma Sehemu ya 3 ya kitengo cha tatu cha Kitabu cha 1, ambacho hujadili uhusiano kati ya roho na mwili. Aya ya utangulizi na nukuu vimesomwa kwa sauti, na muda hutolewa ili kutafakari juu ya mawazo yaliyoelezwa. Sasa kila mmoja anafanya mazoezi peke yake. Kuna ukimya

ndani ya chumba, na mazingira ni yale ya tafakari makini na yenye nidhamu. Je, wewe umefanya nini ili kusaidia kutengeneza mazingira kama hayo?

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

4. Unahudumu kama mkufunzi katika kikundi kimoja cha mafunzo cha vijana katika kijiji au ujirani mmoja ambapo mchakato wa ujengaji jumuiya ungali katika hatua zake za awali. Vikundi vichache vya vijana chipukizi vimeanzishwa na desturi ya kutembelea kaya, hususan zile za washiriki walio katika programu ya uwezeshaji wa kiroho, inaanza kujikita. Matokeo yake, familia zao nyingi zinavutiwa na mafundisho ya Imani. Wewe ndiyo tu umemaliza kusoma Kitabu cha 1 pamoja na vijana katika kikundi cha mafunzo, na wanashauku ya kupata fursa ya kutembelea baadhi ya familia hizi na kushiriki nao sala. Je, jinsi gani utawasaidia kufanya hivyo?

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

5. Unasoma Kitabu cha 2 na kikundi cha wanafunzi wa shule ya sekondari ya upili katika kijiji au ujirani. Wakati wanapitia kitengo cha pili, "Mazungumzo Yainuayo", unashauri wajaribu kutumia kile wanachojifunza kwa kujihusisha katika mazungumzo juu ya mada muhimu za kijamii na kiroho pamoja na wanarika wenzao shuleni. Ni yapi baadhi ya mambo unayoweza kufanya ili kuhakikisha kwamba uwezo wao wa kuzungumzia masuala ya kiroho unaanza kuongezeka? Kwa mfano, kwa nini ni muhimu kwako, kumsaidia kwanza kila mshiriki kuchagua, wakati wa usomaji wa kitengo hicho, angalau mojawapo ya kauli na kubaini marafiki kadhaa wa kuzungumza nao juu ya mawazo yaliyomo?

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

6. Majuma machache baadaye, kikundi hicho hicho cha vijana kimeingia katika kitengo cha tatu cha Kitabu cha 2 na ndiyo tu kimeanza Sehemu ya 3, ambamo wanasoma maelezo juu ya Agano la Mungu la milele. Kwa nini ni muhimu kwamba, baada ya kusoma maelezo haya, washiriki wapate muda kutafakari juu yake aya kwa aya, kubaini mlolongo wa mawazo yaliyomo na kujifunza kuyaeleza kwa ufasaha?

7. Kikundi ambacho umekuwa ukikiongoza kupitia Kitabu cha 2 sasa kimemaliza usomaji wake, na muda umewadia kwa wao kuweka katika vitendo yale waliyojifunza kwa kuzitembelea nyumba na kufanya majadiliano na familia juu ya mfuatano wa mada. Kwa kuzingatia mazingira unamoishi, jinsi gani kila kijana atasindikizwa katika kujiandaa na katika kutekeleza ziara kama hizo, hususan katika hatua za mwanzoni, kadiri uwezo wao unavyoendelea kujengwa? Jinsi gani itawezekana kuhakikisha kwamba ushiriki wao katika programu ya kimpangilio ya ziara za nyumbani hutumika kuimarisha mtindo wa maisha ya jumuiya?

8. Katika nafasi nyingine, unakisaidia kikundi cha marafiki kusoma Kitabu cha 3, *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 1*. Wamefika kwenye kitengo cha pili, ambacho hujumuisha masomo ishirini na manne kwa ajili ya madarasa. Baada ya kupitia seti ya kwanza ya masomo manne kwa utondoti kiasi, unawahamasisha washiriki, kama ilivyopendekezwa katika Sehemu ya 5, kujaribu kuwapa masomo watoto wachache wanaowafahamu—kutoka jamaa zao wenyewe au kutoka kaya za jirani. Jinsi gani utamsaidia kila mmoja wao kuandaa mpango wa utendaji kwa madhumuni hayo? Ni mbinu gani utakayotumia kuwasaidia kutafakari juu ya hatua waliyoichukua wakati mwingine kikundi cha mafunzo kitakapokutana?

9. Ndiyo tu umemaliza, kusoma kitengo cha pili cha Kitabu cha 4 na kikundi cha vijana. Wamefanya mazoezi ya kusimuia kila tukio la maisha ya Báb kwa kuwa wao wamepitia sehemu mbalimbali za kitengo hicho, na wao sasa wamekariri sala mbili Alizozifunua na wanajaribu kukariri hotuba Yake kwa Herufi za Walio Hai. Kumbukizi ya Tangazo la Báb yanakaribia, na kikundi kinajitolea kuandaa programu kwa ajili ya maadhimisho ya Siku Takatifu katika jumuiya. Wana shauku ya kuchota kutoka kile walichojifunza. Wewe utawasaidiaje kupanga programu na kujiandaa kwa ajili ya tukio hilo? Je, ungefanya nini kama mkufunzi ili kuhakikisha kwamba kila mshiriki wa

kikundi anaweza kuchangia kwenye maandalizi ya mkutano wa heshima na wenye furaha?

10. Kwa ombi la mratibu wa mlolongo mkuu, unakisaidia kikundi kidogo cha vijana kupitia Kitabu cha 5. Baada ya kumaliza kitengo cha pili, unawasaidia kufanya mazungumzo na vijana chipukizi wachache ili kupata umaizi kidogo wa jinsi wale waliomo katika kundi-rika hili hufikiria kuhusu baadhi ya mada muhimu. Jinsi gani utakavyowasaidia kulifanya hili? Kwa mfano, je, wataongea na vijana chipukizi mmoja mmoja? Je, watafanya mazungumzo katika kikundi cha wawili wawili, na nani ataambatana nao? Jinsi gani utakavyowaongoza kutafakari juu ya tajiriba yao?

11. Unapitia kitengo cha tatu cha Kitabu cha 6 na kikundi cha vijana, wote ni sehemu ya kiini kipanukacho cha marafiki wanaofanya kazi katika kijiji au ujirani wako. Duru jipya la miezi mitatu ya shughuli litaanza hivi karibuni, na jitihada katika kipindi cha upanuzi zitamakinikia juu ya ufundishaji wa Hoja kwa familia zenye shauku za vijana walio katika shughuli za kielimu za taasisi. Washiriki wamejifunza mazungumzo kati ya Anna na Emilia na wamefanya mazoezi ya kusema mawazo miongoni mwao wenyewe. Je, ni msaada gani utahakikisha wanapata, wakati wa kampeni, ili waweze kupata tajiriba katika kuwasilisha mafundisho ya Imani kwa namna ya kusadikisha?

## SEHEMU YA 30

Mlolongo wa kozi, kikundi cha mafunzo na mkufunzi hufanyiza vipengele vitatu vikuu vya mfumo wa kielimu wa Taasisi ya Ruhi. Ni wazi kwamba sehemu zilizotangulia zimeinua utambuzi wako wa nafasi nyeti ya mkufunzi katika mfumo huu. Sasa pengine ni wakati mzuri

kwako, hivyo, kupitia kile ulichojifunza hadi sasa na kuandika aya moja au mbili kuhusiana na jitihada unazoanza kufanya.

Bila kutazama kile ulichoandika, tunaweza kudhani kwa uhakika kwamba maelezo yako yatakuwa yamezungukia dhana ya huduma. Inapendekezwa kwamba ukariri nukuu mbili zifuatazo kuhusu daraja la utumishi, nukuu ya kwanza kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh na ya pili kutoka Waraka uliofunuliwa na 'Abdu'l-Bahá:

**“Fundo la utumishi lililoanzishwa kati ya mwabudu na Muabudiwa, kati ya kiumbe na Muumba, lenyewe linapaswa kuchukuliwa kama dalili ya fadhili za neema Yake kwa watu, na siyo kama ishara ya ustahilli wowote wanaoweza kuwa nao. Kwa hili hushuhudia kila muumini wa kweli na mwenye utambuzi.”[10]**

**“Ewe mtumishi wa wapendwa wa Mungu! Mtumishi wa marafiki ni mtumishi wa Uzuri Uliobarikiwa. Yeyote ampendaye Yeye huwatumikia wapendwa Wake. Shauku ipendwayo kabisa ya moyo wa mtumishi huyu ni kwamba, katika kuwatumikia marafiki wa Uzuri wa Abhá, niweze kuwa mtumishi mwaminifu na latifu, usiku na mchana niweze kujifunga kibwebwe cha utumishi, na hivyo niweze kuvuna matunda ya mti wa uzima. Mwili ambao haujajipinda katika njia ya huduma kwa marafiki si chochote bali kipande kisichofaa cha mti, na mgongo ambao haujainamishwa kuhimili taabu kwa ajili yao ni sawa na shina la mti tasa. Kwa hiyo, heri ni yako wewe kwa kuwa unatekeleza huduma ya marafiki na ni mtumishi wao mwaminifu. Haya ni mamlaka katika malimwengu yote mawili na utukufu wa hapa na baadaye.”[11]**

## SEHEMU YA 31

Majadiliano yenu juu ya mada mbalimbali zilizowasilishwa katika kitengo hiki huenda yamewahakikishia kwamba uwezo wa kuhudumu kama mkufunzi hupatikana tu kadiri muda unavyopita na kupitia tajiriba. Kusudi la kitabu hiki ni kutambulisha kwenu baadhi ya dhana na kuwaweka katika njia ambamo mtaendelea kuongeza zaidi uwezo wenu wa kukisaidia kikundi hadi kikundi kusonga mbele kupitia mlolongo mkuu wa kozi za Taasisi ya Ruhi, tangu zile za mwanzoni kabisa hadi zile kozi ambazo ni zaidi ya Kitabu cha 7. Moja ya njia yenye manufaa kabisa ya kuongeza uelewa wenu wa dhana husika na kupata umaizi katika sifa za kiroho na mielekeo, hali kadhalika stadi na vipawa, ambavyo kitendo hiki cha huduma huhitaji ni kuhudhuria mikutano ya mara kwa mara ya wakufunzi inayo andaliwa na taasisi katika eneo lenu. Katika mikutano kama hiyo, tajiriba mbalimbali huchambuliwa na majibu ya korija ya maswali hutafutwa.

Sehemu za utangulizi zilizomo katika kila kitabu, “Mawazo Machache kwa Mkufunzi”, aghalabu huchunguzwa kutokana na tajiriba katika mikutano hii. Jambo moja maalum hustahili kutajwa hapa. Sehemu hizi zimekusudiwa zaidi kwa wale wanahudumu kama wakufunzi, na hakuna haja kwa washiriki kuzisoma watakapoanza usomaji wao wa kitabu. Kwa hakika, kwa kufanya hivyo pengine kutakuwa hakuna manufaa. Walakini, mkufunzi ataona inafaa kuchota baadhi ya mawazo yaliyomo katika sehemu hizo katika kuwasaidia washiriki kupata utambuzi wa kusudi la jumla la kila kitengo cha kitabu na kusudi la baadhi ya mazoezi. Lakini hili daima lingefanywa, kwa ukadirifu, katika kuitikia tajiriba ya ufundisha-ujifunzaji ikunjukayo katika kikundi.

Sasa hebu tufikirie asili ya mkutano wa wakufunzi. Sehemu moja ya mkutano pengine ingetengwa maalum kwa ajili ya majadiliano ya baadhi ya vipengele maalum kuhusu kozi za taasisi, ambavyo kwa sehemu kubwa vingeweza kubugwa kutoka katika “Mawazo Machache kwa Mkufunzi” ya Kitabu cha 1. Baadhi ya hivi vimeandikwa hapa chini. Pengine ungependa kuongeza vingine kwenye orodha hii.

- Washiriki wote wa kozi za Taasisi ya Ruhi, iwe wanasoma nyenzo kwa mara ya kwanza au wanatenda kama wakufunzi, wanajihusisha katika mchakato wa kutendeana wa kujifunza.

- Wajibu wa kujifunza hubakia kwa kila mshiriki.

- Mkufunzi, kinyume na kuwa mrahisishaji asiyejali na asiyechangamka katika majadiliano, amsaidie kila mshiriki wa kikundi kufikia kiwango cha kutosha cha uelewa wa nyenzo inayosomwa.

- Uwezo wa mkufunzi kuwahusisha washiriki ipasavyo katika mchakato wa ufundishaji-ujifunzaji huongezeka kadiri anavyokisaidia kikundi hadi kikundi kupitia kozi na kuwasaidia washiriki wake kupata tajiriba kidogo ya awali katika kutekeleza vitendo vya huduma ambavyo kila kitabu hushauriwa.

- Katika mchakato wa elimu, kinyume na ule unaohusiana tu na upataji wa stadi za kawaida, ni muhimu kwamba washiriki wawe wenye utambuzi zaidi wa maana na umuhimu wa kile wanachokifanya.

- Kozi za Taasisi ya Ruhi huchora njia ya huduma kwa wanadamu, ambayo kwayo kila mshiriki hutembea kwa mwendo wake mwenyewe, akisaidia na kusaidiwa na wengine.

- Katika kukanyaga njia hii, washiriki huendeleza kusudi la kimaadili lenye pande mbili-wakishughulikia kwa ukuaji wao wenyewe wa kiroho na kiakili na kuchangia kwenye mabadiliko ya jamii.

- Maendeleo juu ya njia hii hujumuisha ukuaji wa idadi fulani ya stadi zinazohitaji uelewa na maarifa, sifa za kiroho na mielekeo stahiki, hali kadhalika uwezo mwingi na ujuzi.

- Vitabu vya Taasisi ya Ruhi huchota kutoka vyanzo viwili vya ujuzi: mafundisho ya Imani ya Kibahá'í na ukusanyaji tajiriba wa jumuiya ya Kibahá'í ulimwenguni kote katika kuendeleza ustaarabu wa kimwili na wa kiroho.

- Ni muono wa Bahá'u'lláh wa aina ya watu tunaoweza kuwa na wa ustaarabu tuwezao kuujenga ndiyo unaoivuvia Taasisi na inatarajiwa kwamba washiriki wote, licha ya usuli, wako huru kuukumbatia muono huu, ambao ni dhahiri katika kila kitengo cha kila kitabu.

- Kutembea njia ya huduma iliyoanzishwa na kozi za taasisi huhitaji uelewa ulioimarishwa zaidi wa mafundisho ya Bahá'u'lláh, ambao nyenzo zinajitahidi kueleza kwa udhahiri.

- Kitengo cha kwanza cha Kitabu cha 1 kinaongelea suala la uelewa, ambalo ni la msingi kwa kozi zote za Taasisi.

- Kwanza kabisa washiriki wanatarajiwa kuelewa maana ya papo hapo ya vifungu kutoka Maandiko. Kwa msingi huo, kisha wanasaidiwa kuona jinsi mawazo

yaliyomo humo hupata udhihirisho halisi kabla ya kukuza zaidi uelewa wao kwa kufikiria baadhi ya maana zake.

– Uwezo wa kuelekeza umakini juu ya maana ya papo hapo na dhahiri ya vifungu kutoka Maandiko huchangia kwenye uanzishaji wa umoja katika jumuiya za Kibahá'í.

– Majadiliano marefu juu ya maana ya neno moja moja nje ya muktadha wa nyenzo inayosomwa yanaweza yasiwe na manufaa.

– Mdundo wa maendeleo unapaswa uanzishwe katika usomaji wa kila kozi.

– Vikundi vya mafunzo vinapaswa, kwa upande mmoja, viepukane na, mbinu ya kijuu-juu ambamo mazoezi hayachambuliwi kwa umakini na, kwa upande mwingine, majadiliano marefu sana juu ya wazo ambalo huvuruga kusudi kuu la kitengo.

– Baadhi ya maswali hayawezi kujibiwa kirahisi na yamekusudiwa tu kukuza utambuzi wa mada fulani.

– ______________________________________________________________

______________________________________________________________

– ______________________________________________________________

______________________________________________________________

– ______________________________________________________________

______________________________________________________________

– ______________________________________________________________

______________________________________________________________

## SEHEMU YA 32

Shughuli nyingine inayofanyika katika mikusanyiko ya wakufunzi ni upitiaji wa kitengo kimoja au zaidi ya kitabu, ambapo maudhui huchunguzwa kwa kuzingatia tajiriba na vifungu mahsusi na mazoezi hujadiliwa. Ili kuwaelezea aina ya ushauriano ambao mtajihusisha nao wakati wa mikusanyiko hii, tutawawasilishia katika sehemu hii na tatu zinazofuata mazungumzo machache ya kubuni kati ya mtu mwenye tajiriba ya kutosha na kikundi cha wakufunzi wanaoshauriana pamoja kuhusu maudhui ya Kitabu cha 1, Mawazo juu ya Maisha ya Roho, katika mazingira ya kawaida ya kirafiki, unyenyekevu na ujifunzaji. Kila mazungumzo yatafuatwa na zoezi moja au mawili kwa ajili yenu kuyafanya. Kwa kusudi la kurasa hizi, "A", "B" na "C" zitarejelea kwa wakufunzi watatu wanaoshiriki katika mkutano na "M" kwa mratibu wa mlolongo mkuu. Wanajadili mazoezi ya Sehemu ya 2 ya kitengo cha kwanza. Ingekuwa ya msaada kwako kuigeukia sehemu hiyo sasa.

A: *Ningependa kusema kwamba mojawapo ya maoni yaliyopo katika "Mawazo Machache kwa Mkufunzi" yamekuwa yenye msaada mkubwa kwangu. Yanahusiana na kauli iliyomo katika Zoezi la 3 kwamba "Kuna watu wema wachache sana ulimwenguni kwamba matendo yao hayana athari yoyote." Kila mmoja katika kikundi nilichokuwa nakihudumia kama mkufunzi alisema kwa usahihi kwamba kauli hii haikuwa ya kweli. Nilipowauliza kwa nini, walinipa sababu nyingi, ambazo zote zilikuwa nzuri. Lakini mwishowe ilibidi niwaulize watazame nukuu ya kwanza ya sehemu iliyotangulia na kutathmini kauli hiyo katika uzani huo. Kisha kila mmoja alitambua kwamba sentensi hii ilikinzana na maneno ya Bahá'u'lláh. Utambuzi huu ulileta ujasiri na furaha kubwa kwenye kikundi.*

B: *Lakini majibu ya wazi kama hayo kwa mazoezi yote hayapatikani kwa mazoezi yote katika nukuu. Hebu chukulia kauli ifuatayo katika zoezi hilo hilo kwamba "Jambo fulani ni sahihi kama linakubaliana na maoni ya watu wengine." Hakuna nukuu yoyote iliyotangulia inayoongelea kwa uwazi suala hili. Kila mmoja kwa kawaida husema kwamba kauli hiyo siyo kweli. Je, mtu anatakiwa akubali tu jibu au majadiliano machache yanahitajika?*

M: *Hili ni jambo ambalo unapaswa kuliamua kulingana na mazingira ya kikundi. Navijua baadhi ya vikundi ambamo majadiliano machache juu ya athari za kauli hii ziliongeza uelewa wa washiriki. Ni kweli kwamba mafundisho ya Mungu huamua yale ambayo ni sahihi na yale ambayo siyo sahihi, lakini pia tunahitaji kusikiliza mawazo na maoni ya watu. Walakini tunapaswa kuweka umuhimu kiasi gani juu ya maoni haya na kwa kiasi gani tuyaruhu yatuathiri, ni jambo linalostahili tafakari.*

C: *Zoezi la 5 la sehemu hiyo huchunguza hali ambamo maneno ya watu hutofautiana na vitendo vyao. Majibu ya papo hapo ni rahisi, na nafikiri yamekusudiwa kuwa hivyo. Lakini nadhani kuna kusudi nyuma ya zoezi hili. Wakati mwingine tunaweza kuangukia kwenye mazoea ya kuwaambia watu kipi wafanye na kipi wasifanye: Usinywe pombe. Uwe bikira. Usiseme uwongo. Naweza kuona kwamba vitabu vya Taasisi ya Ruhi vinajaribu kukwepa kuwahubiria watu. Huwasaidia watu kufikiri na kufanya maamuzi ya kimaadili. Kuhusu zoezi hili, kutambua kwamba kwa kutenda katika namna fulani wao wangejikuta miongoni mwa wale ambao "maneno yao hutofautiana na matendo yao"—kitu ambacho Bahá'u'lláh ametuonya sana dhidi yake—hili limekuwa na athari kubwa kwa washiriki wa kikundi niliokuwa nasoma nao. Na, nilifurahia zoezi kwa sababu tuliweza kuongea kuhusu hekima ya baadhi ya sheria na kanuni za kimaadili kwa namna ya kujitenga, na wakati huo huo tukilinda heshima ya washiriki.*

M: *Umeibua hoja nzuri. Hapa kuna mfano ambapo zoezi huonekana rahisi, lakini siyo. Linaweka kiwango, bila kusema hivyo kwa uwazi. Badala yake linawaruhusu washiriki wenyewe kuufikia uelewa fulani wa sheria na kanuni za kimaadili. Pengine umeona kuwa maswali matano yanayofuata zoezi hilo yana athari zinazofanana, ingawa hayako wazi sana. Kwa kawaida ni wazo zuri kama washiriki wangeshauriana juu yake. Bila shaka, hutapenda ushauriano uende nje ya mada katika mielekeo mingi sana, bali washiriki wanahitaji nafasi ya kutafakari juu ya mienendo ya kimaadili. Pia wanahitaji wapate utambuzi kwamba matendo ya mtu yanauathiri ulimwengu na usitawi wa wanadamu na kupata utambuzi wa ukweli kwamba kila mtu anawajibika kwa matendo yake, mwenyewe.*

1. Fikiria maoni yaliyotolewa na mkufunzi “B” hapo juu. Si katika hali zote kwamba majibu kwa maswali ya mazoezi yanaweza kupatikani kwa kusoma tu nukuu zilizomo katika nyenzo. Kama mjuavyo, baadhi ya mazoezi hulenga kuwasaidia washiriki kufikiri kuhusu maana halisi ya vifungu kutoka Maandiko katika maisha ya kila siku. Usomaji wa Ufunuo unapaswa uelekeze kwenye jitihada thabiti za kutumia mafundisho, ambazo huhitaji kufikiri, kushauriana na kuchambua uelewa wa mtu kutokana na tajiriba. Kama mchakato huu haujaeleweka vizuri, tabia zisizofaa zinaweza kujitokeza kwa mtu binafsi au hata katika jumuiya. Kwa mfano, ikiwa mtu fulani mara kwa mara hunukuu kutoka “maandiko”, akivipuuzia vyanzo vingine vyote vya maarifa, na hukataa kabisa kuamini tajiriba iliyokusanywa, atakuwa mwenye akili finyu, kwa upande mwingine, mtu anayetilia sana umuhimu juu ya tajiriba na maoni ya watu na kudharau mamlaka ya Maandiko Matakatifu huangukia kwenye mtego wa aina ya uhusianishi wa kuamini kwamba kila kitu kinategemea utamaduni na matakwa ya mtu binafsi. Jadili pamoja na washiriki wa kikundi chako jinsi nafasi zote mbili zinavyoweza kusababisha ushirikina, kutovumiliana, ushupavu na uzembe.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

2. Jibu alilopokea mkufunzi “B” kutoa kwa “M” ambaye anahudumu kama mratibu wa mlolongo mkuu, linastahili tafakari fulani. Inaweza isitosheleze kwa washiriki kuweka tu alama kauli isiyo sahihi “Jambo fulani ni sahihi kama linakubaliana na maoni ya watu wengine.” Pengine utahitaji kujadili pamoja nao, kwa mfano, umuhimu wa kuwasikiliza wale wenye tajiriba husika na kutafuta ushauri wa busara juu ya masuaa mengi yanayotukabili maishani. Ili kuwezesha majadiliano kama hayo, kwa kawaida utapaswa kulifikia suala hili kulingana na ujuzi wako wa Maandiko. Ni yapi kati ya yafuatayo unafikiri mtu anapaswa kutafuta ushauri?

_____ Masomo ya mtu ya siku zijazo

_____ Jinsi ya kutoa umakinifu ufaao kwenye masomo ya mtu na huduma kwa Imani

_____ Ikiwa mtu anapaswa aitumikie Imani au la

_____ Maana ya ndoto anayoiota mtu

_____ Utumiaji wa mojawapo ya sheria za Imani katika mazingira fulani

_____ Ikiwa mtu anapaswa atii sheria za Imani au la

_____ Jinsi ya mtu kulea watoto wake

_____ Ikiwa mtu asanehewe kwa makosa aliyofanya au la

_____ Ikiwa mtu mwenye uhitaji asaidiwe au la

_____ Tiba kwa maradhi ya kimwili

______ Tatizo alilonalo mtu na rafiki yake

______ Ikiwa mtu apewe jukumu zito na mtu asiyemfahamu vizuri au la

3. Ingekusaidia kufikiria kuhusu maoni yaliyotolewa na mkufunzi "C" na maoni yaliyofuata yaliyotolewa na mratibu. Aghalabu, mtu anapojaribu kueleza wazo kwa wengine, mtu huangukia kwenye mazoea ya "kuwahubiria" watu. Lakini mbinu hii kwa nadra huleta matokeo yanayotarajiwa. Tazama zoezi lililojadiliwa na "C". Baada ya kumaliza zoezi, mkufunzi anaweza kuwaambia washiriki wattengeneze orodha ya mambo ambayo hawpaswi kufanya na kisha aongee nao kwa utondoti kiasi kuhusu umuhimu mienendo sahihi, akitambulisha katika mazungumzo matokeo ya kutotii sheria za kimaadili. Elezea kwa nini mbinu kama hiyo isingefaa wala kushauriwa.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 33

Hebu sasa tugeukie kwenye mazungumzo ya kubuni kati ya washiriki katika mkusanyiko wa wakufunzi. Sasa wanajadiliana juu ya sehemu iliyobaki ya kitengo cha kwanza cha Kitabu cha 1.

*A: Nilipata ugumu fulani kwenye swali la nne la Sehemu ya 4 nilipokuwa ninaipitia pamoja na kikundi. Washiriki walikuwa na mawazo tofauti kabisa kuhusu kama inawezekana kwa mtu kujidanganya mwenyewe, na ilikuwa vigumu kufikia muafaka.*

*M: Yapo maswali mengi kupitia vitengo mbalimbali ambayo makusudi yake ni kuchochea fikra na ushauriano. Masuala yaliyohusika yana utata sana kuweza kuamuliwa papo hapo na mtu huyo huyo anaweza kubadilisha maoni yake juu ya mada mara nyingi kadiri miaka inavyopita. Jibu kwa swali ulilolitaja linaonekana kuwa dhahiri: inawezekana kujidanganya mwenyewe na kwa hakika watu wengi hufanya hivyo. Hata hivyo, wapo wale watakao fikiri kwamba, katika uchambuzi wa mwisho, mtu anajua kwamba yeye anadanganya. Hili siyo jambo linaloweza kutatuliwa kwa urahisi. Kile tunachoweza kufanya ni kutoa mifano ya baadhi ya matukio na kuviomba vikundi vyetu kuamua kama kila tukio linawasilisha hali ya kujidanganya mwenyewe au la. Hivyo tunapaswa kusikiliza sababu zote zinazotolewa kwa majibu na kuridhika kwamba swali limeshajadiliwa na kwamba kila mmoja ameongeza uelewa wake. Baada ya yote, swali limeulizwa kwenye ngazi ya mwenendo, na siyo katika maana ya kifalsafa.*

*C: Pengine ninaweza kuwa naenda mbele zaidi lakini ningependa kushiriki pamoja nanyi tajiriba moja na kisha niulize swali. Katika kikundi chetu, nilianza kuhisi kwamba kila mmoja alipitia haraka Zoezi la 4 la Sehemu ya 8, ambalo hutuomba kuamua ikiwa*

*kauli ni kweli au si kweli. Kwa hiyo nilipendekeza kuwa tusite hapo na tuongee kuhusu nidhamu inayohitajika kuushinda usengenyaji—mada ya zoezi hilo. Majadiliano yalikuwa ya kuvutia sana. Tulitambua kwamba usengenyaji kwa kweli ni desturi ya kijamii; ni sehemu ya utamaduni wetu. Tuliendelea kubaini baadhi ya hatua za kivitendo ambazo zingetusaidia kuepukana na usengenyaji. Mazungumzo haya yalichukua takribani dakika kumi na tano. Kisha tulirudi kwenye zoezi, ambalo kwangu lilionekana kuwa lilitekelezwa kwa uelewa mzuri zaidi. Mnafikiri nilistahili kuwaomba kufanya majadilino kama hayo?*

*M: Ninafikiri ulistahili kabisa. Ulichukua fursa ya unyumbulifu ambayo ni sifa muhimu ya nyenzo kwa ajili ya kuongeza uelewa. Sote tunajua, bila shaka, kwamba zoezi la aina hii siyo kama yale ambayo wanafunzi wanapewa katika majaribio shuleni. Mazoezi ambayo hutuomba kuamua kauli zipi ni za kweli, aghalabu huibua mambo yasiyo dhahiri na huweka wazi athari za maneno na vitendo.*

*A: Ninatamani ningefanya kama ulivyofanya wakati kikundi chetu kilipokuwa kinasoma sehemu hiyo. Kwa kutazama baadhi ya matukio ya mafarakano tuliyo kuwa nayo hivi karibuni, ni dhahiri hatutambui kikamilifu madhara yanayoweza kusababishwa na usengenyaji katika kikundi cha marafiki.*

*B: Kuna kitu kilinitokea ambacho huenda kikawavutia. Mara ya kwanza niliposoma kitengo hiki, nilitambua kwamba ni lazima, ikibidi, kuwapa watu mifano ya mwenendo ambayo ni kinyume cha mafundisho ili kuamsha fikra kuhusu matumizi yake yanayofaa. Hivyo wakati kikundi ninachokihudumia sasa kama mkufunzi kilipofika kwenye Zoezi la 2 la Sehemu ya 6, ambalo kama mjuavyo linawaomba washiriki kupitia upya vifungu kadhaa vya maneno na kuamua kama vinatokana na "ulimi mwema", niliandaa maelezo yangu kidogo. Mmoja wa washiriki ana lugha kali na nilifikiri kwamba kama ningeongeza kwenye zoezi sentensi chache ambazo aghalabu yeye huzitumia, basi angeweza kuitambua tabia yake mbaya. Haya, sijui kama nilimuumiza. Maana niliposoma sentensi ya kwanza, kimya cha wasiwasi kilitanda kwenye kikundi na nikamuona akinitazama kwa mshangao. Ghafla, nilitambua kwamba mimi mwenyewe sikuwa mwema na nilijihisi vibaya sana. Hilo ni jambo ambalo kamwe sitalirudia tena.*

*M: Mazoezi yanayoonesha hali hasi yanasaidia pale tu yanapoweza kuchunguzwa kwa namna ya kujitenga, ambayo haiwezekani pale wanapomnyooshea mtu kidole. Sasa, ningependa kuwafahamisha jambo moja la mwisho kabla ya kumaliza majadiliano yetu ya kitengo cha kwanza. Ni muhimu kutopuuzia sehemu ya mwisho inayohusu usomaji wa Maandiko kila siku. Mtahitaji kujadiliana hili wakati wa kuisoma na kikundi na ikibidi, hata kuwasaidia washiriki kuchagua vifungu ambavyo wanaweza kuvisoma asubuhi na jioni kwa kipindi fulani. Kwa lengo hili, unapaswa kuhakikisha kwamba wote wana angalau nakala moja ya "Maneno Yaliyofichwa". La sivyo, itakubidi uhakikishe kwamba waweze kupata nakala moja. Katika mikutano inayofuata ya kikundi cha mafunzo, hivyo, unaweza kuwaomba wale wanaopenda kufanya hivyo kushiriki na wengine baadhi ya vifungu ambavyo wamevisoma.*

1. Katika kujibu maoni ya "A" kuhusu maswali manne yaliyomo katika Sehemu ya 4, mratibu anaeleza kwamba hilo ni mojawapo ya maswali mengi katika kozi zote yaliyokusudiwa tu kuamsha fikra na ushauriano na kwamba, badala ya kutumaini kufikia muafaka wa masuala kama hayo, wakufunzi wanapaswa kuridhika kuwasaidia washiriki kupiga hatua katika uelewa wao. Akiwa na hili akilini, mratibu hushauri

kwamba aghalabu inafaa katika hali hii maalum kwa mkufunzi kutoa mifano ya hali fulani fulani na kukiomba kikundi kuamua kama kila mfano huwakilisha hali ya kujidanganya mwenyewe au la. Jaribu kutoa baadhi ya mifano ambayo ungeweza kuwapa washiriki wa kikundi cha mafunzo kwa ajili ya kuamsha fikra zao.

____________________________________________________________

2. Kama ilivyotajwa na mratibu “M”, mazoezi yaliyomo katika nyenzo za Taasisi ya Ruhi ambamo washiriki wanaombwa kubaini kauli ambazo ni za kweli ni tofauti na aina ya maswali ya kuchagua yanayotolewa katika majaribio shuleni, ambayo aghalabu yanaweza kujibiwa bila kufikiri. Yamebuniwa kuwapitisha washiriki kupitia mlolongo wa mawazo au kuwasaidia kuchunguza dhana kutoka pande mbalimbali. Inapendekezwa kwamba upitie upya mazoezi ya aina hii katika kitengo cha kwanza cha Kitabu cha 1 na kikundi chako leo na mjadili jinsi yatakavyo tumika kukuza uelewa.

## SEHEMU YA 34

Baada ya kutafakari juu ya maoni ya kikundi cha wakufunzi na mratibu wa taasisi juu ya maudhui ya kitengo cha kwanza cha Kitabu cha 1, someni mazungumzo hapa chini kuhusu kitengo cha pili, “Sala”.

*A: Kikundi nilichokuwa nafanya nacho kazi, kilikuwa na shauku kubwa ya kuanza kitengo cha pili. Waliifurahia fursa ya kusoma vifungu virefu zaidi na kutafakari juu ya umuhimu wa sala. Lilionekana jambo la maana sana kwamba, tangu mwanzoni kabisa, waliweza kutambulishiwa dhana ya “njia ya huduma” na “kusudi la kimaadili lenye pande mbili”. lliwasaidia kupata umaizi wa uhusiano wa karibu kati ya sala na huduma kadiri wanavyosonga mbele kupitia sehemu hadi sehemu. Tulipitia nukuu nne katika Sehemu ya 1 na maswali yahusianayo kwa namna hiyo hiyo tuliyoitumia katika kitengo cha kwanza. Walikuwa wepesi kuelewa maana ya papo hapo ya vifungu na kupata kianga cha kusudi la kimaadili lenye pande mbili kwenye msingi wake. Tulipofika kwenye Zoezi la 5, ilikuwa muhimu kusita kidogo na kuchunguza kauli zilizowasilishwa kulingana na nukuu hizo. Kwa mfano, baadhi ya washiriki walipata changamoto kwa kauli: “Kama daima unawasaidia wengine, mwishowe utapoteza mwelekeo wa malengo yako mwenyewe.” Majadiliano yalimsaidia kila mmoja kuona kwamba “huduma kwa wengine” na “malengo binafsi” huhitilafiana ikiwa tu malengo yamewekwa kwa namna ambayo ni ya ubinafsi. Waliweza kuona kwa uwazi kwamba nia yetu ikiwa safi, tutajiwekea malengo bora ya kuwatumikia wengine na kwamba, pindi tutakapo tambua kwamba kusudi la kuumbwa kwetu ni kushughulikia uboreshaji*

*wa ulimwengu, ndipo utafutaji wa maendeleo yetu wenyewe ya kiroho na ya kiakili utakapoonwa kama kitu kisichoweza kutenganishwa na mchango wetu kwa maendeleo ya jamii.*

B: *Tulifanya vivyo hivyo katika kikundi chetu juu ya kauli hizo. Nilihakikisha, bila shaka, kwamba majadiliano hayakurefushwa sana na kwamba tuliendelea kumakinikia kile ambacho zoezi linajaribu kufanikisha. Kwa mfano, watu wengi siku hizi huamini katika kauli "Wewe mwenyewe ndiye rafiki yako wa karibu kabisa." Tunahitaji kuchunguza matokeo yake katika muktadha wa rehema ya Mungu—jinsi moyo safi ulivyo pokevu kwa majaliwa Yake kama ilivyotajwa katika nukuu ya mwisho hiyo sehemu ile. Kwa kawaida washiriki walihitimisha kwamba Mungu ndiye Rafiki yetu wa kweli.*

C: *Katika kusoma kifungu kilichomo katika Maneno Yaliyofichwa kilichonukuliwa katika Sehemu ya 2, tulifanya majadiliano ya kina juu ya maana yake kwamba sisi tumeumbwa "tajiri", tukitambua kwamba siyo mali za kimwili zinazotutajirisha bali ni uwezo tulionao wa kudhihirisha sifa za kiroho kama vile unyenyekevu, ukweli na ukarimu. Ndipo tungeweza kuunganisha wazo na sifa za moyo ambao umesafishwa "kwa mng'ao wa upendo na kuachana na vyote ila Mungu" na kutafakari juu ya jinsi, katika jitihada zetu kutakasa mioyo yetu kutokana na vyote ila Yeye, ni kawaida tutafute "kuangaziwa" kutoka kwenye chanzo cha ujuzi wote, Muumba wetu, Rafiki yetu wa kweli. Majadiliano yetu pia yanatusaidia kupata umaizi zaidi kuhusu asili ya uhusiano wetu na Mungu, kama ule wa upendo, jambo ambalo limetuandalia njia kwa ajili ya mashauriano yetu katika Sehemu ya 3, ambayo huuliza swali, "Kwa nini tunasali?"*

M: *Inaonekana kwamba washiriki ambao umesoma nao kitengo hicho walitafakari kwa kina juu ya Maandiko yaliyonukuliwa katika sehemu hizi za mwanzoni na kwamba mazoezi yalirahisisha majadiliano ya kina na kuongeza uelewa wao wa dhana inayoongelewa.*

C: *Kuhusiana na mazoezi, niligundua washiriki walikuwa makini kufanya yale yanayouliza kuhusu maana ya maneno maalum—"imba", "tongoa", "tawanya", "faradhi". Tulitunga sentensi mbalimbali kwa kila neno ili kuhakikisha kwamba maana yake inaeleweka na, mara moja au mbili, tulitumia kamusi.*

M: *Nafikiri kile ulichofanya ni sawa. Kama ilivyoelezwa katika sehemu ya "Mawazo Machache kwa Mkufunzi", hakuna sheria inayokataza matumizi ya kamusi wakati hadi wakati. Ni kwamba tu maneno yanapaswa kueleweka ndani ya muktadha, hususan pale ambapo vifungu kutoka Maandiko vinahusika. Vinginevyo, majadiliano juu ya maana ya neno moja au mawili yanayofanana na tofauti kati yao, yanaweza kufika mbali sana. Wakati mwingine pale watu wanapojaribu kuitazama nukuu neno kwa neno, kusudi kuu zaidi, ambalo ni kuelewa maana ya kifungu, husahaulika. Hivyo, kwa mfano, katika Sehemu ya 6 katika kitengo kinachohusu sala, maswali kuhusu maana ya maneno "imba", "tongoa" na "tawanya" yamewekwa hapa kwa ajili ya kuwamakinikisha washiriki juu ya baadhi ya dhana zilizomo katika kifungu kilichonukuliwa; dhana hizo siyo mazoezi ya kujua msamiati.*

B: *Kuna aina nyingine ya zoezi lililotambulishwa katika Sehemu ya 2 ya kitengo ambalo washiriki wa kikundi cha mafunzo nilichokitaja awali waliliona la kufaa sana. Ni lile ambamo washiriki wanaombwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi katika sentensi, kulingana na kifungu kutoka kwenye Maandiko.*

*C: Nimetanabahi kwamba hii ni aina ya mbinu inayotumika katika vitengo mbalimbali vya vitabu. Inawasaidia washiriki kufikiri kuhusu kifungu kwa kuwamakinikisha juu ya baadhi ya maneno muhimu.*

*M: Sasa kwa kuwa tumeshajadili kusudi la baadhi ya mazoezi, hebu turudi kwenye fikra ya dhana nyingine muhimu katika kitengo hiki. Jinsi gani washiriki walivyoipokea dhana ya "hali ya sala" iliyotambulishwa katika Sehemu ya 5?*

*B: Washiriki wengi ambao niliokuwa nasoma nao kitengo hicho, kamwe walikuwa hawajawahi kufikiria sala kwa namna hiyo. Kama mimi mwenyewe niliposoma kitengo hicho kwa mara ya kwanza, wao pia waliifikiri sala kama kitu tu ambacho unakifanya, wala siyo kama hali ambayo unajitahidi kuifikia. Hivyo, tulisita kidogo na kuongea kuhusu wazo hilo, kabla ya kuendelea na sehemu inayofuata.*

*C: Nilipata tajiriba kama hiyo hiyo wakati wa kusoma Sehemu ya 8, ambapo majadiliano juu ya kusudi la sala yaliyoanza katika Sehemu ya 3 yanaendelezwa. Kwa washiriki wachache, wazo la kujifungamanisha na Mapenzi ya Mungu lilikuwa jipya. Mwanzoni, halikueleweka kwao jinsi gani tungemuomba Mungu, tukimuomba akidhi mahitaji yetu, na wakati huo huo turidhike na chochote kile ambacho Yeye huamuru kwa ajili yetu. Lakini baada ya kutafakari zaidi juu ya nukuu kutoka kwa 'Abdu'l-Bahá, tuliweza kupata umaizi kidogo wa kiroho katika suala hili.*

*M: Dhana zote hizi ni muhimu kuzichunguza. Kwa bahati mbaya, kadiri hisia ya kidini inavyopoteza kina chake ulimwenguni, watu wengi zaidi na zaidi ama hawasali au huichukulia sala kama kaida. Pia kuna mwelekeo wa kusali pale tu mtu anapokuwa katika hali ya hatari. Ndio maana kutafakari juu ya dhana muhimu kama hizo zinazohusu sala ni jambo la lazima kwa wale wanaotaka kuishi maisha yaliyojikita kwa Mungu na juu ya huduma katika njia Yake. Kwa maana hii, kile tulichosema mwanzoni mwa tafakari yetu, kuhusu jinsi usomaji wa kitengo hicho unavyotoa umaizi wa uhusiano wa karibu kati ya huduma na sala, ni muhimu hasa. Wakati washiriki wanahitimisha kitengo hicho, watahitaji kuwa wamepata utambuzi wa juu zaidi wa uhusiano huu—jinsi sala ya kweli inavyotakasa moyo, kuufanya chombo kinachopokea ujuzi na sifa za mbinguni, na jinsi vitendo vya huduma visivyo na ubinafsi vinavyomwezesha mtu kuchota kutoka sifa hizi ili kuchangia kwenye maendeleo ya Hoja na uinuaji wa jamii ya wanadamu. Sala huongeza sana shauku ya kumtumikia Mungu, na huduma huchochea moto unaotolewa wakati wa kumuomba Yeye—moto ambao huziteketezea mbali tando zinazotuzuia kuufikia uzuri Wake.*

*A: Nina swali kuhusu Sehemu ya 7. Hapa washiriki wanaombwa kukariri vifungu viwili, ambavyo vinatoka kwenye Sala Ndefu ya Faradhi. Je, ningepaswa kuwahamasisha kukariri sala nzima?*

*M: Kama ilivyo kwa mambo mengine mengi, hili hutegemea juu ya washiriki. Baadhi watakuwa ndio tu wanaanza kupata tabia ya kusali kila siku, hivyo kukariri vifungu viwili vilivyopendekezwa itatosha. Baadaye, wanaweza kujifunza sala nzima. Bila shaka, baadhi pengine tayari wamekwishaikariri Sala Ndefu ya Faradhi. Kwa hali yoyote ile, nahisi kwamba, kama wakufunzi wa kozi, lingekuwa wazo zuri kama sote tungeweza kuikariri, kama bado hatujafanya hivyo.*

1. Mathalani, wakati wa kusoma Sehemu ya 8, washiriki wa kikundi cha mafunzo wanapata shida na dhana zilizotajwa na "C" hapo juu. Jinsi gani ungewasaidia kupata umaizi kuhusu nguvu za sala? Ni maswali gani kulingana na nukuu tatu za sehemu hiyo ungeweza kuwauliza ili kukuza uelewa wao wa dhana husika?

____________________________________________________

____________________________________________________

____________________________________________________

____________________________________________________

____________________________________________________

____________________________________________________

2. Tumezungumzia mara nyingi kuhusu umuhimu wa kukariri ikiwemo katika kitengo hiki. Hadi sasa, wewe mwenyewe umekariri vifungu vingi na unajua thamani ya kuweza kuchota kutoka uwezo wa Neno la Uumbaji, iwe katika nyakati za tafakari yako binafsi, nyakati za shida au katika ufundishaji Hoja. Tajiriba kubwa uliyoipata sasa itakuwa ya msaada kwako katika kufanya kazi na washiriki wa kikundi cha mafunzo. Hadi kufikia hapa, ingefaa kwako kuchunguza jinsi ambavyo unaweza kuwahamasisha kufanya jitihada zaidi ya kukariri vifungu kutoka kwenye Maandiko. Baada ya kufanya hivyo, pengine ungependa kukariri kifungu kifupi kifuatacho:

**". . . na kila kifua kitakachokariri Maneno Yake, Mungu atakisababisha, kama kikiwa kile cha muumini, kijazwe na upendo Wake . . ."**[12]

## SEHEMU YA 35

Kitengo cha tatu cha Kitabu cha 1, "Uhai na Kifo", kinatoa changamoto maalum kwa washiriki na wakufunzi kadhalika. Hebu tutazame jinsi kikundi cha wakufunzi kinavyoweza kupitia upya kitengo hiki. Unaweza kukigeukia kitengo hicho sasa.

*A: Ingawa kuhudumu kama mkufunzi wa kozi hii ilikuwa vigumu, niliona ya manufaa. Sasa ninaelewa ina maanisha nini kwa ile kauli katika sehemu ya "Mawazo Machache kwa ajili ya Mkufunzi" kwamba uhusiano kati ya mkufunzi na washiriki wengine siyo yale ya mwalimu-kwa-mwanafunzi, kwamba wote wanajihusisha kwa makusudi katika mchakato ambamo kila mmoja anatafuta kujifunza. Nilipata umaizi mwingi wakati wa kusoma nyenzo hiyo na kikundi. Nilikuwa ninafikiri, kwa mfano, kwamba mazoezi katika sehemu ya tatu yalikuwa wazi kabisa, kwa hiyo nilishangazwa wakati baadhi ya washiriki walipoweka alama ya "kweli" mbele ya kauli katika Zoezi la 2 kwamba "Maisha hujumuisha vitu ambavyo vinatokea kwetu kila siku." Na wakati tulipofikia zoezi la aina hiyo hiyo katika sehemu iliyofuata, wachache miongoni mwa washiriki wale wale waliweka alama ya kweli kwa kauli kwamba "Kifo ni mwisho wa uhai" na "Uhai unakwisha wakati wa kifo". Nilitambua kwamba tunahitaji kuijadili mada hii kidogo zaidi. Baadhi ya maoni yaliyotolewa katika ushauriano wetu yalikuwa ya kuvutia sana na yaliongoza kwenye uwazi katika akili za washiriki.*

*B: Pia niligundua, kwamba, mazoezi haya yalitusaidia sana kufikiria juu ya mawazo. Katika Sehemu ya 9, washiriki wengi waliweka alama ya kweli kwa kauli kwamba*

*"Uhai wa kweli huanza pale mtu anapokufa na kwenda kwenye Ufalme mtakatifu". Kisha wakaja kwenye kauli iliyofuata, "Uhai wa kweli huanza katika ulimwengu huu na huendelea baada ya kifo cha kimwili", na walitambua kwamba, kama kauli hiyo ilikuwa kweli, ile ya hapo juu haikuwa wazi kama walivyodhani. Niliona kwamba kila mmoja alikuwa akifikiria kwa kina kuhusu asili ya roho. Ilitubidi kuahirisha mwishoni mwa sehemu hiyo kwa siku hiyo na, labda ilikuwa fikra zangu tu, lakini niligundua mabadiliko katika kila mmoja tulipokutana juma lililofu.*

A: *Kitengo hiki kiliwasaidia washiriki katika kikundi chetu kupata uelewa kamili wa uwezo wa roho ya mwanadamu. Sehemu chache za mwanzoni, hususan, zilisaidia kuondoa baadhi ya dhana potofu kuhusu roho kadiri wao walivyo endelea kutafakari juu ya kweli za kina za kiroho—kwamba roho haingii wala kutoka mwilini; kwamba ingawa huvitumia viungo vya kimwili kutambua na kufanya ushawishi, inaweza pia kutenda bila viungo hivyo; na kwamba sitiari ya kioo na mwanga hueleza vizuri kabisa uhusiano wake na mwili. Kioo huakisi mwanga, lakini mwanga huendelea kung'aa hata kama kioo hicho kimetandwa na vumbi au kuvunjika.*

M: *Sababu inayowafanya watu waone kitengo hicho kinavutia ni hasa kwa sababu kinauliza maswali mengi kuhusu maisha ya roho katika ulimwengu huu na malimwengu yanayofuata ya Mungu. Kuhusiana na kuishi maisha yanayoelezwa katika mafundisho ya Kibahá'í, 'Abdu'l-Bahá alinukuliwa akisema kwamba jambo la kwanza la kufanya ni kupata kiu kwa ajili ya hali ya kiroho. Ili kupata kiu hii, Yeye ameshauri kuwa mtu anapaswa kutafakari juu ya maisha baada ya kifo.*

C: *Tulipokuwa tunasoma Sehemu ya 12, tulikuwa na majadiliano ya kuvutia sana kuhusu swali hili, "Kwa nini roho ibadilishe makazi yake ya mbinguni kwa ajili ya mavumbi ya ulimwengu huu?" Mshiriki mmoja wa kikundi aliibua hoja kwamba hali ya kiroho siyo kitu ambacho mtu hukipata mara moja tu halafu basi na kwamba mtu daima anatakiwa kujitahidi kuitawala asili yake ya chini. "Daima kuna kitu kinachojaribu kutuvutia chini," yeye alipendekeza. Hili lilimsukuma mshiriki mwingine kuibua suala la tamaa. Aliweka wazi kwamba ni katika asili ya moyo wa mwanadamu kutamani na kwamba inatupasa tuondokane wenyewe na tamaa za kipuuzi. Kisha tulijadiliana kuhusu asili ya tamaa. Tuliongelea kuhusu ukweli kwamba baadhi ya tamaa ni nzuri, kwa mfano, tamaa ya kufanya kazi kwa bidii ili kuboresha hali ya kimwili ya mtu. Lakini tuliamua kwamba hata hizi zinapaswa ziwe na mipaka fulani. Kama mtu hufanya kazi kwa bidii ili kuboresha raha zake za kimwili kiasi kwamba huingilia huduma ya mtu kwa Hoja na jamii ya wanadamu, tamaa hii itakuwa imegeuka kuwa kitu kingine, labda uroho. Halafu mtu mmoja aliuliza, "Vipi kuhusiana na tamaa ya kumpendeza Mungu?" Na tulitambua kwamba kuna tamaa ambazo hatupaswi kujaribu kuziwekea mipaka. Tuliamua kwamba, kwa kweli, kadiri shauku za kiroho zinavyokuwa na nguvu zaidi, ndivyo zinavyoweza kuzidhibiti tamaa zetu za kipuuzi na kuziweka mahali pake panapofaa.*

A: *Kile ulichosema kuhusu tamaa kimenikumbusha sehemu nyingine katika kitengo hicho, ambayo ilinipa ugumu kidogo. Katika Sehemu ya 18, washiriki wanaombwa kutaja baadhi ya "fikra za bure". Kwa sababu yoyote ile, washiriki wa kikundi chetu walipata wakati mgumu kufikiria hata mojawapo. Nilidhani wangeweza kuzitaja japo chache, hivyo nilikuwa sijajiandaa mapema. Hali ilikuwa ya kufedhahesha.*

*M: Ni sawa kuwa na nyakati hizi za fedhaha mara kwa mara. Haupaswi kukata tamaa. Hiyo ndio maana ya "kupata tajiriba". Sasa kwa kuwa umeshiriki nasi tajiriba yako, sote tunatambua kwamba ni wazo zuri kuwa na orodha fupi za "fikra za bure", ikitokea tumejikuta katika hali kama hiyo.*

*B: Pia ningependa kushiriki kidogo kuhusu majadiliano ya Sehemu ya 19 pamoja na marafiki niliosoma nao. Kile alichosema 'Abdu'l-Bahá kuhusu athari ya sala juu ya maendeleo ya roho ya wale waliotangulia kiliwafungua fikra. Wazo kwamba wangeweza kuwasaidia wapendwa wao katika malimwengu ya yajayo liliwafariji na kuwafurahisha sana washiriki wawili ambao hivi karibuni walikuwa wamepatwa na msiba.*

1. Katika mabadilishano ya mawazo hapo juu, mratibu wa mlolongo mkuu hushauri kwamba lingekuwa wazo zuri kwa wakufunzi kuandaa mapema orodha fupi ya mifano ya "fikra za bure" kwa ajili ya kuwasaidia washiriki kutekeleza zoezi la Sehemu ya 18. Ingefaa kutazama sehemu hiyo na kutengeneza orodha kama hiyo katika nafasi hapa chini.

______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________

2. Bila shaka, kuna mazoezi mengine katika kitengo hicho ambayo yanaweza kuwa yenye changamoto kwa washiriki. Pengine ungependa kuorodhesha baadhi hapa:

______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________

## SEHEMU YA 36

Tulianza kitengo hiki kwa kutazama kwa ufupi suala la hamasa, tukichunguza baadhi ya vyanzo vyake vya msingi, ikiwemo kiu ya ujuzi na mvuto kwa uzuri. Hili lilituongoza moja kwa moja kwenye majadiliano juu ya suala la ushiriki. Kisha tulifanya uchunguzi wa mitindo

ya ufundishaji-ujifunzaji ambayo kozi za Taasisi ya Ruhi hujitahidi kuikuza na baadhi ya dhana na kanuni zinazobumba kozi hizi. Hii ilitufungulia njia ya kufikiria vipengele vitatu vikuu vya mfumo wa kielimu wa Taasisi: mlolongo mkuu wa kozi, kikundi cha mafunzo na mkufunzi. Tumetaja kwamba usomaji wa Kitabu cha 7 hukuweka kwenye njia ambamo utaendelea kukuza uwezo uhitajikao kusaidia kikundi hadi ya kikundi kupitia kozi. Utaendelea kukuza uwezo wako kuhudumu kama mkufunzi kupitia tajiriba endelevu kama hiyo na kupitia ushiriki wako katika mikusanyiko ya mara kwa mara ya tafakari ya wakufunzi. Sasa umeshapewa kianga cha kile ambacho mikutano hii itahusisha. Inatumainiwa kwamba, hadi hapa, utakuwa mwenye shauku ya kuingia katika eneo hili la huduma. Wakufunzi wengine wenye tajiriba zaidi wanaohudumu katika jumuiya yako, au mratibu wa klasta kwa ajili ya usomaji wa mlolongo mkuu, wapo tayari kukusaidia.

Katika sehemu hizi za mwisho, kwa hiyo, hebu tuchukue fursa kutazama athari tunazoweza kutarajia kushuhudia kadiri idadi ikuayo ya marafiki katika kijiji au ujirani itakavyo endelea kuhusika katika usomaji wa kozi na vitendo vya huduma zinavyo vipendekeza. Unajua kwamba kuna wahusika watatu katika ujenzi wa ustaarabu mpya: mtu binafsi, jumuiya, na asasi. Mbele zaidi katika mlolongo mkuu, tutachunguza mchango unaotolewa na mchakato wa kielimu kwa maendeleo ya kila mmoja. Kwa sasa, hebu tumtazame mtu binafsi na kufikiria athari juu ya washiriki katika kikundi cha mafunzo. Ikiongelea juu ya "mjongeo usiozuilika" ambao mchakato huu unataka kuuanzisha miongoni mwa watu, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu huandika:

> **"Jambo muhimu ni kwamba ubora wa mchakato wa kielimu unaokuzwa kwenye ngazi ya kikundi cha mafunzo uinuke dhahiri katika kipindi cha mwaka mmoja ujao ili uwezo wa wakazi wa mahali kuunda mtindo kama huo unatambulika. Mengi yataangukia juu ya wale wanaohudumu kama wakufunzi kuhusu suala hili. Yao itakuwa changamoto ya kuweka mazingira ambayo yametazamiwa katika kozi za taasisi, mazingira rafiki kwa ajili ya uwezeshaji wa kiroho wa watu binafsi, ambao watakuja kujiona wenyewe kama mawakala amilifu wa ujifunzaji wao wenyewe, kama wahusika wakuu wa juhudi endelevu za mara kwa mara za kutumia ujuzi ili kuleta mabadiliko ya mtu binafsi na ya pamoja."**[13]

Hapa chini kuna baadhi ya sifa ambazo mchakato wa kielimu ambao ni wa uwezeshwaji wa kimaadili na kiroho huukuza kwa mtu binafsi. Ongeza zingine chache kwenye orodha.

- Unyofu wa mwenendo
- Kumtegemea Mungu
- Furaha tele na wangavu wa moyo
- Ukarimu wa roho, usafi wa moyo na uwazi wa kiakili
- Uelewa unaozidi kuimarika wa mwongozo uliomo katika Ufunuo wa Bahá'u'lláh
- Kiu iongezekayo ya ujuzi
- Kutegemea juu ya uwezo ubadilishao wa Neno la Mungu
- Uhuru kupitia utiifu kwa sheria za Bahá'u'lláh
- Shauku ya kufikia ubora unaowashwa na mvuto kwa uzuri
- Utambuzi wa umoja wa jamii ya wanadamu na upendo wa kina kwa wanadamu

- Utambuzi madhubuti wa historia na nafasi ya mtu ndani yake
- Ari na shauku kali ya kufundisha Hoja na kuitumikia jamii ya wanadamu
- Mweleko wa ujifunzaji
- Shauku ya kuendeleza kusudi la kimaadili lenye pande mbili—kufuatilia ukuaji wake binafsi wa kiroho na wa kiakili na kuchangia kwenye mabadiliko ya jamii
- Uwezo wa kukabidhi mapenzi ya mtu kwenye Mapenzi ya Mungu
- Uthabiti mbele ya mitihani na majaribu
- Kujidhatiti katika utumiaji wa mafundisho katika maisha ya mtu
- Kiwango kikubwa cha kujitoa kwa ajili ya maendeleo ya kiroho ya watu wake
- Utambuzi wa uwezo wa kiroho ambao kwake kila mtu anaweza kuchota
- Uwezo wa kushiriki katika shughuli za jumuiya kama mshiriki mwenye dhamira wakati huo huo mnyenyekevu
- Uwezo wa kuchangia kwenye muafaka na makubaliano kupitia ushauri

- ________________________________________________
- ________________________________________________
- ________________________________________________
- ________________________________________________
- ________________________________________________
- ________________________________________________
- ________________________________________________
- ________________________________________________
- ________________________________________________
- ________________________________________________
- ________________________________________________
- ________________________________________________
- ________________________________________________

## SEHEMU YA 37

Sura mbalimbali za vikundi vya mafunzo ambavyo kwavyo utavihudumia kama mkufunzi zichangia kwenye maendeleo ya tabia ambazo umezibaini. Hapa chini kuna sura hizi kadhaa. Kwa kila moja andika sentensi kadhaa zinazoelezea jinsi inavyokuza tabia moja au zaidi miongoni mwa zile zilizopo hapo juu. Kwa kila moja, mfano umetolewa ili kukusaidia.

1. Mazingira ya upendo ambayo hupenya katika kikundi cha mafunzo:

   a. Mazingira ya upendo ambayo hupenya katika kikundi cha mafunzo huimarisha upendo wa washiriki kwa wanadamu.

b. ____________________

c. ____________________

2. Moyo wa urafiki ulioundwa miongoni mwa washiriki katika kikundi cha mafunzo:

   a. Moyo wa urafiki katika kikundi cha mafunzo huimarisha kujitoa kwa washiriki kwa ajili ya maendele ya kiroho ya watu wao.

   b. ____________________

   c. ____________________

3. Mazingira yenye nidhamu ya kiroho ambamo kikundi cha mafunzo hukutana:

   a. Mazingira yenye nidhamu ya kiroho ambamo kikundi cha mafunzo hukutana, huwasaidia washiriki kupata uhuru kupitia utiifu kwa sheria za Bahá'u'lláh.

   b. ____________________

   c. ____________________

4. Mbinu shirikishi inayotumiwa na Taasisi ya Ruhi:

   a. Mbinu shirikishi inayotumiwa na Taasisi huzalisha shauku ya kuendeleza kusudi la kimaadili lenye pande mbili— kufuatilia ukuaji wake binafsi wa kiroho na wa kiakili na kuchangia kwenye mabadiliko ya jamii.

   b. ____________________

   c. ____________________

5. Mdundo wa ujifunzaji uliowekwa na kila kikundi:

   a. Mdundo wa ujifunzaji uliowekwa na kila kikundi huimarisha uwezo wa washiriki kushiriki katika shughuli za jumuiya kama mshiriki mwenye dhamira wakati huo huo mnyenyekevu.

b. ______________________________

______________________________

c. ______________________________

______________________________

6. Msisitizo unaotolewa kwenye usomaji wa Maandiko Matakatifu:

   a. Msisitizo juu ya usomaji wa Maandiko Matakatifu huibua furaha na wangavu wa moyo.

   b. ______________________________

   ______________________________

   c. ______________________________

   ______________________________

7. Kukariri sala na vifungu kutoka katika Maandiko:

   a. Kukariri sala na vifungu kutoka katika Maandiko huchangia uwazi wa akili.

   b. ______________________________

   ______________________________

   c. ______________________________

   ______________________________

8. Mazoezi katika nyenzo yanayomakinikia juu ya maana ya papo hapo ya vifungu kutoka katika Maandiko:

   a. Mazoezi yanayomakinikia juu ya maana ya papo hapo ya vifungu kutoka katika Maandiko huongeza uwezo wa washiriki kufikia muafaka kupitia ushauriano.

   b. ______________________________

   ______________________________

   c. ______________________________

   ______________________________

9. Mazoezi yanayowasaidia washiriki kuona maana halisi ya Maandiko katika maisha yao ya kila siku:

   a. Mazoezi yanayowasaidia washiriki kuona maana halisi ya Maandiko katika maisha yao ya kila siku huimarisha kujitoa kwao kwa kazi inayoendelea ya utumiaji wa mafundisho.

b. ______________________________________________

______________________________________________

c. ______________________________________________

______________________________________________

10. Mazoezi yanayojaribu kuleta umaizi wa maana ya vifungu kutoka katika Maandiko:

   a. Mazoezi yanayojaribu kuleta umaizi wa maana ya vifungu kutoka katika Maandiko huimarisha uelewa wa washiriki wa mwongozo uliomo katika Ufunuo wa Bahá’u’lláh.

   b. ______________________________________________

   ______________________________________________

   c. ______________________________________________

   ______________________________________________

11. Unyumbulifu ambao kiasili umo katika mbinu ya kielimu ya Taasisi ya Ruhi:

   a. Unyumbulifu ambao kiasili umo katika mbinu ya kielimu huchangia kwenye maendeleo ya mielekeo ya lazima wa mwelekeo wa ujifunzaji.

   b. ______________________________________________

   ______________________________________________

   c. ______________________________________________

   ______________________________________________

12. Vitendo mahsusi vya huduma ambavyo washiriki wa kikundi cha mafunzo hutekeleza:

   a. Vitendo vya huduma ambavyo washiriki wa kikundi cha mafunzo hutekeleza huonesha ari na shauku kali ya kufundisha Hoja na kuitumikia jamii ya wanadamu.

   b. ______________________________________________

   ______________________________________________

   c. ______________________________________________

   ______________________________________________

## SEHEMU YA 38

Tafakari zilizomo katika sehemu mbili zilizotangulia lazima zitakuwa zimekuhakikishia tena Imani yako kwamba ili aweze kuwa mkufunzi anayefaa, mtu lazima ajifunze kuwalea wengine na kutengeneza mazingira rafiki ndani ya kikundi cha mafunzo kwa

ajili ya uwezeshaji wa kimaadili na wa kiroho wa washiriki wake. Unahitaji kujifunza ustadi wa uhamasishaji na kukuza wa uwezo wa kutambua na kuachilia uwezo uliofichika. Hii huwezekana tu kama ukijitenga mwenyewe na mafanikio yako na kufurahia ukuaji na maendeleo ya rafiki zako. Kwa hakika, hii inaweza kuwa siri ya mkufunzi bora.

Hebu tumalizie kitengo hiki kwa kutafakari juu ya vifungu viwili vifuatavyo kutoka katika Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá:

> **"Enyi marafiki, onesheni wazi uaminifu wenu! Enyi wapendwa wangu, dhihirisheni uthabiti wenu na uimara wenu! Ee enyi mliitao Jina Lake, mgeukieni na mlishikilieni kwa uthabiti Yeye! Ee enyi ambao mmeinua mioyo yenu na kusihi msaada Wake, mng'ang'anieni Yeye na tembeeni katika njia Zake! Inampasa kila mmoja wetu kuhamasishana, kufanya jitihada za hali ya juu kueneza manukato Yake matakatifu na kujishughulisha katika utukuzaji wa Neno Lake. Lazima, wakati wote, tuguswe na upepo mwanana uvumao kutoka katika bustani ya mawaridi ya wema Wake wa upendo, na kupuliziwa manukato ya maua ya siri ya neema Yake. Lazima tuipe ari na shauku kubwa ile mioyo ya waadilifu na kuleta shangwe na furaha kubwa kwenye roho za waaminifu."**[14]

> **". . . Hoja ya Uzuri wa Kale ndiyo kiini hasa cha upendo, njia hasa ya umoja, ipo tu ili wote waweze kuwa mawimbi ya bahari moja, na nyota angavu za anga moja isiyo na mwisho, na lulu ndani ya koa la upekee, na vito ving'aavyo vilivyochimbwa kutoka katika migodi ya umoja; kwamba waweze kuwa watumishi mmoja kwa mwingine, wapendane, wabarikiane, wasifiane; kwamba kila mmoja aweze kulegeza ulimi wake na kuwasifu wenzake bila kubagua, kila mmoja akitoa shukrani yake kwa wengine wote; kwamba wote wainue macho yao hadi kwenye upeo wa utukufu, na kukumbuka kwamba wanaunganishwa na Kizingiti Kitakatifu; kwamba wasione chochote bali mazuri ya mmoja kwa mwingine, wasisikie chochote bali sifa za mmoja kwa mwingine, na wasisemezane neno lolote bali la kusifu."**[15]

# MAREJELEO


1. ‘Abdu’l-Bahá, katika *Elimu ya Kibahá’í: Dondoo kutoka Maandiko ya Kibahá’í*, zimekusanywa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu (Ingleside: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, Australia, 2020), na. 27, ku. 18–19.

2. ‘Abdu’l-Bahá, katika *Sala za Kibahá’: Uteuzi wa Sala Zilizofunuliwa na Bahá’u’lláh, Báb, na ‘Abdu’l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2002, chapisho la 2020), ku. 113–14.

3. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1983, chapisho la 2017), CLI, aya. 3, na. 5, ku. 363–65 (toleo la Kiingereza).

4. Shoghi Effendi, *Mungu Yu Nasi* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1974, chapisho la 2022), uk. 340 (toleo la Kiingereza); pia imenukuliwa katika *Kitáb-i-Aqdas: Kitabu Kitakatifu Kabisa* (Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, New Delhi, India chapisho la Kiswahili la 2024), uk. 14.

5. Kutoka ujumbe wa 27 Desemba 2005 kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Mabara iliyochapishwa katika *Mahali pa Kugeukia: Jumbe Zilizoteuliwa za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na Nyenzo za Kujaliza, 1996–2006* (Shirika la Uchapishaji la West Palm Beach: Palabra, 2006), na. 35.5, ku. 196–97.

6. Kutoka ujumbe wa 28 Desemba 2010 kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Mabara, iliyochapishwa katika *Muundo wa Utendaji: Jumbe Zilizoteuliwa za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na Nyenzo za Kujaliza, 2006–2016* (Shirika la Uchapishaji la West Palm Beach: Palabra 2017), na. 16.16, ku. 103–4.

7. Kutoka ujumbe wa 12 Desemba 2011 iliyoandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Mabaraza yote ya Kiroho ya Kitaifa, kama hapo juu, na. 20.5–6, uk. 131.

8. Kutoka ujumbe wa 1 Januari 2022 iliyoandikwa kwa Mabaraza yote ya Kiroho Kitaifa, iliyochapishwa katika *Mpango wa Miaka Tisa, 2022–2031: Jumbe za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu* (Shirika la Uchapishaji la West Palm Beach: Palabra: 2022), na. 7.7, ku. 79–80.

9. Kutoka ujumbe wa Riḍván 2010 wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Wabahá’í wa Ulimwengu, uliochapishwa katika *Muundo wa Kiutendaji*, na. 14.10, uk. 79.

10. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh*, XCIV, aya. 4, uk. 219 (toleo la Kiingereza).

11. Kutoka Waraka wa ‘Abdu’l-Bahá. (tafsiri iliyoidhinishwa)

12. *Mateuzi kutoka Maandiko ya Báb* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2006, chapisho la 2014), na. 3:27:2, uk. 128.

13. Kutoka ujumbe wa Riḍván 2010 wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Wabahá’í wa ulimwengu, iliyochapishwa katika *Muundo wa Kiutendaji*, na. 14.11, uk. 79.

14 *Mwangaza wa Ulimwengu: Nyaraka Zilizoteuliwa za ‘Abdu’l-Bahá* (Haifa: Makao Makuu ya Kiahá’í ya Ulimwengu, 2021), na. 56.7, ku. 139–40.

15. *Mateuzi kutoka Maandiko ya ‘Abdu’l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2010, chapisho la 2015), na. 193.5, uk. 317.



# Ukuzaji Sanaa Mashinani

## Kusudi

Kutambua nafasi ya jitihada za kisanii katika kuendeleza mchakato wa kielimu unaokuzwa na kozi za taasisi na katika kuimarisha mtindo wa maisha ya jumuiya inaoubumba.

## SEHEMU YA 1

Kama mwana-jumuiya wa jumuiya ikuayo na inayoshamiri, umeona jinsi nguvu ya sanaa inavyoweza kutumika katika kuimarisha maisha yake ya pamoja—jinsi mioyo inavyofumwa pamoja kadiri nyimbo nzuri zilizovuviwa na Maandiko zinavyoimbwa katika mikusanyiko ya kiibada na utambuzi wa ujumbe unavyoimarishwa wakati mfululizo wa matukio ya historia ya Imani yanaposimuliwa wakati wa sherehe za Siku Takatifu na matukio mengine. Katika ujumbe wa 30 Desemba 2021, ikiongelea kwa kazi zinazfanyika vijijini na katika ujirani kila mahali, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu huandika:

> **"Mikusanyiko ya kusisimua ya jumuiya, iliyoandaliwa vyema—katika baadhi ya hali hadi kufikia kambi na matamasha—hutokea mara kwa mara zaidi, na muziki na nyimbo hutokeza kwa kiwango cha juu kwenye matukio kama haya. Kwa hakika sanaa kwa jumla, sehemu muhimu sana katika maendeleo ya jumuiya tangu mwanzoni, hujitokeza kipekee katika mazingira kama hayo kama njia muhimu ya kuchochea furaha, kuimarisha mafundo ya umoja, kusambaza maarifa na kuimarisha uelewa, na vile vile kuwafahamisha wale wa jamii pana zaidi kuhusu kanuni za Hoja."**[1]

Vile vile unajua, kwamba shughuli za kisanii zinafumwa katika mchakato wa kielimu unaokuzwa mashinani, hususan kwa ajili ya vizazi vichanga. Walimu wa madarasa ya watoto ya Kibahá'í wanahamasishwa kukuza stadi zao katika sanaa ya utambaji wa hadithi, sanaa itakayosisimua hisia mororo ndani ya moyo wa msikilizaji na kuamsha hisia za kiroho. Wanajifunza kuwaongza watoto katika nyimbo, huwasaidia kuboresha utambuzi wao wa mdundo na uwezo wao wa kushika wimbo, wakati wakikazia mada zinazofundishwa katika masomo. Katika matamasha ya watoto katika eneo lako, bila shaka umewahi kufurahishwa na utamu wa sauti zao na umehamasishwa na maigizo ya kisanii yanayoonesha stadi wanazopata katika madaraja ya juu zaidi. Ikiwa unahudumu kama mhuishaji wa kikundi cha vijana chipukizi, utakuwa umetafuta njia, kama ilivyopendekezwa katika Kitabu cha 5, za kutumia sanaa kwa ajili ya kuimarisha ujifunzaji wao—labda kupitia uandishi wa mashahiri kadiri umahiri wao wa lugha unavyoongezeka au kupitia ufundi ambao, huchotwa kutoka urithi wao, umeimarisha utambuzi wao mpangilio na ulinganifu na kuboresha uwezo wao wa kufanya kazi kwa mikono yao, lengo muhimu la kielimu linalochangia mafunzo ya jumla kwa mtu yeyote. Na kadiri wewe na marafiki zako mnavyoendelea kupitia kozi za mlolongo, pengine umehamasishwa kuanza mazoezi, yanayoonekana katika sehemu zote za ulimwengu, ya kuweka kwenye muziki vifungu kutoka Maandiko, ambao, unapoimbwa wakati wa vipindi vyenu vya masomo, husaidia kuimarisha mafundo ya urafiki, huwezesha ujifunzaji wenye furaha na wenye malengo, na kuhamasisha utafutaji wa ubora.

Kitengo hiki kinataka kuimarisha utambuzi wako wa nafasi ambayo jitihada za kisanii mashinani inayo katika yote mawili, katika kukuza mchakato wa kielimu kwa ujumla na katika kuongeza nguvu za mitindo wa maisha ya jumuiya unaobumbwa nayo. Inatumainiwa kwamba usomaji wa kurasa zake utaimarisha azma yako kama mkufunzi kuwasaidia wale walioanza kutembea katika ya njia ya huduma kupata utambuzi kama huo na kuchangia—kwa kiwango ambacho vipaji na uwezo unavyoruhusu—kwenye uchanuaji wa maonesho ya kisanii yanayovuviwa na uelewa wa kina wa Ufunuo wa Bahá'u'lláh.

## SEHEMU YA 2

Kabla hatujaangalia aina chache mahsusi za sanaa —muziki, utambaji wa hadithi, maigizo na kazi za mikono—tutasoma idadi kadhaa ya nukuu katika sehemu hii na zinazofuata na kutafakari juu ya maana zake. 'Abdu'l-Bahá husema:

> **"Sanaa zote ni kipawa cha Roho Mtakatifu. Wakati mwanga huu unapoangaza kupitia akili ya mwanamuziki, hujidhihirisha wenyewe katika ulinganifu mzuri wa sauti. Tena, ukiangaza kupitia akili ya mshairi, huonekana katika ushairi mzuri na nathari ya kishairi. Wakati mwanga wa Jua la Ukweli unapoivuvia akili ya mchoraji, yeye huchora picha nzuri ajabu. Vipawa hivi vinatimiza kusudi lake la juu kabisa, wanapokuwa wanamsifu Mungu."[2]**

1. Kutokana na nukuu hapo juu, jibu maswali yafuatayo:

   a. Ni lipi kusudi la juu kabisa la maonesho ya kisanii? ________________________

   ________________________________________________________________

   b. Kipawa cha sanaa hutoka wapi? ________________________

   c. Jinsi gani kipawa cha sanaa hujidhihirisha chenyewe kupitia akili ya mwanamuziki? ________________________

   ________________________________________________________________

   ________________________________________________________________

   d. Jiinsi gani kipawa cha sanaa hujidhihirisha chenyewe kupitia akili ya mshahiri?

   ________________________________________________________________

   ________________________________________________________________

   ________________________________________________________________

   e. Jinsi gani kipawa cha sanaa hujidhihirisha chenyewe kupitia akili ya mchoraji?

   ________________________________________________________________

   ________________________________________________________________

   ________________________________________________________________

2. Baini pamoja na washiriki wengine wa kikundi chako, kutoka nyimbo mnazozijua, zile zinazotimiza kusudi la kumsifu Mungu. Ni kwa namna gani hiki ni kipawa cha Roho Mtakatifu?

   ________________________________________________________________

   ________________________________________________________________

   ________________________________________________________________

   ________________________________________________________________

   ________________________________________________________________

## SEHEMU YA 3

'Abdu'l-Bahá husema:

> **"Ni asili ya moyo na roho kufurahia na kuburudika katika vitu vyote vinavyoonesha ulinganifu, upatano na ukamilifu. Kwa mfano: nyumba nzuri, bustani iliyopangiliwa vizuri, mstari linganifu, mjongeo wenye madaha, kitabu kilichoandikwa vyema, mavazi yanayopendeza—kwa kweli, vitu vyote ambavyo ndani mwake vyenyewe mna madaha au uzuri huupendeza moyo na roho . . ."**[3]

1. Ni kipi moyo na roho hufurahia? ______________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

2. Ni zipi kati ya hali zinazofuata huonesha upatano?

_____ Watu wawili wanabishana kuhusu wazo lililoelezwa katika aya ambayo wameisoma hivi punde, wakati mwenzao anatafakari kwa utulivu juu ya maana yake.

_____ Mama anamwimbia mwanaye ili aweze kulala wakati watoto wengine wanacheza kimya kimya.

_____ Mtu mmoja anaendelea kuwakatisha wengine wakati wa ushauriano.

_____ Watu wanajadili wazo muhimu wakati huo huo runinga imewashwa.

_____ Watoto wakubwa hucheza pamoja na wadogo zao wakati wazazi wao wanashiriki katika mkutano wa jumuiya.

_____ Mwalimu anamkaripia mwanafunzi kwa sauti kubwa, akimwambia ajiheshimu.

_____ Nahodha wa meli alikuwa anatoa amri, wakati mabaharia wanatekeleza amri zake.

_____ Vijana wa kijiji huingiza ndani mavuno, wakati watu wazima huyaandaa kwa ajili ya soko.

3. Fikiria jinsi moyo na roho ya mtu inavyofurahia na kuburudika katika vitu vyote vinavyoonesha ulinganifu, upatano, na ukamilifu. Ni vipi baadhi ya vitu unavyoviona au kuvisikia katika maisha yako ya kila siku ambavyo vinafurahisha moyo na roho? Ni vipi baadhi ya vitu ulivyoviona wakati wa ushiriki wako kwenye masuala ya jumuiya au katika usomaji wa kozi za taasisi ambavyo ungependa kuvieleza kama vitu vyenye madaha na uzuri?

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

## SEHEMU YA 4

Kama tulivyosoma katika sehemu iliyotangulia, "vitu vyote ambavyo ndani mwake vyenyewe mna madaha au uzuri huupendeza moyo na roho." Tunajua kutokana na majadiliano yetu juu ya mada ya hamasa kwamba mvuto kwa uzuri ni mojawapo ya nguvu za kiroho ambazo hutuinua kwenye milki za juu zaidi za uwepo. Ni nguvu hii ambayo hutusukuma kutafuta upatano katika maisha yetu ya kila siku na katika husiano wetu na wengine. Hivyo, vile vile, sanaa za maonesho, muziki na stadi za kazi ni udhihirisho wa shauku muhimu ya roho ya mwanadamu. Kile unachohitaji kukumbuka ni kwamba, udhihirisho wa uzuri katika ulimwengu huu ni taswira tu ya Uzuri wa Mpendwa Kabisa. Hivyo vyote huangamia, lakini Uzuri Uliobarikiwa ni wa milele. 'Abdu'l-Bahá hutuambia:

> **"Haiba ya umauti itafifia, mawaridi yatapisha njia kwa miiba, na uzuri na ujana vitafikia hatma yao na havitakuwepo tena. Lakini kile kinachodumu milele ni Uzuri wa Yule wa Kweli, kwa kuwa uzuri wake hauangamii na utukufu wake hudumu milele; haiba yake ni yenye uwezo wote na mvuto wake hauna mwisho. Heri ni yake basi ule wajihi unaoakisi wangavu wa Mwangaza wa Yule Mpendwa! Bwana asifiwe, wewe umeangaziwa kwa Mwangaza huu, umepata lulu ya ujuzi wa kweli, na umesema Neno la Ukweli."[4]**

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. Haiba ________________ ita ______________________________ .

   b. __________________ yatapisha njia kwa ______________________ .

   c. Uzuri na ______________ vitaifikia ______________ na ____________________ .

   d. Kile ambacho ni cha milele _____________________ ni ____________________ wa ____________________________ .

   e. Wangavu wa Uzuri wa Yule wa Kweli ______________________________ .

   f. Utukufu wa Uzuri wa Yule wa Kweli ____________________________________ .

g. Haiba ya Uzuri wa Yule wa Kweli ni ______________________________ .

h. Mvuto wa Uzuri wa Yule wa Kweli ni __________________________ .

2. Pale unapofikiria kuhusu shughuli ya kisanii na nguvu ya mvuto kwa uzuri, ni muhimu kukumbuka kwamba umbile letu la nje hupata thamani yake kutoka hali ya ndani. Kuhusiana na hili ‘Abdu’l-Bahá husema:

**“Mwili bila roho hauna uwezo wa kupata mafanikio halisi. Ingawa unaweza kuwa katika hali ya juu kabisa ya uzuri na ubora, hata hivyo, unahitaji roho. Yai la taa, haidhuru limeng’arishwa kuwa kamilifu jinsi gani, linahitaji mwanga. Bila mwanga, taa au mshumaa hauwezi kuangaza.”**[5]

Katika kutafakari juu ya maana ya kifungu hapo juu, fikiria wakati ambapo ulisikia tukio kutoka katika historia ya Imani ambalo liligusa hisia za wale waliokuwepo. Pengine, muundo ulikuwa sahihi: maneno yalitamkwa kwa uwazi; vituo viliwekwa sehemu sahihi; mdundo unaofaa ulidumishwa; na ishara zilitumika kusisitiza mambo fulani fulani. Lakini yote haya yasingeweza kuwahamasisha wasikilizaji. Hisia ya juu zaidi iliyotakaswa kutokana na ubinafsi na tamaa lazima itakuwa ilionekana kupitia masimulizi haya. Hisia za roho lazima ziliguswa. Jadili na kikundi chako chanzo cha kuguswa huko. Katika uchambuzi wa mwisho, je, siyo Uzuri wa Mpendwa kabisa?

## SEHEMU YA 5

Tukiwa na mawazo ya hapo juu akilini, hebu tutazame aina mbalimbali za sanaa, tukianza na muziki. Bila shaka, kuna ubaya mwingi katika ulimwengu wa leo ambao hujionesha wenyewe katika jina la uzuri, na tunapaswa kuwa waangalifu kuchagua zile sanaa ambazo huvutia kwenye asili yetu ya juu zaidi na kujihadhari na zile ambazo hutupeleka kwenye udhilifu. Maneno yafuatayo ya Bahá’u’lláh kutoka katika Kitáb-i-Aqdas yanajumuisha mwongozo wa kimsingi kwa shughuli hii:

**“Tumefanya iwe halali kwenu kusikiliza muziki na kuimba. Jihadharini walakini, usikilizaji huo usije ukawafanya mvuke mipaka ya staha na heshima. Acheni furaha yenu iwe ile furaha itokanayo na Jina Langu Kuu Kabisa, Jina ambalo huleta furaha kubwa mno moyoni kupita kiasi, na kuzijaza msisimko fikra za wote ambao wamemkaribia Mungu. Sisi, kwa kweli, Tumeufanya muziki kama ngazi kwa ajili ya roho zenu, njia ambayo kwayo ziweze kuinuliwa juu hadi kwenye milki za juu; hivyo msiufanye kama mabawa kwa ajili ya nafsi na tamaa. Kwa kweli, Tunachukizwa kuwaona mkihesabiwa pamoja na wapumbavu.”**[6]

Na, juu ya asili ya muziki, ‘Abdu’l-Bahá husema:

**“. . . katika zama hizi mpya Mwanga Uliodhihirishwa, katika Nyaraka Zake Takatifu, umetangaza mahsusi kwamba muziki, ukiimbwa au kuchezwa, ni chakula cha kiroho kwa roho na moyo.”**[7]

**“. . . lahani, ingawa ni za kimwili, zimeunganishwa na hali ya kiroho, kwa hiyo, huleta matokeo makubwa. Lahani ya aina fulani huifurahisha roho, aina nyingine huihuzunisha, nyingine huisisimua roho kutenda.”**[8]

**“Uimbaji wa lahani utaleta uhai na furaha kwa ulimwengu wa wanadamu, wasikilizaji watafurahishwa na kushangilia na hisia zao za ndani zaidi zitaguswa. Lakini furaha hii, hali hii ya hisia ni ya mpito na itasahaulika ndani muda mfupi. Walakini, sifa ziwe kwa Mungu, wewe umechanganya tuni zako na lahani za Ufalme, utaleta faraja kwa ulimwengu wa roho na daima utachochea hisia za kiroho.”**[9]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. Bahá’u’lláh hutuambia kwamba, tunaposikiliza muziki na kuimba nyimbo tujihadhari _________________ mipaka ya _______________ na ____________ .

   b. Tunahamasishwa kuufikiria muziki kama ngazi kwa ajili ya ______________ zetu, njia ambayo wao wangeweza _____________________ hadi kwenye ______________ ya juu.

   c. Tunaonywa dhidi ya kuufanya muziki kuwa kama ________________ kwa ajili ya ______________ na _______________ .

   d. Katika zama hizi mpya, Bahá’u’lláh __________________________ mahsusi kwamba, __________________ , ukiimbwa au kuchezwa, ni chakula cha kiroho kwa ajili ya _______________ na ________________ .

   e. Katika _________________ , Bahá’u’lláh ametangaza _____________________ kwamba muziki , ________________________ au _____________________ , ni _________________________________ kwa roho na moyo.

   f. Ingawa lahani ni ______________ , ‘Abdu’l-Bahá hutuambia, zimeunganishwa na ______________ .

   g. _________________ , ingawa ni za kimwili, zime _____________________ na hali ya kiroho, kwa hiyo, ___________________ makubwa.

   h. Aina fulani ya lahani huifanya roho _________________ .

   i. Aina nyingine ya lahani huifanya roho _______________ .

   j. Aina fulani ya lahani huisisimua roho __________________ .

2. Jibu maswali yafuatayo:

   a. Nini maana ya kuchanganya “tuni na lahani za Ufalme”?____________________
   ______________________________________________________________
   ______________________________________________________________

   b. Je, “Uchanganyaji huu” hufanya nini?____________________________________
   ______________________________________________________________
   ______________________________________________________________

3. Muziki ni nguvu yenye uwezo ambao sharti utumike kwa busara. Ingefaa kwako kubaini baadhi ya nyimbo unazozijua ambazo humwinua mtu hadi “kwenye milki ya juu” na nyingine ambazo zinaweza kuwa “mabawa ya nafsi na tamaa”.

## SEHEMU YA 6

Vifungu hapo juu huondoa shaka yoyote kwamba muziki huleta mchango mkubwa wa kuinua roho. Kauli ifuatayo ya ‘Abdu’l-Bahá huonesha uwezo wa muziki kujenga, bila kujali mazingira na kusudi, hali zifaazo kwa ajili ya upokevu wa juu zaidi wa kiroho kwa ujumbe unaotolewa:

> **“. . . ingawa muziki ni jambo la kimwili, bado matokeo yake makubwa mno ni ya kiroho, na mwambatano wake mkubwa kabisa ni kwenye milki ya roho. Mtu akipenda kutoa mjadala, utakuwa na matokeo zaidi kwa kutumia lahani za kimuziki. Wagiriki wa kale, pia wanafalsafa wa Kiajemi, walikuwa na desturi ya kutoa mijadala yao kwa namna ifuatayo: —kwanza, kwa kucheza lahani chache za muziki, na pale ambapo wasikilizaji wao walipofikia kiwango fulani cha upokevu hapo wangeacha chombo chao mara moja na kuanza mjadala wao. Miongoni mwa wanamuziki mashuhuri kabisa wa Kiajemi aliyeitwa Barbod, ambaye, wakati wowote suala kubwa lilipojadiliwa katika baraza la Mfalme, na pale Wizara iliposhindwa kumshawishi Mfalme, wao walilipeleka mara moja suala hilo kwa Barbod, ambaye angekwenda na chombo chake hadi kwenye baraza na kucheza muziki uliofaa na wenye mguso kabisa, na hivyo lengo lilifikiwa mara moja, kwa sababu Mfalme papo hapo aliathiriwa kwa kuguswa na lahani za kimuziki, hisia fulani za ukarimu zingefurika moyoni mwake, na yeye angekubali hoja.”[10]**

1. Kamilisha sentensi ziuatazo:

   a. Ingawa muziki ni suala la _______________ , ____________ yake makubwa mno ni _________________ .

   b. Ingawa ___________ ni suala la kimwili, __________________ wake mkubwa kabisa ni _______________ ya ______________ .

c. Mtu akipenda ________________________ , utakuwa na ___________________ zaidi kwa kutumia ______________________________ .

2. Tayari unatambua kutoka katika usomaji wako wa Kitabu cha 3 kwamba nyimbo zinaweza kuwa chombo chenye nguvu cha ufundishaji. Kama mada ya wimbo inahusiana na mada inayoongelewa, uimbaji utakamilisha usomaji wa nyenzo na unaweza kuongeza ufanisi wake. Je, unajua nyimbo zozote zilizotungwa katika eneo lako ambazo zingekamilisha usomaji wa Kitabu cha 1?

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 7

Nguvu ya muziki huongezeka mara nyingi wakati inapovuviwa na mafundisho ya Imani, hata inapotumia maneno ya Mungu. 'Abdu'l-Bahá hutuambia:

> **"Muziki ni mbinu muhimu ya uelimishaji na maendeleo ya jamii ya wanadamu, lakini njia pekee ya kweli ni kupitia Mafundisho ya Mungu. Muziki ni kama bilauri hii, ambayo imetakasika na kung'arishwa kabisa. Hasa ni kama kalisi hii iliyopo mbele yetu, na Mafundisho ya Mungu, maneno ya Mungu, ni kama maji. Pale bilauri au kalisi inapokuwa safi na wazi kabisa, na maji yakiwa safi na maangavu kabisa, ndipo yatakapojalia Uhai; kwa hiyo, Mafundisho ya Mungu, yawe katika umbo la nyimbo au mahubiri au sala, yanapoimbwa kwa lahani tamu, huvutia sana."**[11]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

a. Muziki ni mbinu muhimu ya __________________ na _________________ ya jamii ya wanadamu.

b. Njia pekee ya ____________ ya ___________ hutumika kama mbinu ya uelimishaji na maendeleo ya ________________ ni kupitia ______________________ .

c. Muziki ni kama ________________ , wakati Mafundisho ya Mungu ni kama _______________ .

d. Pale bilauri ikiwa ______________ na ____________ kabisa, na maji yakiwa ________________ na _______________ kabisa, ndipo yatakapojalia _________ .

e. Mafundisho ya Mungu, yawe katika umbo la ___________ au _______________ au _____________ , yanapoimbwa ________________________________ huvutia sana.

2. Kulingana na nukuu hapo juu, kadiri jitihada za kujenga jumuiya hai zinavyoongeza mwendo katika kila sehemu ya ulimwengu, idadi iongezekayo ya sala na vifungu kutoka Maandiko yanaingizwa katika muziki katika lugha zote, kwa namna inayolifaa Neno Takatifu. Wakati wa kampeni ya taasisi au kambi, na hata katika vikundi vya mafunzo, washiriki wanaweza kujifunza nyimbo nyingi kati ya hizi na pengine kuchangia kwenye utungaji wa zingine. Hapo chini kuna wimbo mmoja unaopendwa sana kila mahali katika ulimwengu wa Kibahá'í, lakini bila shaka unajua nyingi zaidi. Imba chache sasa pamoja na washiriki wengine wa kikundi chako.

Heri Pahali

A Amaj7 A7 D
Heri pahali, na nyumba, na mahali,
Bmin E A E7
Na mji, na moyo, na mlima,
A Amaj7 A7 D
Na kimbilio, na pango, na bonde, na nchi,
Bmin E7 A
Na bahari, na kisiwa, na shamba
Bmin E A F#min
Ambapo jina la Mungu limetajwa,
D E E7
Na sifa Zake kutukuzwa.

3. Vipaji vya washiriki katika kozi za taasisi na ujuzi wao wa muziki vitakuzwa kwa viwango tofauti tofauti, na baadhi ambao wana weledi na wengine ambao hawana mwelekeo wa kimuziki kabisa. Wachache wanaweza kuhisi kuzuiliwa kuimba mbele ya wengine. Baadhi wangependa tu kuimba tuni kwa sauti ya chini kabisa kiasi kwamba haiwezekani kuwasikia. Bila kujali mielekeo na vipaji vyao utapaswa kukubali na kuwahamasisha wote na kuhakikisha kwamba hakuna yeyote daima atakayefedheheshwa. Kuhusiana na hili, ni muhimu kwako kutenganisha suala la uimbaji wa mtu mwenye kipaji na ule uimbaji wa kikundi. Vyote viwili ni vya thamani. Lakini wakati mwingine ukamilifu unaotafutwa na mtu unaweza kuzuia ushiriki wa wengine. Jadili na kikundi chako uwezo unaohitajika kujengwa kwa ajili ya maonesho ya pamoja ya sanaa, hususan muziki, ili kuibuka mashinani.

## SEHEMU YA 8

Sasa, kulingana na nukuu mlizozisoma katika sehemu hizi, ingefaa kwenu kusita kidogo na kufikiri kuhusu aina gani za muziki zingefaa zaidi kwa ajili ya matukio mbalimbali ya jumuiya. Ni aina gani ya nyimbo zingeinua roho na kuchangia kwenye hali ya kiroho wakati

wa mkusanyiko wa kiibada? Ni nyimbo zipi zingefaa katika mikutano ya tafakari? Ni nyimbo zipi hususan zingefaa wakati wa kampeni shadidi za taasisi? Ni aina gani ya nyimbo zinafaa kwa ajili ya kampeni za ufundishaji? Ni mifano ipi ya nyimbo ambazo zingefaa zaidi kwa ajili ya matukio ambamo jumuiya nzima hukusanyika kushauriana kuhusu masuala yake? Zipi zingefaa kuimbwa kwenye matamasha ya watoto na vijana chipukizi? Ni ipi baadhi ya mifano ya nyimbo ambazo huongeza ufahamu wa marafiki wa historia ya Imani na upendo wao kwa Bahá'u'lláh na zile zinazogusa mioyo yao na kuwasukuma kutumikia Hoja? Nyimbo zipi hufaa kwa ajili ya maadhimisho ya Siku Takatifu na kwa ajili ya sherehe za Karamu ya Siku Kumi na Tisa? Andikeni mawazo yenu machache hapa chini.

## SEHEMU YA 9

Utambaji wa hadithi ni sanaa inayoweza kuhamasisha, kuhuisha, kuchochea fikra, kufikisha dhana za kina, na kuingiza umaizi wa kiroho. Hadithi zinaweza kutumika katika mazingira mbalimbali—wakati wa ziara kwenye kaya, katika mikusanyiko na sherehe za jumuiya, katika kampeni na katika kambi nyakati za jioni ili kuimarisha uhusiano wa vijana na historia ya Imani.

Uwezo wa kutamba hadithi kwa namna inayovutia na inayohamasisha ni jambo ambalo mtu hulikuza kupitia tajiriba. Kitabu cha 3 hutoa madokezo machache kuhusu mbinu za muundo huu wa sanaa ambao mara nyingi hupuuzwa. Hatutajadili stadi zihitajikazo hapa. Wala hapa si mahali pa kujifunza orodha ndefu ya masimulizi yaliyopendekezwa. Kile unachopaswa kukumbuka kutoka Kitabu cha 5 na kuzingatia akilini kama mkufunzi ni maana maalum ya mfululizo wa matukio kutoka katika historia ya Imani katika kubumba utambulisho, wa mtu binafsi na wa pamoja. Unajua, bila shaka, kwamba *Wana-Mapambazukoi* ni wa thamani ya kipekee kama chanzo cha mfululizo wa matukio hayo. Mlinzi hukielezea kitabu hiki kama "Kiungo cha muhimu" kwa programu za ufundishaji na "kitabu cha kiada kisichopingika" katika shule za kiangazi. Zaidi, yeye hukiita "chanzo cha uvuvio katika shughuli zote za kifasihi na za kisanii," "mwenzi wa thamani mno katika nyakati za mapumziko," "mwanzo usioepukika wa hija za siku zijazo kwenye nchi ya kuzaliwa ya Bahá'u'lláh," na "chombo kisichoshindwa kutuliza hofu na kukabili mashambulizi ya jamii ya wanadamu walioishiwa imani kwa kiwango cha juu kabisa" Juu ya umuhimu wa kitabu hicho, alichotuachia mwanahistoria mkuu Nabíl, Shoghi Effendi huandika:

> **"Tumia, kwa kiwango kikubwa uwezavyo, utajiri wa nyenzo zilizomo katika masimulizi ya Nabil yenye kusisimua na yenye thamani. Na acha yawe chombo chako kikuu ambacho kwacho unaweza kuchochea mwale wa shauku ambao huwaka katika kila moyo wa Mbahá'í na ambayo kwayo mafanikio ya jitihada zako tukufu, zisizochoka lazima hatimaye yategemee."[12]**

Katika barua iliyoandikwa kwa niaba yake, tunasoma:

> **"Masimulizi ya Nabíl siyo tu masimulizi; ni kitabu cha tafakari. Hakifundishi tu. Kwa kweli kinavuvia na kuchochea utendaji. Kinahuisha na kuamsha nguvu zetu zilizolala na kutufanya tupae hadi kwenye upeo wa juu zaidi. Hivyo huu ni msaada wenye thamani kubwa kwa mwanahistoria hali kadhalika kwa kila mwalimu na mfundishaji wa Hoja."[13]**

Ingawa tayari mnajua matukio mengi kutoka katika historia ya Imani na pengine mnaweza kuyasimulia kwa utondoti kiasi, tunajumuisha katika sehemu hii kifungu kutoka katika *Wana-Mapambazuko*, ambacho mnaombwa kukisoma mara kadhaa na kisha kusimulia, mkiwa waangalifu kufanya hivyo kwa usahihi kadiri iwezekanavyo. Kifungu hiki kinawapa aina ya mfano ambao mngependa kujifunza, hususan kusimulia katika kambi na kampeni za pamoja, kwa kuwa kinaweza kusimuliwa sehemu au chote kadiri mazingira yanavyoruhusu.

Kabla ya kukisoma kifungu hicho, mnapaswa kukumbuka hali ya Kipindi kifupi lakini cha kuvutia cha Báb—jinsi, baada ya tangazo Lake kama Yule Mwahidiwa mnamo mwaka 1844, maelfu waliipokea Imani mpya na walianza kueneza Ujumbe Wake, wakiibua hofu na wivu miongoni mwa viongozi wa Iran, ambao walimfukuza na kumhamisha hadi kwenye pembe ya mbali ya nchi, wakitumaini wangeweza kudhibiti wimbi lililoendelea kukua la

ushawishi Wake. Walakini, kama mjuavyo, licha ya jitihada zao, Ujumbe Wake uliendelea kuenea, na kwa hiyo, mnamo Julai 1850, Yeye aliuawa pamoja na mmoja miongoni mwa wafuasi Wake waaminifu, Anís. Tayari, kabla ya tukio hilo la kusikitisha, wafuasi Wake waliteswa kwa ukatili mkubwa wa kuaibisha sana: walishambuliwa, kupigwa na kufungwa, ili waweze kuikana imani yao. Hatimaye maelfu wangeitwa kutoa maisha yao katika njia ya Mpendwa wao. Kwa hakika, miezi minne kabla ya kuuawa kishahidi kwa Báb, "tukio la kuhuzunisha" lilitokea katika mji wa Ṭehrán ambalo lingethibitisha, kulingana na Mlinzi, lilikuwa "mwanzo wa mauaji ya kinyama" ambayo yangewatikisa sana "wakazi wake" na kueneza "hofu kubwa hadi kwenye maeneo ya jirani". "Mashujaa wa janga hilo", yeye hutuambia, "walikuwa Wafiadini Saba wa Ṭehrán".

Wote walitokea katika taaluma zilizoheshimika, roho hizi saba zilizobarikiwa walikamatwa na kufungwa jela kwa siku ishirini na mbili, kipindi ambapo walifanyiwa kila aina ya madhila ili kuwalazimisha waikane Imani yao. Mwishowe, kwa amri ya Waziri Mkuu, walitishiwa kuuawa. Lakini si "maombi ya mara kwa mara yenye nguvu" ya jamaa zao maarufu, wala "kiasi kikubwa cha fedha" kilichotolewa ili waachiliwe, wala "maombi yenye hamasa ya maafisa wa serikali" vingeweza kuwazuia kupata taji la kifo cha kishahidi. "Majibu ya ujasiri" waliyoyatoa kwa watesi wao, "furaha kubwa mno" waliyoionesha wazi kadiri walivyokaribia mahali pa kifo chao, "makelele ya ushindi" waliyopiga kadiri walivyomkaribia muuaji wao, "uchungu wa aya" ambazo baadhi yao walizitongoa katika dakika zao za mwisho, na "mvuto wa hisia na changamoto" walizoupa umati wa watazamaji—hivi ni miongoni mwa "sura kuu za tukio hilo la kuhuzunisha la Wafiadini kishahidi Saba wa Ṭehrán," tukio hilo la kuhuzunisha ambalo Mlinzi hueleza kama "mojawapo ya matukio ya kutisha kabisa kuwahi kushuhudiwa katika kipindi cha mwanzo wa ukunjukaji wa Imani ya Bahá'u'lláh." Hivi ndivyo Nabíl anavyo simulia hadithi zao:

> "1. Ḥájí Mírzá Siyyid 'Alí, aliyeitwa Khál-i-A'ẓam, mjomba Wake Báb, na mmoja wa wafanya biashara maarufu wa mji wa Shíráz. Huyu ndiye alikuwa mjomba aliyekabidhiwa malezi ya Báb, baada ya kifo cha baba Yake, ndiye aliyeaminiwa na ambaye, baada ya Mpwa wake kurejea kutoka hija Yake huko Hijáz na kukamatwa Kwake na Ḥusayn Khán, alitwaa jukumu zima kwa ajili Yake kwa ahadi ya maandishi. Yeye ndiye aliyekuwa pamoja Naye wakati wote, akiwa katika uangalizi wake, kwa upendo usiokoma, aliyemtumikia kwa moyo wote, na aliyekuwa mwakilishi kati Yake na majeshi ya wafuasi Wake walio furika kwenda Shíráz kumuona Yeye. Mwanaye wa pekee, Siyyid Javád, alifariki angali mchanga. Kuelekea katikati ya mwaka 1265 a.h., Ḥájí Mírzá Siyyid 'Alí huyu ndiye aliyeondoka Shíráz na kumtembelea Báb katika kasiri ya Chihríq. Kutoka huko alikwenda Ṭehrán na, ingawa hakuwa na kazi maalum, aliendelea kukaa katika mji huo hadi kuibuka kwa ghasia ambayo hatimaye ilisababisha kifo chake cha kishahidi.
>
> "Ingawa marafiki zake walimsihi aepuke zahama iliyokuwa ikikaribia kwa haraka, yeye alikataa katakata kusikiliza ushauri wao na alikabiliana, hadi saa yake ya mwisho, na mateso yote waliyompa. Idadi kubwa ya wafanyabiashara maarufu kabisa miongoni mwa jamaa zake walijitolea kulipa dhamana yake, yeye alikataa ombi lao. Mwishowe yeye alipelekwa mbele ya Amír-Niẓám. 'Hakimu Mkuu wa milki hiyo,' Wazíri Mkuu alimtaarifu kwamba, 'yeye hakutaka kuwatesa hata kidogo wazawa wa Mtume. Wafanyabiashara maarufu wa Shíráz na Ṭehrán wapo tayari, la, wana shauku kubwa ya kulipa dhamana yako. Maliku't-Tujjár naye hata amekutetea kwa niaba yako. Neno tu la ukanushaji kutoka kwako lingekupa uhuru na kuhakikisha uweze kurudi kwa heshima zote kwenye mji wako wa kuzaliwa. Naahidi neno langu kwamba, ikiwa

utakubali utaishi siku zilizobaki za maisha yako kwa heshima na staha chini ya kivuli cha himaya ya mfalme wako.’ ‘Mheshimiwa,’ Ḥájí Mírzá Siyyid ‘Alí, yeye alimjibu kwa ujasiri, ‘kama wengine waliokuwa kabla yangu, ambao wamegugumiza kwa furaha kikombe cha kifo cha kishahidi, walichagua kukataa ombi kama hilo ambalo wewe unaniambia hivi sasa, jua kwa hakika kwamba hata mimi nina shauku kubwa ya kukataa ombi kama hilo. Ukanushaji wangu wa ukweli uliomo katika Ufunuo huu ungekuwa sawa na ukanushaji wangu wa Funuo zote zilizoutangulia. Kukataa kuutambua Ujumbe wa Siyyid-i-Báb kungekuwa sawa na ukanaji wa Imani za mababu zangu na kuzikana sifa Takatifu za Ujumbe uliofunuliwa na Muḥammad, Yesu, Musa, na Manabii wote waliotangulia. Mungu anajua kwamba chochote nilichokisikia na kukisoma kuhusiana na maneno na vitendo vya Wajumbe hao, nimepata heshima ya kushuhudia hicho hicho kutoka kwa Kijana huyu, Ndugu yangu mpendwa, tangu mwanzoni mwa ujana Wake hadi sasa, mwaka wa thelathini wa maisha Yake. Kila kitu ndani Yake hunikumbusha Babu Yake Mtukufu na maimámu wa Imani Yake ambao maisha yao hadithi zetu zilizoandikwa zimeeleza. Nakuomba kitu kimoja tu, kwamba uniruhusu kuwa wa kwanza kuyatoa maisha yangu katika njia ya Ndugu yangu mpendwa.’

“Amíri alishangazwa sana na jibu kama hilo. Katika taharuki ya kukata tamaa, na bila kusema neno, alitoa ishara kwamba apelekwe nje na kukatwa kichwa. Wakati muhanga huyo alipokuwa anapelekwa mahali pake pa kifo, alisikika, mara kadhaa, akirudia maneno haya ya Ḥáfiẓ: ‘Shukrani yangu ni kubwa Kwako, Ee Mungu wangu, kwa kunijaalia kwa ukarimu yote niliyokuomba.’ ‘Nisikilizeni enyi watu,’ yeye aliupazia sauti umati uliomzunguka; ‘Nimejitoa mwenyewe kama dhabihu ya hiari katika njia ya Hoja ya Mungu. Jimbo zima la Fárs, hali kadhalika ‘Iráq, nje ya mipaka ya Uajemi itashuhudia bila wasi wasi unyofu wangu wa mwenendo, uchaji Mungu wa kweli na nasaba yangu bora. Kwa zaidi ya miaka elfu moja, mmesali na kusali ili Qá’im mwahidiwa adhihirishwe. Kwa mtajo wa jina Lake, ni mara ngapi mmelia kutoka ndani ya mioyo yenu: ‘Harakisha, Ee Mungu, ujio Wake; ondoa kila kikwazo ambacho kipo kwenye njia ya utokeaji Wake!’ na sasa kwamba Yeye amekuja, ninyi mmemfanya akimbilie katika uhamisho wa kukatisha tamaa katika pembe ya mbali na iliyojitenga ya Ádhirbáyján na mmeinuka kuwaangamiza wafuasi Wake. Laiti ningeweza kuita laana ya Mungu juu yenu, nina hakika kwamba hasira Yake yenye kisasi ingewatesa vibaya mno. Hilo, walakini, siyo ombi langu. Kwa pumzi yangu ya mwisho, naomba kwamba Mwenyezi Mungu afute mawaa ya makosa yenu na awawezeshe kuzinduka kutoka katika usingizi wenu wa uzembe.’

“Maneno haya yalimgusa sana muuaji Wake. Akajifanya kwamba upanga aliokuwa tayari ameushika mikononi mwake ulihitaji kunolewa, kwa haraka aliondoka, akidhamiria kamwe kutorudi tena. ‘Pale nilipoteuliwa kwa ajili ya huduma hii,’ yeye alisikika akilalamika, huku akilia kwa uchungu wakati wote, ‘wao waliamua kuwakabidhi katika mikono yangu wale waliohukumiwa kama wauaji na wateka nyara. Sasa nimeamriwa kumwaga damu ya Yule ambaye Utakatifu Wake ni sawa na wa Imám Músáyi-Káẓim mwenyewe!’ Muda mfupi baada ya hapo, yeye aliondoka kuelekea Khurásán na huko alijitafutia riziki yake kama mpagazi na mpiga mbiu. Aliwasimulia waumini wa jimbo lake kisa cha janga hilo, na kuelezea ungamo kake kwa kitendo alicholazimishwa kukifanya. Kila alipolikumbuka tukio hilo na kila aliposikia jina la Ḥájí Mírzá Siyyid ‘Alí likitajwa, alishindwa kuzuia machozi kutiririka machoni mwake, machozi ambayo yalishuhudia huba ambayo mtu huyo mtakatifu alikuwa ameiingiza moyoni mwake.

"2. Mírzá Qurbán-'Alí, mwenyeji wa Bárfurúsh katika jimbo la Mázindarán, na mtu maarufu katika jumuiya aliyejulikana kwa jina la Ni'matu'lláhí. Yeye alikuwa mcha Mungu na alikuwa amejaliwa ubora mkubwa wa asili. Huo ndio ulikuwa usafi wa maisha yake kiasi kwamba watu wengi miongoni mwa wale maarufu wa Mázindarán, wa Khurásán na wa Ṭehrán walimwahidi utii wao, na walimchukulia kama mfano halisi wa njema. Hiyo ndio ilikuwa heshima ambapo wananchi wenzake kwamba, wakati wa tukio la hija yake kwenda Karbilá, umati mkubwa wa wapambe wake waaminifu ulisongamana barabarani ili kumlaki. Katika mji wa Hamadán, hali kadhalika katika mji wa Kirmánsháh, idadi kubwa ya watu walishawishika na haiba yake na walijiunga na kikosi cha wafuasi wake. Popote alikokwenda, alisalimiwa kwa shangwe za watu. Mikusanyiko hii ya watu wenye shauku hata hivyo, ilimchukiza kupita kiasi. Yeye aliepukana na umati huo na aliibeza fahari na hali za uongozi. Alipokuwa njiani kuelekea Karbilá, akipitia mji wa Mandalíj, shaykh mwenye umaarufu mkubwa alitokea kumpenda sana kiasi kwamba alikikana kila kitu alichokuwa akikipenda sana hapo awali na, akiwaacha marafiki na wafuasi wake, alimfuata hadi mji wa Ya'qúbíyya. Mírzá Qurbán-'Alí, hata hivyo, alifanikiwa kumshawishi arejee Mandalíj na kuendelea na kazi aliyokuwa ametelekeza.

"Aliporejea kutoka hija yake, Mírzá Qurbán-'Alí alikutana na Mullá Ḥusayn na kupitia kwake aliukumbatia ukweli wa Hoja. Kwa sababu ya maradhi, alishindwa kujiunga na watetezi wa ngome ya Ṭabarsí, na, lakini kutokana na uchovu wa safari ya Mázindarán, alikuwa wa kwanza kujiunga na wenyeji wake. Baada ya Mullá Ḥusayn, miongoni mwa wafuasi wa Báb, Vaḥíd alikuwa mtu ambaye alimpenda sana. Wakati wa ziara yangu huko Ṭehrán, niliambiwa kwamba huyo wa pili alikuwa ameyaweka wakfu maisha yake kwa ajili ya huduma kwa Hoja na alikuwa ameinuka kwa mfano wa kujitoa ili kuendeleza maslahi yake kote kote. Mara nyingi nilimsikia Mírzá Qurbán-'Alí, ambaye alikuwa katika mji mkuu, akisikitikia juu ya maradhi hayo. 'Ni kwa kiasi kikubwa jinsi gani ninavyosikitika,' nilimsikia akisema mara kadhaa, 'kunyimwa sehemu yangu ya kikombe ambacho Mullá Ḥusayn na wenzake wamekigugumiza! Natamani sana kujiunga na Vaḥíd na kujiandikisha chini ya beramu Yake na kujaribu kuyasahihisha mapungufu yangu ya awali.' Yeye alikuwa anajiandaa kuondoka Ṭehrán, pale ghafla alipokamatwa. Mavazi yake kawaida yalishuhudia kiwango cha kujitenga kwake. Alivaa kanzu nyeupe, kama ile ya Waarabu, na kujifunika 'abá, akivaa kilemba cha watu wa 'Iráq, alipokuwa akitembea barabarani, alionekana kama mfano halisi wa ukanaji. Alifuata kwa uangalifu sana sheria zote za Imani yake, na kwa mfano wa ucha Mungu alifanya ibada zake. 'Báb Mwenyewe alifuata kanuni zote za Imani Yake hadi kwenye tondoti zake ndogo kabisa,' yeye aghalabu alisema. 'Nawezaje kupuuzia mambo ambayo yanafuatwa na Kiongozi wangu?'

"Wakati Mírzá Qurbán-'Alí alipokamatwa na kuletwa mbele ya Amír-Niẓám, ghasia kubwa iliibuka ambayo kwa nadra kutoea katika mji wa Ṭehrán. Umati mkubwa wa watu uliosongamana uliyakaribia makao makuu ya serikali, wakiwa na shauku ya kujua nini kingemtokea. 'Tangu jana usiku,' mara tu alipomuona, Amír alisema, 'Nimezungukwa na matabaka yote ya maafisa wa Serikali ambao wamekutetea kwa nguvu. Kutokana na ninachokigundua kuhusu daraja lako na ushawishi wa maneno yako, wewe si wa chini kuliko Siyyid-i-Báb Mwenyewe. Laiti ungedai kwa ajili yako mwenyewe nafasi ya uongozi, ingekuwa bora zaidi kuliko kutangaza utii wako kwa yule ambaye kwa hahika ni wa chini kwako katika maarifa.' 'Maarifa niliyoyapata,' yeye kwa ujasiri alijibu, 'ndiyo yaliyoniongoza kukubali kutii mbele ya Yule ambaye nimemtambua kuwa Bwana na Kiongozi wangu. Tangu nimefikia umri wa utu uzima,

nimechukulia haki na kutopendelea kama kusudi linalotawala maisha yangu. Nimemhukumu kwa haki, na nimefikia uamuzi kwamba ikiwa Kijana huyu, ambaye uwezo wake wa juu sana unashuhudiwa na wote, marafiki na maadui ni muongo, basi, kila Mtume wa Mungu, tangu zama zisizokumbukika hadi siku hii, anapaswa kushitakiwa kama mfano halisi wa uwongo! Nina uhakika wa uaminifu usio na shaka wa zaidi ya wapambe elfu moja, na bado sina uwezo wa kubadilisha moyo wa mtu mdogo kabisa miongoni mwao. Kijana huyu, walakini, amejithibitisha mwenyewe kuweza kuzibadilisha, kupitia kioevu bora cha upendo Wake, roho za wadhilifu kabisa miongoni mwa wanadamu wenzake. Juu ya watu elfu kama mimi, bila msaada na pekee, ametumia ushawishi Wake ambao, hata bila kukutana Naye, wametupilia mbali tamaa zao wenyewe na wameshikilia kwa shauku kwenye mapenzi Yake. Wakitambua kikamilifu juu ya mapungufu ya dhabihu yao, hawa wanatamani kutoa maisha yao kwa ajili Yake, kwa matumaini kwamba ushahidi huu wa nyongeza wa kujitoa kwao uweze kustahili kutajwa katika Kitala Chake.’

“‘Ninachukizwa,’ Amír-Niẓám alisema, ‘iwe maneno yako ni ya Mungu au la, kutamka hukumu ya kifo dhidi ya mwenye daraja lililotukuka sana.’ ‘Kwa nini unasita?’ alifoka muhanga asiye na subira. ‘Kwani wewe hutambui kwamba majina yote huteremka kutoka Mbinguni? Yule Ambaye jina Lake ni ‘Alí, Ambaye katika njia Yake nimeweka maisha yangu, tangu nyakati zisizo kumbukika ameandika jina langu, Qurbán-‘Alí, katika gombo la wafiadini Wake wateule. Hii kwa uhakika ni siku ya kusherehekea sherehe ya Qurbán, siku ambayo nitagonga muhuri kwa damu ya uhai wangu Imani yangu katika Hoja Yake. Kwa hiyo, usisite, na uwe na hakika kwamba kamwe sitakulaumu kwa kitendo chako. Kadiri utakavyo kikata kichwa changu mapema zaidi ndivyo itakavyokuwa kubwa shukurani yangu kwako.’ ‘Mwondoeni mahali hapa!’ Amír alipaza sauti. ‘Wakati mwingine, na darweshi huyu atakuwa amefanikiwa kuniroga!’ ‘Wewe ndiye uthibitisho dhidi ya uchawi huo,’ Mírzá Qurbán-‘Alí alimjibu, ‘ambao unaweza kuwateka wale tu wenye moyo safi. Wewe na watu wa aina yako kamwe hamuwezi kufanywa kuutambua uwezo unaovutia wa kile kioevu kitakatifu, ambacho kwa wepesi wa kufumba na kufumbua, hubadilisha roho za watu.’

“Akighadhibishwa na jibu hilo, Amír-Niẓám aliinuka kutoka kwenye kiti chake, mwili mzima ukimtetemeka kwa hasira, aliguta: ‘Hakuna chochote ila ncha ya upanga ndiyo inayoweza kuzinyamazisha sauti za watu hawa waliodanganywa!’ ‘Hakuna haja,’ aliwaambia wauaji waliokuwa wanamhudumia, ‘kuwaleta waumini wengine zaidi wa madhehebu hayo ya kuchukiza mbele yangu. Maneno hayana uwezo kuushinda ukaidi wao usioyumba. Yeyote utakayeweza kumshawishi aikane imani yake, mwachie huru; na kuhusu wengine, vikate vichwa vyao.’

“Kadiri alivyokaribia mahali pa kifo chake, Mírzá Qurbán-‘Alí, alileweshwa kwa matarajio yaliyokuwa yakikaribia ya muungano tena na Mpendwa wake, aliangukia katika udhihirisho wa furaha kubwa kabisa. ‘Harakisheni kunichinja,’ alipaza sauti kwa furaha kubwa, ‘kwani kupitia kifo hiki utakuwa umenipa kalisi ya maisha ya milele. Ingawa pumzi yangu iliyosinyaa sasa unaizima, kwa maisha lukuki Mpendwa wangu atanizawadia; maisha kama hayo ambayo moyo wa umauti hauwezi kuyafikiria!’ ‘Sikilizeni maneno yangu, ninyi ambao mnadai kuwa wafuasi wa Mtume wa Mungu,’ yeye aliwasihi, huku akiutazama umati wa watazamaji. ‘Muḥammad, Nyota ya Mchana ya uongozi Mtakatifu, ambaye katika zama zilizopita aliinuka juu ya upeo wa Ḥijáz, leo, katika utu wa ‘Alí-Muḥammad, ameinuka tena kutoka Chimbuko la Shíráz, akitawanya wangavu ule ule na akitoa joto lile lile. Waridi ni waridi tu, katika bustani

yoyote na wakati wowote ule liwezapo kuchanua.' Akiona kila upande jinsi watu walivyokuwa viziwi kwa mwito wake, alipaza kwa sauti: 'Ah, ukaidi wa kizazi hiki! Jinsi gani wasivyojali manukato ambayo lile Waridi lisiloharibika llimetawanya! Ingawa roho yangu imejaa furaha kubwa, ole, siwezi kupata hata mmoja moyo wa kushiriki nao uzuri wake, wala akili ya kuutambua utukufu wake.'

"Alipouona mwili wa Ḥájí Mírzá Siyyid 'Alí, ambao ulikuwa umekatwa kichwa na umejaa damu kwenye miguu yake, msisimko wake uliongezeka hadi kwenye kilele chake cha juu kabisa. 'Salam,' alipaza sauti wakati akijitupa juu ya mwili, 'Salam siku ya kufurahi pamoja, siku ya muungano tena na Mpendwa wetu!' 'Sogea,' alimwita kwa sauti yule muuaji, huku akiushikilia mwili mikononi mwake, 'na piga kipigo chako, kwa kuwa sahibu wangu mwaminifu hayupo radhi kujiachilia mwenyewe kutoka kwenye pambaja langu, na ananiita niharakie pamoja naye kwenye kitala cha Mpendwa Kabisa.' Kipigo kutoka kwa yule muuaji kilishuka papo hapo kwenye ukosi wa shingoni yake. Muda mfupi baadaye, mtu huyo mkuu alifariki. Kipigo hicho cha kikatili kiligusa hisia za watazamaji zikichanganyika na kuchukizwa na huruma. Vilio vya huzuni na masikitiko viliibuka kutoka katika mioyo ya halaiki, na kuchochea uchungu ambao ulikumbusha matukio ya kusikitisha ambayo kwayo kila mwaka umma ulipokea siku ya 'Áshúrá.

"3. Kisha ilikuja zamu ya Ḥájí Mullá Ismá 'íl-i-Qumí, ambaye alikuwa mwenyeji wa Faráhán. Katika ujana wake wa mwanzoni, yeye aliondoka kwenda Karbilá kwa ajili ya kutafuta Ukweli ambao aliutafuta kwa dhati. Aliungana na 'maulamá wote wakubwa wa Najaf na Karbilá, alikaa kwenye miguu ya Siyyid Káẓim, na kutoka kwake alipata ujuzi na uelewa ambao, miaka michache baadaye alipokuwa katika mji wa Shíráz, ulimwezesha kuukubali Ufunuo wa Báb. Yeye alijipambanua mwenyewe kwa uthabiti wa Imani yake na shauku kuu ya upendo wake. Mara baada ya amri ya Báb, akiwaambia wafuasi Wake kuharakia kwenda Khurásán, ilipomfikia, yeye kwa shauku aliitikia, aliungana na wenzake waliokuwa wanaelekea Badasht, na huko walipewa wadhifa wa Sirru'l-Vujúd. Wakati alipokuwa miongoni mwao, uelewa wake wa Hoja uliongezeka kwa kina zaidi na ari yake ya kuiendeleza vile vile iliongezeka sambamba. Yeye aliendelea na akawa mfano halisi wa kujitenga, na alikosa subira zaidi na zaidi ya kudhihirisha kwa namna iliyofaa roho ambayo kwayo Imani yake ilimvuvia. Katika uelezaji wa maana ya aya za Qur'án na hadithi za Kiislám, alionesha umaizi ambao watu wachache wangeweza kuushinda, na ufasaha alioutumia wakati wa kueleza zile kweli, ulimpatia mvuto ka wafuasi wenzake. Katika zile siku wakati ngome ya Ṭabarsí ilipokuwa pahali pa kukutana kwa wafuasi wa Báb, yeye alisononeka bila faraja akiugua kitandani, hakuweza kutoa msaada wake na kushiriki katika ulinzi wake. Mara tu alipopata nafuu, akigundua kwamba lile shambulio la kihistoria lilikuwa limekwisha pamoja na mauaji ya wafuasi wenzake, yeye aliinuka kwa dhamira zaidi, kufidia kwa jitihada zake za kujitolea kwa ajili ya hasara ambayo Hoja ilikuwa imepata. Dhamira hiyo hatimaye ilimfikisha kwenye uwanja wa kifo cha kishahidi na kumpatia taji lake.

"Akipelekwa kwenye uwanja wa mauaji na alipokuwa akisubiri muda wa mauaji yake, yeye aligeuza macho yake kuelekea wafia dini pacha waliomtangulia na ambao walikuwa bado wamelala wakiwa wamekumbatiana. 'Kongole, marafiki zangu wapendwa!' yeye alipaza sauti, huku akikazia macho yake kwenye vichwa vyao vilivyotapakaa damu. 'Ninyi mmeigeuza Ṭehrán kuwa paradiso! Laiti ningekuwa nimewatangulia!' Akitoa sarafu mfukoni mwake, ambayo alimpa muuaji wake, na alimuomba amnunulie kitu fulani ambacho kwacho kingetia utamu mdomoni mwake.

Yeye alikula kidogo na akampa kilichobakia, akisema: 'nimekusamehe kwa kitendo chako; sogea na unipige. Kwa kipindi cha miaka thelathini nilitamani sana kuishuhudia siku hii iliyobarikiwa, na nilihofia kuwa ningekwenda kaburini bila kutimiza tamanio hili.' 'Naomba unipokee Ee Mungu wangu,' yeye alilia, huku akigeuzia macho yake mbinguni, 'ingawa sistahili, na ridhia kuliandika jina langu juu ya gombo la wale wasiokufa milele ambao wametoa maisha yao juu ya madhabahu ya dhabihu.' Yeye alikuwa bado anafanya ibada zake ambapo muuaji, kutokana na ombi lake, ghafla aliikatisha sala yake.

"4. Alikuwa ndio kwanza ameuawa, ndipo Siyyid Ḥusayn-i-Turshízí, mujtahid, alipopelekwa kwa zamu yake kwenye uwanja wa mauaji. Yeye alikuwa mwenyeji wa Turshíz, kijiji cha Khurásán, na alikuwa anaheshimika sana kutokana na ucha Mungu na unyofu wa mwenendo wake. Alikuwa amesoma kwa miaka kadhaa katika mji wa Najaf na aliagizwa na mujtahid wenzake kwenda Khurásán na huko aeneze kanuni alizokuwa amefundishwa. Alipofika Káẓimayn, alikutana na Ḥájí Muḥammad-Taqíy-i-Kirmání, rafiki yake wa zamani, ambaye alihesabika miongoni mwa wafanyabiashara wakuu kabisa wa Kirmán, na ambaye alikuwa amefungua tawi la biashara yake huko Khurásán. Wakati akiwa njiani kuelekea Uajemi, yeye aliamua kuambatana naye. Huyu Ḥájí Muḥammad-Taqí alikuwa rafiki wa karibu wa Ḥájí Mírzá Siyyid 'Alí, mjomba wake Báb, ambaye kupitia kwake yeye aliikubali Hoja mnamo mwaka 1264 a.h., wakati akijiandaa kuondoka Shíráz kwenda hija huko Karbilá. Alipopewa habari za safari iliyotarajiwa ya Ḥájí Mírzá Siyyid 'Alí kuelekea Chihríq kwa kusudi la kumtembelea Báb, yeye alionesha shauku kubwa ya kuambatana naye. Ḥájí Mírzá Siyyid 'Alí alimshauri atekeleze kusudi lake la mwanzo na kuendelea na safari ya Karbilá na huko aisubiri barua yake, ambayo ingemfahamisha kama ingefaa kujiunga naye. Kutoka Chihríq, Ḥájí Mírzá Siyyid 'Alí aliamrishwa kuondoka na kuelekea Ṭehrán, kwa matumaini kwamba baada ya kukaa kwa muda mfupi katika mji mkuu huo angeweza kupanga upya ziara yake kwa Mpwa wake. Akiwa Chihríq, yeye alionesha kusita kwake kurudi Shíráz, kwa kuwa hakuweza kuvumilia kiburi kilichokuwa kinaongezeka cha wakazi wake. Baada ya kuwasili kwake Ṭehrán, alimuomba Ḥájí Muḥammad-Taqí kuungana naye. Siyyid Ḥusayn alimsindikiza kutoka Baghdád hadi kwenye mji mkuu na kupitia yeye aliikubali Imani.

"Wakati akiwatazama halaiki waliokusanyika kushuhudia kifo chake cha kishahidi, Siyyid Ḥusayn alipaza sauti yake na kusema: 'Nisikilizeni enyi wafuasi wa Uislamu! Jina langu ni Ḥusayn, na mimi ni mzawa wa Siyyidu'sh-Shuhadá, ambaye pia alikuwa na jina hilo. Wamujtahid wa miji mitakatifu ya Najaf na Karbilá kwa pamoja wameshuhudia juu ya daraja langu kama mfasiri anayetambulika mwenye mamlaka ya kueleza sheria na mafundisho ya Imani yao. Nilikuwa sijasikia hadi hivi karibuni jina la Siyyid-i-Báb. Weledi nilioupata juu ya tondoti za mafundisho ya Kiislamu umeniwezesha na kutambua thamani ya Ujumbe ambao Siyyid-i-Báb ameuleta. Ninaamini kwamba, kama ningeukanusha Ukweli ambao Yeye ameufunua, kwa kitendo hiki chenyewe, nimekanusha utii wangu kwa kila Ufunuo ulioutangulia. Ninamsihi kila mmoja wenu kuwaomba ma 'ulamá na mujtahid wa mji huu na kuitisha mkusanyiko, ambamo mimi nitachukua jukumu mbele yao kuthibitisha ukweli wa Hoja hii. Kisha acha waamue kama nitaweza kuthibitisha ukweli wa madai yaliyoendelezwa na Báb. Kama wataridhishwa na mathibitisho nitakayoyatoa kutetea hoja yangu, basi waache kumwaga damu ya watu wasiokuwa na hatia; na nikishindwa, basi wanipe adhabu ninayostahili.' Mara maneno haya adimu yalipotoka kinywani mwake, wakati afisa aliyekuwa katika utumishi wa Amír-Niẓám alimkatisha kwa majivuno: 'Hapa

nina hukumu ya kifo chako iliyosainiwa na kutiwa muhuri na mujtahid saba maarufu wa Ṭehrán, ambao kwa maandishi yao wenyewe wametamka kuwa wewe ni kafiri. Mimi mwenyewe nitawajibika kwa Mungu Siku ya Hukumu kwa ajili ya damu yako, na nitaweka jukumu hilo kwa wale viongozi ambao maamuzi yao tumeambiwa tuyaamini na ambao tumekuwa tukishurutishwa kutii maamuzi yao.' Kwa maneno haya alichomoa jambia lake na kumchoma kwa nguvu sana kiasi kwamba papo hapo alianguka na kufia miguuni pake.

"5. Baadaye kidogo, Ḥájí Muḥammad-Taqíy-i-Kirmání alipelekwa mahali pa kifo. Uchungu wa tukio alililoliona ulichochea hasira yake kali. 'Sogea, wewe dhalimu katili na dhalili,' alifoka wakati akimgeukia muuaji wake, 'na harakisha unichinje, kwa kuwa siwezi kusubiri zaidi kuungana na mpendwa wangu Ḥusayn. Kuendelea kuishi bila yeye ni mateso ambayo siwezi kuyastahimili.'

"6. Mara tu Ḥájí Muḥammad-Taqí alipotamka maneno haya, ndipo Siyyid Murtaḍá, ambaye alikuwa mmoja wa wafanyabiahara mashuhuri wa Zanján, aliharakia kuwatangulia wenzake. Alijitupa juu ya mwili wa Ḥájí Muḥammad-Taqí, na alisihi kwamba, kwa kuwa yeye alikuwa siyyid, kifo chake cha kishahidi kingekuwa cha thamani zaidi mbele ya Mungu kuliko kile cha Ḥájí Muḥammad-Taqí. Wakati yule muuaji alipochomoa upanga wake kutoka katika ala, Siyyid Murtaḍá alikumbuka kifo cha kishahidi cha kaka yake, ambaye alihangaika bega kwa bega na Mullá Ḥusayn; na hayo ndiyo yalikuwa maneno yake kiasi kwamba watazamaji walishangazwa na uthabiti usioyumba wa imani aliyovuviwa nayo.

"7. Katikati ya zahama iliyoibuliwa na maneno yenye mguso ya Siyyid Murtaḍá, Muḥammad-Ḥusayn-i-Marághi'í aliharakia mbele na aliomba auawe kishahidi papo hapo kabla wenzake hawajauawa. Mara tu macho yake yaliposhuhudia mwili wa Ḥájí Mullá Ismá 'íl-i-Qumí, ambaye alikuwa anampenda sana, yeye alijibwaga juu yake huku akimshikilia katika pambaja lake, yeye aliguta: 'Kamwe sitaruhusu kutenganishwa na rafiki yangu mpendwa sana, ambaye kwake nimeweka imani yangu yote na ambaye kutoka kwake nimepata mathibitisho mengi ya huba ya kweli na ya dhati!'

"Shauku yao ya kutanguliana katika kuyatoa maisha yao kwa ajili ya Imani yao, iliushangaza umati ambao ulijiuliza ni yupi kati ya watatu angependelewa zaidi ya wenzake. Walimsihi sana kiasi kwamba hatimaye walikatwa vichwa, wote watatu, kwa wakati mmoja. Imani kubwa kama hiyo, mathibitisho ya ukatili wa hali ya juu, macho ya mwanadamu kwa nadra yamepata kushuhudia.

"Japokuwa walikuwa wachache kwa idadi, bado tunakumbuka hali ya mauaji yao ya kishahidi, tunalazimika kuikiri sifa ya ajabu ya ile nguvu ambayo ingeweza kuamsha kwa nadra sana roho ya kujitoa dhabihu. Tunapokumbuka daraja ambalo wahanga hawa walilipata, tulipoona kiwango cha kujikana kwao na nguvu ya imani yao, tunapokumbuka shinikizo lililofanywa na watu maarufu kwa ajili ya kuepusha hatari ambayo kwayo maisha yao yalitishiwa, na zaidi ya yote tunapopata picha akilini mwetu, roho zilizokabiliana na mauaji ambayo maadui wasio na huruma hadi hapo walijidhalilisha wenyewe kiasi cha kuwatesa, tunalazimika kuliona tukio hilo kama mojawapo ya matukio ya kusikitisha kabisa katika historia ya Hoja hii."[14]

## SEHEMU YA 10

Aina nyingine ya sanaa yenye nguvu ni maigizo. Utunzi wa maigizo unaweza kuwa wa kifahari, pamoja na mandhari yenye mapambo, mavazi na vifaa. Bila shaka, hatuongelei maigizo kwa namna yenye utata kama hiyo. Hii haimaanishi kwamba tunahitaji kuachana na mapambo yote; wakati mwingine kitendo kidogo, kama kuvaa kofia, kinaweza kuongeza thamani ya shughuli za kisanii. Lakini hata matumizi ya msingi kabisa ya maigizo yanaweza kuwa na athari kubwa. Kwa kuwa, mbali na thamani yake kama sanaa, ni mbinu muhimu ya kielimu. Kupitia hiyo, mtu anaweza kujiona katika hali za kubuni na bila kutambua anaweza kutathmini mienendo na tabia zake mwenyewe.

Kwa hakika, kadiri watoto wanavyoendelea kupitia programu kwa ajili ya elimu yao ya kiroho, masomo hutumia mbinu hii hii katika kukuza zile tabia na mitindo ya mwenendo ambayo ni udhihirisho wa sifa za kiroho ambazo wanajitahidi kuzikuza, na walimu wanapewa mpangilio unaofaa wa matukio kwa kusudi hili. Lakini walimu wanatahadharishwa kwamba katika madaraja ya juu zaidi, watakapofika kwenye historia ya Imani, wanapaswa kuliendea suala hili kwa uangalifu mkubwa. Wanatafakari juu ya mwongozo ufuatao, ambao hutumika vivyo hivyo kwa hatua zote za mchakato wa kielimu na kwa mapana zaidi katika shughuli za sanaa kwa jumla. Kifungu cha kwanza kinatoka katika barua iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi:

> **"Kuhusu swali lako linalohusiana na ufaaji wa kuigiza matukio ya kihistoria ya Kibahá'í: Mlinzi kwa hakika angeridhia, na hata kuhamasisha kwamba marafiki wanapaswa wajihusishe na shughuli za kifasihi kama hizo ambazo, bila shaka, zinaweza kuwa za thamani kubwa ya ufundishaji. Kile anachowataka waumini wakiepuke ni uigizaji wa utu wa Báb, Bahá'u'lláh na 'Abdu'l-Bahá, ndiyo kusema wasiwaigize watu hao kama wahusika wakuu jukwaani. Hili, kama ilivyokwishatajwa, yeye huona ungekuwa utovu mkubwa wa adabu. Ukweli tu kwamba kuonekana jukwaani chenyewe kingekuwa kitendo cha ukosefu mkubwa wa adabu ambacho hakiendani kwa vyovyote na daraja lao lililotukuka kabisa. Ujumbe wao, au maneno yao halisi, ikiwezekana yanapaswa yafikishwe na kuwasilishwa na wafuasi wao waliopo jukwani."[15]**

Nukuu ifuatayo kutoka barua iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu hufafanua wazo hili zaidi:

> **"Makatazo juu ya uwasilishwaji wa Mdhihirishaji wa Mungu katika picha na michoro au katika maonesho ya maigizo hutumika kwa Wadhihirishaji wote wa Mungu. Bila shaka, zipo kazi kubwa na za kustaajabisha za sanaa za Vipindi Vitakatifu vilivyopita, ambazo kwa sehemu kubwa ziliwaonesha Wadhihirishaji wa Mungu katika roho ya unyenyekevu na upendo. Walakini katika Kipindi hiki kitakatifu, ukomavu mkubwa zaidi wa wanadamu na utambuzi mkubwa zaidi wa uhusiano kati ya Mdhihirishaji Mkuu kabisa watumishi Wake hutuwezesha kutambua kuwa haiwezekani kuwakilisha, katika umbo lolote ile la kibinadamu, iwe kwa picha, katika sanamu au katika maonesho ya maigizo, Utu wa Mdhihirishaji wa Mungu. Katika kueleza makatazo ya Kibahá'í, mpendwa Mlinzi aliweka wazi kutokuwezekana huku."[16]**

Na dondoo iliyopo hapa chini kutoka barua iliyoandikwa na Nyumba ya Haki hutoa mwongozo wa nyongeza.

> **“. . . uchunguzi wa barua za mpendwa Mlinzi huweka wazi kabisa kwamba hairuhusiwi kuigiza jukwaani umbo la Mdhihirishaji wa Mungu, wala hata la Bwana. . . .**
>
> **“Utumiaji wa mwanga, uwe ni mkali sana au wa rangi tofauti tofauti, unahitaji uangalifu wenu mkubwa. Kwa namna yoyote ile ikiwa utumiaji wa mwanga utaonesha utu wa Mdhihirishaji wa Mungu, haupaswi kutumika, lakini kama unaweza kutumika kwa namna yoyote bila kuonesha kwamba Mtume anawakilishwa au kufananishwa, basi hakuna kizuizi cha utumiaji.”**[17]

Kuhusiana na hili, wakati baadhi ya mfululizo wa matukio tangu siku za mwanzo za Imani yangeweza kuigizwa tena, yangehitaji kufanyika kwa busara kubwa. Katika hali za matukio fulani, kwa mfano, inaweza kuthibitisha uwezekano kwa mtu kuchukua wajibu wa msimuliaji, akitoa muundo kwa ajili ya mlolongo wa matukio na kusita katika wakati unaofaa na kuruhusu wengine kuigiza sehemu zilizo teuliwa. Pamoja na washiriki wa kikundi chako leo, chagueni tukio moja kutoka katika Historia ya mwanzo ya Imani, na kisha amueni sehemu zipi za hadithi zinapaswa kusimuliwa na zipi zinazoweza kuigizwa. Jadilini ni wakati gani katika usomaji wa mlolongo mkuu ingefaa kwa kikundi cha vijana kusaidiwa katika kuandaa igizo kama hilo.

__________________________________________________________
__________________________________________________________
__________________________________________________________
__________________________________________________________
__________________________________________________________
__________________________________________________________
__________________________________________________________
__________________________________________________________

Shughuli za uigizaji, bila shaka, hazihitaji kufungiwa kwenye maigizo ya historia. Kama ilivyotajwa awali, miundo rahisi ya maigizo yanaweza kuwa kama nyenzo ili kuongeza tajiriba ya ufundishaji na ujifunzaji. ili nyenzo kama hiyo iweze kufaa, hata hivyo, ni muhimu kwamba roho ya urafiki wenye upendo, bila kuwa na upuuzi na mzaha, itawale katika mazingira ambamo kikundi hujifunza kinasoma na kutafakari, ikiwa ni kikundi cha mafunzo, kampeni ya taasisi au kambi. Pale ambapo nidhamu ya kiroho ihitajikayo ipo miongoni mwa washiriki wake, wale ambao ni hodari na wenye vipaji wanaweza kuandaa na kuigiza maigizo mafupi ya michezo ya uhusika ambayo hutoa maana halisi kwa baadhi ya dhana na kanuni za kiroho wao wanazojifunza katika kozi za taasisi. Fikirieni kitengo cha kwanza cha Kitabu cha 1, na mjadili ni yapi mawazo na dhana za kiroho zingeweza kukaziwa kwa maigizo mafupi na michezo ya uhusika. Jinsi gani ungeweza kuhakikisha kwamba shughuli hii inafanyika kwa madaha na uzuri na bila upuuzi na ukosefu wa heshima kwa utu wa binadamu ambavyo kwa bahati mbaya vimekuja kudhalilisha muundo huu wa sanaa?

__________________________________________________________
__________________________________________________________
__________________________________________________________

Kutakuwa na matukio ambapo washiriki wa kikundi cha mafunzo watapenda kujumuisha uwasilishaji wa maigizo katika programu wanayo ipanga kwa ajili ya hadhira. Tukio mojawapo kama hilo ni sherehe ambayo aghalabu kufanyika wakati wa kumaliza kozi, ambapo familia na marafiki wa washiriki kwa kawaida hukaribishwa. Desturi hii pia hufuatwa na kikundi cha vijana chipukizi pale wanapomaliza usomaji wa matini. Katika matukio kama haya, washiriki wangeweza siyo tu kufanya uwasilishaji wa maigizo bali pia kughani mshahiri, kutoa hotuba, kutamba hadithi na kucheza muziki.

## SEHEMU YA 11

Onesho la kisanii linajumuisha eneo pana la jitihada za mwanadamu zinazoitwa stadi za mikono. Hapa, korija za vifaa—kama vile ngozi, sufu, pamba, hariri, mawe, udongo wa mfinyanzi, kioo, chuma, mbao, nta, majani makavu, maua yaliyokaushwa—vinabadilishwa katika namna lukuki kwa mikono yenye ustadi kuwa vitu, vyenye manufaa au la, kubadili sifa za asili za vifaa ili kuunda uzuri. Orodha ya kazi za mikono ni ndefu kwa uhakika. Miongoni mwa zile maarufu zaidi ni ususi, kutarizi, ushonaji wa mikono, ufumaji, ushonaji wa viatu, ufundi cherehani, upakaji wa rangi, sanaa ya ufinyanzi, vyombo vya udongo, usonara, ufundi wa ngozi, usukaji wa vikapu, uchongaji, useremala, utengenezaji viunzi, utengenezaji wa mishumaa, uchezeshaji wa vikaragosi, utengenezaji wanasesere, uchapishaji, utengenezaji kamba za viatu na ufarishi. Upaswa kuongeza nyingine zaidi kwenye orodha. Baada ya kufanya hivyo, jadili pamoja na kikundi chako kazi zipi ni maarufu zaidi katika eneo lako.

Ikiwa umewahi kuhudumu kama mhuishaji wa kikundi cha vijana chipukizi, pengine tayari una tajiriba kidogo katika kuwasaidia kujifunza kuhusu baadhi ya stadi za mikono za asili. Jinsi utakavyoweza kutambulisha kwa ufasaha ufanyaji wa stadi za mikono katika mchakato wa kielimu kwa ajili ya vijana na watu wazima wenye umri mkubwa huhitaji fikra zenye umakini. Itakuwa yenye umuhimu kwako kufikiria hali za washiriki wa kila kikundi na vipaji vyao, upatikanaji wa rasilimali na kadhalika. Zaidi, kama hautakuwa na umahiri katika stadi ya mikono moja au zaidi, utahitaji kumtafuta mtu mwenye ujuzi unaohitajika ili akusaidie na zinaweza kuwepo fursa, hususan wakati wa kambi au kampeni shadidi, kuandaa vipindi

kadhaa kwa ajili ya washiriki kujifunza stadi za mikono mahsusi. Ili kukusaidia kutafakari juu ya umuhimu wa muundo huu maonesho ya kisanaa, soma nukuu mbili zifuatazo kutoka Maandiko na jadili na washiriki wengine wa kikundi chako:

> **"Mojawapo ya majina ya Mungu ni Mfanyiza. Yeye hupenda ufundi stadi. Kwa hiyo yeyote kati ya watumishi wake ambaye hudhihirisha sifa hii anakubaliwa machoni pa Mdhulumiwa huyu. Ufundi stadi ni kitabu miongoni mwa vitabu vya sayansi vitakatifu, na hazina miongoni mwa hazina za hekima yake ya mbinguni. Huu ni ujuzi wenye maana, kwani baadhi ya sayansi huletwa na maneno na huishia kwa maneno."**[18]

> **"Mungu mmoja wa kweli, atukuzwe Yeye, hupenda kushuhudia kazi za mikono zenye ufundi stadi wa juu zilizofanyizwa na wapendwa Wake. Umebarikiwa wewe, kwa kuwa kile ambacho ujuzi wako umekifanyiza kimefikia uwepo wa Bwana wako, Mhamishwa, Mdhulumiwa. Tunamuomba Mungu kuwa kila mmoja wa marafiki Wake wawezeshwe kupata mojawapo ya stadi za mikono na watathibishwa katika kufuata kile ambacho kimeamriwa katika Kitabu cha Mungu, Mtukufu kabisa, Mwenye Hekima kabisa."**[19]

## SEHEMU YA 12

Inatumainiwa kwamba sehemu zilizotangulia zimeongeza utambuzi wako juu ya nafasi ya jitihada za kisanii inavyohusika katika uboreshaji wa mchakato wa kielimu unaoendelea kukuzwa mashinani, hali kadhalika katika nguvu za jitihada zetu za pamoja. Pia utakuwa umetambua kwamba jitihada kama hizo, hususan katika suala la stadi za mikono, huchota, kadiri ziwezavyo, kutoka desturi za kisanii za eneo, zinaweza kwenda mbali katika kuinua utambuzi kwa ajili ya utajiri wa tamaduni anuai. Katika hili, bila shaka mtakumbuka suala lililoibuliwa katika Kitabu cha 5 kwamba, kama onesho la utamaduni, shughuli ya kisanaa hubeba maadili. Utakuwa mwangalifu, basi, kuchagua shughuli za kisanii zinazofaa, zile ambazo bila uangalifu huingiza maadili yanayobomoa, katika njia zisizokuwa wazi, mchakato wa kielimu au ruwaza za maisha ya jumuiya zinazobumbwa nazo. Ruwaza kama hizo, lazima zitambulike, ziakisi maadili ya utamaduni mpya uibukao, unaovuviwa na Ufunuo wa Bahá'u'lláh. Soma nukuu ifuatayo kutoka ujumbe ulioandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ambayo mliisoma, kwa kiasi fulani katika Kitabu cha 6:

> **"Wakisukumwa na nguvu zinazofanyizwa kote ndani na nje ya jumuiya ya Kibaha'i, watu wa dunia wanaweza kuonekana wakijongea kutoka sehemu tofauti tofauti kuja karibu zaidi na zaidi mmoja kwa mwingine, kuelekea kile kitakachokuwa ustaarabu wa ulimwengu wenye tabia ya kustaajabisha sana kiasi kwamba ingekuwa ni kazi bure kwetu kujaribu kuufikiria kwa wakati huu. Kadiri kani hii ya mjongeo wa watu inavyochapuzwa kote ulimwenguni, baadhi ya vipengele katika kila utamaduni, ambavyo haviendani na mafundisho ya Imani, pole pole vitaachwa kando ambapo vingine vitaimarishwa. Vile vile, vipengele vipya vya utamaduni vitaendelea kukua kipindi hadi kipindi kadiri watu kutoka kila kundi la wanadamu wanavyovuviwa na Ufunuo wa Baha'u'llah, kudhihirisha ruwaza za fikra na vitendo vinavyoletwa na mafundisho Yake, kwa kiasi fulani kupitia kazi za kisanaa na fasihi. Ni pamoja na mtazamo kama huo akilini kwamba tunaupokea uamuzi wa Taasisi ya Ruhi, katika uandaaji wa kozi**

**zake, kuwaachia marafiki kushughulikia masuala yanayohusiana na shughuli za kisanii katika ngazi ya eneo. Tunachokiomba kwenye hatua hii, basi, pale ambapo nguvu zinapohitaji kuwekezwa katika uongezaji wa madarasa ya watoto na vikundi ya vijana chipukizi, ni kwamba uzidishwaji wa nyenzo za ziada kwa ajili ya kusudi hili, sharti ujitokeze kiasilia, kama matokeo ya mchakato wa ujengaji jumuiya ukuavyo zaidi na kushika hatamu katika vijiji na ujirani, tuna shauku ya kuona, kwa mfano, uibukaji wa nyimbo zinazovutia kutoka kila sehemu ya ulimwengu, katika kila lugha, ambazo zitatilia mkazo juu ya utambuzi wa vijana kuhusu dhana za kina zilizomo katika mafundisho ya Kibahá'í. Hata hivyo msukumo huu wa mawazo yenye ubunifu hautatimia, ikiwa marafiki wataanguka, bila uangalifu, katika ruwaza zilizoenea ulimwenguni ambazo huwaruhusu wale wenye vyanzo vya kifedha kulazimisha mitazamo yao ya kitamaduni kwa wengine, wakiwamiminia nyenzo na bidhaa zinazo tangazwa kwa nguvu. Zaidi, kila jitihada lazima ifanywe kwa ajili ya kulinda elimu ya kiroho dhidi ya hatari za kugeuzwa kuwa biashara."[20]**

Kwa hiyo, utamaduni, utakuwa mojawapo ya shughuli zako enedelevu za kila mara. Utahitaji kuwa mwangalifu, ikiwa unataka kuushinda ushawishi wa utamaduni wa kiyakinifu unao shambulia maisha ya jamii ya wanadamu, na utapenda kuhakikisha kwamba angalau baadhi ya maonesho ya kisanii utakayochagua yanawakilisha ubora wa utamaduni wa watu wako, ukitumia mbinu na vyombo vya kitamaduni, lakini pamoja na maudhui mapya ya kiroho na kimaadili yaliyovuviwa na Imani. Basi hii inaweza kuwa fursa nzuri kwako, kuchukua muda kidogo wa kutafakari juu ya urithi wa kisanaa wa watu wako. Jibu maswali yafuatayo na andika aya fupi juu ya mada hii:

a. Ni aina zipi za muziki ambazo watu hucheza au kusikiliza katika eneo lako? Je, eneo lako lina nyimbo zake maalum za kitamaduni, kama zile zinazoimbwa shambani wakati wa mavuno au wakati wa kuchunga mifugo, au nyimbo zake za upendo, nyimbo za kubembeleza, nyimbo za watoto na muziki mtakatifu? Je, kuna aina fulani ya muziki unaotumika kitamaduni katika matukio maalum, kama vile harusi, msiba, au sherehe? Ni ipi baadhi ya mifano ya nyimbo na muziki ambayo imeibuka katika eneo lako kadiri mchakato wa taasisi ulivyoimarika?

b. Je, kuna ala zozote za muziki ambazo ni maalum kwa eneo hilo? Je, hufaa kwa aina gani ya muziki? Je, kuna zozote ambazo vijana na watu wazima wenye umri mkubwa ili kuchangamsha matukio ya jumuiya?

c. Je, utambaji hadithi ni utamaduni miongoni mwa watu wako? Je, utamaduni huu umesitawishwa kupitia kushiriki hadithi kutoka kwenye maisha ya 'Abdu'l-Bahá na Historia ya Imani wakati wa ziara za nyumbani na katika mikusanyiko ya jumuiya?

d. Ni zipi baadhi ya aina pendwa za maigizo katika eneo lako? Jinsi gani yanavyoonesha mfululizo wa matukio kutoka katika historia ya watu wako na visa vya mashujaa wake wa kiume na wa kike? Je, aina hii ya sanaa inatumika kuinua utambuzi wa pamoja wa dhana za kiroho na kanuni zinazosomwa katika kozi za taasisi?

e. Jinsi gani stadi za mikono za kiutamaduni za eneo lako zinavyoeleza uzuri, ulinganifu na madaha? Jinsi gani zinatumika kuongeza maendeleo kwa ujumla ya vijana, hususan wale wanaoshiriki katika programu ya uwezeshaji wa kiroho wa vijana chipukizi?

## SEHEMU YA 13

Kwa hakika, kama ulivyoelewa kutokana na usomaji wenu wa kitengo hiki, hauhitaji kuwa mwigizaji, mtunzi wa maigizo, mshahiri, au mwana muziki kwa ajili ya kuendeleza sanaa

mashinani. Kile unachopaswa kukumbuka ni kwamba kozi za taasisi kimsingi zinahusika na uwezeshaji wa kiroho na wa kimaadili, pamoja na uachiliaji wa uwezo wa roho ya mwanadamu. Kama mkufunzi, katika uendelezaji wa sanaa na stadi za mikono katika namna zilizoelezwa hapa, utachangia katika kufungua njia za ubunifu ambamo kupitia humo utaweza kutiririka uvuvio na nguvu ya mvuto kwa uzuri.

# MAREJELEO


1. Kutoka ujumbe wa 30 Desemba 2021 kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Mabara, iliyochapishwa katika *Mpango wa Miaka Tisa, 2022–2031: Jumbe za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu* (West Palm Beach: Palabra, Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2022), na. 6.12, uk. 50.

2. 'Abdu'l-Bahá, katika *Umuhimu wa Sanaa katika Kuendeleza Imani: Dondoo kutoka Maandiko ya Kibahá'í*, zimekusanywa na Idaa ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu (Ingleside: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, Australia, 2020), na. 23, uk. 20.

3. Kama hapo juu, na. 24, uk. 20 (toleo la Kiingereza).

4. *Mateuzi kutoka kwa Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2010, chapisho la 2015), na. 175.1, uk. 282.

5. Kutoka Mazungumzo ya 18 Juni 1912, yaliyochapishwa katika *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu: Mazungumzo yaliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá wakati wa ziara Yake huko Marekani na Canada mnamo 1912* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2012), aya. 2, uk. 287.

6. Bahá'u'lláh, katika *Kitáb-i-Aqdas* (Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, New Delhi, India chapisho la Kiswahili la 2024), aya. 51, uk. 33.

7. *Mateuzi kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá*, na. 74.1, uk. 159.

8. 'Abdu'l-Bahá, katika *Muziki: Dondoo kutoka Maandiko ya Kibahá'í*, zimekusanywa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu (Ingleside: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, Australia, 2020), na. 15.8, uk. 17.

9. 'Abdu'l-Bahá, katika *Umuhimu wa Sanaa katika Kuendeleza Imani*, na. 10, ku. 12–13.

10. 'Abdu'l-Bahá, katika makusanyo ya *Muziki*, na. 14.1, uk. 14.

11. Kama hapo juu, na. 14.2, uk. 15 (toleo la Kiingereza).

12. Nyongeza ya maneno kwa mwandiko wa Shoghi Effendi kwenye barua ya 17 Novemba 1932 iliyoandikwa kwa niaba yake kwa mtu binafsi.

13. Kutoka barua ya 8 Juni 1933 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa mtu binafsi.

14. *Wana-Mapambazuko*: Masimulizi ya Nabíl ya Siku za Mwanzo za Ufunuo wa Kibahá'í (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1932, chapisho la 2021), ku. 446–58.

15. Kutoka barua ya 25 Julai 1936 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa mtu binafsi, katika '*Umuhimu wa Sanaa katika Kuendeleza Imani*, na. 35, uk. 28.

16. Kutoka barua ya 9 Machi 1977 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa mtu binafsi, kama hapo juu, na. 49, ku. 36–37.

17. Kutoka barua ya 12 Agosti 1975 iliyoandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa mtu binafsi, katika "Kuwaigiza Wakuu wa Imani: Makusanyo ya Dondoo kutoka Barua zilizoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu", zimekusanywa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, na. 6; pia imenukuliwa kwa sehemu, katika *Miangaza ya Uongozi*: *Faili la Marejeleo ya Kibahá'í* (New Delhi: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1988, chapisho la 2016), na. 343, uk. 99 (toleo la Kiingereza).

18. Bahá'u'lláh, katika "Dondoo kutoka Maandiko kuhusIiana na Sanaa na Stadi za Kazi", zilizochapishwa katika *Makusanyo ya Makusanyo* (Maryborough: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, Australia, 1991), toleo. 1, na. 2, uk. 1 (toleo la Kiingereza).

19. Kama hapo juu, na. 4, uk. 1.

20. Kutoka ujumbe wa 12 Desemba 2011 ulioandikwa kwa Mabaraza yote ya Kiroho ya Kitaifa, kuchapishwa katika *Muundo wa Kiutendaji: Jumbe Zilizoteuliwa za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na Nyenzo za Kujaliza, 2006–2016* (West Palm Beach: Palabra Shirika la Uchapishaji, 2017), na. 20.19, ku. 136-37.